
**Mwongozo wa Pili**

# Mafunzo Ya Omega

## *Mafunzo ya Vitendo Kwa wapanda Kanisa*



*Na Muungano wa Kueneza Upandaji kanisa Wakishirikiana na Huduma ya Peter Dayneka wa Urusi*

**Kozi ya Omega:**
**Mafunzo ya Vitendo Kwa Wapanda kanisa**
**Mwongozo wa Pili**

Tafsiri ya asili ilichapishwa na
The Bible League, P.O. Box 28000, Chicago, IL 60625 USA
Tel: (800) 334-7017 E-mail: info@BibleLeague.org www.bibleleague.org

Copyright © 2000,2006 United World Mission.
Machapishwo haya kwa asili yalinukuliwa na *The Alliance for saturation Church Planting* na yaliandaliwa na ushirika huo kwa kushirikiana na huduma ya Peter Deyneka wa Urusi, mradi 250.

Unaruhusiwa na Unashauriwa kuzalisha na kusambaza zana hii katika mfumo wowote endapo kama: (1) Unampa sifa mwandishi, (2) unaonyesha kama marekebisho yamefanyika, (3) Hulipishi zaidi ya gharama ya kuzalishia tena, na (4) hutengenezi kopi zaidi ya 1000.
Kama utapenda kuweka nakala za nyenzo hii kwenye internet au kama matarajio yako ya matumizi ni tofauti na vichwa vya habari hapo juu tafadhali wasiliana na
United World Mission: Jay Weaver/Omega, 9401-B Southern Pines Blvd.
Charlotte, NC 28273-5596, or omega_course@alliancescp.org

Kutafsiri na kurithi katika lugha yako pia kunashauriwa. Tena, tafadhali wasiliana na omega_course@alliancescp.org ili kwamba tuweze kutia moyo na kuwajulisha wengine wanaoweza pia kuwa wamevutiwa katika lugha yako au matumizi yaliyokusudiwa.

Kwa taarifa zaidi juu ya huduma zao za kuheshimika, tafadhali wasiliana na :

THE ALLIANCE
FOR SATURATION CHURCH PLANTING

(tovoti/rasilimali zinapatikana ila kwa sasa ushirikiano huo haupo tena)
http://www.alliancescp.org/resources/interchanges/2005_aug.html

Peter Deyneka
Russian Ministries

P.O. Box 496
Wheaton, IL , USA 60189
Tel: (630) 462-1739 Fax: (630) 690-2976
info@russian-ministries.org
www.russian-ministries.org

Kwa asili yalipigwa chapa au yalichapishwa katika nchi ya Marekani (USA).

# SHUKURANI


Tunatoa shukurani zetu kwa moyo wa dhati na za pekee kwa wote waliochangia katika matayarisho ya miongozo hii ya mafunzo. Wafuatao ni watu waliojitoa sana kwa kiwango kikubwa kwenye hatua ya kuandika na kutengeneza miongozo hii. Bwana, panda kanisa lako…mpaka miisho ya dunia.

Jay Weaver, Mtengenezaji, Timu ya Ulimwengu

| | |
|---|---|
| Richard Beckham | *Greater Europe Mission* |
| David & Lisa Bromlow | *Christ For Russia* |
| Ron Brunson | *World Witness and United World Mission* |
| Don Crane | *Greater Europe Mission* |
| Bea Crane | *Greater Europe Mission* |
| Hunter Dockery | *World Harvest Mission* |
| Mike Elwood | *Greater Europe Mission* |
| Jeff Geske | *United World Mission* |
| Dave Henderson | *C B International —Project 250 of Peter Deyneka Russian Ministries* |
| Bob Mackey | *United World Mission* |
| Bob Martin | *United World Mission* |
| Paul Michaels | *Grace Brethren Intl. Mission* |
| Norie Roeder | *United World Mission* |
| Ki Sanders | *World Team* |
| Larry Sallee | *UFM International —Project 250 of Peter Deyneka Russian Ministries* |
| Eric Villanueva | *United World Mission* |
| David Westrum | *Interlink Ministries —Project 250 of Peter Deyneka Russian Ministries* |

**SHUKRANI ZA PEKEE KWA AJILI YA MSAADA WAO WA KIUONGOZI NA UTALAAM**

| | |
|---|---|
| Edith Bond | *The Alliance Regional Resource Team* |
| David Gál | *The Alliance Regional Resource Team* |
| Nell Harden | *Retired English Professor* |

# MWONGOZO WA PILI

## Yaliyomo

**DIBAJI** ........ **8**

**MAELEZO KUHUSU MUUNGANO** ........ **10**

**MZUNGUKO WA UPANDAJI KANISA** ........ **11**

**MITAALA** ........ **12**

**MTAZAMO WA UTARATIBU** ........ **14**

**MAONO YA KUM** ........ **19**

**SOMO LA 5: Misingi ya Kibiblia ya Kueneza Upandaji kanisa** ........ **20**

I. Kueneza katika Agano la Kale ........ 20
II. Huduma ya Yesu ........ 21
III. Misingi ya Kibiblia ya Keneza Upandaji Kanisa ........ 21
IV. Makanisa Mangapi Yameenezwa? ........ 23
V. Kueneza upandaji Kanisa katika Historia ........ 24

**SOMO LA 6: Warsha ya Utafiti** ........ **26**

I. Sehemu ya kwanza—Taarifa za Msingi Zilizokusanywa (Dakika 5-7): ........ 26
II. Sehemu ya Pili—Mchanganuo wa Habari za Utafiti (Dakika 5-8) ........ 27

**SOMO LA 7: Kuhamasisha Raslimali Kwa Kupitia Utafiti** ........ **28**

I. Wito Kwenye Utendaji ........ 28
II. Mipaka Kwenye Kushirikisha Habari ........ 29
III. Kutazama Jinsi ya Kuhamasisha Nguvu ya mavuno ........ 30
IV. Mchanganuo Juu ya Jinsi Utafiti Unavyoweza Kutumiwa Kuhahamasisha Rasilimali ........ 31

**KANISA** ........ **33**

**SOMO LA 5: Asili ya Kanisa** ........ **33**

I. Maana na Matumizi ya Neno “Kanisa” ........ 34
II. Dhana ya Uongo Juu ya Kanisa ........ 35
III. Methali Zinazoelezea Kanisa Kama Kiumbe Hai ........ 37
IV. Kupanda Kanisa Hai ........ 38

**SOMO LA 6: Kazi za Umoja za Kanisa** ........ **40**

I. Umoja Dhidi ya Majukumu ya Binafsi ya Kanisa ........ 40
II. Kazi za Umoja wa Kanisa ........ 41
III. Ni Wakati Gani wa Kufanya Kazi ya Umoja ........ 45
***Ziada: Ubatizo Katika Agano Jipya*** ........ ***47***

**SOMO LA 7: Kuanzisha Maelezo ya Kusudi la Kanisa** ........ **49**

I. Ni nini Maelezo ya Kusudi? ........ 49
II. Kutafuta Kusudi la Kanisa Lako ........ 50
III. Kuandika Maelezo ya Kusudi la Kanisa la Mtaa ........ 50

**SOMO LA 8: Falsafa ya Huduma ya Upandaji Kanisa ... 52**

I. Ni nini Falsafa ya Huduma ya Upandaji Kanisa ... 52
II. Hitaji la Falsafa ya Huduma ya Upandaji Kanisa ... 54
III. Yaliyomo Katika Falsafa Yenye Ufanisi ya Huduma ya Upandaji Kanisa ... 56
IV. Kutengeneza Falsafa Yako Mwenyewe ya Huduma ya Upandaji Kanisa ... 56
V. Mfano wa Falsafa ya Huduma ... 57
***Ziada: Kuanzisha Falsafa ya Huduma ya Upandaji Kanisa ...59***

**TABIA YA KIROHO ...63**

**SOMO LA 6: Kuishi Kama Wana Badala Ya Kuishi Kama Yatima ... 64**

I. Maisha Kama Yatima ... 64
II. Wakristo Wanaofikiri na Kutenda Kama Mayatima ... 65
III. Uwana Wetu na Mungu ... 66
IV. Jinsi Tunavyoshindwa Kuelewa Uwana Wetu ... 67

**SOMO LA 7: Kujifunza Kuwa Wana ... 69**

I. Moyo Uliolemewa Dhidi ya Moyo Uliowekwa Huru ... 69
II. Moyo wa Majigambo Dhidi ya Moyo Ulio Katika Ushirika na Baba ... 70
III. Moyo wa Ubinafsi Dhidi ya Moyo Ulio Huru Kuwapenda Wengine ... 71
***Ziada: Mayatima Dhidi ya Wana ...73***

**MAOMBI ...75**

**SOMO LA 4: Kongamano la Maombi ... 76**

I. Kumsherehekea Bwana (Zaburi 95:1-5) ... 76
II. Kumwabudu Bwana (Zaburi 95:6-7) ... 77
III. Kuisikia Sauti Yake (Zaburi 95:8-11) ... 77

**UONGOZI ...79**

**SOMO LA 1: Kanuni za Kibiblia za Uongozi ... 80**

I. Tafsiri ya Uongozi ... 80
II. Kanuni za Uongozi wa Kibiblia ... 81
***Ziada: Michanganuo ya Uongozi ...85***

**SOMO LA 2: Sura ya Kiongozi ... 87**

I. Kutunza Tabia Inayofanana na ya-Kristo ... 87
II. Fanya Kazi Vizuri na Timu ... 88
III. Endeleza Kujaliwa Vipawa na Uwezo wa Wengine ... 88
IV. Jua Jinsi ya Kugawa Majukumu ... 88
V. Weka Malengo, Maazimio na Makusudio na Yafanyie Kazi ... 89
VI. Kueleza Wazi Maono katika Njia Ambayo Inawavuta Wengine ... 89
VII. Dumu na Shinda Vikwazo ... 90
VIII. Ongoza katikaUinjilisti ... 90
***Ziada: Kiongozi ...92***

**VIKUNDI KIINI ....95**

**SOMO LA 1: Kazi na Faida za Vikundi Kiini .... 96**

I. Misingi ya Kikundi Kiini .... 96
II. Kazi za Vikundi Kiini .... 97
III. Faida za Vikundi Kiini .... 98

**SOMO LA 2: Kanuni za Uongozi wa Kikundi Kiini .... 103**

I. Wazo la Uongozi Kwa Ujumla .... 103
II. Kuongoza Mkutano wa Kikundi Kiini .... 104
III. Utawala wa Kikundi Kiini .... 107
***Ziada: Kikundi Kiini Kivunja Barafu ....108***
***Ziada: Mfano wa Shughuli Katika Mkutano wa Kikundi Kiini ....113***

**SOMO LA 3: Kuanzisha kikundi Kiini .... 114**

I. Andaa Kwa Ajili ya Kikundi Kiini Kipya .... 114
II. Fanya Mawasiliano .... 115
III. Chagua Mahali .... 115
IV. Andaa Kwa Ajili ya Mkutano wa Kwanza .... 116
***Ziada: Karatasi ya Kupangia ....118***

**SOMO LA 4: Uinjilisti wa Kikundi Kiini .... 119**

I. Aina Mbili za Wasioamini .... 119
II. Kuitambua Oikos .... 120
III. Vikundi vya Kushirikisha .... 121
IV. Utaratibu wa Uinjilist wa Kikundi Kiini .... 121
***Ziada: Kuhusu Oikos ....124***

**SOMO LA 5: Onyesho la Kikundi Kiini .... 127**

I. Onyesho la Kikundi Kiini .... 127
II. Tathimini .... 129

**SOMO LA 6: Falsafa ya Huduma ya Kikundi Kiini .... 130**

I. Falsafa ya Kikundi Kiini .... 130
II. Vielezo vya Huduma ya Kikundi Kiini .... 132
III. Kuanzisha Mkakati wa Huduma ya Kikundi Kiini .... 135

**NJIA ZA KUJIFUNZA BIBLIA ....137**

**SOMO LA 8: Njia Tofauti Tofauti za Kutumia Kujifunza Biblia kwa Kufata Neno .... 138**

I. Marudio ya Kanuni za Mafunzo ya Biblia kwa Kufata Neno .... 138
II. Mfunzo ya Habari za Maisha .... 139
III. Mafunzo ya Kitabu .... 142
IV. Mafunzo ya Kisa .... 145
***Ziada: Mafunzo ya Habari za Maisha ya Barnaba ....147***

**SOMO LA 9: Kuongoza Mafunzo ya Biblia kwa kufata Neno .... 152**

I. Tabia za Kikundi Cha Kujifunza Kwa Kufata neno .... 152
II. Maandalizi ya Mafunzo .... 153
III. Kuongoza Mafunzo .... 154
***Ziada: Mafunzo ya Biblia Kwa Kufata Neno Katika Mathayo 20:17-28 ....157***
***Ziada: Mafunzo ya Biblia Kwa Kufata Neno Katika Luka 15:1-7 ....160***

**SOMO LA 10, 11: Warsha Juu ya Kuongoza Mafunzo ya Biblia Kwa Kufata Neno ............. 163**

***Ziada: Vifungu vya Kujifunza kwa Kufata Neno ...........................................167***

**UINJILISTI .........................................................................................................169**

**SOMO LA 4: Uinjilisti na Upandaji Kanisa ......................................................................... 170**

I. Hitaji la Njia Mpya ........................................................................................................ 170
II. Mbio za Kupokezana ..................................................................................................... 171
III. Kanuni za Uinjilisti ...................................................................................................... 172
***Ziada: Kutathimini Mikakati ya Uinjilist .........................................................176***

**SOMO LA 5: Vizuizi Vya Uinjilisti wa Mafanikio ................................................................... 178**

I. Tazizo la Vizuizi na Hitaji la Madaraja .............................................................................. 178
II. Kuelewa Vizuizi Vinavyorudisha Nyuma Uinjilsti ............................................................ 179
III. Vizuizi Vya Nje Kwa Uinjilisti Wenye Mafanikio ............................................................. 180
IV. Vizuizi vya Ndani kwa Uinjilisti wa Ufanisi ..................................................................... 181
V. Mkakati wa Kushinda Vizuizi ........................................................................................ 182
***Ziada: "Kanisa Kwa Watu Wote: Maongezi Laini Juu ya Ugumu wa Somo"..........................................................................................................184***
***Ziada:Kujibu Upinzani wa Kawaida ..............................................................189***

**SOMO LA 6, 7: Utaratibu Wa Kukata Shauri .......................................................................... 191**

I. Kuchunguza Mahitaji ya Watu ......................................................................................... 192
II. Kutathimini Watu Walipo Katika Kuelewa Kwao kwa Injili ............................................... 193
III. Kuelewa Awamu Nne za Shughuli Zinazoendana na Kuwaleta Watu Kwa Kristo .......... 194
IV. Kuonyesha Mkakati wa Uinjilisti ..................................................................................... 195
***Ziada: Hali ya Mtu Unayetaka Kuinjilisha ......................................................197***
***Ziada: Kanuni Tatu Kwa Uinjilisti wa Kimkakati ...........................................199***
***Ziada: Kuchunguza Njia Aliyotumia Yesu Kwa Mtu Binafsi .........................201***

# DIBAJI

## KUSUDI LA NYENZO HII

Wapanda kanisa mara nyingi wanafunzwa na kupelekwa nje wakiwa na mafunzo kidogo au bila mafunzo kwa ajili ya kazi iliyo mbele yao. Viongozi wa kanisa ambao wamezidiwa na matatizo ya huduma mara nyingi wanakosa maono wazi ya kile Mungu anachotaka kukamilisha kupitia wao. Wote wapanda kanisa na viongozi wa kanisa wanahitaji mafunzo na maono, lakini shule za Biblia na seminari siyo uchaguzi unaofahamika kwa wengi.

Nyenzo hii imeandaliwa siyo kutoa maono tu kwa wapanda kanisa na viongozi wa kanisa, lakini pia msingi wa kibiblia na ujuzi wa vitendo wa huduma ili kuona maono hayo yanakuwa kitu halisi. Siyo kielimisho cha "maazimio." Badala yake, inatoa misingi muhimu ya kibiblia na kielimu, vilevile na ujuzi wa vitendo wa huduma, unaohitajika kwa upandaji kanisa. Ingawa kozi ya Omega iliandaliwa kwa ajili ya Ulaya ya mashariki na Kati na Muungano wa Urusi ya zamani, tumetiwa moyo na taarifa ambazo zimeshapatikana kuwa za msaada zinaporithiwa katika mandhali zingine.

Kozi yote hii imeandaliwa kukamilisha malengo mawili:

1. Kutoa mafunzo muhimu kwa makanisa kuweza kupandwa.
2. Kutia moyo uhamasishaji katika mwili mzima wa Kristo kuelekea harakati za upandaji kanisa.

Leo tunaona harakati za upandaji kanisa zikitokea katika nchi nyingi ulimwenguni kote, ikiwemo, Brazil, Roma, Ufilipino, Nigeria, na kwingine. Tunaamini kwamba kanisa la mtaa ni chombo cha msingi cha kuinjilisha ulimwengu, na kwamba upandaji wa kanisa unaotokana na kanuni ya kuongezeka mara dufu ni njia yenye mafanikio zaidi ya kutumia kuelekea kwenye kukamilisha utume mkuu. Makanisa mapya lazima yapandwe kwa maono ya kuongezeka mara dufu na uwezo wa kupanda makanisa mengine mapya. Hili linapotokea, kuna uwezekano wa harakati za makanisa zinazoweza kupangusa kuzunguka taifa na kubadilisha maisha ya watu katika nchi yote.

Harakati za upandaji kanisa zinahitaji watu waliohusika katika ngazi zote za kazi ya upandaji kanisa, kutokea kwa waumini wachanga walio na shauku ya imani yao mpya, hadi kwa viongozi wa madhehebu. Wapanda kanisa peke yao hawawezi kuwa kiungo cha harakati za upandaji kanisa. Nyenzo hii inafaa na ina manufaa makubwa katika ngazi zote za wafanya kazi wa kanisa na viongozi wa kanisa ambao wanaweza kuunga mkono juhudi za wapanda kanisa moja kwa moja au kwa namna nyingine wanapokuwa wanajitahidi kutimiza huduma aliyowaitia Bwana.

## MTAZAMO WA TARATIBU

Mwomngozo huu ni moja ya miongozo mitano, ambayo kila mmoja una wastani wa masomo 26 ya saa moja. Ili kukamilisha malengo yaliyoelezewa hapo juu, kozi yote inatosheleza mapana mbalimbali ya masomo ambayo ni muhimu kwa kazi ya upandaji kanisa. Haya ni pamoja na maono ya KUM, huduma ya kikundi kiini, ufuasishaji, kanisa, uinjilisti, mafunzo ya Biblia kwa kufata neno, uongozi, maombi, tabia ya kiroho na mengine mengi.

Taratibu ziligawanywa katika miongozo mitano ili kutoa njia inayozidi kupanuka kwenye kozi ya mafunzo. Wakati kila mshiriki anapomaliza mwongozo, anatumia mda kabla ya mwongozo unaofuata akiziweka katika matendo kanuni alizojifunza. Kwa hiyo vipindi vingi vya baadaye vinajengwa juu ya kanuni na ujuzi uliojifunzwa na kufanyiwa mazoezi katika masomo ya mwanzoni.

Kwa maneno mengine, taratibu zimeandaliwa kujifunzwa na kutumiwa sambamba na upandaji halisi wa makanisa. Washiriki wanapofanya kazi kwa juhudi kwa ajili ya kuanzisha kanisa jipya, watahitaji kiwango fulani cha ujuzi na ufahamu, na watakutana na matatizo mbalimbali wanapoendelea. Ujuzi na ufahamu unaohitajika mwanzoni mwa upandji kanisa unatolewa katika mwongozo wa kwanza, wakati shughuli na kanuni zinazohitajika baadaye katika upandaji kanisa zinatolewa katika miongozo ya mbeleni. Kila mwongozo umeandaliwa kutoa ujuzi, kujibu maswali, na kujadili matatizo nyeti ambayao yanahusiana na hatua sambamba ya upandaji kanisa ambapo washiriki wanafanya kwa juhudi. Baada ya dibaji hii utaona orodha ya shughuli muhimu za maendeleo au "mapito**"** ambayo wafunzwa wameandaliwa na kutarajiwa kuutumia wakati wa mafunzo ya semina.

Masomo yamegawanywa kwa mada, na kila moja ya miongozo mitano ina masomo kutoka baadhi ya mada. Baadhi ya visa, kama vile "maono" na "kanisa" yote yamo katika miongozo yote mitano. Mengine, kama vile "kufuasa" kunatokea baadaye kwenye kozi, wakati mshiriki anapokuwa kwenye

hatua katika huduma yake ambapo visa hivi ni muhimu. Mtazamo wa kozi yote ulio na orodha ya mada ya somo kwa kila moja ya miongozo mitano imehusishwa baadaye katika hatua hii.

**UTUMIAJI WA NYENZO**

**Ushauri Kwa Washiriki**

Mda wa kutosha, maombi na juhudi yamewezesha utayarishaji wa miongozo yote hii mitano katika kozi yote. Kila mwongozo umeandaliwa kugusia ujuzi maalumu wa huduma na ufahamu unaohitajika wakati wa utaratibu wa kuanzisha kanisa jipya. Kwa hiyo inashauriwa kabisa kwamba unaanza na mwongozo wa kwanza, siyo mwongozo mmojawapo wa baadaye. Kwa heshima hiyohiyo, kila somo limechaguliwa kwa uangalifu na kufanyiwa ufundi ili lifae, kutumika na la lazima katika kazi ya upandaji kanisa. Ni kwa manufaa yako pia kutovuka somo.

Tambua kuwa kusoma halisi kunatokea unapoyatumia mawazo yaliyotolewa katika masaomo haya katika maisha yako binafsi na katika huduma yako. Masomo mengi yana utekelezaji wa azimio mwishoni. Utekelezaji huu wa azimio umeandaliwa kukusaidia wewe kutumia mawazo katika somo na unatakiwa umalizike kabla hujaanza kufanyia kazi mwongozo unaofata. Inaweza kuwa msaada wa hali ya juu kuwa na mshauri wa kukutia moyo na kukushauri unapofanya mwenyewe upandaji kanisa. Mshauri pia anaweza kusaidia hitaji lako la uwajibikaji unapokuwa unayatumia mawzo yaliyojifunzwa katika maisha yako na huduma. Kuwa na mtu anayekuwa nawe bega kwa bega siyo tu maandalizi ua ufanisi, lakini wapanda kanisa wengi wanashuhudia msaada ambao hili linatoa katika maisha yao na katika huduma yao. Kwa hiyo, tunakutia moyo kabisa kwa maombi kutafuta aina fulani ya ushauri kuwezesha na kudumisha huduma yako ya upandaji kanisa.

**Ushauri kwa Wakufunzi**

Nyenzo hii inaweza kutumika kwa aina mbalimbali ya maandalizi kama vile shule ya Biblia, semimari au semina ya kikanisa. Kwa jinsi hiyo hii siyo tu kama nyenzo ya kuanzia ya kuelimishia. Ni nyenzo ya kufundishia. Elimu inayokazia katika ufahamu na habari.Kusudi la nyenzo siyo tu kukuwezesha kupata ujuzi, lakini pia ni kuchochea kuelekea kufikia kuweka huduma inayofanana na ya kibiblia. Mwongozo huu ni kwa ajili ya ‘watendaji’.

Ingawa njia unayochagua kufundishia masomo kwa kila mwongozo itategemeana na mandhali yako, kila mwongozo unaweza kufundishwa katika semina ya wiki nzima. Kutokana na maelekezo haya, vituo mbalimbali vya mafunzo vimefanikiwa kwa kutumia mpangilio tofauti unaoendana na mtiririko wa maisha na huduma zilizopo. Wakati mwingine wamechagua siku mbili mfululizo za mapumziko ama vipindi vya kila wiki. Inashauriwa kwamba utekelezaji wa azimio mwishoni mwa kila somo usisitizwe ili kwamba uwe umemalizika kabula ya semina nyingine. Kipindi cha kati ya miezi minne hadi sita ni kipindi kinachofaa kujatarajia kati ya semina na semina. Faida ya njia hii ya ufundishaji ni kwamba inaunganisha kanunu ulizojifunza kwenye semina na ushiriki kwenye semina.

Wakati wa semina siyo lazima kufundisha kila kiini kilichopo kwenye mwongozo kwa sababu washiriki wanaweza kusoma nyenzo wenyewe. Wakati mwingine kufanya wafunzwa kusoma soma na kujadiliana jinsi linavyogusa uzoefu wao ni njia nzuri. Na wakati mwingine, maelezo kutoka kwa mtu ambaye ana uzoefu wa somo lililomalizika inaweza kuwa njia nzuri ya kujenge mawazo. LAKINI USIKALIE NJIA YA MAELEZO. Uwe mbunifu wakati ukijaribu njia mablimbali kujenga kanuni na ujuzi uliomo kwenye masomo. Wakufunzi wengine wamepata mchanganyiko kama vile kujadiliana kwenye makundi, karakana, na inaonekana kufanya kazi na kuwafurahisha.

Umetengwa kwa kutumainiwa, Mungu wa makanisa anahitaji mataifa yafuasishwe, na viongozi wanahitajika.

Una uwezo wa ajabu kusaidia kuandaa wengi watakaoendeleza harakati za upandaji kanisa na kuwezesha wengine katika huduma za kuzaliana kwa kanisa

**Msaada Zaidi**

Usisite kuwasiliana nasi kama tunaweza kuwa msaada zaidi kwako katika kueneza maono ya kueneza upandaji kanisa au kwa vitendo kuandaa wapanda kanisa.

Jay Weaver, General Editor
Budapest, Hungary, January 2000
JayWeaver@compuserve.com

# KUHUSU MUUNGANO

Taratibu hii imetayarishwa na *Muungano wa Kueneza Upandaji Kanisa* wakishirikiana na huduma ya Peter Deyneka wa Urusi, mradi 250. *Muungano* ni ushirikiano wa makanisa na mawakala wa umishenari waliojitoa kuwahamasisha waumini kuenea katka kila nchi zilizopo kati na mashariki ya Ulaya na ushirika wa makanisa ya kiinjili ya Urusi ya zamani. Kueneza upandaji kanisa ni mbinu ambayo inakusudia kuanzisha makanisa katika kila mji, vijiji, na maeneo unayopakana nayo ili kwamba kila atakayemwamini Yesu apate kuwa na kanisa jirani atakaloweza kushiriki na kukua ndani ya Yesu na kujengwa au kuandaliwa kwa huduma. *Muungano* umejengwa juu ya msingi ambao kuunganisha nguvu kutaongeza ufanisi, kupunguza marudio na kuonyesha umoja kati kati ya mwili wa Kristo.

**TUNACHOAMINI**

- Kanisa la mtaa ni zana ya msingi ya Mungu anayoitumia kueneza injili na ufuasishaji
- Ushirikiano na makanisa pamoja na mashirika ya kimishenari ni madhubuti kwa ongezeko la makanisa ya mtaa na maendeleo ya harakati za kueneza upandaji kanisa.
- Kuelimisha viongozi ni mhimu kwa upandaji kanisa na ukuuaji wa kanisa.
- Maagano ya Lausanne ni maelezo ya imani ya Muungano (Alliance)

**TUNACHOFANYA**

**Kuelimisha na Kushauri Wapanda Kanisa**

*Muungano* unatoa ujuzi unaotokana na mafundisho katika mtindo wa semina pamoja na mazoezi ya huduma yanayolenga kwenye kuanzisha makanisa yanayozaliana.

**Ukusanyaji Bayana wa Taarifa.**

Taarifa makini zinapelekea uamuzi mzuri katika kazi za upandaji kanisa. *Muungano* unaweza kuhusika katika kufundisha na kushauri katika hitaji la kukusanya taarifa zinazohitajika katika eneo la upandaji kanisa na kukua kwa kanisa.

**Harakati za Kuhusisha Maombi**

Harakati za upandaji kanisa zinaanza na maono, ambayo yanagunduliwa na kuandaliwa kwa kutafuta moyo wa Mungu kwa maombi. *Muungano* unaweza kukusaidia kuelewa zaidi nafasi ya harakati za maombi katika kazi ya upandaji kanisa, na namna unavyoweza kuwezesha harakati za maombi katika eneo au sehemu yako.


**Utupaji Maono**

Ni kitu gani Mungu anataka kwa nchi yako? Anataka makanisa kila mahali! *Muungano* unaweza kusaidia kuendeleza maono ya makanisa mapya kwa zana ya semina katika kanuni ya kuendeleza upandaji kanisa.

**KWA TAARIFA ZAIDI WASILIANA NA:**

*The Alliance For Saturation Church Planning* (*Muungano wa Kueneza Upandaji wa Kanis*a)
Regional Resource Team
H-1111 Budapest
Budafoki ut 34/B III/2, Hungary
Tel: + (36-1) 466-5978 or 385-8199
Fax: (36-1) 365-4606
E-mail: KUMAAlliance@compuserve.com

# MZUNGUKO WA KUPANDA KANISA




Kupanda kanisa siyo mfuatano wa matukio na shughulu zilizounganishwa bila utaratibu; Ni utaratibu wenye msukumo wa lengo. Utaratibu huu unahitaji ulinganifu wa shughuli, mchanganyiko wa ujuzi, falsafa ya kawaida na ujasili katika uongozi. Maendeleo katika maeneo haya nyeti ndilo lengo la kufundisha wapanda kanisa. "mzunguko wa kupanda kanisa" ni mchoro wa utaratibu wa kupanda kanisa ambao kwa macho unaonyesha, kutoka katika wazo fulani la mtazamo, mwingiliano wa kanuni za ufunguo na kufanya mazoezi ya kazi katika utaratibu huo. Hii inawakilisha 'ramani ya barabara' kwa mpanda kanisa, kuruhusu watu kuonyesha ni wapi wametoka na wapi wanaelekea.

# MITAALA

### Ya Utaratibu wa Upandaji Kanisa kwa Kozi ya Omega

**Mitaala** (vianzio) ni msingi mugumu wa shughuli za huduma ambazo zimeshirikishwa katika utaratibu huu. Kila mtaala unaweza kufikiriwa kama jiwe la kuvukia la mtu binafsi katikati ya utaratibu mkubwa wa kuanzisha kusanyiko jipya. Mitaala inatoa hatua ya utekelezaji imara ambao unaweza kusaidia wafunzwa kuweza kwa vitendo kutumia mawazo yaliyomo kwenye Kozi ya Omega. Zote ni mawe ya mbali ambato yanaonyesha maendeleo, vile vile ubao wa alama ambao unasaidia kutoa mwelekeo zaidi. Zifuatazo ni orodha za mitaala na msisitizo katika Kozi ya Omega

| | |
|---|---|
| **MWONGOZO WA KWANZA:** | **Msisitizo juu ya Maono ya KUM, Kusudi la Kanisa, Kujifunza Biblia kwa Kufata Neno na Utafiti** |

**Vitu Maalumu vya Kutekeleza**

- Kuchunguza kusudi la Kanisa katika mwanga wa Utume Mkuu
- Kuanzisha mkakati wa jumla wa huduma ukizingatia maono ya “Z-kufikiri”
- Kuchunguza “mfumo na kazi” katika Kanisa la kwanza na Kanisa la sasa
- Kujifunza na kufanya majaribio ya Kujifunza Biblia kwa kufata neno
- Kuandika na kushirikisha ushuhuda binafsi
- Kuanzisha vikundi vya kusaidia maombi kwenye uinjilisti na upandaji kanisa
- Kukamilisha mradi wenye mambo mengi wa utafiti katika eneo linalolengwa

| | |
|---|---|
| **MWONGOZO WA PIL:** | **Msisitizo Juu ya Uinjilisti na Vikundi Kiini** |

**Vitu Maalumu vya Kutekeleza**

- Kushirikishana yaliyopatikana katika mradi wa utafiti na wengine katika eneo linalolengwa
- Kuandika maelezo ya kusudi la kanisa
- Kuanzisha falsafa ya huduma ya upandaji kanisa
- Kuanzisha mkakati wa binafsi wa uinjilisti, ikiwemo uinjilisti wa mmoja kwa mmoja
- Kuanzisha vikundi kiini kwa msisitiza juu ya uinjilisti
- Kutumia njia ya kujifunza neno kwa kulifuata binafisi na kwenye vikundi kiini

| | |
|---|---|
| **MWONGOZO WA TATU:** | **Msisitizo juu ya Ufuasishaji, Vita Vya kiroho, Vikundi na Kufanya Kazi Kwa Timu** |

**Vitu Maalumu vya Kutekeleza**

- Kuwatambua na kuwaelimisha viongozi nyeti wa vikundi kiini
- Kutumia muda katika maombi na kufunga
- Kutathimini mtazamo wa dunia wa wapanda kanisa ukilinganishwa na mtazamo wa dunia kibiblia
- Kutumia ukweli wa maandiko kupinga vipingamizi vya kiroho katika maisha na katika huduma ya wapanda kanisa
- Kuunda mpango binafsi wa kufanya ufuasishaji kwa watu wanaojihusisha katka huduma ya upandaji kanisa
- Kufanya maendeleo ya timu na shughuli za kutathimini
- Kuchanganua vipawa vya kiroho vya wapanda kanisa na vya timu ya upandaji kanisa

| MONGOZO WA NNE: | Msisitizo Juu ya Uongozi na Uwakili Mwema |
|---|---|

**Vitu Maalumuu vya Kutekeleza**

- Kutathimini uwezo na udhaifu wa mtindo wa uongozi wa huduma ya mpanda kanisa, kwa msisitizo juu ya njia za mwingiliano wa mtu binafisi na wengine
- Kushirikisha kanuni za kiongozi mtumishi kwenye maisha na huduma ya mpanda kanisa
- Kufuatilia matumizi ya muda katika maisha na huduma ya mpanda kanisa, kuweka vipao mbele, na kutengeneza ratiba
- Kutathimini utoaji fedha wa mpanda kanisa, vilevile na wa kanisa lenyewe lililopandwa
- Kutazama kwa upya nafasi ya mke na mme kibiblia na wajibu ambao wapanda kanisa wanao kwenye famila zao
- Kuongoza vikundi kiini vilivyopo katika utaratibu wa kuongezeka mara dufu
- Kuandaa mpango wenye mkakati utakaoelekeza kwenye huduma ya kueneza upandaji kanisa

| MWONGOZO WA TANO: | Msisitizo Juu ya Kuongezeka Mara Dufu, Kuhamasisha Wengine, na Kuchochea Harakati za KUM |
|---|---|

**Vitu Maalumu vya Kutekeleza**

- Kuanzisha Ushirikiano wa huduma na vikundi vingine vya kiinjili katika eneo linalolengwa
- Kupanga na kuweka muundo wa usimamizi kwa vikundi kiini ambao utachochea kukua kunakoendelea na kuongezeka mara dufu
- Kuwafundisha watu kuomba kwa ajili ya Ongezeko la upandaji kanisa; kuhamasisha maombi katika mji, mkoa na hata katika ngazi ya Taifa
- Kuanzisha na kuweka mpango kwa mkufundisha na kushauri wapanda kanisa wapya
- Kuwezesha na kutoa viongozi wapya kwa ajili ya huduma ya upandaji kanisa
- Kuchochea maono katika makanisa mapya kwa wamisionari kujihusisha siyo tu katka eneo lao wanalolenga, bali pia mpaka “miisho ya dunia”

# Kimsingi Inagusia **Awamu ya MISINGI** ya Mzunguko wa Upandaji Kanisa

## MTAZAMO WA MWONGOZO WA KWANZA

| Maono ya KUM (MO) | Kanisa (KA) | Tabia ya Kiroho (TK) | Maombi (MB) | Njia za Kujifunza Biblia (NKB) | Uinjilisti (UI) |
|---|---|---|---|---|---|
| **Somo la 1:**<br>**"**Z" Kufikiri<br><br>**Somo la 2:**<br>Utume Mkuu na Upandji Kanisa<br><br>**Somo la 3(3A):**<br>Mzunguko wa Upandaji Kanisa 3A: *Vielezo vya Upandaji Kanisa*<br><br>**Somo la 4 (4A, 4B)**<br>Kanuni za Utafiti 4A: *Kulifahamu Eneo unalolenga*<br>*4B: Mifano ya Maswali ya Utafiti* | **Somo la 1:**<br>Misingi ya Kibiblia kwa Ajili ya Kanisa<br><br>**Somo la 2 (2A):**<br>Kusudi la Kanisa<br>2A: *Karatasi ya Mazoezi Kwa Utume Mkuu*<br><br>**Somo la 3 (3A):**Mfumo na Kazi<br>3A: *Mfumo na Kazi Iliyotumika*<br><br>**Somo la 4:** Kutafsiri Maana ya Kanisa la Mtaa | **Somo la 1 (1A)**<br>Kuhesabiwa Haki Kwa Imani<br><br>**Somo la 2:** Kuishi Kufuatana na Injili<br><br>**Somo la 3:**<br>Ukuaji wa Mkristo<br><br>**Somo la 4:**<br>Nguvu ya Injili Inayobadilisha<br><br>**Somo la 5:**<br>Kutunza Kumbukumbu za Maisha ya Kiroho | **Somo la 1, 2:**<br>Kongamano la Maombi: Kuombea Uamsho<br><br>**Somo la 3 (3A):**<br>Jinsi ya Kuwezesha Maombi<br>3A: *Maombi ya Utatu* | **Somo la 1 (1A):**<br>Utangulizi wa Njia za Kujifunza Biblia Kwa Kufata Neno<br>1A: *Jinsi Tulivyopata Biblia*<br><br>**Somo la 2 (2A):**<br>Kulichunguza Neno la Mungu<br>2A: *Lugha ya Biblia*<br><br>**Somo la 3:**<br>Warsha ya Uchunguzi<br><br>**Somo la 4 (4A):**<br>Kufafanua Neno la Mungu<br>4A: *Majedwali ya Biblia*<br><br>**Somo la 5:**<br>Warsha ya Ufafanuzi<br><br>**Somo la 6:**<br>Kulitumia Neno la Mungu<br><br>**Somo la 7 (7A):**<br>Warsha ya Kulitumia Neno la Mungu<br>7A Waefeso-an 1.B.S. | **Somo la 1:**<br>Utangulizi Juu ya Uinjilisti<br><br>**Somo la 2,3:** Kutayarisha Ushuhuda Binafsi |
| **4** | **4** | **5** | **3** | **7** | **3** |

Namba katika mabano (26) zina maanisha mwishoni

# Kimsingi Inagusia **Awamu ya KULETA** ya Mzunguko wa Upandaji Kanisa

## MTAZAMO WA MWONGOZO WA PILI

| Maono ya KUM (MO) | Kanisa (KA) | Tabia ya Kiroho (TK) | Maombi (MB) | Uongozi (UO) | Vikundi Kiini (VK) | Njia za Kujifunza Biblia (NKB) | Uinjilisti (UI) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Somo la 5:**<br>Misingi ya Kibiblia ya Kueneza Upandaji Kanisa<br><br>**Somo la 6:**<br>Warsha ya Utafiti<br><br>**Somo la 7:**<br>Kuhamasisha Rasilimali Kupitia Utafiti | **Somo la 5:**<br>Asili ya Kanisa<br><br>**Somo la 6 (6A):**<br>Kazi za Umoja za kanisa<br>*6A: Ubatizo Katika Agano Jpya*<br><br>**Somo la 7:**<br>Kuandaa Maelezo ya Kusudi la Kanisa<br><br>**Somo la 8 (8A):**<br>Falsafa ya Huduma ya Upandji Kanisa<br>*8A: Kuanzisha Falsafa ya Huduma ya Upandaji Kanisa* | **Somo la 6:**<br>Kuishi Kama Wana Badala ya Mayatima<br><br>**Somo la 7 (7A):**<br>Kujifunza Kuwa Wana<br>*7A*: *Yatima Dhidi ya Wana* | **Somo la 4:**<br>Kongamano la Maombi: Kuabudu na Kuritafakari neno | **Somo la 1 (1A):**<br>Misingi ya Kibiblia ya Uongozi *1A: Mchanganuo wa Uongozi*<br><br>**Somo la 2 (2A):** Sura ya kiongozi<br>*2A*: *Hadhi ya Kiongozi* | **Somo la 1:**<br>Kazi na Faida za Vikundi Kiini<br><br>**Somo la 2 (2A, B):**<br>Kanuni za Uongozi wa vikundi Kiini<br>*2A: Vikundi Kiini Vivunja Barafu*<br><br>2B: *Mifano ya Shughuli*<br><br>**Somo la 3 (3A):**<br>Kuanzisha Vikundi Kiini<br>3A: *Karatasi ya Upangaji*<br><br>**Somo la 4 (4A):**<br>Uinjilisti wa Vikundi Kiini<br>4A: *Kuhusu "Oikos"*<br>**Somo la 5:**<br>Kuonyesha Mfano wa Kikundi Kiini<br><br>**Somo la 6**:<br>Falsafa ya Huduma ya Vkundi Kiini | **Somo la 8 (8A):**<br>Njia Tofauti Tofauti za Kutumia Njia ya Kujifunza Biblia Kwa Kulifata Neno<br><br>**Somo la 9 (9A,9B)**<br>Kuongoza Mafunzo ya Biblia Kwa Kulifuata Neno<br>9A: Mafunzo ya Mathayo 20:17-28<br>9B: Kujifunza Juu ya LK 15:1-7<br><br>**Somo la 10, 11 (10A):**<br>Warsha ya Kuongoza Mafunzo ya Biblia Kwa Kufata Neno<br>*10A: Vfungu Kwa Ajili ya IBS* | **Somo la 4 (4A):**<br>Uinjilisti na Upandaji wa Kanisa<br>*4A:Kutathimini Mikakati ya Uinjilisti*<br>**Somo la 5 (5A.5B):**<br>Vizuizi dhidi ya Mafanikio ya Injili<br>*5A: "Kanisa kwa Watu Wote"*<br>*5B: Kujibu Juu ya Kupinga kwa Kawaida*<br>**Somo la 6;7 (6A,6B,6C)**<br>Utaratibu wa kukata Shauri<br>*6A: Sura ya Mtu katika Kuinjilisha*<br>*6B:Kanuni Tatu*<br>*6C: Kuchunguza Njia Aliyotumia Yesu* |
| **3** | **4** | **2** | **1** | **2** | **6** | **4** | **4** |

Namba katika mabano (27) zina maanisha mwishoni

# Kimsingi inagusia **Awamu ya UANZILISHI** ya Mzunguko wa Upandaji Kanisa

## MTAZAMO WA MEONGOZO WA TATU

| Maono ya KUM (MO) | Kanisa (KA) | Tabia ya Kiroho (TK) | Maombi (MB) | Uongozi (UO) | Vikundi Kiini (VK) | Uinjilisti (UI) | Kufuasa (KS) | Vita Vya Kiroho (VK) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Somo la 8:** Kusonga Mbele kwa Kwanza<br><br>**Somo la 9:** Asili ya Harakati za Upandaji kanisa | **Somo la 9,10:** Kanisa na Vipawa Vya Kiroho<br><br>**Somo la 11:** Nguvu Za Kijamii za Kanisani | **Somo la 8,9:** Sheria na Injili<br><br>**Somo la 10 (10A):** Toba Kama Njia ya Maisha<br>*10A: Sehemu ya Wenye Dhambi* | **Somo la 5:** Maombi na Kufunga<br><br>**Somo la 6,7:** Kongamano la Maombi: Kuombea Kuenea kwa injli | **Somo la 3:** Mzunguko wa Uongozi<br><br>**Somo la 4:** Utangulizi kwa Kazi ya Timu<br><br>**Somo la 5:** Maendeleo ya Timu | **Somo la 7 (7A)** Nguvu ya Majadiliano ya Vikundi Kiini<br><br>**Somo la 8:** Kutunza Watu Walio Kwenye Vikundi Kiini<br><br>**Somo la 9:** Kufundisha Viongozi Wapya wa Vikundi Kiini | **Somo la 8:** Injili ya Mahusiano | **Somo la 1:** Utangulizi katika kufuasa<br>**Somo la 2 (2A):** Jukumu lako Katika Kufanya Wanafunzi<br>*2A:Tabia ya Upendo wa Kikiristo*<br><br>**Somo la 3 (3A):** Fahamu Lengo Lako, Fahamu Watu Wako<br>*3A:Imani, Tumaini na Upendo*<br><br>**Somo la 4 (4A)**:Kuwasaidia Wanafunzi Kukua Kiroho<br>*4A:Kukua Kiroho Kunahitaji Tathimini*<br><br>**Somo la 5(5A):** Mifumo ya Kufuasa<br>*5A: Kufanya Mpango wa Kufuasa* | **Somo la 1:** Kuelewa Mtazamo wa Kidunia<br><br>**Somo la 2:** Nguvu za Vita vya Kiroho<br>*2A: Mafunzo ya Waefeso 4:17-5:21*<br><br>**Somo la 3: (3A,3B):** Mashambulizi ya Kiroho<br>*3A: Kujifunza Biblia*<br>*3B: Mchanganuo Kutoka Ulimwenguni Kote* |
| **2** | **3** | **3** | **3** | **3** | **3** | **1** | **5** | **3** |

Namba katika mabano (26) zina maanisha mwishoni

# Kimsingi Inagusia **Awamu ya KUFUNDISHA** ya Mzunguko wa Upandaji Kanisa

## MTZAMO WA MWNGOZO WA 4

| Maono ya KUM (MO) | Kanisa (KA) | Tabia ya Kiroho (TK) | Maombi (MB) | Uongozi (UO) | Vikundi Kiini (VK) | Kufuasa (KS) | Uwakili Mwema (UM) | Familia (FA) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Somo la 10 (10A, 10B):** Vipengele vya Mkakati kwa Harakati za Upandaji Kanisa *10A: Imani na Utii dhidi ya Hofu na Kutokuamini* *10B: Vitu Vinavyoamsha Ukuaji wa Asili*<br><br>**Somo la 11:** Dalili za Harakati<br><br>**Somo la 12:** Uangalizi Kati Kati ya Harakati | **Somo la 12:** Nguvu ya Makanisa yanayoibuka<br><br>**Somo la 13:** Tabia ya Makanisa Yanayokua<br><br>**Somo la 14:** Serikali ya Kanisa na Ofisi za Kanisa: | **Somo la 11:** **U**pendo Kama Msingi kwa Huduma<br><br>**Somo la 12:** **K**uuelewa Moyo wa Baba<br><br>**Somo la 13:** Neema ni Kwa Wanyenyekevu | **Somo la 8, 9:** Kongamano la Maombi Kuomba Kibiblia | **Somo la 6 (6A):** Uongozi wa Kitumishi *6A: Orodha ya Viongozi*<br><br>**Somo la 7:** Nguvu za Uongozi<br>**Somo la 8:** Mitindo ya Mwingiliano<br><br>**Somo la 9:** Mahitaji ya Uongozi<br><br>**Somo la 10 (10A):** Kufunza Viongozi Wapya *10A:Hadhi za Kutia katika Uongozi Mpya* | **Somo la 10:** Majadi-liano ya Maswali na Matatizo ya Vikundi Kiini<br><br>**Somo la 11:** Kuzidisha Kwa Kikundi Kiini | **Somo la 1:** Warsha ya Kufuasa | **Somo la 6:** Utangulizi juu ya Uwakili Mwema<br><br>**Somola 2:** Uwakili mwema Kwenye Fedha<br><br>**Somo la 3:** Matumizi ya Muda<br><br>**Somo la 4:** Utaratibu wa Upangaji Kimikakati<br><br>**Somo la 5:** Warsha juu ya Utaratibu wa Upangaji Kimikakati | **Somo la 1:** Majukumu ya Kibiblia Katika Familia<br><br>**Somo la 2:** Kulea |
| **3** | **3** | **3** | **2** | **5** | **2** | **1** | | |

Namba katika mabano (25) zina maanisha mwishoni

# Kimsingi Inagusia **Awamu ya KUZIDISHA NA HARAKATI** Katika Mzunguko wa Upandaji Kanisa

## MTAZAMO WA MWONGOZO WA TANO

| Maono ya KUM (MO) | Kanisa (KA) | Tabia ya Kiroho (TK) | Maombi (MB) | Uongozi (UO) | Vikundi Kiini (VK) | Kuhubiri (KR) | Familia (FA) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Somo la 13:** Maono na Kupiga Darubini<br><br>**Somo la 14:** Kuhamasisha<br><br>**Somo la 15:** Hatua Inayofuata<br><br>**Somo la 16:** Mafunzo Kama Sehemu ya Harakati za Upandaji Kanisa<br><br>**Somo la 17:** Kuhamasisha Viongozi Kupitia Uanzilishi wa Kitaifa | **Somo la 15:** Malezi ya Kanisa<br><br>**Somo la 16:** Ibada ya Umoja katika Kanisa la Mtaa<br><br>**Somo la 17:** Jinsi ya Kuongoza Ibada ya Pamoja Katika Kanisa la Mtaa<br><br>**Somo la 18:** Kanisa la Mtaa na Mwili Mkubwa wa Kristo<br><br>**Somo la 19:** Mguso wa Kihistoria wa Kanisa __<br>(Historia ya Kanisa Katika Mandhali ya Nchi) | **Somo la 15:** Huduma ya Upatanishi<br><br>**Somo la 16:** Unyoofu wa Maadili Kwa Wapanda Kanisa | **Somo la 10:** Maombi ya Kuwezesha kwa Harakati za Upandaji Kanisa<br><br>**Somo la 11,12:** Kongamano la Maombi: Kumshukuru Mungu Kwa Ajili ya Uaminifu wake | **Somo la 11:** Kutoa Viongozi<br><br>**Somo la 12:** Uongozi wa Harakati<br>*12A: Viongozi wa Harakati* | **Somo la 12:** Viini Vinavyoenea Kupitia Makanisa ya Mtaa<br><br>**Somo la 13 (13A):** Kusimamia vikundi Kiini<br>*12A: Hatua ya Mwisho* | **Somo la 1:** Mahubiri ya Kibiblia 1: Kuelewa Ujumbe<br><br>**Somo la 2:** Mahubiri ya kibiblia 11: Kuelewa Wasikilizaji<br><br>**Somo la 3:** Mahubiri ya kibiblia 111: Kujielewa Mwenyewe | **Somo la 3:** Huduma Kwa Famila |
| **5** | **5** | **5** | **3** | **2** | **2** | **3** | **1** |

Namba katika mabano (23) zina maanisha mwishoni

**JUMLA YA MASAA YA KOZI YOTE: 127**

# MAONO YA KUM

MAONO YA KUM

SOMO LA 5

# Misingi ya Kibiblia ya Kueneza Upandaji kanisa

## KUIJAZA DUNIA KWA MWANGA WA UTUKUFU WA MUNGU

☞ **Kusudi la Somo**

Kusudi la somo hili ni kuonyesha kwamba kueneza upandaji kanisa ni wazo la kibiblia na ni njia ambayo Mungu anayotumia kutimiza kusudi lake.

☞ **Wazo Kuu**

- Kueneza upandaji kanisa ni njia ya kibiblia ya kutimiza Utume Mkuu.
- Kueneza upandaji kanisa ni njia ya kihistoria

☞ **Matokeo Yanayotarajiwa**

Wakati yaliyoma katika somo hili yanapoeleweka, kila mshiriki anatakiwa:

- Kuelewa maana wazi ya "kueneza."
- Kujua kuwa kuneza ni kanuni ya kiblia inayotumika kwa kazi ya Mungu katika historia
- Kushiriki katika kueneza upandaji kanisa kama kanuni ya msingi katika falsafa ya wapanda kanisa ya huduma na mkakati wa upandaji kanisa.

### KUENEZA INAELEZEWA KAMA

Nini maana ya kueneza upandaji kanisa? Kujibu hilo ni lazima tuelezee neno "kueneza."

Neno kueneza ni mfumo wa kivumishi cha tenzi "eneza," ambalo ni neno la kisayansi lenye maana "tendea au jaza na kitu fulani mpaka kwenye hatua ambapo hakuna tena kinachoweza kuingia, kuyeyushwa au kuwekwa" (kamusi ya Webster Merriam. Ukumbusho kwa watafsiri: Tumia tafsiri katika lugha yako.) Picha ni kama ya sponji iliyojaa maji kiasi kwamba haiwezi kuchukua hata tone moja zaidi.

Mungu anatumia kanuni ya "kueneza" au "kutimiza" katika maandiko yote, ikianza na kujaza dunia kwa watu na kufanya wafuasi kwa mataifa yote. Lengo ni kwamba ufahamu wa utukufu wa Bwana utaijaza dunia kama maji yaifunikavyo bahari (Hab 2:14, Isa 11:9).

Kwa kutumia neno "kueneza" kwenye upandaji kanisa, tunawakilisha wazo la kujaza nchi kwa makanisa ili kwamba kila, mwanaume, mwanamke na mtoto wapate nafasi ya kusikia na kuelewa injili, na kupokea au kukataa Yesu Kristo kama mwokozi wao kwa utukufu wa Mungu.

### I. KUENEZA KATIKA AGANO LA KALE

#### A. Kutokea Mwanzoni—kuijaza Nchi (kueneza) ilikuwa ni kisa cha Agano la Kale

Amri ya Mungu ilikuwa kujaza dunia kwa watu (Mwanzo 1:28,9:1, na 9:7). Baada ya mafuriko, taifa lilitawanyika duniani kote (Mwanzo 10:32). Lakini kisha watu "wakakaa Chini" (Mwanzo 11:1-2). Walianza kujenga mji "…ili kwamba tujifanyie jina wenyewe na tusitawanyike usoni mwa dunia" (Mwa 11:4). Kwa hiyo Mungu akachanganya lugha zao "na kuwatawanya ulimwenguni kote" (Mwanzo 11:7,8).

*Kwa majadiliano: Ni nini unafikiri kwamba Mungu alitaka kujaza dunia yote kwa watu?*

#### B. Hatima ya Kusudi la Mungu ni Dunia Yote kuenezwa kwa Ufahamu Wake

Kutoka mwanzo wa maandiko mpaka mwisho, ni wazi kwamba Mungu anahitaji utukufu wake kujaa au kufunika dunia yote—kila taifa na kila sehemu ya kila taifa. Kwa mfano, Mungu alimchagua Ibrahimu na kumbariki ili kwamba awe baraka. Ahadi ya Mungu kwa Ibrahimu

ilikuwa kwamba “watu wote duniani wabarikiwe kupitia kwake” (Mwanzo 12:3). Hii ndiyo inamaanisha “watu walioteuliwa.”

Haja ya Mungu kwamba dunia yote imfahamu imeelezewa katika mistari ifuatayo”

- Dunia yote itajawa na utukufu wa Mungu (Hes 14:21).
- Jina lake tukufu na lihimidiwe milele! Dunia yote na ijae utukufu wake (Zab 72:19).
- Maana dunia itajawa na kumjua Bwana, kama vile maji yanavyoifunika bahari (Isa 11:9).
- Nitakapokusanya mataifa yote na lugha zote; nao watakuja, nao watauona utukufu wangu…kila chenye mwili kitaniabudu (Isa 66:18).

## II. HUDUMA YA YESU

### A. Yesu Alitumia Kueneza Kama Mkakati wa Huduma yake Galilaya

Yesu alikusudia kuieneza Galilaya (Mt 4:23). Alikwenda katika miji yote na vijiji (Mt 9:35). Yesu alituma 72 katika makundi ya wawili kwenye “kila mji na kila sehemu alipokuwa anataka kwenda” (Luk 10:1). Na makundi haya, injili ilitolewa si chini ya miji 36 na vijiji vya Galilaya!

Inafurahisha kwamba, katika kuikusudia Galilaya, matokeo ya huduma yake hayakuweza kuzuilika. “Habari juu yake zilienea mpaka Siria,” na “kusanyiko kubwa” kutoka Dekapoli,Yerusalemu, na Uyahudi ya ng’ambo ya Yordani kuja kumsikia huko Galilaya

(Mt 4:23-25). Ionekanavyo Galilaya ulikuwa mji wa kimikakati kuweza kuuhubiri kwa kuwa matokeo yake yalikuwa mapana sana.

### B. Mfano Wa Yesu wa Ufalme Unaonyesha Kanuni ya Kueneza

Katika Mathayo 13, Yesu anawafundisha wanafunzi wake kuhusu ufalme wa Mungu kwa mfuatano wa mifano. Katika mfano wa kwanza, anaeleza jinsi ufalme utakavyopokelewa na wasikilizaji mbalimbali. Katika mfano unaofata, mfano wa magugu, anaelezea juu ya kazi ya adui anayepanda magugu miongoni mwa mbegu mbaya. Mfano wa mwisho una matumizi sawa: Ni kazi ya Mungu kutenga ukweli kutoka kwenye uongo. Mfano wa tano na wa sita (hazina iliyofichika na lulu) akisisitiza furaha ya wale wanaotafuta “hazina” hiyo. Katikati kuna mifano miwili inayozungumzia kupanuka kwa ufalme wake.

1. *Mfano wa mbegu ya haradali (Mathayo 13:31-32)*

   Katika mfano huu kuna ukuaji mkubwa. Kutoka katika mwanzo mdogo (“ndogo kuliko mbegu zako zote”) ikakua na kuwa kubwa kuliko mimea yote katika bustani. Ujumbe uko wazi: Kutoka katika mwanzo mdogo ufalme wa Mungu ungekua na kuwa “mmea mkubwa.”

2. *Mfano wa hamira (Mathayo 13:33)*

   Katika mfano huu, donge dogo la hamira linaingia kwenye unga uliokandwa. Ujumbe unaonekana sawa na huo wa mbegu ya haradali, lakini kwa nyongeza ya msisitizo katika mabadiliko yanayotokea wakati hamira inapopenya kwenye mkando. Kutoka katika mwanzo mdogo ufalme wa Mungu utaendelea kupenya mpaka utakapojaza dunia (linganisha na Uf 11:15).

   Mwishoni mwa mafundisho haya, Yesu aliwauliza wanafunzi wake, “Mmeyaelewa mambo yote haya?” (Mt 13:51). Jibu la wazi ni hapana, kwa kuwa baada ya ufufuko wake alikaa siku 40 akiwaambia juu ya ufalme wa Mungu (Mdo 1:3).

## III. MISINGI YA KBIBLIA YA KUENEZA UPANDAJI KANISA

Tumeona, hatima ya kusudi la Mungu ni kwa dunia yote kuenezwa na ufahamu wake. Kueneza upandaji kanisa ni kueneza mikoa kwa makanisa katika namna kwamba kila mwanaume, mwanamke na mtoto anapata nafasi ya kukubali au kukataa injili kupitia ushuhuda wa kanisa la mtaa. Je kueneza eneo kwa makanisa ni la hivi karibuni lililofifia au ni la kibiblia lililokuwepo na linaloendelea? Kama ambavyo kanuni zifutazo zitatuonyesha, kueneza upandaji kanisa ni la kibiblia.

**A. Chombo: Kanisa**

Wakati Yesu aliposema, "*nitalijenga kanisa langu na milango ya kuzimu haitaliweza*" (Mt 16:18), Alifanya lengo lake kujulikana la kuimarisha watu kwa ajili yake. Kutoka katika maelezo haya mambo mawili yako wazi. La kwanza, kanisa na kazi ya kulijenga ni vya Kristo na kwa hiyo kwa undani zaidi amehusika katika kuliendeleza. La pili, Kanisa litakuwa mshindi. Mateso, umasikini au hata milango ya kuzimu haiwezi kulizuia kanisa. Ujengaji wa kanisa ni mapenzi ya Mungu na kujenga kanisa ni misheni kubwa ya Yesu duniani leo.

Katika waraka wake mzuri kwa Waefeso juu ya kanisa, Paulo anasema, '*kusudio la (Mungu) ilikuwa kwamba sasa, kwa kupitia kanisa, hekima ya Mungu iliyo ya namna nyingi ijulikane…'* (Efe 4:10). Tena kanisa limeelezewa kama chombo ambacho kwacho injili inaenea.

**B. Amri: Injili Lazima Ihubiriwe Kila Mahali**

Kabla ya kupaa kwake, Yesu aliwambia wanafunzi wake kwamba wangepokea Roho Mtakatifu na kisha kuwa mashahidi mpaka miisho ya dunia, kuanzia Yerusalemu (Matendo 1:8). Inapendeza kwamba Yesu anafungua na kufunga huduma yake kwa kueneza kama kisa. Katika mfano wa mpanzi na wavu (Mt 13),Yesu alimaanisha kwamba kazi ya ufalme inajaa katika ardhi yote na kufikia kila aina ya samaki. Katika kumalizia huduma yake, Yesu anawaelekeza mitume wake kueneza dunia kwa habari njema

Injili lazima ihubiriwe kila mahali. Hii ni wazo kutoka kwenye kifungu cha Utume Mkuu (Mt 28:18-20, Luk 24:46-49, Mdo 1:8). Kama vile Ibrahimu alivyobarikiwa ili kwamba awe baraka kwa wengine (Mwa 12:1-3), ili kwamba watu wa Mungu waliopokea baraka za Mungu wanatakiwa wazipeleke kwa wengine.

Utume Mkuu ni "kufanya wafuasi katika mataifa yote" kwa kuwabatiza na kuwafundisha utii kwa Kristo. Malengo yote haya yanakamilishwa zaidi na watu wa Mungu, kanisa. Amri haikuwa amri ya mda kwa watu wa kwanza kuisikia. Kujirudia kwa neno "Yote" Mamlaka yote, mataifa yote, vitu vyote (niliyokuamru) na siku zote, inaonyesha matumizi ya kufika kwake mbali. Kukamilisha Utume Mkuu kunapelekea katika kuneneza kwa kuwa wakata shauri wanafanywa katika mataifa yote.'

**C. Kusonga Mbele: Mpaka Miisho ya Dunia**

Ni jinsi gani mitume, hao waliosikia mara ya kwanza juu ya Utume Mkuu, walikwenda kuutimiza? Jibu ni rahisi. Kama ilivyorudiwa kuhesabiwa katika kitabu cha Matendo, mitume walikuwa wanahubiri mara ya kwanza Yerusalemu. Watu walipoitikia injili , walikusanyika katika makundi kwa ajili ya mafundisho, ushirika, kumega mkate na maombi (Matendo 2:42). Makundi haya yaliimarishwa kwa uongozi na kujulikana kama kanisa. Mateso yalipotokea, waumini walitawanyika kutoka Yerusalemu na kila sehemu walipokwenda walihubiri injili na kuanzisha makanisa mapya yaliyowezekana (Matendo 8:1-4).


Kanisa la Antiokia lilimtuma Paulo na Barnabas kama wamishenari kuiendeleza kazi. Kila mahali walipokwenda, walianzisha makanisa. Katika kitabu kizima cha Matendo, kuenea kwa injili na kupanuka kwa makanisa vilikwenda sambamba. Kila mahali injili ilikofika kanisa lilianzishwa.

Katika Matendo 19:9-10, eneo alilokusudia Paulo ilikuwa ni jimbo la Asia ndogo. Alichagua Efeso, mji mashuhuri magharibi mwa mji huo, kama makao makuu yake. Kule alikutana na wafuasi wake, ambao walitawanyika katika mji *"ili kwamba Wayahudi na Mataifa walioishi katika jimbo la Asia wakalisikia neno la Bwana."* Kwa kadiri iwezekanavyo Paulo alieneza ujumbe wa injili Asia yote ndogo. Aliwezaje kufanya hivyo? Kutoka katika sehemi zingine za Agano Jipya, tunajua kwamba makanisa yalianza angalau katika miji mikubwa saba katika eneo (Uf 2,3, Wakolosai 1:2). Nani aliyepanda makanisa haya? Inavyoonekana makanisa haya yalipandwa na wale aliowafundisha Paulo Efeso.

Kanuni tatu za kibiblia zilizoelezewa hapo juu, zinapofikiriwa kwa pamoja, zinapelekea kwenye suluhu kwamba Utume Mkuu utatimizwa kwa kueneza upandaji kanisa (Angalia kielelzo 5.1)

**Kielelezo 5.1 "Msingi wa Kibiblia wa Kueneza Upandaji Kanisa**

**Hab 2:14 "Dunia itajawa na kumjua Bwana Kama maji yanavyoifunika barahari ."**




**Zab 127:1 "Bwana asipoijenga nyumba, wanaoijenga wafanya kazi bure."**

## IV. MAKANISA MANGAPI YAMEENEA?

> Taifa lililofuasishwa ni lile ambalo kila mtu amepata nafasi ya kusikia na kuelewa injili ya Yesu Kristo, ILI KWAMBA waweze kumpokea au kumkataa Yesu kama mwokozi.

Kama kazi yetu ni kueneza makanisa kwenye maeneo yetu , ni makanisa mangapi yanasimamisha kueneza? Njia nyingine ya kuuliza swali ni: Taifa lililofuasishwa linafanana namna gani? Taifa lililofuasishwa ni lile ambalo kila mtu amepata nafasi ya kusikia na kuelewa injili ya Yesu Kristo, ILI KWAMBA waweze kumpokea au kumkataa Yesu kama mwokozi. Kama hilo ndilo lengo, ni makanisa mangapi yanahitajika kulitimiza?

Katika kujibu swali hili, baadhi wanasisistiza jiografia, wakidai kanisa kwa kila ujirani wa kusafiri umbali wa kawaida kwa kila mtu litakuwa ni lengo zuri. Wazo jingine la kuangalia ni kufikiria hali halisi ya jamii na kabila, kupendekeza kwamba makanisa lazima yaanzishwe kwa kila aina ya kundi la watu katika kila eneo. Kanisa la kihindi kwa Wahindi waliotawanyikia Ulaya. kanisa la kundi la kihungari kwa kundi la Wahungari walioko vijijini. Bado wengine wanaweka malengo ya kanisa moja la mtaa kwa kila wakazi 1000. Hii inatokana na maelezo kwamba kanisa la wastani lenye uwezo, waumini wa kikristo wanaoshuhudia wanauwezo wa kugusa maisha ya watu 1000.

*Ni makanisa mangapi yako katika ujirani wako, mji, kata, au nchi? Ni kwa jinsi gani uko karibu na lengo la kueneza upandjia kanisa?*

## V. KUENEZA UPANDAJI KANISA KATIKA HISTORIA

### A. Ireland, katka Karne ya 5

Patrick aliongoza harakati zilizopelekea Ireland kujaa makanisa katika kila kijiji. Alipenya na kubadilisha upotofu wa eneo la kikuhani kwa kuwaongoza viongozi wa kikuhani kwa Kristo vilevile na watu wote kwa ujumla. Alitumia mfumo wa kikuhani uliokuwepo wa viongozi katika kijiji, na kubadirisha mahekalu ya kikuhani na huduma za ibada kwenye ukristo wa kibiblia. Kutoka Ireland, hadithi za makundi ya kimishenari waliokwenda nje na kupanda makanisa miongoni mwa makabila makali ya Ulaya ya Kaskazini.

### B. Hungari katika karne ya 16

Matengenezo yalikuja Hungari katika karne ya 6. Kanisa lililotengenezwa lilianzisha kituo huko Debrecen kilichoitwa Geneva ya pili. Kutoka pale, Kanisa lililotengenezwa lilifanya utaratibu wa kueneza upandaji kanisa kijiographia katika Transylvania, na kujaza vijiji kwa mafundisho ya kibiblia ya makanisa yaliyorekebishwa.

### C. Scotland katika karne ya 16

Harakati zilizoongozwa na John Knox katika Scotland alieneza eneo kwa makanisa yaliyotengenezwa. Harakati hizi zilijulikana kwa ajili ya kuwajibika kwake kwenye maombi ya kuombea. Malkia Mary alisema kuwa aliogopa maombi ya John Knox kuliko majeshi yote ya Uingereza.

### D. Uingereza katika karne ya 18

Uamsho uliongozwa na John Wesley na George Whitefield huko Uingereza haukupelekea tu kueneza upandaji kanisa, lakini mabadiliko ya kijamii ambayo yangechukiza mageuzi kama yale ya Ufaransa. Wesley alikuwa muhubiri mashuhuri na mpangaji wa kimikakati. Ungeweza kusema kuwa alikuwa "Z" Kufikiri aliyeishi kwa kanuni "kwa kila tendo liliashiria mwisho." Wesley alihubiri injili miongoni mwa wenyeji kwenye mikutano ya wazi katika Uingereza yote. Wakati wa kipindi cha miaka 40 kwenye huduma, alisafiri umbali wa km 550 000 kwenye mgongo wa Farasi. Alihubiri mahubiri mara 42,000 na kuandika vitabu 200. Wesley, alifikiria juu ya mwisho, Wesley alikusanya waumini kwenye 'madarasa' ambayo sasa tunaweza kuyaita 'vikundi kiini.' Baadhi ya watu 100,000 walikusanyika katika makundi haya 10,000 ambayo yaliongezeka kila mara walipoongezeka 12 au zaidi (Joel Comiskey, mlipuko wa vindi kiini vya majumbani. 1998).

George Whitefield, kiongozi vile vile wakati wa uamsho huu, alidhaniwa kuwa muhubiri mzuri kuliko Wesley. Kwa jinsi hiyo, Mguso wa Whitefield haukuwa na nguvu kama wa Wesley kwa sababu ya uwezo wa Wesley wa kukusanya waliokata shauri katika makundi. Kuhusu hili Whitefield alisema, "Kaka yangu Wesley alitenda kihekima. Roho ambazo zilikuwa zimeamshwa chini ya huduma yake aliyojiunga nayo katika jamii, na hivyo kutunza tunda la jasho lake. Hili nililikataa, na watu wangu ni kamba ya mchanga" (Miller p97).

Uamsho wa Wesley ulimwagikia Marekani yote na, ukaendeshwa na Jonathani Edwards na Francis Asbury, ulipelekea kueneza upandaji kanisa la mkusanyiko na makanisa ya Methodisti.

### E. Ufilipino na sehemu zinginezo katika karne ya 20

Katika mwaka 1973, mchungaji wa kifilipino aliyeitwa Jun Balayo alipata maono ya kueneza taifa lake kwa makanisa. Aliongoza juhudi za makanisa mbalimbali ambazo bado zina nguvu. Walipanda makanisa mapya 10,000 katika kipindi cha chini ya miaka kumi na tano. Waumini waliweka malengo ya mda mrefu ya makanisa mapya 50,000 ufilipino kufikia mwaka 2003. Leo, wako kwenye kusudio! Haya ni matokeo makubwa ya maombi ya kukusanyika, matukio ya kawaida kuendelea kuendeleza maono ya upandaji kanisa na kufanya kazi kwa juhudi kupanda makanisa.

Harakati zinazofanana zinaendelea kutokea duniani leo. Harakati za nguvu ziko njiani huko Latino Amerika; hasa Brazili, China, Korea, na Africa ya kati (iliyojulikana kama "Bara lenye giza" inasemekana kwamba Africa ya Kati imekuwa, "Bara la Wakristo") lenya harakati za nguvu huko Ghana. Harakati za upandaji kanisa zinaanza kupata nguvu ya kwenda huko Ukreini na Romania pia.

## SULUHU

Kueneza dunia na utukufu wa Mungu imekuwa ni haja yake tangu mwanzo. Upandaji kanisa ulikuwa ni kanuni na msingi wa njia ya kueneza injili katika agano Jipya na kuendelea kuwa hivyo leo. Kwa taifa kuona na kuelewa injili ya neema, inahitaji mtu binafsi kujitoa vya kutosha kushuhudia, kijogorafia na kiutamaduni karibu kwa kila mkaaji wa sehemu hiyo. Hii ina maana kwamba kueneza kwa kila sehemu na kila taifa kwa makanisa mapya hai na yanayozaliana.

Agizo hili halijabadilika. Katika kila taifa, watu wa Mungu wameitwa kuwa nguvu ya kuhusika katika ulimwengu uliopotea. Kuhusika huku kunaweza kuanza kwenye ngazi ya chini, na kisha kuendelea kwenye vituo vya mizunguko kuunganisha tamaduni, mahusiano, rangi ya ngozi na lugha—kanisa linatakiwa kufika nje ya mipaka ya dunia. “Mungu atatubariki na mwisho wa dunia utamwogopa!” (Zab 67:7).

## MASWALI YA KUTAFAKARI, MARUDIO NA MATUMIZI

- Inawezekana kutimiza Utume Mkuu katika eneo maalumu bila upandaji makanisa?
- Kanisa lako linavutwa na kusudi la kuongezeka mara dufu na kueneza?
- Una mpango wa kupanda makanisa miongoni mwa mataifa mengine nchini mwako?
- Ni makanisa mangapi eneo lako linahitaji ili liweze kuenezwa?
- Unaamini kwamba Mungu anataka kuongeza kwenye taifa lako ukurasa katika historia ya kanisa?

## VYANZO

- Comiskey, Joel. *Home Cell Group Explosion*. Houston, TX: Touch Ministries, 1998.
- Miller, Basil, John Wesley. Minneapolis: *Dimension Books*, 1943.

MAONO YA KUM

SOMO LA 6

# Warsha ya Utafiti

## KUTOA MATOKEO YA UTAFITI WA ENEO LINALOLENGWA

☞ **Kusudi la Somo**

Lengo la somo hili ni kuwaruhusu wafunzwa kushirikishana waliyojifunza kwenye utafiti wao.

☞ **Wazo Kuu**

- Kuonyesha taarifa za utafiti katika mtindo ulioandaliwa ambao unazifanya kuelekeweka zaidi.
- Kujibu baadhi ya maswali ya ufunguo yanayoweza kuufanya wa thamani zaidi.

☞ **Matokeo Yanayotarajiwa**

Wakati yaliyomo katika somo hili yanapoeleweka, kila mshiriki anatakiwa:

- Kuelewa jinsi ukusanyaji wa habari ulivyo wa kimikakati kuendeleza uinjilisti wenye mafanikio na mikakati ya upandaji kanisa.
- Kujua jinsi ya kutoa taarifa ya utafiti iliyofupishwa.
- Kushiriki katika kutathimini uhusiano wa njia za ukusanyaji wa habari mbalimbali za kuendeleza injili na mikakati ya upandaji kanisa.

☞ **Ushauri kwa Wakufunzi**

Somo hili ni warsha. Ruhusu kila mfunzwa kutoa aliyopata kwenye agizo la utafiti wao kutoka kwenye Mwongozo wa Kwanza (Maono ya KUM Ziada 4A, “Kuelewa Eneo Lako Unalokusudia”). Kama wana michoro, ramani, vibao vya matangazo, n.k. Viweke mahali vinapoonekana ili viweze kuonwa wakati wa mapumziko na mda wa uhuru.

Kama kuna taarifa nne zaidi zinazotakiwa kutolewa wakati wa saa hiyo, mnaweza kufikiri juu ya kufanya katika vikundi vidogo. Vinginevyo, unaweza kuamua kuchagua taarifa chache nzuri kwa kila mmoja kusikia na kujadili.

### UTANGULIZI

Katika somo la maono ya KUM “Kanuni za Utafiti” katika Mwongozo wa Kwanza , washiriki walipewa agizo kukusanya habari za eneo amabalo watapanda kanisa (Maono ya KUM Ziada 4A, Kuelewa Eneo Lako Unalolenga”). Sasa habari hizo za kutosha iwezekanavyo juu ya nguvu ya mavuno na (rasilimali za kikristo) shamba la mavuno (mahali ambapo kazi itafanyika) zimekusanywa, habari hizi zinahitaji kuchanganuliwa na kuwekwa pamoja katika taarifa inayoelezea taarifa na umuhimu wake kwenye mikakati ya uinjilisti na upandaji kanisa katika eneo linalolengwa. Warsha hii itakupa nafasi ya kufanya hivyo.

### SAEHEMU YA KWANZA—TAARIFA ZA MSINGI ZILIZOKUSANYWA (DAKIKA 5-7):

- Elezea eneo lako linalolengwwa. Weka kwa ufupi uliyojifunza katika hatua ya 1 na ya 2 na ya 3 ya Maono ya KUM Ziada 4A ‘Kufahamu Eneo Lako Unalolenga.”
- Ni jinsi gani umekusanya habari zako za utafiti (kuzulu eneo, mahojiano ya kawaida, uchunguzi, kuweka ramani, utafiti kwenye maktaba, n.k.)?
- Elezea matatizo yoyote mazito na ugumu ulioukuta na jinsi gani uliushinda. Ni nini ungefanya wakati mwingine.

**SEHEMU YA PILI—MUCHANGANUO WA TAARIFA ZA UTAFITI (DAKIKA 5-8):**

Msisitizo wa maonyesho unatakiwa kuwa juu ya matokeo yaliyopatikana. Kwa kujibu maswali ya ufunguo yaliyoorodheshwa hapo chini inaweza kusaidia.

- Ni taarifa ipi uliyojifunza iliyokuvutia juu ya eneo lako unalokusudia na watu wanaoishi mahali pale?
- Kulikuwa na taarifa yoyote iliyokushangaza?
- Ni kitu gani maalumu ulichojifunza ambacho kitakusaidia kuonyesha mkakati wako wa upandaji kanisa katika eneo unalolenga?
- Ni nini kimoja cha kweli muhimu kwenye upandaji kanisa ulichodhihirisha kwamba umeshakifahamu juu ya shamba la mavuno?
- Ni ugunduzi gani mpya ambao ni muhimu kwa upandaji kanisa uliofanya juu ya shamba la mavuno ambao hukuujua mwanzoni?
- Ni nafasi zipi ulizopata kama mlango wazi kwa ajili ya injili?
- Ni vipingamizi gani ulivyopata na jinsi gani vinaweza kudhibitiwa?
- Ni utafiti gani ufuatao unaohitaji kufanya ili kuendeleza uinjilisti na mikakati ya upandaji kanisa katika eneo unalolenga?

MAONO YA KUM

SOMO LA 7

# Kuhamasisha Rasilimali Kupitia Utafiti

☞ **Kusudi la Somo**

Kusudi la somo hili ni kujifunza jinsi ya kutumia utafiti kuhamasisha wengine kujiunga na kazi ya upandaji kanisa.

☞ **Wazo Kuu**

- Kuunda "wito wa Utekelezaji" inawavuta wengine kujiunga na mradi
- Kushirikishana habari ni kwa maana sana kwenye kazi ya kuhamasisha wengine.

☞ **Matokeo Yanayotarajiwa**

Wakati yaliyoma katika somo hili yanapoeleweka, kila mshiriki anatakiwa"

- Kuelewa umuhimu wa kuainisha taarifa za utafiti kwa maombi kama sehemu ya kundeleza mkakati wa upandaji kanisa.
- Kujua jinsi ya kushirikisha taarifa za utafiti katika njia inayofaa kwa kuhamasisha wengine kwa upandaji kanisa.
- Kuanzisha mkakati wa uhamasishaji wa huduma yake ya upadaji kanisa na kujaribu kuhamasisha wengine kuomba, kutoa sadaka, au kuungana naye kwenye huduma yake ya upandaji kanisa.

☞ **Ushauri kwa Wakufunzi**

Katika kufundisha somo hili, jaribu kutoa mifamo maalumu ya wapi kushirikisha utafiti kumepelekea katika kuhamasisha watu, maombi au rasilimali za juhudi za upandaji kanisa. Pia, jaribu kutoa mfano wa taarifa ambazo zimeshirikishwa isivyopasa zilivyopelekea mtokeo mabaya. Wasaidie wafunzwa kuona jinsi ambavyo hili lingekuwa limezuiliwa na nini wanahitaji kujifunza kutokana na makosa yao.

## UTANGULIZI

Katika somo, "Kanuni za Utafiti" (Maono ya KUM 4) katika mwongozo namba moja, washiriki walipewa agizo kukusanya habari kuhusu eneo watakalokuwa wanapanda kanisa (Maono ya KUM Ziada 4A, "Kuelewa Eneo Lako Unalolenga"). Zoezi hilo la utafiti lilikuandaa kukusanya habari na kuzichambua taarifa kufuatana na nguvu ya mavuno (rasilimali ambazo zingeweza kusaidia katika huduma ya upandaji kanisa) na katika shamba la mavuno (watu na eneo unalojaribu kufikia kwa injili). Katika somo, tutajadili jinsi ya kushirikisha utafiti wako watu wengine ili kufanya hitaji la watu katika eneo unalolenga kujulikana…na kuwatia moyo wengine kushiriki katika kazi ya ufalme katika eneo hilo.

## I. WITO WA UTEKELEZAJI

> "Wito wa utekelezaji" inajibu swali la "nini Mungu anataka katika eneo ninalolenga?"

"Wito wa utekelezaji" ni ufupisho wa taarifa ya kile unachoamini au timu yako inachoamini kwamba Mungu anataka kufanya katika kufikia eneo lako unalolenga kwa injili. Ni matokeo ya kuomba na kusali juu ya habari ulizokusanya na kuainisha katika zoezi lako la kufanya utafiti. "Wito wa kutenda" unagusia hitaji na hali ya kiroho ya watu katika eneo unalolenga na nini watu wa Mungu lazima wafanye kuitikia mahitaji haya na hali. Inatoa habari za nyuma au mjengo wa huduma yako ya upandaji kanisa. Inakusaidia kujibu swali, "*Nini Mungu anataka katika eneo langu ninalokusudia?" na "jinsi gani kila mwanaume, mwanamke, na mtoto katika eneo hili waweze kuona na kusikia injili katika njia inayoendana nao?"*

Wito wako wa kutenda unatakiwa uwe na mawazo na kuelewa kwa:

**A. Hali ya Watu**

Katika Mathayo 9:35-38, wakati Bwana alipokwenda miongoni mwa watu, alisema kuwa walikuwa wamesumbuka na wasio na msaada, kama kondoo wasio na mchungaji. Aliona kuwa kulikuwa na magonjwa mengi miongoni mwao, na akawaponya. Walikuwa katika hali ya maumivu. Alipokwenda miongoni mwao aliyaona maumivu.

Kutoka katika zoezi lako la utafiti, jinsi gani unaweza kuelezea hali ya watu walioko katika eneo lako unalolenga? Tumia takwimu ya kawaida kuangalia watu na mahitaji, mahitaji unayoweza kuyahisi, n.k. (Tazama maono ya KUM Ziada 4A, “Kuelewa Eneo Unalolenga.”)

**B. Hali Yao ya Kiroho**

Yesu aliona watu wakiwa hawana mwelekeo wa maisha ya kiroho. Hawakuwa na mwelekeo wowote (Mt 9:36).

Weka kwa kifupi hali ya kiroho ya watu katika eneo lako unalolenga. Kuna kanisa lolote miongoni mwa watu hao? Ni asilimia ngapi ya watu wanaokwenda kanisani au wanaojitambulisha wenyewe kama wafuasi wa Kristo? Wako wazi kupokea injili? Ni aina gani ya makundi mengine ya kidini yanayofanya kazi miongoni mwao? Ni makanisa mangapi yanahitaji kupandwa katika eneo lako unalolenga ili kwamba kila mtu anapata nafasi ya kusikia na kuona injili katika namna ambayo inaendana na hali zao? (Angalia Maono ya KUM Ziada 4A, “Kuelewa Eneo Lako Unalokusudia.”)

**C. Ni Nini Watu wa Mungu Lazima Wafanye**

Kisha Bwana akatoa amri ya kuomba (Mt 9:38). Baada ya kuamrisha kuomba, Alitafuta wafanyakazi na kuwafundisha na kisha akawatuma nje na hata akawaambia juu ya kutafuta msaada wa fedha! (Angalia Mathayo sura ya 10).

Ni wapi hasa Mungu anakuita na kundi lako kufanya kuwafikia watu katika eneo lako unalolenga? Ni jinsi gani utajitoa mwenyewe kwenye maombi kwa ajili ya watu katika eneo lako unalolenga? Ni rasilimali gani (watu, makanisa, na huduma) vinazoweza kuhamasishwa kusaidia kuwafikia watu katika eneo lako unalolenga? Ni wajibu gani wewe na timu yako mtafanya kuwaanda wengine kuomba na kufanya kazi nanyi katika kuwafikia watu wa eneo hilo unalolenga?

## II. MIPAKA KATIKA KUSHIRIKISHA HABARI

Habari sahihi, katika mikono sahihi, katika wakati muafaka, ni nyenzo yenye nguvu katia kubadilisha mtazamo wa watu na kuwatia moyo kwenye utendaji. Kwa jinsi hiyo, habari zilizoshirikishwa isivyopasa zinaweza kusababisha aibu au kujisikia vibaya, itakayopelekea katika hasira, upinzani na mkao kubadilika.

> Habari sahihi, katika mikonoi sahihi, katika wakati muafaka, ni nyenzo yenye nguvu katia kubadilisha mtazamo wa watu na kuwatia moyo kwenye utendaji.

Taarifa yako ya utafiti inaweza kuwa zana yenye nguvu ambayo Mungu anaweza kutumia kuwapa wengine mzigo wa mahitaji ya watu katika eneo unalolenga na haja ya kuona watu wanaoishi katika eneo hilo unalolenga wakiwa wafuasi wa Yesu Kristo.

**A. Kwa Nani Utoe Matokeo ya Utafiti Wako?**

Anza kuwashirikisha wenzio mmoja au wawili wanaoaminika ulichogundua juu ya nguvu ya mavuno na shamba la mavuno. Kushirikisha taarifa zako za utafiti watu wachache kunaweza kuonyesha jinsi wengine watakavyoitikia na kusaidia kutarajia jinsi ya kutia moyo mwitikio mzuri wa kutia moyo na kushughulikia kwa upole vizuizi vibaya. Uliza ushauri na maoni yao ya jinsi ya kuhamasisha waumini kwenye upandji kanisa kutokana na utafiti wako unavyoonyesha.

Kushirikisha wenye mamlaka kisiri na kupata baraka zao kuonyesha utafiti wako kwa wengine inaweza kuwa moja ya njia bora ya kuendelea. Waonyeshe viongozi jinsi upandji kanisa utakavyozidi huduma zao. Waonyeshe kwamba china ya mamlaka yao, utafanya mapenzi ya Bwana.

Mwisho na muhimu zaidi, Washirikishe wengine walio na moyo wa kazi ya upandaji kanisa. Ufahamu huu unaweza kukusaidia kujenga kundi la wasaidizi wa maombi, wanaotoa fedha na timu ya wajumbe.

**B. Ni Nini Malengo ya Kushiriklisha Utafiti WakoYanachopelekea kwa Wengine?**

*1. Kulinganisha Waliopotea*

Habari za sasa zinazoonyesha ukame wa kiroho wa watu. Wambie masimulizi ya kitu fulani kitakachosababisha watu kujisikia maumivu kwamba hao wasiokuwa na Kristo wanateseka mahali ulipofanya utafiti.

*2. Maombi*

Makanisa yaliyopandwa ambayo yana maombi yanadhihirisha kufanikiwa zaidi kuliko hayo yasiyokuwa na maombi. Unapotoa taarifa yako ya utafiti, toa mahitaji muhimu ambayo Mungu peke yake anaweza kuyajibu. Waombe wengine kuombea mahitaji hayo.

*3. Kuhamasisha Watu Wengine Kusaidia Upandaji Kanisa*

Habari mpya zinazosaidia watu kuona nini wanachoweza kusaidia. Fanya kwa vitendo na onyesha vitu maalumu wanavyweza kufanya kama vile kufanya kazi na watoto, kusaidia katika ujenzi, kutoa fedha, kusaidia kupiga vyombo vya kwaya, uinjilisti au hata msaada wa vitendo.

*4. Utoaji*

Uwe wazi ni wapi unahitaji la kifedha. Uwe wazi na mwaminifu na usisite kutoa hitaji.

**C. Jinsi Gani Utoe Utafiti Wako?**

- Omba kwa ajili ya hekima. Utatakiwa kuwa mwenye busara na usitoe taarifa katika tabia ya upinzani kama inaonyesha maeneo ambayo wakristo wamekuwa hawafanyi vya kutosha kuwafikia wasioamini.
- Tumia busara . Usishirikishe kila kitu, lakini shirikisha taarifa muhimu ambazo zitasaidia watu kuona jinsi ambavyo wanaweza kushiriki katika kazi ya upandaji kanisa.
- Onyesha jinsi ya kutoa utafiti wako kulivyo bora kwa wengine. Tumia ramani, masimulizi juu ya watu wanaochekesha, na toa maono kulingana na mtazamo wa Mungu.
- Usisikilize majibu mabaya yanayosema kuwa haiwezekani. Kumbuka Yesu yuko pamoja nawe.

## III. ONYESHA JINSI YA KUHAMASISHA NGUVU YA MAVUNO

Moja ya kipengele cha agizo lako la utafiti (Maono ya KUM Ziada 4A, “Kuelewa Eneo Lako Unalolenga”) ilikuwa kuonyesha ni vyanzo gani (nguvu ya mavuno) vilikuwepo tayari kukusaidia kuwafikia watu katika eneo lako unalolenga kwa injili. Kwa kushirikisha matokeo ya utafiti wako na wengine, unaweza ukahamasisha baadhi ya rasilimali hizi kusaidia katika kupanda kwako kanisa.

**A. Tambua Rasilimali Zilizopo Kusaidia Eneo Linalolengwa**

*1. Watu*

Nani anataka kushiriki? Waulize watu na wape nafasi ya kujitolea katika upandaji kanisa. Ni mda kisasi gani watu waliovutiwa watapenda kutoa kwenye huduma hii?

Watu wa kanisa lako wana moyo wa kutaka kusaidia katika huduma yako ya upandaji kanisa? Nani atasaidia? Kawaida kanisa unalosali kwa wakati huo ndiyo chanzo kizuri cha watu, fedha na maombi. Waumini wa kanisa hilo wanakufahamu na wangependa kujitoa zaidi kwenye huduma yako kuliko wengeine.

*2. Fedha*

Ni kiasi gani cha fedha kilichopo? Tia changamoto watu kutoa kwa kujitoa wenyewe upanuzi wa ufalme.

3. *Nyenzo*

   Ni nini kilichopo? Kama vile vitabu vya maandishi, senema, vifaa vya mziki, n.k.?

**B. Anzisha Mkakati wa Kuhamasisha Kwa Kupanda Kanisa Lako**

Ni mkakati gani utakaoanzisha kwa ajili ya kuhamasisha nguvu ya mavuno? Kwa sababu kwenye habari zilizotolewa katika somo hili, andika mkakati wako wa kushirikisha wengine utafiti wako kuwawezesha kushiriki.

## IV. MCHANGANUO JUU YA JINSI UTAFITI UNAVYOWEZA KUTUMIKA KUHAMASISHA RASILIMALI

***Nguvu ya taarifa*** *Na Stan na Donna Downes*

Katika mwaka 1996, mmishenari wa Romania OC ya kimataifa walifanya onyesho la mradi wa utafiti wa nchi nzima kwa kuchagua kata ya Brosv kama mfano. Alizalisha mfuatano wa ramani ambazo zilionyesha aina kadhaa za makanisa na maeneo yasiyo na makanisa. Aliacha nakala za kazi yake kwa viongozi wa kanisa la mtaa, akitumaini kazi yake itazaa matunda.

Miezi kadhaa baadaye, Valerica Tudor, kiongozi wa makanisa ya Brethren huko Brasov, alichunguza umuhimu wa ramani hizo na kuona waziwazi hitaji la upandaji kanisa katika kata yake. Alitumia ramani kama hatua yake ya uamsho wa juhudi za upandaji kanisa katika kata ya Brasov.

Tangu mwaka 1997, Valerica na viongozi wengine wa makanisa wamesaidia kufanya utafiti wa kata ya Brasov, kwa bidii kabisa na wamekuwa wakizalisha ramani mpya kila mwaka—kutunza mwendo wa hatua za upandaji kanisa. Makanisa mapya kumi na mawili yamepandwa, na karibu vikundi kiini 20 vimeanzishwa katika vijiji. Katika seti nyingine ya vijiji, viongozi wa makanisa wamegundua wakristo walio tayari kuanzisha vikundi kiini.

Viongozi kadhaa wa makanisa wanakutana kila mwezi kwa ajili ya maombi, kujifunza neno, kufanya mpango wa robo mwaka na kutoa taarifa. Wameanzisha orodha ya vijiji 89 visivyokuwa na kanisa la kiinjili, kutumia orodha hiyo kutia moyo makanisa ya mitaa kupanda makanisa zaidi na kuelekeza juhudi za upandaji kanisa.

Mwitikio wa makanisa umekuwa wa shauku. Kanisa moja liliuliza kwa nini watu hawakuleta habari hizi mapema! Jingine likauliza kutaka kujua kinachokuwa kinaendelea baada ya mda kwenye mradi. Makanisa kadhaa yamechangia kwenye kazi kifedha. Ingawa ramani ya kwanza haina matumaini kwa kupitwa na wakati, inatunza sehemu ya heshima katika nyumba ya Valerica, ukumbusho wa jinsi Mungu anvyotumia habari kuwatia moyo watu wake kwa njia yenye nguvu.

### MASWALI YA KUTAFAKARI, MARUDIO NA MATUMINZI

- Ni kwa jinsi gani utafiti umetumika kendeleza mkakati wa utafiti?
- Katika mfano wa utafiti, Ni kwa jinsi gani habari za utafiti zinaposhirikishwa kwa kanisa na watu wengine, zinavyowawezesha kuhamasisha rasilimali kuwasaidia katika juhudi zao za upandaji kanisa?
- Ni kwa jinsi gani kushirikisha utafiti wako kunaweza kupelekea faida kwenye juhudi zako za upandaji kanisa?
- Ni kwa jinsi gani kushirikisha utafiti kunaweza kuharibu uhusiano wako na viongozi wakristo?

### UTEKELEZAJI WA AZIMIO

- Na timu yako ya upandaji kanisa, chunguza tena taarifa zako za utafiti na andika kile Mungu anachokuonyesha kwa upandaji wako wa kanisa. Shirikisha wito huu kwenye utendaji na mkufunzi wako au mshauri au watu wengine wanaofaa.
- Andika harakati za kuhamasisha kushauri wengine kukusaidia katika juhudi za upandaji kanisa. Weka na wale utakaowashirikisha matokeo ya utafiti wako, nini utakachowashirikisha, jinsi gani unadhani watashiriki kwenye kazi yako (maombi, utoaji, kujiunga na timu yako, n.k.). Shirikisha mkakati huu kwa mkufunzi au mshauri.

- Weka mkakati wako wa kuhamasisha na shirikisha matokeo na mkufunzi au mshauri au katika kipindi kingine cha mafunzo.

**VYANZO**

Downes, Stan and Donna. *The Alliance Impact*. Budapest, Hungary: The Alliance for Saturation Church Planting, Spring, 1999.

# KANISA

KANISA

SOMO LA 5

# Asili ya Kanisa

## KANISA NI KIUMBE HAI

☞ **Kusudi la Somo**

Lengo la somo hili ni kuweka wazi mafundisho ya kibiblia kwamba kanisa ni kiumbe hai, na kuchunguza maana halisi ya huduma ya upandaji kanisa.

☞ **Wazo Kuu**

- Kanisa siyo jengo au sehemu
- Kanisa ni mwili hai wa Kristo, ukiwa na wote waliomwanini Yeye.

☞ **Matokeo Yanayotarajiwa**

Wakati yaliyomo katika somo hili yanapoeleweka, kila mshriki anatakiwa:

- Kujua mafundisho ya msingi ya kibiblia ya kanisa kama kiumbe hai.
- Kupambanua jinsi gani mawazo yasiyotoshereza ya kanisa yalivyoibuka katika utamaduni au mandhali, na jinsi gani mawazo haya yanarudisha nyuma maendeleo ya kanisa hai.

☞ **Ushauri kwa Wakufunzi**

Somo hili lina maswali mengi mazuri ya majadiliano ambayo yamejaa katika somo zima. Mkufunzi anatakiwa kujisikia huru kutumia lolote au yote kuwasaidia wafunzwa kuainisha na kuyatafakari katika kuelewa kwao kwa zana iliyofundishwa.

**UTANGULIZI**

Wazo la kanisa ambalo ni wazi kwenye maandiko, mara nyingi limewekwa kiutamaduni kwa makosa au kwa nia isiyo ya lazima. Haya yanatofautiana kutoka utamadunu hadi utamaduni, lakini yote yanarudisha kanisa la mtaa kuwa vile kabisa ambavyo Kristo alikusudia. Kufahamu asili ya kanisa kutoka katika mtazamo wa msimamo wa kibiblia itasaidia wapanda kanisa katika kuanzisha kanisa ambalo linakazia katika mambo muhimu na matokeo yake linakuwa lenye afya, la kung'aa, linaloendana na utamaduni na la asili ya kibiblia.

### I. MAANA NA MATUMIZI YA NENO "KANISA"

#### A. Maana ya Kihistoria ya Neno "Kanisa"

Neno la kiingereza "kanisa" limetolewa kwenye neno la Kijerumani <u>Kirche</u>, ambalo linatoka katika neno la Kiyunani <u>kuriakon,</u> likiwa na maana "iliyo ya Bwana" (angalia 1Kor 11:20; Uf 1:10). *(Nukuru kwa mtafasiri: Andika upya sentensi hii kujadili asili ya lugha ya neno linalokusudiwa au neno kanisa.)*

Neno ya kiyunani lililotafsiriwa "kanisa"-<u>ekklesia2,</u> maana yake "kusanyiko lililoitwa nje."

- Katika matumizi yasiyokuwa ya kibiblia (ya kawaida)- "kusanyiko la raia huru walioitwa pamoja na Herald."
- Katika toleo la Kiyunani la Agano la Kale (maandiko matakatifu ya Wayahudi), ekklesia walitafsiri neno la kiebrania qahal3 , likiwa na maana "kusanyiko." Neno hili lilitumiwa na Waisraeli mara kwa mara wanapoitwa pamoja kwa kusudi maalumu (Mwa 49"6; Zab 26:5).

- Agano Jipya linadhihirisha maendeleo ya neno, kutoka kwenye maana rahisi isiyo ya kiufundi, mpaka kuwa lenye maana kwa watu wa Mungu. Neno limetumika mara 114 katika Agani Jipya. Mara tisini na mbili neno linamaanisha kusanyiko maalumu la waumini la mtaa. Neno ekklesia karibu kila mara linatafsiriwa kama "kanisa", Kusanyiko, mkutano au mkusanyiko."

### B. Matumizi ya Neno Ekklesia (Kanisa) Katika Agano Jipya

Limetumika kijografia, kuzungumzia wakristo waliokuanyika pamoja

- Katika nyumba ya mtaa (Kol 4:15).
- Kujikusanya katika mji (1Kor 4:17; Gal 1:22; 1The 1:1).
- Makundi makubwa, kujikusanya kimkoa (Mdo 9:31).
- Kwa wakristo waliotawanyika katika maeneo yote ya sehemu (mdo 8:1-3, au "kanisa la Algeria").

<u>Linatumiwa na waumini wa kila umri na wa kutoka kila mahali, ambao kiroho wameungana na Kristo.</u> Kichwa cha kanisa (Efe 1:22-23; Kol 1:18). Hili linajulikana kama kanisa la wote. Neno linazunguka mwili wote wa waumini katika Yesu Kristo (1Kor 12:28; Efe 1:22-23; Ebr 12:23). Watu hawa wametengwa na Mungu, walioitwa kutoka katika ulimwengu kwa ajili ya sifa yake, kusudi lake jema na mapenzi ya milele (1Kor 1:2; Rum 1:7, 8"28).

Hasa hasa, neno "kanisa" linawekwa katika herufi kubwa kama linamaanisha kanisa la wote (vilevile linaloitwa kanisa lisiloonekana). Linapokuwa linamaanisha kanisa la mtaa, mara nyingi linaandikwa kwa Herufi ndogo. Matokeo yake, linafanana kama hivi:

- Kanisa la Yesu Kristo
- Kanisa la Odessa

### C. Matumizi kwa Ujumla ya Neno "Kanisa" Leo

Neno "kanisa" linatumika kwa namna mbalimbali katika jamii na utamaduni. Linatumika kuelezea jengo la shughuli za kidini ("kanisa" chini mtaani), au dhehebu au kundi la wanaojitenga walio na mahusiano ya kimuungano (kanisa la Kristo). Inaweza kumaanisha kusanyiko la mtaa (Presbiterian ya kwanza la Odessa) au jamii ya wakristo wanaotabili (kanisa linalokusanyika katika nyumba ya Marr). Neno linatumika kuelezea wakristo katika nchi fulani (kanisa la Urusi), Katika mkondo fulani wa theolojia wa mawazo (kanisa lililotengenezwa) au mapokeo (kanisa la Utakatifu la pentekosti).

## II. DHANA YA UONGO JUU YA KANISA

Kabla ya ujenzi wa aina yeyote kuanza, moja ya hatua ya kwanza ni kusafisha takataka na vizuizi vingine. Ni sawa pia na katika kujenga wazo la kanisa. Ni muhimu kusafisha fikira mbaya au za uongo kabla hatujaweza kujenga kueleweka kwa kweli juu ya maana halisi ya neno.

### A. Vivuli vya Agano la Kale Dhidi ya Ukweli wa Agano Jipya

Kosa kubwa la kawaida katika kuelewa kanisa linatokea kutokana na kushindwa kutofautisha fikira za Agano la Kale na Agano Jipya. Katika Agano la Kale, mitindo, aina, au vivuli vilitumika mara nyingi kuonyesha sehemu tu ya ukweli wa kiroho ambao haukuwa umedhihirishwa mpaka baada ya Agano Jipya. Mfano mmojawapo mzuri ni kondoo wa pasaka sanamu iliyosimama badala ya *dhambi mpaka tu* wakati Kristo alipokuwa amedhihirishwa kama kondoo wa Mungu anayezichukua dhambi za ulimwengu (Yoh 1:29). Kondoo huyu wa pasaka ilikuwa ni sanamu ya mda. Ilielekeza kwa Kristo na haina umuhimu tena. Kuna aina nyingi za sanamu kama hizo, lakini hekalu ndiyo hasa imeeleweka vibaya zaidi.

### B. Kanisa Siyo Hekalu

Makanisa mengi yanadhani hekalu la Wayahudi katika Agano la Kale kuwa kielelezo cha waumini kukusanyika. Makanisa ya Othodox na Romani Katoliki wanalichukulia hili kupita kiasi. Katika mtindo huu, kiongozi wa ibada anaitwa "kuhani" na jengo linaweza kuitwa "hekalu" Vilevile, wafuasi wa mtindo huu wanaamini kujitoa kwa Bwana kunafanyika kila wakati wanapokuwa wanashiriki meza ya Bwana. Wakati wanakataa sheria ya kuabudu

sanamu iliyopambwa kwa rangi mbalimbali, kawaida kuna kufanana kwa karibu kwa ibada na utaratibu wa ibada.

Mtindo huu, katika matokeo, unajaribu kuunda toleo la "wakristo" la hekalu la Wayahudi. Kumuona Mungu kunafanyika kwa njia ya huduma ya makuhani kwenye hekalu. Kwa sababu ya huduma ya kujitoa ya hekalu la Agano la Kale, mimbali inasimama kati ya watu na makuhani, na kuhani peke yake anaruhusiwa kuwa nyuma ya mimbali. Makanisa yaliyofanywa katika mtindo huu mara nyingi wana kusanyiko mbele ya mimbali (au meza ya ushirika), na kuhani au mtu mwingine "maalumu" peke yake anaruhusiwa kuwa nyuma ya mimbali.

Kuna idadi ya mistari ya kibiblia inayopinga wazo la kanisa kama mtindo wa hekalu la kisasa sawa na hekalu la Wayahudi wakati wa Agano la Kale. Kwa mfano, Paulo alifundisha kwamba waumini pekee yao—na siyo jengo wanakutana—ni hekalu la Mungu (1Kor 6:19). Mungu hakai ndani ya jengo tena, lakini ndani ya watu (Mdo 17:24). Ni nyumba za kiroho zilizojengwa kwa jiwe hai (Rum 12:1).

> Paulo alifundisha kwamba waumini pekee ni hekalu la Mungu—na siyo jengo wanamokutana.

Zaidi ya hayo, Kristo alitoa sadaka moja kwa wakati wote (Ebr 9:26; 10:12). Amemaliza kazi kama kuhani mkuu , hakuna hata mmoja anayeweza kuongeza zaidi.(Ebr 7:27). Wakati wa kifo cha Kristo, pazia la hekalu lilifunguka kuanzia juu mpaka chini—hakuna mgawanyo kati ya mwanadamu na Mungu (Mk 15:38). Hakuna tena mgawanyo wa madaraja ya makuhani (1Pet 2:9). Waumini wote ni makuhani na watumishi wa Mungu na wanaweza kujitoa wenyewe na ibada yao kama sadaka bila kuwa na mtu wa katikati wala hekalu la kidunia (Rum 12:1).

Waumini katika Agano Jpya waliishi katika utamaduni ambapo ilitarajiwa kwamba kila kikundi cha kidini wajenge "hekalu" la miungu yao. Baadhi ya hekalu za wapagani hawa wazuri zilikuwa za kuvutia na kwamba masalia yake yanaendelea kuwa sehemu kubwa za vivutio vya watalii leo! Zaidi ya haya, utamaduni wa pale wakati ambapo wakristo wa kwanza waliishi wakitarajia na kuthamini hekalu zilizovutia. Lakini kanisa lilielewa kwamba hekalu pekee ni miili yao, na walikataa kutangaza mtazamo usio wa kweli wa injili kwa kudhihirishia mfumo huo wa kiutamaduni.

### C. Kanisa siyo Sinagogi

Baadhi ya watu wanadhani kwamba masinagogi ya Wayahudi yalikuwa sehemu ya kanisa badala ya hekalu. Kulikuwa na hekalu moja tu—lililokuwa Yerusalemu. Kwa jinsi hiyo, kulikuwa na sinagogi katika kila mji ambao kulikuwa na idadi ya familia za kiyahudi. Sinagogi ilikuwa ni sehemu ya kufanyia maombi na kusoma maandiko. Kulikuwa hakuna kutoa sadaka wala makuhani. Badala yake, watu kutoka katika kikundi walichaguliwa kama "watawala" wa sinagogi. Kuabudu kulikuwa hakuna utaratibu zaidi kama ilvyokuwa kwenye hekalu. Kukuanyika kwa kawaida walikaa katika duara, na mzungumzaji akiwa amesimama katikati au akiwa amekaa miongoni mwao.

> Wakristo wa kwanza hawakujaribu kurudia kutengeneza hekalu la Wayahudi. Kwa hakika, jengo la kanisa la kwanza halikujengwa mpaka karne ya 4!

Sinagogi ni mtindo mzuri wa kanisa kuliko hekalu lilivyo. Kadiri wakristo walivyotapakaa kwenye majimbo ya Asia ndogo. Hawakujaribu kuiga mtindo wa hekalu. Kwa hakika, jengo la kanisa la kwanza halikujengwa mpaka karne ya 4! Badala yake, Waumini walianzisha makanisa ya kwenye miji yaliyofanana na mafundisho na maombi yasiyo ya utaratibu wa sinagogi za wayahudi. Makanisa leo yanatakiwa kufikiri kwa kirefu na zaidi endapo majengo yao na mifumo ya kuabudu inafanana na huo usio wa utaratibu., kuabubudu kwa starehe.

Wakati mtindo wa sinagogi unafanana na kanisa la Agano Jipya kuliko hekalu lilivyo, bado linakosa kitu fulani muhimu. Ingawa kawaida na bila kufata utaratibu, sinagogi halikuwahi kuwa zaidi ya jengo ambamo Wayahudi walikutana kwa ajili ya maelekezo. Sinagogi ilikuwa ni mkusanyiko wa mawe na mtangio—na siyo wa waumini. Kama kwamba, siyo mtindo unaotosha kwa kanisa hai.


## III. METHALI ZINAZOELEZEA KANISA KAMA KIUMBE HAI

Kam kanisa siyo jengo, ni nini hasa? Kanisa lilikuwa kwa ujumla jambo "jipya" ambalo Kristo alianzisha lenye kuwa na kufanana kidogo na jengo au hekalu la dini zingine za siku hizo. Badala ya *kuwa tu jengo*, *ni mwili ha*i na wenye waumini ndani ya Kristo.

Kuna mafumbo mengi ya kanisa katika Agano Jipya. Inastusha jinsi wanavyoliona kanisa kama kiumbe hai kutoka pande nyingi. Machache ya haya yameorodheshwa hapa.

- Ni familia (1Tim 3:14-16; Efe 3:15). Katika familia hii, Mungu ni "Baba," Yesu ni mtoto wake wa pekee, na tuko watoto tuliorithiwa kama vijana na mabinti (Yoh 1:12-13, Efe 1:5); kaka na dada katika Kristo (2The 3:15, 1Pet 2:17).
- Ni mwili (1Kor 12:12ff). Fumbo hili waziwazi linaonyesha uhusiano wa sehemu ya kiungo cha mkristo pekee ("viungo ") kwa wote kanisa ("mwili") na kwa kristo ("kichwa"). Waumini ni "wajumbe" wake waliounganа mmoja kwa mwingine, kama vile viungo vya mwili vilivyoungana na kichwa.
- Ni umati (Mdo 20:28-29). Yesu ni mchungaji mmoja wa kweli (Ebr 13:20-21) anayeumiliki, na kuutolea. waumini ni "kondoo" wake wanaojitoa kwenye uongozi wa mchungaji.
- Ni watu (1Pet 2:9-10). Uhusiano wa wajumbe wa kanisa la Kristo hauendani na tabia ya kabila, mipaka ya rangi, lakini ikizingatia urithi wao mpya kama "taifa" takatifu.
- Ni bibi arusi (Efe5:25-33; Uf 21:2; Yoh 3:29). Kwa kuwa, anapendwa na Kristo, lakini anawajibika kwake. Ni Bwana arusi, aliyetoa maisha yake kwa ajili ya bibi arusi.
- Ni jengo (hekalu hai) (Efe 2:20; 4:11). Kristo ni "jiwe kuu la pembeni" hai. Kanisa linafananishwa na hekalu hai ambalo ni takatifu (1Kor 3:16-17), linalokua, (Efe 2:21:-22), na la kiroho (1Pet 2:5). Waumini ni mawe hai katika hekalu.
- Ni kuhani mkuu (Uf 1:5-6). Chanzo cha ukuhani mkuu ni Yesu. Waumini wote ni sehemu ya ukuhani huu mkuu (1Pet 2"5-9), na wanaweza kuja kwa ujasiri wakileta sadaka zinazokubaliwa (Rum 12:1-2; Ebr 13:15) kwenye uwepo wa mfalme (Ebr 4:16).
- Ni tawi (Yoh 15:1-16). Waumini ni matawi hai wanaozaa matunda yanayosalia.

**Kielelezo 5.1 Ni Lipi ni Kanisa?**




Kutokana na mafumbo yaliyoorodheshwa hapo juu, ni lipi kati ya vivuli viwili katika kielelezo 5.1 kinaonyesha kanisa zaidi? Kwa nini? Ni kwa jinsi gani hii inaendana na wazo lako la kanisa la mtaa?

## IV. UPANDAJI KANISA HAI

Ni kwa jinsi gani ukweli kwamba kanisa ni kiumbe hai kunachangia namna ya kupanda kwetu kanisa la mtaa? Kuna idadi ya sehemu ambazo ni muhimu kuzifikiria wakati kanisa jipya linapangwa.

### A. Wajumbe wa Kanisa la Mtaa Wanatakiwa Wawe Waumini

Kanisa la mtaa linatakiwa liwe picha ya kanisa la wote. Kuwa mjumbe au sehemu ya kanisa la wote (kiumbe hai), mtu lazima awe kiasilia anahusiana na Kristo. Mahitaji ya muhimu ya msingi ya kanisa la mtaa ni sawa—kuungana na Kristo. Kwa hiyo, hitaji la pekee kuwa mwanachama wa kanisa la mtaa linatakiwa liwe kuzaliwa upya. Pia inafuata kwamba kila waumini wa mtaa wanatakiwa wawe wajumbe wa kanisa la mtaa. Hakuna misingi ya kibiblia kwa kanisa kukataa uanachama wa muumini isipokuwa dhambi ya zinaa. (1Kor 5:2).

### B. Majengo Yanatakiwa Yasiwe Jambo La Msingi Kufikiriwa

Kama ilivyoonyeshwa mapema, majengo siyo kanisa, au hata kuwe kigezo mpaka karne nyingi baada ya kanisa kuanza. Yote mara nyingi, wapanda kanisa wanaweka mkazo zaidi au raslimali nyingi zaidi kutoa jengo. Msisitizo huu unaweza kukatiza uinjilisti na kufuasisha—sehemu ya kweli muhimu katika kuanzisha “kanisa.

### C. Mahusiano ni Ufunguo

Kama majengo si funguo, Ni nini basi? Jibu ni kwamba mahusiano ni matofali ya kujengea kanisa la mtaa linaloshamiri. Hii ni pamoja na uhusiano wa waumini kwa Kristo na kwa wao kwa wao. Lakini pia ni pamoja na uhusiano na wasioamini ambao pengine Mungu amewachagua kwa ajili ya wokovu. Mpanda kanisa mwenye busara atakazia mda wake na nguvu katika kuanzisha mahusiano haya. Atakuwa anajitoa kutumia mda kujenga daraja la uaminifu kwa wasioamini, na kutoa malezi kwa waumini walioko kanisani.

### D. Kanisa la Mtaa Lazima Lirithi Utamaduni

Kama kiumbe hai, kanisa siyo mlingoti au lisilobadirika. Ni hai, lenye nguvu, linalobadirika kila wakati kukidhi mahaitaji ya wakat huo. Hakuna mfumo mmoja au sura ambayo lazima liwe nalo. Mifumo ya kanisa inatakiwa iendelezwe kwa kila kanisa la mtaa na hata mpanda kanisa, wakiongozwa na Roho Mtakatifu, anatafuta kuelezea kazi za kibiblia katika namna ambayo inafaa kwa kusudio lake maalumu la watazamaji na hali ya kiutamaduni.

### E. Lazima Kuwe na Baadhi ya Mifumo ya Utaratibu

Mwili wa mwanadamu, ingawa ni kiumbe hai, una muungano. Kila kiungo kinafanya kazi pamoja kawaidia kwa uzuri. Kanisa la mtaa pia lazima liwe na muungano , lakini muungano lazima wakati wote uzingatie kukidhi mahitaji,  yote kiroho na kimwili, ya mwili (waumini).

Mfano wa muungano katika Agano Jipya ni pamoja na:

- Ulikuwa Umeeleza nyakati za kukutana (Mdo 20:7)
- Viongozi walichaguliwa (Mdo 20:23)
- Malezi kwa ushirikiano yalifanyika (1Kor 5)
- Pesa zilikusanywa kusaidia katika mahitaji ya vitendo
- Orodha ya wajane waliostahili kusaidiwa ilitunzwa (1Tim 5:9)

Bila kujali ukweli kwamba  muungano ulikuwepo, msisitizo wa makanisa ya Agano Jipya ilikuwa wakati wote kwenye kukua kiroho, kimafundisho, na usafi wa maadili mema ya waumini. Muungano wowote ulikuwa unatokana kipekee kwenye uwezo wa kusaidia mwili kukua na kuwatunza wajumbe wake.

### F. Kanisa la Mtaa Lazima Likue na Kuzaliana

Kama kanisa ingekuwa jengo au mashine, ingehitaji tu kutunzwa. Kwa jinsi jiyo, ukweli kwamba kanisa ni kiumbe hai ina maana kwamba lazima likue na kuzaliana—kama ilivyokawaida kwa viumbe vyote hai. Kanisa linakua kadiri mtu pekee anapoamini ujumbe wa injili na kuzaliwa katika familia ya Mungu. Ukuaji huu hata ni wa kishindo wakati makanisa mapya ya mtaa yanapopandwa—kila moja likiwa na waumini wapya wengi. Kwa kuwa kazi

yetu ni kutimiza Utume Mkuu kwa kuayafikia mataifa yote, ni lazima wakati wote tutafute ukuaji wa hali ya juu. Unaotokea wakati kanisa la mtaa linapozaliana kwa upandaji makanisa mengine mapya ya mtaa.

**G. Vikundi Kiini Vinatakiwa Kusimama katika Nafasi Nyeti**

Vipindi vy kanisa la mtaa na shughuli zinatakiwa kuonyesha ukweli kwamba ni kiumbe hai. Mfumo hasa unaofaa wa mtindo wa kanisa hai la mtaa ni kiini hai kinachoufanya mwili.Viongozi wengi wa kanisa la mtaa wanaamini kuwa mtindo wa kikundi kiini uliofundishwa katika zana hii ni mtindo pekee ambao kwa utosherevu unaelezea kipimo cha maisha kilichoongezwa ambacho lazima kiwepo kanisani. Vikundi kiini vinakazia zaidi mkazo kwenye ukuaji na uzima wa kila mjumbe, na katika kuzaliana. Rasilimali za chini zinagawanywa kwenye maswala ya majengo na vipindi. Mtindo huu unaonekana kuwa karibu zaidi na wastani wa ushirika wa mtu na mahusiano yaliyokuwepo katika kanisa la kwanza (Mdo 2:42-46).

**MASWALI YA KUTAFAKARI, MARUDIO NA MATUMIZI**

- Ni nini unachoweza kusema kwa mkristo na muumini na kwa hiyo mjumbe wa kanisa la wote ambaye hashiriki kwenye kanisa la mtaa?
- Ni nini mtu anatakiwa kufanya kuwa sehemu ya kanisa la Yesu Kristo (mwili wa Kristo)? Maswali yako yazingatie maandiko.
- Ni nini mkristo anatakiwa kufanya kuwa sehemu ya kanisa la mtaa?
- Kwa nini mtindo wa hekalu la kwenye Agano la Kale siyo mtindo unaotoshereza kwa kuelewa kanisa katika Agano Jipya?
- Ni kwa njia zipi uzoefu wa kanisa lako unaonyesha mafundisho ya Agano Jipya juu ya asili ya kanisa?

**VYANZO**


- Cook, Dr. Robert. *Unpublished Notes on Ecclesiology*. Western Seminary, Portland, OR: 1980.
- Getz, Gene. *Sharpening the Focus of the Church.* Chicago, IL: Moody Press, 1975.
- Hodges, Melvin L. *The Indigenous Church. Springfield*, MO: Gospel Publishing House, 1953.
- Lightner, Robert P. *Handbook of Evangelical Theology*. Grand Rapids, MI: Kregel, 1995.
- Radmacher, E. *The Nature of the Church. Portland*, OR: Western Baptist Press, 1972.
- Ryrie, Charles. *Biblical Theology of the New Testament*. Chicago, IL: Moody Press, 1986.
- Saucy, Robert. *The Church in God's Program*. Chicago, IL: Moody Press, 1972.

KANISA

SOMO LA 6

# Kazi za Umoja za kanisa

## NINI KINATOKEA MNAPOUNGANA PAMOJA

☞ **Kusudi la Somo**

Lengo la somo hili ni kujadili matumizi ya kiblia ambayo kanisa lazima litekeleze linapokutana pamoja na kujadili mahusiano kati ya mtu binafsi, kikundi kidogo, na kazi ya kanisa la mtaa.

☞ **Wazo Kuu**

- Kazi ya kanisa ni pamoja na kuabudu, kushirikisha meza ya Bwana, kuhubiri na kufundisha, utoaji, kuadilisha, na kulea.
- Vikundi vidogo vinapaswa kuanza kutimiza mengi, kama siyo yote, ya kazi ya kibiblia ya kanisa.

☞ **Matoke Yanayotarajiwa**

Wakati yaliyoma katika somo hili yanapoeleweka, kila mshiriki anatakiwa:

- Kujua kazi ya kibiblia ya kanisa lililokusanyika.
- Kuanzisha mpango wa kukusanyika kwa umoja kwa vikundi vidogo ambavyo vitajenga msingi mzuri wa kati vinapokuwa kanisa la mtaa.

☞ **Ziada**

6A Ubatizo katika Agano Jipya

☞ **Ushauri kwa Wakufunzi**

Somo hili linashauri kwamba vikundi vidogo au vikundi kiini vinatakiwa vianze kutimiza kazi nyingi za kanisa lililopangwa. Hii inaleta mabishano, lakini ni hatua muhimu. Unatakiwa kutoa mda wa kutosha kujadili mchoro 6.1 baada ya yaliyomo kuwa yametolewa.

### UTANGULIZI

Somo hili litakazia kwenye kazi ambayo kanisa linatakiwa kutimiza linapokutana pamoja. Kazi hizi ni pamoja na kuabudu, kushirikisha meza ya Bwana, kuhubiri, kufundisha neno, kuadilisha, uinjilisti, kutunza malezi bora na utoaji. Orodha hii haitarajiwi kutoshereza—badala yake, inaonyesha kazi kuu za kazi ya kanisa kama kianzio kwa mafunzo yajayo. Tofauti kati ya kazi za kanisa na mfumo wa kanisa ilielezewa katika Somo la Kanisa 3.

- Kazi za Kanisa = ***kile*** kanisa ambacho lazima lifanye.
- Mfumo wa Knisa = ***Jinsi*** kanisa linavyochagua kufanya kazi.

Kazi za kanisa zimeamriwa katika Agano Jipya na lazima ziwekwe na kanisa. Kwa jinsi hiyo, haiwezi kusonga sana kiasi kwamba mifumo ya kanisa inaweza na inatakiwa kubadilika na kuweza kuendana ili kufaa zaidi kwa watu maalumu wanaotarajiwa. Kwa ukumbusho huo, somo hili litakazia kwenye kazi ya umoja ya kanisa na kudhani kwamba mpanda kanisa atakuwa mwangalifu kuchagua mifumo inayofaa kwa kanisa linaloanza.

### I. UMOJA DHIDI YA MAJUKUMU BINAFSI YA KANISA

Agano Jipya inaorodhesha majukumu mengi ya kanisa. Baadhi ya haya yanaweza kufanyika na kila muumini. Shughuli zingine zinahitaji kikundi—kanisa lililojikusanya. Bado zingine zinaweza kujaribiwa binafsi au kwa kiushirikiano. Kwa mfano, kuishi kimungu ni wajibu wa binafsi. Malezi ya kanisa, kwa jinsi hiyo, yanajitwalia kuwa kuna kikundi. Na uinjilisti umeamriwa kwa mtu binafsi na

kanisa kwa ujumla. Somo hili linashughulikia kazi ambazo zinatakiwa zifanywe na waliokusanyika, au ushirika wa mwili. Ukiwa na tofauti hii kichwani, tunatakiwa kujiuliza ni wakati gani kundi la waumini wanawajibika kutimiza kazi ya ushirika ya kanisa.

### A. Ni Wakati Gani "Tufanya Umoja?"

Somo la 4 la Kanisa limesaidia kueleza maana ya kanisa. Katika somo hilo tumeona kwamba tafsiri halisi inaweza kuwa na

- Kundi la waumini waliojipanga
- Viongozi wenye ujuzi
- Waangalizi wa ushirika mtakatifu
- Mikutano ya mara moja moja

Watu wengi wanaweza kuongeza kwenye orodha hii katika namna nyingi. Hakuna swali kwamba kanisa la mtaa lililojipanga lina sifa zilizotajwa hapo juu na kutimiza kazi zilizoelezwa katika somo hili.. Kwa jinsi hiyo, hizi "kazi za ushirika" siyo tu kwa kanisa la mtaa lilojipanga. Zinahusu pia vikundi vidogo vya waumini.

### B. Kukutana Kama Kikundi

Lengo la nyenzo hii ni kuwezesha upandaji wa kanisa la mtaa. Kwa jinsi hiyo, ni muhimu kutambua kwamba kazi za ushirika wa kanisa hazihitaji kusubiri kanisa kujipanga. Ni muhimu sana kuziacha mpaka kipindi hicho.

> Kazi za umoja wa kanisa la mtaa lazima pia zifanyike katika kundi dogo la waumini.

Ni waumini wangapi wanatakiwa kuweza kujaribu kazi za ushirika za kanisa? Mfano mzuri unaopatikana katika Mathayo 18:19. Katika fungu hili, Yesu anaeleza kwamba atakuwepo katika namna ya ajabu wakati wowote watu wawili au watatu watakapokutana pamoja."Ni muhimu kutambua kuwa mandhali inazungumzia juu ya malezi ya kanisa—hasa hasa kazi ya umoja wa kanisa. Kwa hakika, neno "kanisa" na shughuli za waumini wawili au watatu zinawekwa mapacha katika mandhali. Lengo siyo kudai kwamba waumini wawili au watatu wanafanya kanisa la mtaa, kinyume na tafsiri ya sehemu zilizopita. Badala, inaonekana kuonyesha kwamba kazi za *kanisa la mtaa* pia zinatakiwa zitumike na *kundi dogo la waumini.*

Waebrania 10:25 inatuamuru pia tusiache kukusanyika pamoja. Wakati mahudhurio ktika kanisa la mtaa yangeweza kutimiza amri hii kwa hakika, kuna hali nyingi ambapo kanisa la mtaa halipo. Kisha tunafanya nini? Tena, mstari *unakazia kukusanyika pamoja* lakini hauhitaji kanisa lililojipangilia. Hata kama kuna waumini wachache sana, ni muhimu kuanza kuwa mnakutana kwa ushirkiano ili kuweza kufanya kazi za ushirika ambazo haziwezi kufanywa na mtu binafsi.

## II. KAZI ZA UMOJA ZA KANISA

### A. Kuabudu kwa Umoja

Moja ya sababu kubwa za kanisa kukusanyika pamoja ni kumwabudu Bwana. Kuabudu kwa umoja kwa kanisa kutazungumziwa kwa kirefu kwenye Mwongozo wa Tano, somo la kanisa la16, "Kuabudu katika Kanisa la Mtaa" na somo la kanisa la 17, "Jinsi ya Kuongoza Kuabudu." Kwa jinsi hiyo, mara tu kundi dogo la waumini linapokuwa limehudumiwa, wanapaswa kuanza kumwabudu Bwana kwa pamoja.

Kuabudu kwa umoja kunawaruhusu wakristo kujilinganisha na mwili wa kristo mkubwa na wa aina mbalimbali kuliko tu vikundi vyao maalumu vidogo. Inatoa pia ushuhuda wa wazi kwenye jumuia wa uhai na nguvu za Mungu, na pia kuwatia moyo waumini ya kwamba hawako peke yao na kwamba Roho wa Mungu anafanya kazi katika maisha ya watu wengi mbalimbali. Kwa kuongeza, ushirika wa kuabudu unatoa zoezi kubwa la kufanyia mazoezi vipawa vya kiroho katika kuadilisha watu wa Mungu kama mwili.

## B. Ushirika Mtakatifu

Aina mbili za uaratibu wa kimamlaka wa kanisa unaokubaliwa na wote ni ubatizo na meza ya Bwana. Wakati makanisa yote yanakubali aina hizi mbili za ushirik, kuna tofauti ya maoni juu ya jinsi ya wanavyoweza kuufanya. Mapokeo ya madhehebu kawaida wanabishana juu ya hili. Unapoanza kanisa lako jipya, ni muhimu kwako na wajumbe wa kanisa hilo kuelewa jinsi utaratibu huo utakavyofanyika.

### 1. *Ubatizo*

Wakristo wa kiinjili wanashikiria nafasi inayotofautiana ya maana ya ubatizo. Nafasi tatu kubwa za maana ya ubatizo zimejadiliwa chini. Inatakiwa ifahamike, kwa jinsi hiyo, kwamba ubatizo kwenye Agano Jipya ulifanyaka mara baada tu ya kuokoka, na muumini yeyote ambaye ameongoza aliyekata shauri kwenye imani (Mdo 8:36). Hata katika maeneo mapya, hawakusubiri kanisa kuanzishwa ili kuwabatiza waliokata shauri (Mdo 16:33). Zaidi ya hayo, mtu mwenye cheo cha juu haikuwa lazima afanye ubatizo hata kama alikuwepo. (1Kor 1:14-17).

a. Ubatizo kama dalili ya imani ya mtu katika Kristo

Baadhi wanaamini kuwa ubatizo ni alama ya nje ya mabadiliko ya ndani kwa muumini. Inasimama kama ushuhuda kwa jumuia wa imani ya mtu ndani ya Yesu Kristo (Mdo 2:41; 10:48). Kuna utofauti wa mitindo ya ubatizo, lakini mara nyingi ni kwa kuzamisha ambako kunaonyesha kujifananisha kwa waumini na Kristo katika kifo chake, mazishi na kufufuka.

b. Ubatizo kama mapatano kati ya Mungu na mtu

Wengine wanaamini kwamba ubatizo ni hatua ya imani ambapo tunaletwa katika mapatano mapya kwa njia ya Kristo (Mt 26:28; Luk 22:20) na hatimaye kufurahia faida zake. Kutokana na mtazamo huu, watu wazima wanaoamini na familia zao, wakiwamo watoto wachanga na watoto, wanabatizwa. Kama kutahiri kulivyokuwa dalili ya mapatano ya zamani (Mwa 15, 17), hivyo ubatizo ni dalili ya mapatano mapya, Ukweli, badala ya mtindo wa ubatizo, ni kitu chenye maana.

c. Ubatizo kama dalili ya uanachama wa kanisa

Kuna kundi jingine la watu ambao wanaoweza kueleweka kushikilia nafasi ya tatu—ambayo ubatizo unaonyesha uanachama wa kanisa la mtaa, wakati wakiwa wanaweza kueleza kuwa wanashikilia moja ya imani mbili, katika matendo halisi wanakataa ubatizo kwa waumini wapya mpaka watakapokua kufikia hatua watakayokubaliwa kuwa wajumbe. Wakati wachache wangejaribu kuharalisha nafasi hii kutoka katika maandiko, wengi wanalifanya hili.

### 2. *Meza ya Bwana*

Bwana mwenyewe alituamuru kula mkate na kunywa damu kwa ukumbusho wake. Alitoa ushirika huu mara ya kwanza kwa wanafunzi wake katika chumba cha juu siku moja kabla ya kifo chake (Mt 26:26-28; Mk 14:22-26; Lk 22:19-20). Paulo aliwakumbusha Wakorintho juu ya umuhimu wa meza ya Bwana katika mandhali ya kanisa la mtaa (1Kor 11:23-34). Ni wazi kidogo kama inaweza kusherehekewa tu katika kanisa lenye utaratibu, nani atahudumia, ni mara ngapi kuliwa. Ingawa hili ni kamili kabisa, inaonekana kutoruhusiwa kuliwekea mipaka kwenye mandhali ya kanisa. Imeamriwa kwa waumini kama njia ya kukumbuka kujitoa kwa Bwana kwa ajili yetu.

Yesu mwenyewe alielezea maana ya kila kipengele. Vinawakilisha mwili wake ulivunjwa na damu yake iliyomwagika. Kifungu kidogo cha ufunguo ni “fanya hivi kwa ukumbusho wangu” (1Kor 11:25-26). Meza ya Bwana inatusaidia kukumbuka gharama ya wokovu wetu. Inatufanya kukazia kwenye kifo cha Kristo msalabani kalvari. Kila mara tunaula mwili na damu, tunatangaza uhalisi wa kujitoa kwake. Mtume Paulo akitoa maelekezo namna hili lilivyotakiwa kufanyika anasema kwamba kula mwili na damu tunakumbuka kufa kwa Bwana mpaka atakaporudi tena. Hii inawafanya waumini kukazia juu ya yote gharama ya wokovu na ukweli kwamba Kristo atarudi tena.

**C. Huduma ya Neno**

Usomaji wa neno, kuhubiri, na kufundisha inatakiwe iwe sehemu ya ushirika wa kusanyiko la waumini. Yesu aliwambia wanafunzi kuwafundisha waliokata shauri "kutii yote niliyowaamuru" (Mt 28:20). Paulo alimwelekeza Timotheo kufanya "bidii katika kuwasomea maandiko na kuhubiri na kufundisha" (1Tim 4:13).

> Inatakiwa ifahamike kwamba kuna tofauti kubwa kati ya kulihubiri neno la Mungu na kuzungumzia tu juu ya neno.

Inatakiwa ifahamike kwamba kuna tofauti kubwa kati ya kulihubiri neno la Mungu na kuzungumzia tu juu ya neno. Mara nyingi pia wahubiri, wafundishaji wa Biblia, viongozi wa majadiliano ya Biblia wanatoa mawazo yao na maoni ya maandiko—au tu kuupitia ujumbe waliousikia nyuma—badala ya kusoama halisi kwa neno na kumruhusu Mungu kusema kupitia neno hilo. Kusoma mistari michache tu kabula ya mahubiri au wakati wa kufanya mafunzo ya Biblia hakutoshi. Ni tendo la dharau kwa watu wa Mungu wakati viongozi wanapotoa maoni yao badala ya kulifungua neno la Mungu na kuonyesha ujumbe wa Bwana waziwazi kwenye Biblia.

Mwanafunzi wa maadiko anatakiwa kusoma, kujiandaa, kusali, kuomba, kutafakari kuchunguza, kutafiti na kusikiliza anapokuja kwenye neno. Biblia ni hai na yenye nguvu, na ni chanzo cha maarifa na busara. Somo la kujifunza Biblia kwa kufata neno katika utaratibu huu limeaandaliwa kuwezesha Mafunzo ya Biblia na kuhubiri *kunakokazia Kwenye Biblia!* Lengo la kutumia njia ya kujifunza kwa kufata neno siyo tu kupata ufahamu wa Biblia lakini kuutumia ukweli wa Mungu ili kwamba maisha yabadilishwe kufuatana na mapenzi ya Mungu.

**D. Kujengana Mmoja Kwa Mwingine**

Kwenye maandiko ya Biblia yote kuna mfuatano wa amri jinsi ambavyo waumini wanatakiwa kuhusiana mmoja na mwingine. Hizi amri "mmjo kwa mwingine" zinaelezea jinsi wakristo wanavyotakiwa kutendeana. Moja ya kazi za kanisa ni kutia moyo kufanya majaribio ya amri ya "mmoja kwa mwingine" Msisitizo huu wa umoja na kujaliana mmoja kwa mwingine unaliweka kanisa mbali na makundi mengine. Ni kwa Roho wa Mungu tu kufanya kazi ndani ya mioyo ya waumini kuweza kutii amri hizi. Moja ya amri za "mmoja kwa mwingine" zilizoandikwa katika maandiko ni:

- Kuoshana miguu (Yoh 13:14)
- Kupendana (Yoh 13:34; 15:12,17)
- Kujitoa mmoja kwa mwingine ( Rum 12:10)
- Kukubaliana (Rum 15:7)
- Kuelekezana (Rum 15:14)
- Kusalimiana (Rum 16:20)
- Kusaidiana (Gal 5:13)
- Kusameheana (Efe 4:32)
- Kuonyana (Col 3:16)
- Kutiana moyo (1Tim 4:18)
- Kutiana moyo (Ebr 3:13)

**E. Uinjilisti**

Kanisa lipo kuwafikia waliopotea kwa injili. Uinjilisti ni moja ya kazi za kanisa zinazohitajika katika kila ngazi ya kanisa, Tunatakiwa kuinjilisha binafsi, katika makundi na ama kanisa la mtaa. Kila moja ya haya inahitaji kwamba injili itolewe waziwazi. Kwa jinsi hiyo, kuna tofauti ya njia ambazo zinafanya kwa mafanikio zaidi. Uinjilisti wa kirafiki au wa mahusiano unaonekana kuwa njia yenye mafanikio kwa mtu binafsi. Makundi madogo yanaweza kuanza kutumia hali iliyoundwa. Kanisa la mtaa linaweza kutumia kwa mafanikio mziki au aina ya vipindi vingine kuwashawishi wasioamini kusikiliza ujumbe. Kiakili, vipindi vya kanisa la mtaa vinatakiwa kuweka na kushauri njia zote hizi. Urafiki wa pekee unatakiwa kumshawisha aliyepotea kuhudhuria kikundi kidogo kisichotisha. Na uzoefu mzuri kwenye kikundi kidogo

unatakiwa kuwashawishi kuhudhuria matukio ya kiinjili ya kanisa la mtaa. Wanaweza wakamwamini Kristo katika hatua yeyote kwenye safari hiyo.

## F. Utoaji

Kanisa la kwanza lilikuwa linajihusisha kiundani katika kutimiza mahitaji ya mwili kwa wengine. Ingawa msisitizo maalumu wa kutoa kwao ilikuwa kwa waumini wengine, fikira zao ilikuwa ni pamoja na makaka na madada wa makanisa yao, pia katika maeneo mengine. Kwa nyongeza, walitoa pia kwa ajili ya mahitaji ya hao waliokwenda nje kupanda makanisa mapya na kuwafikia waliopotea. Kunaonekana kulikuwa na utaratibu wa vipindi vya kanisa la mtaa vya kutoa, lakini pia kulikuwa na utoaji wa hiari wa waumini. Aina za utoaji zilizoorodheshwa chini zinaweza kuanza pengine kama kundi dogo na kuwa zaidi za kiutaratibu mara kanisa linapoanzishwa.

### *1. Masikini*

Waumini waliuza mali zao na kuwapa wahitaji kaka zao tangu mwanzo wa kanisa (mdo 2:45l; 4:34-35). Kwa jinsi hiyo, inaonekana kwamba utoaji huu ulihusu utaratibu ulioandaliwa kwenye kanisa. Walileta fedha zilizopatikana kutokana na kuuza vitu vyao na ardhi na kuzitoa kwa manabii kwa ajili ya kusambazwa kwa masikini (Mdo 4:35).

Wafuasishaji walifanya hivyo hivyo huko Antiokia. Walipotuma misaada kwenye makanisa ya Yudea, walifanya hivyo kwa kutuma michango yao kwa watu wawili waliochaguliwa. (Barnabas na Sauli) kwa wazee wa Yudea (Mdo 11:28-30). Na wazee matokeo yake wangezigawa zawadi hizo. Kanisa ilikuwa kwamba wakusanye pesa hizo kila wiki katika mtindo uliandaliwa (1Kor 16:2).

### *2. Wajane*

Mtindo unaofanana ulikuwepo pia kusaidia wajane. Mabishano katika Matendo 6 yalitokea kwa sababu idadi ya wajane waliohitaji msaada ilikua kufikia hatua kwamba mitume hawawezi kutoshereza kusimamia fedha. Hivyo wakaomba kanisa lichague watu saba waliojazwa roho kusimamia kazi hiyo. Kulikuwa pia na orodha ya wajane iliyoandaliwa huko kwenye kanisa la Efeso wakati Timotheo alipohudumu huko (1Tim 5:3-16). Paulo alimpatia Timotheo mipaka ili kwamba wajane tu waliokuwa na hitaji kweli wangewekwa kwenye orodha ya kusaidiwa. Kama wangekuwa na familia za wanaoamini, kanisa lisingewajibika kwa ajili yao. Pia, kama wangekuwa bodo kufaa kuoa na kuolewa tena, wangefanya hivyo na wasiwe mzigo kwa kanisa.

Hili linaonekana wazi kufaa kwa siku hizi kwa kanisa lenye utaratibu wa kusambaza misaada kwa wajumbe wenye mahitaji. Wakati utaratibu huo unapopangwa, ni sharti watu wa Mungu wachaguliwe kusimamia, kama katika Matendo 6. Ni busara pia kuhakikisha kuwa kuna watu mbalimbali wamehusika, ili kwamba isiwepo nafasi ya majungu.

### *3. Wapanda Kanisa.*

> Wafilipi 4:19 ni ahadi kwa wale wanaosaidia wapanda kanisa.

Mtume Paulo alikuwa mpokeaji wa misaada kutoka kwenye makanisa alipokuwa anahudumu kwa waliopotea katika maeneo ambayo hayajafikiwa. Kwa hakika, kipindi cha kuandika kitabu cha Wafilipi kilikuwa wakati wa kutuma zawadi kutoka kwenye kanisa la Wafilipi kwenda kwa Paulo alipokuwa akihudumu Urumi. Katika hatua ya mwisho wa kitabu, Paulo anawashangilia na kuwashukuru kwa ukarimu wao, na kuwahakikishia kwamba Mungu atatoa mahitaji yao *yote kama kuitikia kwa utoaji wao kwake* (Flp 4:18-19). Waumini mara nyingi wanadai ukweli wa mstari wa 19 *bila kutambua umuhimu wa mandhali, na kwa nani ilikuwa imeahidiwa!* Zawadi kama hizo ziliruhusu Paulo na wengine kujitoa mda- wote kwenye huduma badala ya kushona nyavu.

Kuna wakati mwingi kwenye maandiko wakati waumini waliposaidia huduma, lakini mwingine anahitaji kunena maalumu. Mtume wa kawaida mpole na anayependeza anaonekana kuandika waraka wake wa tatu kama maonyo ya uchungu kwa Diotrefe, aliyekataa kusaidia ndugu waliokuwa wakisafiri na kuhubiri injili (3Yoh 9-10). Kutoa kwa ajili ya kazi ya Bwana siyo uchaguzi—wala haiwezi kubadilishwa kwa kusaidia masikini walio miongoni mwetu.

*4. Wachungaji na Viongozi*

Ni wajibu wa kanisa la mtaa kutunza mahitaji ya mchungaji na viongozi wengine wa kanisa. Kanuni ya Agano la kale ya kutoa 'fungu la kumi' linaweka msingi kwa kusanyiko kuwajibika kuwalipa viongozi wao. Katika Agano Jipya kila kanisa kawaida liliangalia mahitaji ya viongozi wake. Kwa mfano, Paulo aliwaambia Wagalatia kuwasaidia walimu wao (Gal 6:6. Alimwambia Timotheo kufundisha makanisa kuwalipa walimu wao wa neno la Mungu (1Tim 5:18). Makanisa yanayochukua wajibu huu bila mzaha kawaida huwa wanabarikiwa na Mungu kwa uaminifu wao.

## III. WAKATI WA KUFANYA KAZI YA UMOJA

Sehemu iliyopita imeelezea idadi ya kazi za kanisa kibiblia. Hizi ni muhimu na kwamba itasaidia kufikiri kwa uangalifu juu ya swala la lini kundi la waumini wanatakiwa kuanza kizifanya. Wasubiri mpaka watakapokuwa kanisa lililo na taratibu au kuanza hata wanapokuwa wachache sana?

Mchoro 6.1 unaorodhesha idadi ya kazi za safu ya kushoto, na kuna nafasi ya kuweza kuongeza. Kama kikundi, jadili mchoro na fanya shughuli zifuatazo.

- Nukuru kama unakubaliana na kazi hizo zilizoorodheshwa.
- Ongeza kazi zingine ambazo unadhani kuwa ni muhimu, lakini hazimo.
- Weka alama ya "ndiyo" au "Hapana" kwenye safu ya katikati na ya kuria kuonyesha kama unadhani hizi zinahitajika na kundi dogo, kanisa la mtaa au yote. Jadili hoja zako.

| **Kazi za Kibiblia** | **Kikundi Kidogo**  | **Kanisa la Mtaa**  |
|---|---|---|
| Kutoa Kwa Wapanda Kanisa | | |
| Kuinjilisha | | |
| Ushirika wa Kuabudu | | |
| Kuhubiri | | |
| Ushuhuda Binafsi | | |
| Ubatizo | | |
| Meza ya Bwana | | |
| Kutoa kwa Masikini | | |
| Kuimba katika Vikundi | | |
| Kuwatunza Viongozi wa Kanisa | | |
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |

## MASWALI YA KUTAFAKARI, MARUDIO NA MATUMIZI

- Ni nini kazi ya umoja wa kanisa?
- Ni kwa jinsi gani kazi za kanisa zinaendana na za vikundi vidogo?
- Ni nini kazi ya kuhubiri katika ushirika wa kusanyiko? Ni nini kazi ya kikundi cha kujifunza Biblia?
- Ni nini unachoelewa kuwa maana kuu ya ubatizo wa maji?
- kwa nini utoaji ni kazi ya ushirika wa kanisa?

## UTEKELEZAJI WA AZIMIO

Ukiwa na wajumbe wa timu yako ya upandaji kanisa, amua ni lini mtaanza kuzingatia ushirika wa kukusanyika. Ni mfumo gani mikusanyiko hii itakuwa nao?

KANISA
*ZIADA*
6A

# Ubatizo Katika Agano Jipya

## KUJIFUNZA BIBLIA KWA KUFATA NENO

**UTANGULIZI**

Mafuzo ya mwanzo au ya kimsingi ya maisha ya kikristo, kufuatana na Waebrania 6:1,2 ni haya ya ubatizo. Ubatizo mbalmbali tofauti umetajwa katika Agano Jipya, lakini mafundisho haya yanakomea kwenye mfano wa ubatizo wa maji uliofanywa na mitume na viongozi wengine katika kanisa la kwanza, pamoja na maelezo mengine kutoka kwenye nyaraka za mtume Paulo. Kwa mafundisho kamili, tumia kamusi ya Biblia kutafuta marejeo ya ubatizo.

**I. UCHUNGUZI**

Kutoka katika vifungu vifuatavyo, sema NANI aliyebatizwa, NANI alifanya ubatizo, LINI na WAPI ubatizo ulifanyika; NINI ilikuwa maana ya ubatizo.

| | NANI aliyebatizwa? | NANI Aliyefanya Ubatizo? | LINI? | WAPI? | NINI ilikuwa maana yake? |
|---|---|---|---|---|---|
| Mdo 2:38-41 | | | | | |
| Mdo 8:12,13 | | | | | |
| Mdo 8:36-38 | | | | | |
| Mdo 16:31-34 | | | | | |

## II. UFAFANUZI

Kutokana na uchunguzi, weka kwa kifupi nafasi ya ubatizo katika kanisa la kwanza.

Kutoka kwenye mafundisho ya Mtume Paulo, tunajifunza zaidi juu ya maana ya ubatizo wa wakristo. Kutoka katika Warumi 6:1-4, elezea uhusiano kati ya ubatizo na kifo na ufufuko wa Kristo.

Baadhi ya mistari kwa ajili yako kujifunza: 1Kor 15:12-20; Gal 3:26, 27; pet 3:21-22

## III. MATUMIZI

Ni jinsi gani utaweza kutumia kanuni ulizojifunza kupitia mafunzo haya katika kanisa lako jipya?

Kumbuka: Baadhi ya ubatizo ambao umesemwa kwenye vitabu vya injili unaopatikana katika Mathayo 3; Mark 3; Luka 3; na Yohana 3.

KANISA

SOMO LA 7

# Kuanzisha Maelezo ya Kusudi la Kanisa

## KWA NINI KANISA LAKO LIWEPO?

☞ **Kusudi la Somo**

Kusudi la somo hili ni kusaidia wapanda kanisa kuanzisha maelezo ya kusudi la kanisa linaloibuka.

☞ **Wazo Kuu**

- Maelezo ya kusudi la kanisa yanajibu “kwa nini kanisa la mtaa lipo?
- Maelezo ya kusudi la kanisa la mtaa yanatakiwa kuungwa kwenye kusudi la kanisa kwa ujumla

☞ **Matoke Yanayotarajiwa**

Wakati yaliyoma katika somo hili yanapoeleweka, kila mshiriki anatakiwa:

- Kutambua kwamba kuelewa sawasawa kusudi la kanisa kutabadili namna wapanda kanisa wanavyofanya kazi ya upandaji kanisa na huduma.
- Kuweza kuandika waziwazi na kwa kifupi maelezo ya kusudi la kanisa la mtaa kwa kanisa lake linaloibuka.

☞ **Ushauri kwa Wakufunzi**

Hii ni warsha. Washiriki wanatakiwa kuandika maelezo yao ya kusudi la kanisa na kuyashirikisha kwa washiriki wengine.

**UTANGULIZI**

Makanisa yanayoleta mabadiliko yanaongozwa na ufahamu wa kusudi. Wana ufahamu wazi wa kusudi la kibiblia ulimwenguni vilevile na uthibitisho wazi wa kile Mungu anataka kwa ajili ya kanisa lao hasa la mtaa. Wanafahamu kuwa wajibu wao haushii tu kwa upandaji wa kanisa moja isipokuwa kuchangia katika kuzaliana kwa makanisa. Kanisa la Agano Jipya lilikuwa limeanzishwa ili kuleta utukufu kwa Mungu kwa kuadilishwa kwa waumini na uinjilisti kwa waliopotea. Kazi ya malezi kwa mataifa yote kwa ajili ya Kristo ilitolewa kwa waumini wote na kwa vizazi vyote. Zamani wakati wa utaratibu wa upandaji kanisa, ni muhimu kufikiri wajibu ambao kanisa litasimama kutimiza Utume Mkuu, kufikiri juu ya kusudi kwa ajili ya kanisa maalumu la mtaa linalokusudiwa kupandwa. Hatua ya kuandika maelezo ya kusudi la kanisa inaweza kuunganisha waumini, kuainisha malengo yao, kuvutia kazi kutoa.

Mwelekeo kwenye juhudi zao, na kuleta nguvu na uwezo. Maelezo hayo ya kusudi la kanisa siyo tu kusudio -la lengo; yanaeleza waziwazi kusudi la kuwepo kwa kanisa hilo maalumu. Kazi ya mwanzo ya uongozi ni kuweka wazi na kuwakilisha kusudi na maono ya kanisa linaloibuka kwa watu wa kusanyiko. Somo hili litatoa nafasi ya kufanya hivyo.

> Kazi ya mwanzo ya uongozi ni kuweka wazi na kuwakilisha kusudi na maono ya kanisa linaloibuka kwa watu wa kusanyiko.

**I. NI NINI MAELEZO YA KUSUDI LA KANISA**

Katika somo la 4, “kutafasiri maana ya kanisa la mtaa,” ulianzisha *tafsiri* ya kanisa la mtaa. Tafsiri inajibu swali “**Nini?”** Kwa kutofautisha, *maelezo ya kusudi la kanisa* yanajibu “**kwa nini?”** Haya ni, maelezo ya kanisa la mtaa yakijibu swali la “kwa nini kanisa hili maalumu lipo?”

## II. KUTAFUTA KUSUDI LA KANISA LAKO

Neno la Mungu mara zote ni sehemu nzuri ya kuanzia tunapokuwa tunataka kujua kitu fulani juu ya kanisa. Maelezo yako ya kusudi la kanisa yanatakiwa yasiende kinyume na kile ambacho Biblia inathibitisha juu ya kanisa. Soma mafungu yafuatayo kuona ni nini kila moja linasema juu ya kusudi la kanisa. Andika kanuni yeyote utakayogundua katika nafasi iliyotolewa. Umeshaangalia kwenye baadhi ya mistari hii katika somo la 4 ulipokuwa unauliza swali la "nini" kwenye tafsiri kama hiyo. Wakati huu, unauliza hasa swali "kwa nini" katika kutafuta kusudi.

Mt 16:18 ______

Mt 28:18-20 ______

Mdo 1:6-8 ______

Mdo 2:42-47 ______

Efe 3:10-11 ______

Efe 4:11-16 ______

Col 3:12-17 ______

Ebr 10:22-25 ______

1Pet 2:1-5, 9-12 1:22 ______

Mengine ______

## III. KUANDIKA MAELEZO YA KUSUDI LA KANISA

Kusudi la kuandika maelezo ya kusudi la kanisa ni moja ya shughuli inayosisimua katika maisha ya kanisa. Kusudi linatakiwa lijadiliwe kwa kirefu, kuombewa, kukubaliwa na viongozi kwa imani na kisha kutangazwa na kuelezewa kanisani, na kutolewa kopi na kuchapishwa katika maandishi yeyote ya kanisa (kama vile mwaliko au karatasi ili kwamba iingizwe kwenye ufahamu wa washiriki wa kanisa.

Kuandika maelezo yako ya kusudi, jiulize mwenyewe maswali haya:

- Kwa nini kanisa ulilоitwa kupanda lipo?
- Ni nini itakuwa kazi ya kipekee na maalumu katika kazi ya ufalme wa Bwana?
- Kama muwakilishi wa Mungu katika sehemu yako inayokusudiwa, uko pale kufanya nini?

*Tumia nafasi hapo chini kuorodhesha sababu kwa nini watu wahudhurie na kushiriki katika kanisa hili jipya. Uwe wazi uwezavyo.*

______

______

______

______

______

______

______

______

______

______

Maelezo ya kusudi lazima yakubaliane na kusudi la kibiblia kwa ujumla, lakini zingatia mandhali ya kiutamaduni kwa watu maalumu wanaokusudiwa. Lazima ielezewe kipekee kwa kanisa lako lililopandwa. Maelezo mengi ya kusudi la kanisa yanaweka bayana kusudio la huduma. Kusudio linatakiwa liwe la eneo la kijografia, utamaduni wa kundi la watu, au kwa uzuri zaidi, au muungano wa yote.

Hii hapa ni mifano michache ya kubuni ya maelezo ya kusudi la kanisa.

- Kanisa la habari njema lipo kumwabudu Bwana, kuadilisha waumini na kutangaza injili kwa waliopotea sehemu ya Smithville.
- Kanisa la Ushirika wa Injili lipo kutangaza injili katika mji wa Grant City, Kata ya Brown, taifa letu na ulimwengu.
- Kanisa la Ufufuko lipo kuhudumia kwenye familia katika mji wa Riverbend.
- Kanisa la Imani lipo kuwafanya watu wa umri wa chuo kikuu kuwakamilisha wafuasi wa Yesu Kristo.

Ni maelezo yapi ya kusudi la kanisa unayaona kuwa ya msaada na kwa nini?

Ukiunganisha yale uliyokusanya kutoka katika maandiko na yale uliyogundua kama ya kipekee kwenye kupanda kwako kanisa, sasa unakaribia kuwa tayari kuandika maelezo ya kusudi lako. Kumbuka, maelezo ya kusudi yanatakiwa yawe na mambo matano:

1. Yanatakiwa yawe wazi na mafupi iwezekanavyo
2. Watu wanatakiwa watamani maana ya maelezo kwa undani.
3. Yanatakiwa yaamshe dukuduku
4. Yanatakiwa yafuatwe kwa uaminifu
5. Yanatakiwa yarudiwe kuangaliwa na kurekebishwa baada ya kipindi fulani

Katika nafasi hapo chini, Chukua mda sasa wa kuandika maelezo ya kusudi la kanisa lako. Yanatakiwa yajibu swali rahisi, “Kwa nini Kanisa Hili Lipo?”

## MASWALI YA KUTAFAKARI, MARUDIO NA MATUMIZI

- Kama tafsiri yako ya kanisa, na maelezo ya kusudi lako la kanisa yanatokana na uzoefu wako katika kanisa, au katika maandishi?
- Maelezo yako ya kusudi la kanisa yanaendana na kusudi la kibiblia la kanisa lililozungumziwa katika somo la 2? Kama siyo, nini kinakosekana?
- Kwa nini maelezo yaliyoandikwa ya kusudi la kanisa ni muhimu?
- Jinsi gani kanisa lako litakuwa tofauti na makanisa mengine?

## UTEKELEZAJI WA AZIMIO

Ruduia hatua hii ya kufanaya na kuandika maelezo ya kusudi la kanisa na viongozi wa kanisa lako lililopandwa. Haya yanaweza yakawa yaliyotunzwa hivi karibuni, viongozi wanaoibuka, au wengine ambao unashirikiana nao kupanda kanisa. Kama hili ni kanisa binti, haya yanaweza kutoka kwenye kanisa mama; viongozi ambao wanajihusisha zaidi katika hatua ya kuzalisha makanisa binti mapya.

## VYANZO

Jenson, Ron, and Jim Stevens. *Dynamic of Church Growth*. Grand Rapids, MI: 1981.

KANISA

SOMO LA 8

# Falsafa ya Huduma ya Upandaji Kanisa

## JINSI GANI KANISA LINAWEZA KUHUDUMU KWA WALIOPOTEA?

☞ **Kusudi la Somo**

Somo hili linaelezea falsafa ya huduma ya upandaji kanisa ni nini, na kwa nini ni muhimu. Inakusudiwa kutia changamoto wafunzwa kutafakari kuhusu maswala yanayoendana na "jinsi" ya huduma ya upandaji kanisa

☞ **Kiini Kikuu**

- Falsafa ya huduma ya upandaji kanisa inajengwa kwenye tafsiri ya Biblia na asili ya kanisa badala ya mapokeo ya binadamu.
- Mandhali-maalumu ya falsafa ya huduma ya upandaji kanisa inaongeza ufanisi wa mpanda kanisa na timu yake.

☞ **Matokeo Yanayotarajiwa**

Wakati yaliyomo katika somo hili yanapoeleweka, kila mshiriki anatakiwa:

- Kufahamu ulazima wa hitaji la falsafa ya huduma ya upandaji kanisa na madhara ya kutokuwa nayo.
- Kujua vipengele muhimu na vipao mbele vya falsafa yenye mafanikio ya huduma ya upandaji kanisa.
- Kuanzisha maelezo ya falsafa ya huduma.

☞ **Ziada**

8A Karatasi ya maswali: Kuanzisha falsafa ya huduma-ya upandaji kanisa

☞ **Ushauri kwa Wakufunzi**

Somo hili litasogeza karibu maelezo ya kusudi la kanisa la mtaa yaliyojariwa katika somo la kanisa 7. Wafunzwa wanatakiwa waelekezwe kusoma somo hili kabla ya kipindi cha darasa. Wakati wa kuanza, hakikisha unaelezea kwa wafunzwa kwamba tupo hapa kujadiliana hoja kabisa ya vitendo ya mkakati, misingi, kanuni, na matazamio. Neno "falsafa" linatakiwa lisiwafanye kuona mashaka ya umuhimu wake, ingawa neno hilo linatumika katika ulimwengu wa kidunia kuwaondoa watu na kuwapeleka katika mfumo ambao hautokani na Mungu wala neno lake. Kazi yetu ya upandaji kanisa lazima ijengwe kwenye maelezo na mawazo (i.e. falsafa) ambayo yanaendana sawa na Yesu Kristo, Bwana wa kanisa. Wakati wa kipindi cha somo, nyenzo hii inatakiwa imalizike haraka ili kutumia mda mwingi wa darasa kama mda wa warsha kwa kutumia karatasi ya maswali katika ziada 8A.

### I. NI NINI FALSAFA YA HUDUMA YA UPANDAJI KANISA?

Falsafa ya kanisa inaweza kutumika kama wazo la jumla kwa kila aina ya huduma. Inaweza kutumika pia kwa mkazo finyu wa huduma maalumu. Somo hili litakazia hasa falsafa ya huduma ya upandaji kanisa. Kanuni, kwa jinsi hiyo, zinaweza kutumiwa na kanisa lolote, huduma, au kiongozi wa kikristo.

#### A. Falsafa ya Huduma

Kwa ujumla, falsafa ya huduma ni maelezo au ufahamu unaosaidia kujibu swali "JINSI GANI tutafanya huduma yetu?" Ni mwongozo unaotusaidia kutathimini kama tunafanya *vitu sahihi* na katika *njia sahihi*. Falsafa ya huduma inachukua thamani zetu katika kuwajibika, na kwa hiyo itakuwa tofauti kwa kila mtu na kwa kila kikundi.

Ni muhimu pia kutofautisha *falsafa ya huduma* na "*falsafa ya upotovu*." Katika Wakolosai 2:8, Paulo anatuonya kuepuka "mateka na madanganyo matupu, yanayotegemea mapokeo ya wanadamu, na mafundisho ya awali ya ulimwengu, badala ya Kristo." Mstari juu unaeleza waziwazi jinsi falsafa yetu inavyoweza kuwa:

- Falsafa inayotokana na mapokeo ya kibinadamu—epukana nayo
- Falsafa inayotokana na Kristo—ikumbatie

> Tunapochagua kutokufikiria juu ya falsafa yetu ya huduma, tunaishia upofu kushikilia falsafa yao ya sasa, ambayo mara nyingi inatokana na mnapokeo yetu.

Mara nyingi haionekani kama mstari huu haulaumi *wazo la falsafa,* lakini badala inatofautisha vyanzo viwili vya falsafa. Huku kuelewa vibaya kumewafanya waumini wengi kuitikia kinyume kwenye wazo la falsafa ya huduma. Lakusikitisha, wanapochagua *kutokufikiria juu ya* falsafa yao ya huduma, *wanaishia kukumbatia kwa upofu falsafa yao ya sasa*, ambayo mara nyingi inatokana na mnapokeo yao. Matokeo yake, wanakuwa na hatia ya kufanya sawa na vitu ambavyo Paulo alikuwa anahubiri kinyume navyo. Kusudi la somo hili ni kutafakari juu ya "jinsi tunavyofanya mambo" ili kwamba kwa ujasiri tuweze kusema yanatokana na Kristo na neno lake badala ya mapokeo yetu ya kibinadamu.


**B. Falsafa ya Huduma ya Upandaji Kanisa**

Masomo ya nyuma yameshazungumzia juu ya tafsiri ya kanisa na maelezo yake ya kusudi. Yote haya matatu yanajenga juu ya mwenzake katika tabia ifuatayo:

- Tafsiri - ***Kanisa*** ni nini
- Kusudi – ***Kwa*** nini kanisa lipo
- Mkakati wa Falsafa – ***Jinsi*** gani Kanisa linahudumu.

Katika somo hili, swali hasa ni "Jinsi gani mpanda kanisa ahudumu?" Kila mfunzwa atakuwa na nafasi ya kutafakari juu ya swali hili muhimu anapokamilisha warsha katika ziada 8A.

**Kielelezo 8.1 Mwendelezo wa Kimaana**



## II. HITAJI LA FALSAFA YA HUDUMA YA UPANDAJI KANISA

Kuna sababu nyingi kwa nini kila mpanda kanisa anatakiwa kuwa na falsafa ya huduma ambayo imeandaliwa maalumu kwa ajili ya huduma yake. Sababu hizi ni pamoja na za mafundisho ya kibiblia na pia kuitumia falsafa kwa vitendo.

### A. Biblia Inafundisha Hitaji la Upangaji kwa Kufikiria

Neno "falsafa ya huduma" halipo kwenye ,maandiko, lakini wazo la kupanga kwa kufikiria, kwa kumtegemea Mungu, inapatikana kwenye Biblia.

- Mithali 14:15: "Mjinga huamini kila neno; bali mwenye busara huangalia sana aendavyo."
- Mithali 15:5: "Mpumbavu hudharau kurudiwa na babaye; bali yeye aangaliaye maonyo hupata busara."

#### 1. *Mfano wa Yesu Kristo*

Maisha ya Yesu na huduma ni kielelezo kwamba alikuwa na kusudi halisi na njia halisi za kuyafikia malengo hayo. Tunaona kwamba Yesu alikuwa na matokeo ya mwisho akilini. Hakuruhusu kitu chochote kumkatiza kutoka kwenye malengo yake. Fikiri juu ya maandishi haya:

- Mathayo 16:21-23: Yesu kwa ujasiri alielekeza hatua zake kuelekea msalabani.
- Marko 1:45: Tunaona kwamba Yesu alijizuia kuacha kufanya baadhi ya mambo mazuri na kuhubiri kwa watu wengi, ili aendelee kuzingatia misheni yake.
- Yohana 6:5: Yesu alipanga kabla ya mda kwa ajili ya muujiza ambao alikuwa anataka kuufanya, ingawa hakuwa ameonyesha kwa wanafunzi wake.

#### 2. *Mfano wa Paulo*

Mtume Paulo pia alipanga nini na jinsi gani atahudumu kulingana na kanuni zake za kikristo na imani.. Alitambua kwamba Mungu angeweza, na mara nyingi alifanya, kubadili mipango yake. Kwa jinsi hiyo, ni wazi Paulo hakufikiri kama hili lingemzuia kutokupanga kwa kufikiri jinsi ambavyo angefanya huduma yake. Mifano michache ya mipango ya Paulo inapatikana katika:

- Warumi 15:20: Paulo aliamua kwamba mkakati wake ungekuwa kumhubiri Kristo katika sehemu ambazo alikuwa bado hajulikani.
- 1Wakorintho 2:1-2: Paulo aliamua kupunguza mahubiri yake ya ukweli rahisi wa msalaba wa Kristo.
- 1Wakorintho 9:12: Paulo aliamua kukataa kupokea misaada ili kwamaba kusiwe na swali kwenye kusudi lake la kuhubiri.
- Matendo 16:3: Paulo alimtahili Timotheo ili kutokuwa kikwazo kwa Wayahudi.

### B. Falsafa ya Huduma ya Upandaji Kanisa ni ya Kivitendo

Falsafa ya huduma inatusaidia kukazia kwenye "kazi njema ambayo Mungu ameiandaa kwa ajili yetu kufanya" (Efe 2:10). Inaweza kutuelekeza na kutusaidia kufanya maamzi katika hali ngumu wakati njia mbili au uchaguzi unapoonekana kufaa. Ni kama fimbo ya kupimia kuona ni nini kinafaa katika huduma yetu na nini hakifai.

> Kila mmoja anayejishughulisha na huduma ameshakuwa na falsafa ya huduma—wawe wanafahamu au hawafamu.

Ni ukweli kwamba kila mmoja anayejishughulisha katika huduma ana falsafa ya huduma. Inaweza ikawa haijaandikwa. Wanaweza wasiweze kuielezea waziwazi. Wanaweza wasiwe na habari kwamba ipo—lakini ipo. Hii ni *kwa sababu wote tuna ufahamu wa jinsi ya kuhudumu*! Na hiyo inaweka falsafa ya huduma. Kwa hiyo, haiwezekani kutokuwa na falsafa ya huduma. Kuna aina mbili tu za uchaguzi zilizopo. Tunaweza:

- Kwa makini kuchunguza falsafa zetu kuhakikisha zinasimama katika maandiko.
- Kuidharau na kutangaza ya mapokeo ya binadamu badala ya ukweli.

Waziwazi, njia ya kwanza ni bora zaidi. Somo na karatasi ya mazoezi katika Ziada ifuatayo imeandaliwa kukusaidia kuifanyia ujuzi falsafa yako ya upandaji kanisa, na kwa ustadi ichunguze kama ni inayofaa zaidi.

**C. Falsafa Wazi ya Huduma ya Upandaji Kanisa Inazingatia Utendaji Wetu**

Tafsiri ya kanisa na kusudi la kanisa inabakia maelezo tu mpaka tunapoviruhusu kuunda falsafa zetu za huduma ya upandaji kanisa. Katika hatua hiyo tunahama kutoka kwenye maelezo kwenda kwenye swala la tendo la "Jinsi gani nipande kanisa?" Maelezo ya falsafa ya huduma ya upandaji kanisa ambayo utaandika yatafanya mawazo yako juu ya hatua maalimu na vipao mbele ambavyo utakuwa navyo unapoanzisha kanisa mpaya. Itakufanya kuepuka makosa yafuatayo:

- Kutumia mda katika shughuli na vipindi visivyokuwa na manufaa
- Kuangalia vibaya shughuli za maana au vipengele ambavyo kanisa linalokua linahitaji

**D. Falsafa ya Huduma ya Upandaji Kanisa Inatakiwa Kuwa Dhahiri**

Kila mpanda kanisa, timu ya upandaji kanisa, au kanisa inatakiwa kuwa na falsafa yake ya huduma ya upandaji kanisa. Mungu amempa kila muumini vipawa tofauti vya kiroho. Pia, kila mtu yuko tofauti kimwili, kiroho, na kihisia. Matokeo yake, njia moja anayoitumia mtu mmoja kwa ufanisi katika huduma inaweza isifae kwa mtu mwingine. Sawasawa na watu tunaowahudumia wako tofauti. Zaidi sana, kila mji au eneo linalolengwa lina historia tofauti na utamaduni. Kwa hiyo falsafa ya huduma ya upandaji kanisa inatakiwa iwe maalumu kwa maeneo haya.

1. *Mpanda Kanisa*

Falsafa ya huduma ya upandaji kanisa inatakiwa ianze kwa kuelewa uwezo na unyonge wa mpanda kanisa. Inatakiwa itafasiri jinsi gani anaweza kutumia uwezo wake, na kupunguza udhaifu wake. Kwa mfano, mpanda kanisa ambaye hawezi kujieleza vizuri anaweza kuanzisha falsafa ya huduma ya upandaji kanisa ambayo itakazia uinjiliti pekee wa mahusiano na urafiki. Mahitaji ya familia yanaweza kuruhusu au kuondoa kuishi halisi katika sehemu inayotarajiwa. Katika kila hali falsafa inatakiwa iwe inayotumika na inayofaa kwa mtu atakayeiweka.

2. *Timu ya Upandaji Kanisa*

Timu ni njia thabiti ya upandaji makanisa. Katika baadhi ya hali kwa kifupi timu haipo, lakini kila inapowezekana, timu zinatakiwa zitumike. Ni mara chache sana kumkuta mtu ambaye ana uwiano mzurini mzuri sana na mwenye uwezo kiasi anaweza kukamilisha zaidi kuliko timu. Mchanganyiko wa watu katika timu nzuri wanazidisha idadi ya vipawa vya kiroho na uwezo, vilevile uzoefu na nguvu ambayo inaweza kuwekwa katika upandaji wa kanisa jipya.

Falsafa nzuri iliyofikiriwa ya huduma ya upandaji kanisa itauchukulia uwezo na udhaifu wa kila mjumbe na kukuza ufanisi wao.

Kwa mchanganyiko huu wa vipawa mbalimbali, uwezo na hadhi ya kufikia maarufu wake, lazima pawepo na mpango unaotumika kuunganisha wajumbe wa timu na kuongoza shughuli zao. Falsafa nzuri iliyofikiriwa ya huduma ya upandaji kanisa itauchukulia uwezo na udhaifu wa kila mjumbe na kukuza ufanisi wao. Kwa kuwa kila mchanganyiko wa wajumbe wa timu ni tofauti, falsafa lazima iundwe kufaa kila timu.

3. *Kanisa Mpya*

Kila kanisa mpya linatofautiana sana kulingana na utamaduni, lugha, na mapendeleo ya pekee ya wajumbe wake. Haiwezekani kutumia kwa ufanisi mpango unaofanana katika hali zote. Falsafa inayofaa ya huduma ya upandaji kanisa itachunguza eneo linalolengwa na watu kuona ni jinsi gani ya kuwafikia kwa ufanisi. Itaona pia ni mfumo gani ambao utafaa zaidi kwa ukuaji kiroho wa kundi maalumu.

## III. YALIYOMO KATIKA FALSAFA YENYE UFANISI YA HUDUMA YA UPANDAJI KANISA

Wakati kila falsafa ya huduma ya upandaji kanisa itakuwa tofauti, kuna matofali ya kawaida ya kujengea ambayo yanatakiwa yawemo katika kila moja. Kila moja ya haya linahitaji kufikiriwa na maandalizi, lakini litafanya yaliyokamilishwa kuwa ya msaada na ya ufanisi.

### A. Inajenga Juu ya Tafsiri na Kusudi

Kama ilivyoonyeshwa katika kielelzo 8.1, falsafa ya upandaji kanisa inajenga juu ya tafsiri ya kanisa na kusudi la kanisa ambalo umelianzisha mapema. Mara unapoelewa kanisa ni nini na kwa nini kanisa mpya utakalopanda litakuwepo, hatua inayofata ni kuamua jinsi gani utakamilisha kazi hiyo.

> Falsafa ya huduma ya upandaji kanisa lazima iwe inatokana na tafsiri ya kibiblia na kusudi la kanisa, badala ya kurudia kueleza jinsi tulivyofanya mambo wakati uliopita.

Wazo la muhimu hapa ni kwamba falsafa ya huduma ya upandaji-kanisa *lazima iwe inatokana na tafsiri ya kibiblia na kusudi la kanisa*, badala ya kurudia kueleza jinsi tulivyofanya mambo wakati uliopita. Kujenga kwenye mapokeo ya mwanadamu, bila kujali ni kiasi gani inamaanisha, haikubaliwi kabisa kuwa badala kwenye kufanya juhudi za kujifunza neno na kufata maelekezo yake.

### B. Mandhali ni Maalumu

Falsafa inayofaa itatokana na mandhali maalumu ambamo itatumika. Hii inahitaji kwamba tufanye utafiti unaofaa katika eneo linalolengwa. Sehemu nyingine ya nyenzo hii inaeleza jinsi ya kubuni na kuchambua utafiti huu. Juhudi hizi za mwanzo katika utafiti na kupanga zinaweza kupunguza sana mda uliopotezwa na juhudi baadaye kwa kutuongoza katika njia sahihi na kutusaidia kuchagua njia sahihi na namna ya kuendea.

### C. Je Watu-Ni kitovu

Majengo, vifaa, njia za usafiri, fedha, na vitu vingine vya kutendea vinatakiwa kufikiriwa katika falsafa ya huduma ya upandaji kanisa. Kwa jinsi hiyo, havitakiwi kabisa kuchukua nafasi kubwa kwenye utaratibu! Lazima kila mara, ikumbukwe kwamba watu ndio mkazo muhimu na kwamba wokovu wao na ukuaji kiroho ndiyo kusudio la juhudi zetu. Falsafa nzuri ya huduma ya upandaji kanisa itahakikisha kuwa tunatimiza mahitaji ya *kanisa* la kweli—watu-badala ya kukazia vitu vya baadaye.

### D. Inatumika Kama Chombo cha Kutathimini

Falsafa ya huduma ya upandaji kanisa, iliyoandaliwa kiusahihi, itakuwa ya kivitendo na ya kutumika. Itatusaidia kuendelea kufanya mambo sahihi katika wakati sahihi, na katika njia sahihi. Tunatakiwa kuona matunda kutokana na juhudi zetu, kwa kuwa tunatumia maamzi sahihi kwa kila hatua ya huduma. Hii ndiyo sababu tunatumia mda kuandaa maelezo.

Kutambua matokeo ya hakika ya hali ya juu, tunatakiwa kuwa waangalifu kuifanya falsafa rahisi, wazi, na ya kueleweka. Timu nzima ya upandaji kanisa inatakiwa kuielewa na kukubaliana nayo. Inatakiwa ieleze ridhaa ya kwa *jinsi gani, kiusahihi, tutakwenda kupanda kanisa hili jipya.*

## IV. KUFANYA FALSAFA YAKO MWENYEWE YA HUDUMA YA UPANDAJI KANISA

Ziada 8A ni karatasi ya mazoezi ya kukusaidia katika utaratibu wa kuandika falsafa ya huduma ya upandaji kanisa. Mda mwingi wa darasa unatakiwa utumike katika utaratibu huu. Kama una timu ya upandaji kansia, unatakiwa urudie utaratibu huu na timu kufika katika falsafa ambayo wote mtakubaliana na kwa moyo wa umoja kufanya kazi pamoja.

## V. MFANO WA FALSAFA YA HUDUMA

Kielelezo 8.2 kinachofata ni mfano wa falsafa ya huduma ya kanisa. Siyo maalumu kwa kanisa jipya lililopandwa, na kwa hiyo maelezo yako kwa namna fulani yatakuwa tofauti. Inaweza, kwa jinsi hiyo, kusaidia kama kiongozi kwako unapoandika ya kwako.

Unapokuwa unasoma katika mfano huu, tambua msisitizo kwa watu, kuabudu, na ukuaji wao wa kiroho. Ni kwa njia zipi zingine maelezo haya ni falsafa nzuri? Ni eneo gani linahitaji maraekebisho, kutokana na kanuni ambayo tumemaliza kujifunza?

**Kielezo 8.2 Mfano wa Maelezo ya Kanisa la Mtaa**

**MFANO WA MAELEZO YA UMISHENARI**

*Kanisa la Jumuia ya Smithville lipo kwa:*

**1. KUMTUKUZA Mungu Baba, Mwana na Roho Mtakatifu**

a. Kutukuza, Maombi, kuabudu na kusherehekea utukufu wa Mungu, utakatifu, ukweli, uzuri na upendo.
b. Ushirika na Yesu Kristo anayetupenda, Mwokozi wa ajabu, Bwana na Mfalme.
c. Kuwa wamoja na utukufu unaletwa na uwepo wa Roho Mtakatifu na kuonyeshwa kwa ushirika kupitia matunda ya roho na vipawa.

**2. KUANZISHA jumuia inayojali kupitia waumini**

a. Kushauri mazingira ya upendo, kukubalika na msamaha
b. Kuanzisha ukarimu, kujali na uhusiano unaokubaliwa
c. Huduma na kujitoa kutimiziana mahitaji

**3. KUWAANDAA waumini kwa huduma yenye mafanikio kupitia**

a. Mahubiri na mafundisho ambayo kwa uaminifu yanaeleza neno la Mungu wakati likihusishwa kwenye mambo ya siku hiyo na mahitaji ya watu.
b. Mafundisho, ugunduzi, utambuzi, maendeleo na matumizi ya vipawa vya Roho kwa kila muumini.
c. Mafundisho ya huduma na kuwaandaa waumini kujua mapenzi ya Kristo, Kuona nguvu za Kristo na kufanya kazi ya Kristo.

**4. KUONGEZA habari njema za Kristo ulimwengini kwa**

a. Kuifikia jamii katika maeneo yanayozunguka iliyo kubwa, wepesi na huruma kwa kutumia mifumo bunifu ya uinjilisti na mawasiliano, kutangaza kwamba watu lazima watubu, wamukili Kristo, waweke matumaini yao ndani ya Mungu kwa njia ya Kristo, wamkuabali yeye kama mwokozi na kumtumikia kama mfalme wao katika ushirika wa kanisa lake.
b. Kumjali mtu mzima wakimuhudumia kihisia, kimwili, mahitaji ya kijamii na kiroho kuyaleta katika umoja katika jumuia zetu.
c. Kujitoa kwa upandaji wa kanisa na kuweka uhai wa kanisa ulimwenguni kote.

### MASWALI YA KUTAFAKARI

- Ni jinsi gani falsafa ya huduma inasaidia wapanda kanisa?
- Ni jinsi gani falsafa ya huduma ni ya kibiblia?
- Nini falsafa ya huduma inakuwa nacho?

## UTEKELEZAJI WA AZIMIO

Malizia Ziada 8A, “Kuanzisha Falsafa ya Huduma ya Upandaji Kanisa.”

## VYANZO


- DeWitt, Larry. *Unpublished Notes from CPR2000*, Calvary Community Church, 1985.
- Fuller, Charles E. *How To Plant A Church; Advanced Seminar*. Church Growth Institute. 1986.
- Logan, Robert. *Beyond Church Growth*. Grand Rapids, MI: Revell, 1989.
- Martin, Robert W. *Notes on a Philosophy of Ministry*. Camino Real Community Church. 1993.
- Morris, Linus J. *The High Impact Church*. Thousand Oaks, CA: Christian Associates International, 1998.

**KANISA**
***ZIADA***

# 8A

# Kuanzisha Falsafa ya Huduma ya Upandaji Kanisa

**UTANGULIZI**

Ili kuanzisha falsafa wazi ya huduma ya upandaji kanisa, unahitaji kufikiria yafuatayo:

- Unatakiwa uwe unaelewa wazi juu ya nini Mungu ameliitia kanisa kuwa (Maelezo ya Kusudi) na kile Mungu anacholiitia kanisa lako mpya kuwa na kufanya. Ni nini Mungu anakutaka kukamilisha katika miaka 3-5 ijayo kama kanisa mpya?
- Unatakiwa kuwa na ufahamu wa watazamaji unaokusudia. Ni watu gani unatafuta kuwafikia?
- Ni baadhi ya miundo gani unaweza kutumia kuanzisha kanisa lako mpya (huduma ya kuabudu, vikundi vidogo, shule ya Biblia, Maombi ya utatu ya kuombea watu waokoke, n.k. )
- Ni nini vipawa, uwezo, na udhaifu wako na wa timu yako?

## I. MASWALI YA KUFIKIRI KWA KUANZISHA FALSAFA YA HUDUMA

Jibu maswali yafuatayo na wengine katika timu yako-ya upandaji kanisa

**A. Ni maneno yapi matatu unayopenda kutumia kuelezea kanisa mpya unalopanda?**

**B. Ni watu wa namna gani wapo katika jumuia unayotaka kuifikia? Ni watu wa aina gani watakuwa sehemu ya kanisa lako?**

**C. Ni nini kitalifanya kanisa hili kuwa tofauti**

**D. Ni kitu gani kingekuwa kivutio zaidi juu ya kanisa lako?**

**E. Ni nini kuhusu kanisa lako ambacho kitawaita watu unaotaka kufikia katika mji/kijiji?**

**F. Ni kwa nani kanisa lako litakata rufaa?**

**G. Ni kwa nani ungependa kanisa lako likate rufaa?**

**H. Ni vipindi gani na shughuli zinaweza kuwa na mafanikio kwa kanisa? Ni kwa jinsi gani utapima mafanikio haya?**

## II. TOFAUTI ZA KIPEKEE JUU YA KANISA LAKO

Ni nini cha kipekee au tofauti juu ya jinsi kanisa lako linavyofanya linachofanya (litakachofanya) katika maeneo yafuatayo—kuabudu, mafundisho ya maandiko, uinjilisti, ushirika, uongozi, kazi za vijana na watoto, mahusiano ya jumuia, huduma za kijamii, misheni, elimu, fedha, rasilimali, majengo na mengineyo.

## III. MTINDO WA HUDUMA

Katika aya moja au mbili, eleza mtindo wa huduma unayowazia kwa ajili ya kanisa lako. Ni nini itakuwa kanisa lako la pekee “hadhi?”

## IV. Thamani

Ni vitu gani vinalithamanisha kanisa lako? Ni mvuto gani utaelekeza juhudi za huduma yako katika miezi iyayo na miaka? Orodhesha angalau thamani 10 sasa.

## V. ELEZEA FALSAFA YA HUDUMA YAKO

Katika aya mbili, jaribu kuandika maelezo ya falsafa ya huduma yako ambayo yatakuwa na vipengele kutoka katika karatasi hii ya mazoezi. Unaweza kubuni maneno machache ya kukumbukwa ambayo yanatwaa falsafa ya huduma yako ?

| |
|---|
| *Falsafa yangu ya huduma ya upandaji kansia :* |
| *Maneno ya kukumbuka ya kanisa langu:* |

## VI. JADILI NA LINGANISHA MAELEZO YAKO NA YA WENGINE

Kumbuka kwamba hakuna hali mbili zinazofanana, na kwa hiyo hakuna falsafa mbili ambazo zitafanana, jadili na linganisha maelezo yako na waliofundishwa na wengine. Kisha jadili na viongozi wa kanisa na wajumbe wa timu yako ya upandaji kanisa. Fanya marudio ya maelezo hayo mara kwa mara, na yatumie wakati wa utaratibu wa upandaji kanisa kutathimini kama unafanya kitu sahihi au la na katika njia sahihi.

# TABIA YA KIROHO

TABIA YA KIROHO

SOMO LA 6

# Kuishi Kama Wana Badala ya Mayatima

## WAGALATIA 4:1-7

☞ **Kusudi la Somo**

Kusudi la somo hili ni kumsaidia mpanda kanisa kuwa mnyoofu katika uhusiano wake na Mungu, anapouelewa ukweli na maana halisi ya kurithiwa na Mungu.

☞ **Wazo Kuu**

- Maisha kama mtoto yatima yanakufanya kuwa na mashaka na kujitegemea mwenyewe.
- Maisha kama mtoto wa kiroho wa Mungu yanapelekea kutembea na Mungu kwa shukurani na imani.

☞ **Matokeo Yanayotarajiwa**

Wakati yaliyoma katika somo hili yanapoeleweka, kila mshiriki anatakiwa:

- Kufahamu kuwa wamerithiwa na Mungu na kuwa kama wasichana na wavulana wapendwao.
- Kufahamu jinsi wanavyoweza kurudi kwenye uyatima kitabia.
- Kuwa na ujasiri zaidi wa upendo wa Mungu kama wana , wanaoweza kushughulikia udhaifu, mashaka, na hofu kwa misingi ya uhusiano wao na Mungu na si kwa misingi ya matendo.
- Kuinjilisha kwa ujasiri na kuendeleza kazi ya upandaji kanisa na siyo kama hao walio peke yao, lakini kama wana wapendwao walio katika ushirika na baba yao wa mbinguni.

☞ **Ushauri kwa wakufunzi**

Wapatie wafunzwa “zoezi la kutokulipiza kwa kila jambo baya wanalotendewa” katika siku ya kwanza (linalopatikana katika sehemu ya mwisho wa somo hili), kisha tazama baada ya siku chache kuona ni kwa jinsi gani wamelitekeleza. Zoezi hili kifupi ni kutusaidia kuwa waminifu zaidi juu ya nguvu ya dhambi ndani yetu na hitaji letu la kweli la neema na nguvu.

Tafadhali tambua: neno ‘wakiume’ halijakusudiwa kuondoa wakike. ‘wakiume’ linatumika kwa sababu Paulo analitumia katika barua zake kwa Wagalatia. Wakike pia ni watoto wa Mungu.

Itasaidia wewe mwenyewe kushirikisha uzoefu wako unaohusiana na nyenzo hii, Uhusike!

### UTANGULIZI

Neno la Mungu linatufundisha kuwa wote tuna muumbaji anayetaka kuwa baba anayetupenda (Mt 6:26, 32). Kwa sababu ya kupenda kwetu kuasi, tumemwacha na kuishi maisha yetu tunavyotaka. Uamzi huu wa kumwacha Mungu unaathiri sana tabia yetu na kufikiri kwetu. Kwa njia nyingi, kunatusababisha kufikiri na kutenda kama yatima.

Katika somo hili, tutafikiri kwa pamoja jinsi tunavyofikiria na kutenda kama yatima, hata kama wakristo. Tutaangalia Wagalatia 4:1-7, ambayo inaeleza aina ya uhusiano amabao kila mkristo anaoingia na Mungu. Na mwisho, tutajifunza jinsi ya kuishi kama wana tulio wa baba wa mbinguni na milele wanaopendwa naye.

### I. MAISHA KAMA YATIMA

Kama umewahi kutembelea kituo cha watoto yatima na kupata mda mzuri wa kuwajua watoto hawa maalumu, unaweza ukawa umegundua baadhi ya vipande vya kufikiri na kutenda ambavyo ni vya kawaida miongoni mwao. Hapa kuna vichache.

### A. Mayatima wamejawa sana na hofu na mashaka makuu

Kutojaliwa, na wakati mwingine kuachwa, na wazazi kunaacha yatima na kutokuwa na uhakika juu ya maisha na pengine kinachoweza kutokea baadaye. Kwa wengi wetu, kutokuonekana kwa mbele si kitu tunachohofia (Sana), lakini kwa mtoto ambaye janga limeshamtokea (mama na baba hawapo kwa ajili yake), mbeleni kunaonekana kuogopesha sana.

### B. Mayatima wanaishi kwa kujijali kusikokuwa kwa kawaida

Kila yatima analinganisha alichonacho kwa kile walichonacho watoto wengine. Kwa sababu hii, 'mama wa nyumbani' anaeleza kuwa kila wakati zawadi inapotolewa kwa mtoto mmoja, ilipaswa kutolewa kwa kila mtoto. Hata hivyo, watoto wanapendelea rangi fulani, na wivu wa ajabu unatokea wakati mtoto mmoja "anapopata rangi maalumu."

### C. Mayatima wanabeba hisia kali za upweke

Yatima waliowekwa vituoni wanahisia kwamba kwa sababu mama na baba wamewaacha (au wamechukuliwa), kwamba si wa mtu yeyote. Wa kuwazaa, 'hasa' wamewaacha, hakuna hata mmoja "wanayeungana" naye na ni vigumu kwa hawa yatima kuamini kama kuna mtu anawajli kweli kweli.

## II. WAKRISTO WANAOFIKIRI NA KUTENDA KAMA MAYATIMA

Na sasa ngoja tufikirie tunavyofikiri na kutenda kama yatima wenyewe. Yatima, kama tulivyosema, anajisikia upweke ulimwenguni. Ni wenye hofu nyingi na mashaka. Bila baba wala mama wa kuwatunza, wanajali mahitaji yao wenyewe. Wanajisikia kama wanahitaji kujilinda wenyewe. Je hii inaonyesha chochote kuhusu maisha yako?

Pengine tunajisikia hivi wakati maisha yanapoonekana kuanguka au kitu fulani kutokuwa sahihi. Ni jinsi gani tunavyoitikia magumu yetu? Tunafikiria nini? Hatuogopi na kuchanganyikiwa? Wakati mwngine hatufikirii mambo yanakwenda vibaya kwa sababu Mungu na kujali kwake kwingi ametusahau? Tunaanza kuogopa au tunakatishwa tamaa na kukata tamaa. Mara nyingi, tukijisikia kana kwamba hatueleweki, tunamlaumu mtu mwingine kwa ajili ya matatizo yetu. Tunajiona kana kwamba ni "waathirika." Wakati mwingine, tunachanganyikiwa na kuyachukulia mambo mikononi mwetu wenyewe kwa kuweka utawala mkali. Kwa utawaala huu, tunajaribu kuukataza ulimwengu kuanguka zaidi. Katika majibu yote haya tunaonyesha kiburi chetu au kukosa imani kwa yale Mungu aliyodhihirisha kuhusu yeye mwenyewe na uhusiano wake na sisi. Tunageuka kuwa yatima wa kiroho.

**Mfano**

Mwanamke alikuwa amekuwa mkristo, lakini hakuwa na hakika na upendo wa Mungu kwake. Moja ya sababu ilikuwa ni tukio la utotoni la baba yake. Alipokuwa mdogo sana, yeye na dada yake walikuwa wanaanika nguo nje. Hakuwa anafikia kamba ya kuanikia nguo, kwa hiyo aliamua kutundika shati jeupe la baba yake kwenye taili ya gari dogo , iliyokuwa na kutu. Hakika, shati ilipokauka, lilikuwa limewekewa kutu na taili hiyo. Shati lilikuwa limeharibiwa. Baba yake alipogundua, alimchukia bila kujali.

Mtoto huyu hakuwa amefanya kosa lolote akilini mwake. Alitundika shati kwa kusudi jema, bila kujua matokeo ya kuliweka kwenye tairi. Baba wengi wangemsamehe mtoto kwa kosa kama hilo au angalau angemkaripia kidogo sana. Hata hivyo baba huyu alimkaripia kana kwamba hakutii kwa makusudi, au ameasi dhidi yake. Alikua akijua kwamba baba hakuwahi kumpenda.

Hivi ndivyo mara nyingi tunavyomtazama Mungu. Tunafikiri ametukasirikia, kwamba yuko mbali, kwamba anasubiri kutuadhibu. Tunajisikia kana kwamba hatujawahi kukubaliwa na kupendwa naye kwelikweli. Mtazamo wetu kwa Mungu ni mojawapo ya wa kisheria, hakimu asiyejali. Uhusiano wetu na yeye unaonekana kuwa mwembamba na usio wa uhakika, kulingana na jinsi tunavyofanya.

Lakini hivi sivyo ambavyo uhusiano wetu na Mungu umeelezewa katika Wagalatia 4. Hatutaacha kufikiri na kutenda kama yatima mpaka tutakapoamini maelezo ya Mungu ya uhusiano wetu na yeye. Tunahitaji kuelewa msingi wa uhusiano wetu, na maana halisi ya uwana wetu. Tunaporudi kwa Wagalatia 4 ngoja tufikilie ulinganifu huu wa uhusiano wetu na Mungu (soma Gal 4:1-7).

## III. UWANA WETU NA MUNGU

### A. Ulinganifu wa mwana "aliyekua"

Mtume Paulo anakabili kosa ambalo wakristo wa Galatia wameangukia. Tunapoliangalia andiko, tunaona wagalatia wameanza kusahau jinsi walivyoingia katika uhusiano sahihi na Mungu, jinsi ambavyo walitakiwa waendelee na uhusiano huu, na jinsi ambavyo wangepokea ahadi ya Mungu. Wamerudi nyuma kufikiri kwamba wamepokea wokovu na kukubaliwa na Mungu, angalua sehemu tu, kwa sababu ya utii wa sheria za Mungu. Paulo anawafundisha tena, kwamba ni kwa imani peke yake katika injili kwamba wamehesabiwa haki mbele za Mungu na kwamba wamepokea Roho Mtakatifu. Kwa misingi ya imani kwa ahadi zilizofanywa na Mungu kwa njia ya Kristo, wanaona baraka zake za wakati huo na kazi yake katika maisha yao. Anamalizia mwisho wa ukurasa wa tatu kwamba sheria ilitolewa na Mungu kudhihirisha hali yetu ya dhambi na kutuongoza kwa Kristo. Baada ya kuiamini injili na tukiwa ndani ya Kristo, hatuko tena chini ya sheria hiyo. Sasa tuko wana wa Mungu.

Kisha Paulo, katika ukurasa wa nne anaelezea kwa kina jinsi tulivyorithiwa na Mungu na uwana wetu kweli kweli unachomaanisha. Anatumia matendo ya kawaida ya siku hizo kutupa picha ya uhusiano huu tulionao sasa na Mungu:

Mwanae alipokuwa mdogo, ingawa alikuwa mrithi wa urithi wa baba yake, aliendelea kuwa chini ya waangalizi na mawakili, waliowajibika kumlea na haki za mtoto. Wakati wa kipindi hicho, kijana hakuwa na haki ya kufanya biashara au kufanya maamuzi ambayo yangehusu shamba la baba yake. Katika akili, hakuwa tofauti na mtumwa. Kwa kipindi fulani ambacho kilionyeshwa na baba yake, vizuizi hivi viliondolewa, na shamba lilikabidhiwa kwa kijana kulitawala alipoona ni sawa. Katika kipindi hiki, mrithi alikuwa kijana aliyekua "anayestahili." Hivi ndivyo tunavyoelezewa katika uhusiano wetu na Mungu. Tumekua, ni vijana tunaostahili. Sasa, hili linamaanisha nini kwetu?

### B. Maana ya ulinganifu huu

Kama mtume Paulo anavyoelezea, tumekandamizwa katika kifungo kwa kanuni ya asili ya ulimwengu. Kwa Muyahudi, sheria ya Musa inamkandamiza katika kifungo na kumlaumu, kuzuia ahadi za Mungu kutokupokelewa. Mataifa pia walipata lawama kwa kushuhudiwa na dhamiri zao (Rum 2:14-15) kutokana na kawaida ya dini na maadili yalivyoundwa. Kanuni iwayo yote ambayo tunaishi chini yake mara ya kwanza, kanuni hizi zinatushitaki udhaifu wetu na kutokufaa kupendwa na Mungu. Tumewekwa nazo kwenye kifungo na kujihisi lawama.

> Mungu siyo tena hakimu kwetu ila ni Baba anayetupenda.

Lakini ndani yaYesu, Adhabu ya dhambi zetu imesamehewa kabisa. Tumeondolewa katika kifungo cha lawama (Rum 8:1). Kwa hiyo, hatuwezi kuendelea kujiweka chini ya kifungo hiki. Tunatakiwa kuamini kwamba tumewekwa huru, tumeshamilikiwa na Mungu kama wana walio na haki; kupokea ahadi zote walizopewa wote waliokombolewa na Yesu Kristo. Kutuhakikishia kuwa kutolewa huku kumetokea, Mungu amemtuma Roho wake kukaa ndani yetu, kuziamsha nafsi zetu kuwa shauri la kulaumiwa limeondolewa. Mungu siyo hakimu tena kwetu lakini sasa ni Baba anayetupenda. Paulo anatumia neno "Abba" ambalo kwa siku hizo lilikuwa neno la kupendeza zaidi kuelezea Baba (Rum 8:15-17). Maelezo yetu ya siki hizi "baba" Papa" linagusa wazo la neno hili linaloeleza kupendeza kwa Mungu kwetu. Hukumu ya Mungu imegeuzwa kuwa rehema. Hatulaumu tena, lakini ameturithi ili kwamba atupatie ahadi zake zote.

Tunaweza kuishi kwa uhakika na ujasiri kwa sababu ya jinsi alivyo baba yetu. Hakuna tena kutokujiamini, hakuna sababu ya kuhakikisha kustahili kwetu. Hakuna hofu ya adhabu ya kikatili. Hakuna upweke tena. Tuna baba anayetupenda ambaye hatatuacha. Anatupenda.

## IV. JINSI TUNAVYOSHINDWA KUELEWA UWANA WETU

> Injili ndiyo msingi wa uwana wetu. Tuanposhindwa kuitambua injili, tunashindwa kuelewa uhusiano wetu kama wana wa Mungu.

Kwa nini ni kwamba sisi, wavulana na wasichana waliorithiwa, mara nyingi tunajikuta tukitenda kama yatima? Kwa nini tunajisikia upweke kabisa, wenye hufu kuu, na wanaojifikiria? Ni kwa sababu tunaifanya injili ya Yesu Kristo kuwa hafifu na uhusiano kwa maisha yetu. Injili ni msingi wa uwana wetu. Tunaposhindwa kuitambua injili, tunashindwa kuelewa uhusiano wetu kama wana wa Mungu. Tunafanya haya kwa njia tofauti tofauti.

### A. Kutoitambua Injili Kwa Ajili ya Kiburi

Injili ni habari njema lakini pia ni dawa kali ambayo inaweza kuwa vigumu kuinywa. Inatunyenyekesha, kutukumbusha kuwa tu wenye dhambi ambao hatuwezi kujiokoa. Hata kama wakristo, mara nyingi tunajiinua juu ya wengine. Hata tunadhani kuwa hatuhitaji msaada wa Mungu. Tunaishi kwa ajili ya utukufu wetu na kwa kusudi la ubinafsi wetu. Tunaishi kukamilisha malengo yetu wenyewe, kujiinua wenyewe. Kama baadhi ya shughuli au mtu hachangii kwenye agenda zetu, kisha tunakuwa hatutaki tena kujishughulisha naye. Kujitegemea kwetu kunamlazimisha kutuacha kuhangaika peke yetu. Tunakuwa yatima kwa sababu ya kiburi chetu.

Ukweli ni, tuna tatizo kubwa tunapoweka ujasiri katika uwezo wetu (katika “mwili” – Gal 3:3). Tunapokuwa wenye kiburi, tunajaribu kuanzisha utakatifu wetu badala ya kutegemea utakatifu wa Kristo. Dalili moja ya hili ni kufikiri mara kwa mara jinsi wengine watakavyoyachukulia matendo yetu.

Kwa mfano, tunafanya hivi hata katika eneo la kupenda familia zetu. Fikiria mtu anayedhani “naweza kumpenda mke wangu na watoto, jinsi gani itakavyokuwa vigumu?” Anapoweka ujasiri katika uwezo wake, anafanya yale ambayo anadhani yatamfurahisha mke wake. Siku moja, baada ya kuja nyumbani na zawadi ya maua kwa mke wake, anamshika na kumtikisa mkono na kusema, “mpendwa, najisikia kama hunipendi. Ninajua kuwa tunakuwa na marafiki tutakaokula nao chakula jioni. Kila tunapokuwa na mtu nyumabani, unaninunulia maua. Kujionyesha (kujiinua—mwenyewe) nia ya kujionyesha mbele za watu kama mwamnaume anayependa ilikuwa imejificha ndani ya moyo wa huyu mwanaume., kwa hiyo hakugundua hata alichokuwa anafanya. Kama tukiangalia kwa karibu jinsi tunavyowapenda wake zetu au waume zetu, tungeweza kuona pengine ni jinsi gani ilivyo dhaifu.

Tumezaliwa upya na Roho Mtakatifu na tumewekwa huru kutoka utumwa wa dhambi. Roho sasa anakaa ndani yetu kutusaidia kushinda dhambi. Kwa jinsi hiyo, tumekosea kama tunadhani kuwa hii inamaanisha mwili kwa namna fulani umeoshwa (Rum 7:17-18) na hatuwezi kushindana tena na haja yake ya uovu. **Lazima tuwe waaminifu sana na Mungu juu ya dhambi zetu.** Bado tuna tatizo kubwa la mwili wetu, na lazima tuvunjike kwa undani juu ya hili. Tunahitaji kukua katika kumtegemea Roho Mtakatifu kutusaidia kushinda msukumo mkubwa wa uovu ndani yetu. Nguvu ya Roho inaweza kutolewa tu tunapogundua hitaji la msaada wake, lakini kiburi kitatufanya tusiweze kugundua hitaji hili.

### B. Kutotambua Injili Kutokana na Kutoamini

Njia nyingine ambayo hatutambui injili ni kwamba tunaacha kuamini ahadi za Mungu za neema kutokana na kifo cha Kristo msalabani pekee yake. Kwa upendo, wengi wetu tunatafuta kumtumikia Mungu na kumheshimu. Tunashindwa, na kukumbwa na kushindwa kwetu. Tena, ni lazima tutubu- kwa ajili ya dhambi yetu ya kutokuamini. Lazima tuendelee kuamini ukweli wa injili, ambayo inatuambia kwamba ni kwa neema, na hakuna sababu nyingine, tumefanywa watoto wa Mungu.

Lazima tuwe waaminifu zaidi juu ya dhambi zetu na tuache kutoitambua injili kama tunataka kujua asili ya kweli ya upendo wa Mungu kwetu na utajiri wa baraka ya uwana wetu na yeye. Hii ni muhimu. Vinginevyo, tunaendelea kujisikia upweke, tukifikiria kuwa maisha yote yako juu yetu. Kushindwa kwetu kutaendelea kututesa, hatia yetu inapogeuka kuwa lawama. Huduma yetu kwa Mungu itakuwa uchaguzi wa kitumwa, uzito ambao hatuwezi kuubeba. Tutakuwa wasio na shukurani kwa Mungu na wengine, wasiotikishwa kwa ukweli kwamba Yesu Kristo aliteseka na kufa kwa ajili ya dhambi zetu ili kutufanya wana waliojaliwa.

## MASWALI YA KUTAFAKARI, MARUDIO NA MATUMIZI

- Jinsi gani huitambui dhambi yako?
- Jinsi gani huitambui injili?
- Ni kwa njia zipi unatenda kama yatima?
- Mungu analaumu watoto wake kama anavyowafanya hao wasiomjua?
- Kwa nini Mungu ametupa upendeleo wa uwana?
- Kwa jinsi gani kuufahamu uwana kunatusaidia kuwa waaminifu juu ya dhambi zetu?

## UTEKELEZAJI WA AZIMIO

***"Agizo la ulimi"***

Kwa siku mbila zijazo, usiongee upuuzi, usiseme vibaya juu ya mtu, usilalamike, usijitetee mwenyewe mtu anapokuambia vibaya, na usijivune kwa ajili ya mafanikio yako. Sema mazuri tu kwa ajili ya wengine, mshukuru Mungu kwa kila jambo, kiri kwa uaminifu unapokuwa na makosa, na ujivune tu kwa ajili ya udhaifu wako.

Zoezi la ulimi litakusaidia kuona matokea ya nguvu ambayo dhambi bado inayo katika maisha yetu na mahitaji yetu yanayoendelea ya neema ya Mungu. Baada ya zoezi hili utakuwa na shukurani ya ndani ya jinsi Mungu alivyokufanya mwana na siyo kwa ajili ya utii wako, lakini kwa ajili ya ukombozi wa Yesu kwa ajili yako. Hili ni zoezi la maisha yote, lakini kwa uangalifu timiza hili kwa siku mbili zijazo.

TABIA YA KIROHO

SOMO LA 7

# Kujifunza Kuwa Wana

☞ **Kusudi la Somo**

Kusudi la somo hili ni kusogea kwa undani kwenye matumizi ya uwana wa waumini na Mungu. Kivutio cha kukua kiroho na huduma lazima vitoke kwenye moyo wa upendo na shukurani kwa Mungu badala ya hofu na hatia.

☞ **Wazom Kuu**

- Moyo mzito unaweza kuwekwa huru
- Moyo wa kiburi unaweza kubadilishwa kuwa moyo wa ushirika na baba
- Moyo wa ubinafsi unaweza kujifunza kuwapenda wengine

☞ **Matokeo Yanayotarajiwa**

Wakati yaliyomo katika somo hili yanapoeleweka, kila mshiriki anatakiwa:

- Kuelewa maana hasa ya kurithiwa na Mungu
- Kuelewa kwa vitendo, kuonyesha kufikiri kwa kila siku kama mwana dhidi ya yatima.
- Kuishi na kutumika kwa uthibitisho mkubwa wa uwepo wa Mungu na ushirika.
- Kuishi na kutumika kwa huruma mpya kwa watu, kuonyesha neema ya Mungu kwao
- Kumtumikia Bwana kwa nguvu nyingi, na kwa upendo mkuu

☞ **Ziada**

7A Yatima Dhidi ya Wana

☞ **Ushauri kwa Wakufunzi**

Kama kwenye somo la mwisho, neno “wana”limetumika sana katika somo hili halijakusudiwa kuwatenga wanawake. Neno “wana” limetumika kwa sababu Wagalatia wanalitumia neno. Wanawake pia ni watoto wa Mungu.

**UTANGULIZI**

Wazo la kurithiwa ni la kimusingi kwa jinsi Mungu anavyohusiana nasi. Jinsi muumini anavyolielewa hili lina matokeo ya kila siku juu ya anvyofikiri, matendo ya uhusiano wa sasa na Mungu. Haya ni – mafunzo kwa undani juu ya maeneo na matumizi ya kurithiwa na Mungu.

Ili mtu kujua kwa undani kurithiwa kwake na Mungu (ambako kumemfanya muumini kuwa “mwana wa kujaliwa”), ni muhimu kufikiri kwenye mkao wa kawaida wa akili uliopo kufikiri siku kwa siku. Ni mara ngapi tunafanya kama yatima badala ya kama watoto wa Mungu? Ni muhimu kwamba Roho Mtakatifu anafungua macho yetu kwa mambo haya.

Kuna maeneo matatu ya msingi ambayo tunaweza kujichunguza kama tunaishi kama yatima au wana. Fikiria yafuatayo:

## I. MOYO ULIOLEMEWA SANA DHIDI YA MOYO ULIOWEKWA HURU

Fimbo ya kwanza “ya kupimia” ni kama endapo au la una moyo hasa uliolemewa sana na kujisikia kushindwa, au moyo uliowekwa huru. Ni wazi, kuna sababu tofauti kwa nini moyo wa mtu

unaweza kuwa umelemewa sana, lakini katika mandhali hii, moyo mzito unasababishwa na uzito wa hatia zetu na kujihisi kutokufaa.

Tunapokua katika maisha ya ukristo, tunakua katika ufahamu wa dhambi. Mfalme Daudi alisema, "Ninajua makosa yangu na dhambi yangu iko mbele yangu daima" (Zab 51:13). Kwa mkristo mchanga, inaweza kumteka kujisikia uzito na hali halisi ya dhambi yake.

Kwa mfano, wakati "Sergei) alimrudia Mungu kwa mara ya kwanza na kupokea msamaha wa dhambi zake kwa njia ya Yesu Kristo, alijisikia furaha kubwa. Alikuwa kama mtu aliyeachiliwa kutoka gerezani, na haja yake kuu ilikuwa kumpendeza Mungu kwa kila kitu alichofanya. Haikuchukua mda mrefu kabla hajashindwa na jambo fulani na kukatishwa tamaa sana. Dhambi yake ilimfunika kiasi kwamba kwa mda wa wiki nyingi, alikuwa amekata tamaa na hata kudhoofika. Alihangaika kuamini kwamba Mungu bado anampenda na kumkubali. Hakuweza kutulia mpaka mwishoni alipogundua ukweli juu ya uhusiano wake na Mungu.

Katika Warumi 8, Mungu anatuambia anachowafikiria watoto wake, hata wanaposhindwa. Maswali sita yameulizwa: "Basi tusema nini juu ya haya? Kama Mungu yuko upande wetu, nani atakuwa juu yetu? Yeye asiyemwachilia mwana wake mwenyewe, bali alimtoa kwa ajili yetu sote-atakosaje kutukirimia mambo yote pamoja naye? Ni nani atakayewashitaki wateule wa Mungu? Ni Mungu anayehesabia haki. Ni nani anayehukumu? …Ni nini kitakachotutenga na upendo wa Kristo?" (Rum 8:31-35).

Kila mara mtu anapouliza maswali sita katika mstari, ni wazi hatafuti jibu. Ni swala sawa hapa katika fungu hili. Jibu ni wazi: Mungu hatafuti jibu, kutoka kwa mwanadamu, lakini anatoa maelezo kwake. "ninakupenda, sikulaumu, na hakuna kitu kitakachokutenga na upendo wangu."

> Mungu hawezi kamwe kutokupenda watoto wake.

Azimio hili lilikuwa wazi kwa Sergei mwisho alipoona msingi wa upendo wa Mungu kwake katika mstari wa 39. Mungu anasema hakuna kitu "kitakachotutenga na upendo wa Mungu ulio *katika Kristo Yesu Bwana wetu."* Kifungu hicho kidogo cha mwisho kinatoa msingi wa upendo wa Mungu usiobadilika. Unatokana na Kristo Yesu Bwana. Siyo kwa waumini, Lakini ndani yake kwa sababu ya kile alichofanya badala yetu. Sergei aligundua kwamba kama Mungu ilikuwa asimamishe kumpenda, angekuwa anakataa Yesu Kristo alichokamilisha msalabani. Angetakiwa aseme kwamba kifo cha mwanae hakikutosha! Mungu asingesema hivyo, na kwa hiyo, Mungu hawezi kuacha kuwapenda watoto wake.

Wakati Sergei alipogundua hili, alikuwa tena kama mfungwa aliyewekwa huru. Mzigo wa kushindwa kwake uliinuliwa, na alipewa uhuru mpya kuzifahamu dhambi zake na kisha kuzing'oa, kudai damu ya Kristo na utakatifu wake yeye mwenyewe. Nyuma, Sergei alikuwa ametubu kwa ajili ya dhambi zake , lakini hakuendelea kuamini katika kazi iliyokamilika ya Kristo msalabani. Kwa ubishi, aligundua kuwa kiburi chake kilimfanya asifanye hivi. Ilikuwa Vigumu kwa Sergei kukukubali kwa Mungu kuwa hitaji lake la Kristo lilikuwa kubwa kama ilivyokuwa mwanzo alipoamini. Alikubali kwa unyenyekevu hitaji lake, furaha tena ikaujaza moyo wake. Hakuwahi kujisikia kwa undani hivyo na kupendwa bila masharti.

Mungu anataka kuweka huru moyo wa kila muumini kwa aina ya upendo huu. Upendo ambao hatuustahili; upendo usio wa masharti, upendo kupita kiasi, ambao watu hawawezi isipokuwa kumurudishia Mungu kumpenda.

Ni rahisi kujisikia kutofaa na kutostahili. Kwa jinsi hiyo, Mungu anaendelea kuonyesha upendo hata hivyo. Na kama moyo wa mfungwa haukuwekwa huru na upendo huu, kisha imani yake kwa kazi ya Yesu msalabani ni ndogo sana. Nafisini, anaikana habari ya injili. Mungu alisema, "Ilikuwa kwa ajili ya uhuru kwamba Kristo ametuweka huru. Simama imara, kisha, na usikubali mwenyewe kulemewa tena na nira ya utumwa" (Gal 5:1). Yesu alisema, "kwa kuwa nira yangu ni laini na mzigo kwangu ni mwepesi" (Mt 11:30). Ni pale tu tunapojenga maisha yetu katika uwana na Mungu ndipo tunapoona uhuru huu. Kama maisha yamesimama juu ya kitu kingine, moyo wetu utaendelea kuwa mzito.

## II. MOYO WENYE MAJIGAMBO DHIDI YA MOYO ULIO KATIKA USHIRIKA NA BABA

Anatoli alikuwa amezaliwa katika mji wa wakristo hasa. Aliungama dhambi zake na kupata wokovu katika umri mdogo. Katika maisha yake yote, ameweza kutunza ushuhuda mzuri wa kikristo bila kujali wote wliojaribu kutompa sifa. Kujitoa kwa nguvu kwa Anatoli kwa Bwana kulimvuta kuwa mmishenari huko Siberia ambako alipanda makanisa matatu miongoni mwa

wabudha katika miaka michache iliyopita. Wengi walimwangalia Anatoli kama kielelezo cha mkristo, na kama Anatoli alikuwa mwaminifu, angekubali kwamba alijisikia kama mmoja wao. Angalau angependa kujisikia kama mmoja wao, ndani ya moyo wake, Anatoli alikuwa akijisikia kwa ajili ya kujitoa kwake kwa nguvu kwa Bwana na alijitwalia kuwa Mungu alikuwa akijisikia kwa ajili ya hilo pia.

Kama ungekuwa, Anatoli, Fikiria Mungu anakubariki kwa sababu umejitoa kwake, unajifikiria sana mwenyewe kwa hali ya juu. Anatoli hakuwa na dhambi ya kutokuamini kama Sergei, lakini alikuwa, pia, yatima. Yatima anajifikiria mwenyewe kuwa anaweza kutatua matatizo. Kinachoonyesha hili kuliko kitu kingine ni mtu kujitegemea mwenyewe ilivyo kinyume na kutegemea (imani) ndani ya Mungu. Kujitegemea mwenyewe kunaondoa ushirika wa Mungu katika huduma. Anaondolewa nje kwa nguvu, na mtu anakuwa hakika peke yake, lakini si kwa sababu Mungu amemwacha. Anakuwa yatima kwa kuchagua.

Matunda ya maisha ya mtu yanaweza kuonyesha muvuto kwenye huduma. Kujitegemea mwenyewe kunazaa matunda ya hofu, kutawala wengine, wasiwasi, kutokupata usingizi mzuri, mashaka, kushindwa na roho ya kulalamika. Kama mtu anadhani anaweza kufanya kila kitu kuwezekana, hiki ndicho atakachozalisha. Anaweza kujaribu kwa bidii, lakini anaishia kuchanganyikiwa kwa sababu mara nyingi hawezi kutatua matatizo yake kwa nguvu zake mwenyewe. Hii inaweza kujionyesha yenyewe kwenye mda uliopotezwa au kukataa maeneo mengine ya huduma au hali ya familia. Kama tatizo la mtu liko akilini mwake mara kwa mara, itaondoa usikivu wake wa kujali wengine. Inaweza pia kusababisha kutokulala usingizi vizuri, kulalamika kwa mara kwa mara, na matatizo mengine.

> Kama watoto wa Mungu, “machafuko” ya huduma yasingetuachisha, kama tunaamini kwamba Mungu anatawala; na kama tunamwekea yeye machafuko yetu.

Ili kuvunja kujitegemea huku, Mungu mara nyingi ataleta changamoto katika maisha ya muumini ili kwamba atafute uwepo wa Mungu na uhusiano katika maisha yake na huduma. Hiki ndicho Yesu alichofanya katika maisha ya wanafunzi wake. Kwa mfano, Yesu alipowalisha elfu tano (Yoh 6), inaonekana kama alikuwa na somo maalumu la kuwafundisha wanafunzi-hasa Philipo, “wapi tununue mkate, kwa ajili ya watu hawa kula?” maandishi yanasema kwamba alimuuliza hili ili “kumjaribu” (Yoh 6:6). Ilikuwa wazi kwamba hakukuwa na chanzo cha mwanadamu cha kuweza kuhudumia umati kama huo wa watu. Alikuwa akimjaribu Philipo kuona kama amejifunza nguvu ya kweli ya Yesu na kumtambua, na kama amejifunza kumtegemea Bwana wake.

Unapokutana na changamoto inayojaribu uhusiano wako na Mungu, Utakavyojibu kutaonyesha mtazamo wako kwa Mungu. Umejawa na hofu au unajua Mungu ni wa upendo, Baba wa kutumainiwa? Umeongeza juhudi zako—pengine kurudi nyuma sana—kwa mtu mwingine ili kuweza kupata kutawala juu ya hali ya machafuko? (Mchungaji mmoja aliacha mengi ya makanisa yake kwa sababu hawakutaka kufanya kile alichotaka wafanye!)

Kama wazo la uwana linatumiwa tunavyofikiri na kufanya kazi katika maisha yetu ya kila siku tunapaswa kuwa watu wa maombi, kuendelea kutumainisha maisha yetu na huduma kwenye ulinzi wa Mungu, tukiwa na uhakika kuwa ana uwezo. Neno la Mungu linasema kwamba Mungu anakazi zilizokwisha andaliwa kwa ajili ya watoto wake kuzikamilisha (Efe 2:10). Kwa kutii kwa maombi, tunakuja kwenye hatua za kile Mungu anachotaka kukamilisha kupitia sisi. Kwa hiyo tunapaswa kuendelea kuwaalika watu kuungana nasi katika maombi, na kuenedelea kumwendea Mungu kwa siri, ili kwamba tuweze kuelewa Mungu alichokwisha kutuandalia.

Mwana ana ujasiri sana kwamba Mungu ni baba yake anayempenda ambaye anajali juu ya fikira zake. Kama watoto wa Mungu, “machafuko”ya huduma yasingetuachisha, kama tunaamini kwamba Mungu anatawala; na kama tunamwekea yeye machafuko yetu.

## III. MOYO WA UBINAFSI DHIDI YA MOYO HURU WA KUPENDA WENGINE

Endapo tunafikiri kama yatima au wana yanapenya katika maeneo mengine. Inaharibu uhusiano wako na wengine kwa hali ya juu. Tunapokuwa tumezungukwa kwanza na matatizo yetu, tunapokuwa chini ya mzigo wa fikira, tunapojiona tuko peke yetu katika ulimwengu huu, tunageuka watu wa kujijali wenyewe.

Fikiria juu ya kijana mdogo aliyeitwa Dennis, yatima wa kirusi. Ni mwenye nguvu nyingi na anayependa kufurahia. Pia ni mwenye utundu mwingi. Mara wakristo walipomtembelea Dennis na yatima wengine wakati wa mapumziko ya mwaka mpya, walileta vitu vichache vya watoto

kuchezea. Kuna mchezo mmoja ambao watoto waliupenda hasa, kwa hiyo wageni waliamua kuwaachia watoto kukaa nao. Dennis alipogundua kuwa watu hao walikuwa wanaacha mchezo huo kwao, alinyakua huo mchezo na kutotaka kuachilia. Yatima wengine waliupigania, na ikabidi wageni waingilie kati, wakachukua mchezo kutoka kwa Dennis na kumpatia mama anayewatunza.

Kilichokuwa kimetolewa bure kwa Dennis na watoto wengine iligeuka kuwa kila mmoja alijisikia kuwa angekimiliki peke yake ili kwamba asiweze kukipoteza. Hawakuweza kuchangia na wengine.

Tunageuka kuwa sawa tunapofikiri baba yetu wa mbinguni hatujali kweli kweli. Tunafanya kana kwamba hana nguvu za kutosha kutunza alichokitoa bure kupendeza mioyo yetu. Mara nyingi, akili zetu za kiyatima zinatupofusha kutokuona baraka ya asili aliyotoa kuiridhisha mioyo yetu safarini. Hata tunapoona baraka zake, hizi zinakuwa miungu katika maisha yetu, kwa sababu tunafikiri ni lazima tuzikumbatie kuzitunza. Hii pengine ni matokeo ya kusikitisha zaidi ya yote. Hatuongozwi kumfurahia mtoaji wa zawadi au kufurahia katika namna anavyotupenda kweli kweli. Kinyume chake, Wakati mali zetu zinapokuwa kitu cha upendo wetu, hatuwezi kamwe kujisikia kama kweli tunapendwa. Umiungu wetu unafanya kama mwizi, kuiba uzoefu wetu wa ajabu wa maisha yetu—ya kupendwa na Mungu mwenyezi.

Hii imetokea katika maishga yako? Akili yako ya kiyatima-imekuacha ukijisikia kutokupendwa? Au unajisikia lazima unga'ng'ane kwa kile Mungu alichokupa kwa hofu ya kukipoteza. Unajisikia huru kukitoa kwa wengine, kwa sababu unaamini kwamba Mungu amekupatia kwa uhuru na kwa wingi?

## SULUHU

Kama unavyoona, jinsi tunavyomtazama Mungu na uhusiano wake na sisi kunagusa hali ya maisha yetu ya kila siku. Mvuto wa kukua kiroho na huduma unatakiwa utoke katika moyo wa upendo na tabia ya utu wa mwana, badala ya tabia ya moyo wa hofu na hatia ya yatima. Ni kwa njia zipi unaona umekuwa ukiishi kama yatima badala ya mwana?

## MASWALI YA KUTAFAKARI, MARUDIO NA MATUMIZI

- Jinsi gani yatima anamuona Mungu?
- Jinsi gani mwana anamuona Mungu?
- Ni kwa sababu zipi tunamuona kwa jinsi maalumu tunavyomuona?
- Jinsi gani tunajua kwamba Mungu bado anatupenda?

## UTEKELEZAJI WA AZIMIO

Katika Ziada 7A ya somo lako utaona orodha ya nakala ya "mayatima dhidi ya wana." Ipitie orodha hiyo, na kisha chukua maeneo matatu ambayo umeona unahangaika nayo. Kwa kila mfano, jinsi gani unaona Mungu akubadilishe? Kisha weka hili katika maombi kwa baba yako wa mbinguni.

**TABIA YA KIROHO**
***ZIADA***

**7A**

# Mayatima Dhidi ya Wana

Soma orodha hapo chini na kisha chagua maeneo matatu ambayo unahangaika nayo zaidi. Fikiri mfano wa kila moja ya maeneo matatu ambapo umepata mahangaiko haya. Kwa kila mfano jinsi gani unataka Mungu akubadilishe? Kisha litoe hili katika maombi kwa *Baba yako* wa mbinguni.

| YATIMA | | WANA |
|---|---|---|
| **KUISHI KWA "KUJARIBU SANA."**<br>**YESU "MSAADA" WA MWILI**<br>***Yoh 14:18 "Sitawaacha kama yatima"*** | | **KUISHI KWA IMANI.**<br>**KRISTO MAISHA YETU! Gal 2:20**<br>***Rum 8:15 "Atupa roho ya uwana"*** |
| Kujisikia upweke; kukosa maana ya ukaribu wa kila siku na Mungu; "uwazi wa kujifikilia binafsi." | 1. | Kuwa na uhakika unaokua kwamba Mungu ni mpendwa wangu baba wa mbinguni (1Yoh 4:16) |
| Kuwa na mahangaiko mengi juu ya "mahitaji wanayohisi;" marafiki, fedha, n.k.; "niko peke yangu na hakuna anayejali." | 2. | Kumtumaini baba na kuwa na ujasiri unaokua katika ulinzi wake; huru kutokana na wasiwasi. |
| Kuishi kwa mafanikio/msingi wa kushindwa; lazima "uonekane vizuri kwa gharama yoyote; inayotokana na –utendaji. | 3. | Kujifunza kuishi katika uhusiano wa -kujifahamu kwa kila siku na Mungu; bila hofu. |
| Kujisikia kulaumiwa, hatia na kutofaa mbele za Mungu na wengine. | 4. | Kujisikia unapendwa, umesamehewa na kukubaliwa kwa ujumla kwa sababu uzuri wa Kristo unanifunika. |
| Kuwa na "imani kidogo" hofu nyingi, hakuna uwezo wa kumtumaini Mungu. "Ninatakiwa kusawazisha." | 5. | Kutembea kwa kila siku kwa matumaini ndani ya mpango mtakatifu wa Mungu katika maisha yangu kama mpendwa, mwenye hekima na mipango bora. |
| Kulemewa kwa kufikiri wajibu usio na mwisho, kujaribu sana kuridhisha, kuteketezwa. | 6. | Maombi ni kitu cha kwanza kukimbilia; "Ninakwenda kumuuliza baba yangu kwanza!" Baba (papa), Baba! |
| Kumwasi Mungu na wengine; mara nyingi baridi kiroho na vigumu kuchochewa. | 7. | Uwezo wa kuwa mtiifu; moyo (aliyevunjika na majuto) laini (Zab 51:17). |
| Anayejitetea; asiyetaka kusikiliza; mugumu anaposhitakiwa kujitakia haki- binafsi (kutoa mashitaka yanayoonekana kweli) | 8. | Aliyewazi kwenye upinzani, kwa kuwa ninafahamu kuwa ninasimama katika ukamilifu wa Kristo, siyo wangu; ninaweza kuangalia nia zangu za ndani. |
| Lazima kila mara awe sawa, salama, kutunzwa, asiyekubali kushindwa; kujitetea; asiyestahimili upinzani; anayestahimili sifa tu. | 9. | Kuweza kuchukua tahadhari—hata kushindwa. Kwa kuwa haki iko ndani ya Kristo, sihitaji kitu kujigamba juu yake, kulinda au kujitetea. |
| Mwenye-ujasiri lakini aliyekata tamaa, aliyeshindwa na asiye na nguvu za Roho. | 10. | Ujasiri-wa Kristo na kutiwa moyo kwa sababu ya Roho anayefanya kazi ndani yangu. |
| "Nitawaonyesha—wewe tazama moshi wangu tu!" "Waliposhindwa wengine." (nguvu zitaweza). | 11. | "Nayaweza yote katika Kristo anitiaye nguvu. |

| YATIMA | | WANA |
|---|---|---|
| **KUISHI KWA "KUJARIBU SANA."<br>YESU "MSAADA" WA MWILI<br>Yoh 14:18 "Sitawaacha kama yatima"** | | **KUISHI KWA IMANI.<br>KRISTO MAISHA YETU! Gal 2:20<br>Rum 8:15 "Atupa roho ya uwana"** |
| Juhudi binafsi; kutegemea vipawa na uwezo kuingia katika maisha na huduma. | 12. | Kujiamini kidogo mwenyewe na zaidi katika Roho Mtakatifu (na ufahamu binafsi- wa kumtegemea kila siku). |
| Kulalamika na kutoshukuru Mungu na wengine; lazima uangushe wengine chini; kuonyesha uchungu, roho ya upinzani. | 13. | Kumtegemea Roho Mtakatifu kuongoza ulimi wake kuutumia katika kutukuza, kuadilisha, na kutoa shukurani na kutia moyo (Efe 4:29). |
| Mtaalamu wa kuonyesha makosa; mara nyingi asiyetosheka na kitu fulani. | 14. | Asiye kipofu kufanya vibaya lakini anyechagua kuzingatia kilicho kizuri na cha kupendeza (Plp 4:8). |
| Maneno ya upuuzi (kukiri dhambi za watu wengine); kutaka kuwapinga wengine kujisikia thabiti; mjasiri wa kuchambua udhaifu wa wengine; aliye na kipawa cha "utambuzi." | 15. | Kuwa huru kuungama makosa kwa wengine na anayependa kupima mafanikio yao; ambaye mara zote si lazima awe sawa; anatafuta mara nyingi kuwa nina makosa; mwenye utayari wa kukua. |
| Mara kwa mara anayejilinganisha na wengine, anayeongoza kwa kiburi au udhaifu (kutegemeana na jinsi gani wengine wanaona vizuri au vibaya). | 16. | Anayesimama kwa ujasiri katika Kristo; kufaa kwa binafsi-kunatoka katika damu ya Yesu kristo na utakatifu, siyo katika mhimili uliotengenezwa na mwanadamu. |
| Asiye na nguvu ya kushinda mwili; hakuna ushindi hasa wa moyo juu ya "dhambi ya mnyama" hata hivyo hana hisia ya "kuwa mwenye dhambi mkubwa." | 17. | Anayetulia ndani ya Yesu, na anayeona zaidi na zaidi ushindi dhidi ya mwili (Rum 8:1-9)., bado anayejiona kama "mwenye dhambi mkubwa." |
| Karibu asiye mwombaji, maombi ni "kimbilio la mwisho;" anaomba mara nyingi mbele za watu, mara chache akiwa peke yake. | 18. | Maombi ni sehemu ya maana katika siku, asiyefungwa na kawaida tu "mda wa ukimya;" Kuongea na baba ni furaha (1The 5:16-18). |
| Ahadi za Biblia za nguvu za kiroho na amani kuzidhihaki: "Nini kimetokea kwa amani yako yote?" (Gal 4:15). | 19. | Ahadi za Mungu za nguvu na furaha zinaanza kujieleza zenyewe (Rum 15:13). |
| Anahitaji kujigamba; lazima kila wakati kuonyesha yale aliyokamilisha kuogopa kwamba mtu mwingine anaweza kuyaona. | 20. | Anayejua kuwa Yesu ni kichwa cha mazungumzo yake; anayejigamba katika Bwana na katika udhaifu wake (2Kor 12:9-10). |
| Kujenga kwa kutokujitambua "kumbukumbu" ya kazi ambazo zinahitaji kuonekana na kujitetea. | 21. | Haki ya Kristo ndiyo pekee "kumbukumbu" zinazosimama kamilifu ndani yake (1Kor 1:28ff). |
| Kujijali-mwenyewe: "kama wangeweza kuona vitu jinsi ninavyotaka!" Kuhitaji sana kutawala hali na wengine. | 22. | Kuwa anayetawaliwa-na Kristo; kuhudumu katika nguvu za Roho Mtakatifu, siyo katika uwezo binafgsi "mwili uliokombolewa." |
| Kitu kingine kuliko Yesu kinaweza kutoshereza; "miungu" katika maisha (mali, cheo, haja) inatoa hisia ya kufaa na haki. | 23. | Kristo ni nyama na kinywaji; Mungu anatoshereza roho. "…na dunia haina ninachohitaji zaidi yako" (zab 73:25). |
| Hitaji dogo la kushirikisha injili (kwa kuwa ukristo wake ni wa ovyo) anaposhirikisha, anaonekana kuvutiwa na hisia ya wajibu na kazi na siyo upendo | 24. | Haja ya kuona waliopotea wanapata kumjua Yesu, kushirikisha injili wengine, *hata anapokuwa nje ya msukumo wa utaratibu wa kanisa.* "..upendo wa Kristo unatuteka" (2Kor 5:14). |

# MAOMBI

MAOMBI

SOMO LA 4

# Kongamano la Maombi

## KUABUDU NA KUSALI

☞ **Kusudi la Somo**

Kusudi la somo hili ni kumwabudu Bwana pamoja na kutiana moyo katika Bwana.

☞ **Wazo Kuu**

Mungu anathibitisha na kutuelekeza tunapochukua mda kumwabudu na kutafakari neno lake.

☞ **Matokeo Yanayotarajiwa**

Hili siyo somo, lakini ni warsha. Watu watakuwa wamepata uzoefu wa maombi ya mkakati na kupata fikira za jinsi ya kuongoza kongamano la maombi.

☞ **Ushauri kwa Wakufunzi**

Mda huu wa kongamano la maombi siyo mda wa kutoa maelezo lakini kuwaongoza wafunzwa kwenye kipindi cha maombi. Utahitaji kusoma Zaburi 95 kabla ya mda na kutambua mgawanyo uliotolewa katika somo.

Mda wa maombi haya na kuabudu unatakiwa utoe nafasi kwa kila mfunzwa kutafakari kwenye yaliyomo katika semina na kwa unyenyekevu kutafuta mwelekezo wa Mungu wa kwa jinsi gani itabadilisha maisha yake na huduma.

**UTANGULIZI**

Zaburi iliandikwa kuwashawishi watu na kumsherehekea Mungu , kumwabudu na kumtii Mungu baba yetu. Haikuandikwa ili kusomwa tu. Kwa kongamano hili la maombi, fata utaratibu uliotolewa katika Zaburi 95 kama ufupisho wako wa kutukuza, kuabudu na maombi.

Zaburi hii inatuongoza katika hatua tatu, kama zilivyoonyeshwa katika jedwali chini:

| **Zaburi 95** | |
|---|---|
| **1. Mwimbie Bwana** | **vv. 1-5** |
| **2. Inama mbeleza ZA Bwana** | **vv. 6-7** |
| **3. Msikilize Bwana** | **vv. 8-11** |

**I. MSHEREHEKEE BWANA (ZABURI 95:1-5)**

***Njoni tumwimbie Bwana kwa furaha***

- Imba nyimbo za furaha

***Piga Kelelekwa Sauti katika Mima wa Wkovu Wetu***

- Soma kwa pamoja kwa sauti ya juu kutoka Zaburi ya ukombozi: Zaburi 18:1-3, 30-36

***Njonim Mbele za Bwana kwa Shukurani***

- Muwe na mda wa kutoa ushuhuda, hasa kumshukuru Mungu kwa anachokifanya katika maombi ya utatu na maeneo mengine ya upandaji kanisa

***Tumwinue kwa Mziki na Nyimbo***

- Mwe na mda mwingine wa kumwimbia Bwana
- Soma pamoja mstari wa 3-5; mshukuru kwa ukuu wake wa kutawala anga lote

**II. MWABUDU BWANA (ZABURI 95: 6-7)**

Inama chini… piga magoti mbele za Bwana muumbaji wetu

- Watie moyo wafunzwa kuomba katika roho ya utu. Kama wako huru kufanya hivyo, piga magoti.

Ni Mungu wetu…tu watu wa malisho yake

- Mtambue kama mchungaji wako. Mtukuze kwa ulinzi juu yako

**III. SIKIA SAUTI YAKE (ZABURI 95: 8-11)**

***Usifanye moyo wako kuwa mugumu…***

- Ungama kila dhambi inayojulikana katika maisha yako. Soma 1Yohana 1:9.
- Chukua mda kumsikiliza Bwana. Muulize kukuonyesha kama kuna maeneno ambayo unahitaji kuachilia mfumo wa zamani, tabia, au njia za upandaji kanisa ambazo hazionekani tena kuwa za kibiblia kutokana na mistari uliyosomwa katika semina hii. Bishana na Mungu juu ya kitu gani uenmdelee nacho na kitu gani unahitaji kubadilika katika maisha yako na huduma.
- Soma Waebrania 3:7-19. Mstari wa 13 unasema kutiana moyo kila siku. Gawanyika katika jozi. Ombeaneni maombi ya kutiana moyo.

# UONGOZI

UONGOZI

SOMO LA 1

# Kanuni za Kibiblia za Uongozi

☞ **Kusudi la Somo**

Somo hili linatafasiri uongozi na kutambulisha mafundisho matano ya kibiblia kuhusu uongozi. Tunapojadiri uongozi, ni muhimu kwamba tunaanza na ukweli kabisa wa maandishi, badala ya mawazo yetu binafsi.

☞ **Wazo Kuu**

- Uongozi ni kuongoza
- Mamlaka yote yanatoka kwa Mungu

☞ **Matokeo Yanayotarajiwa**

Wakati yaliyomo katika somo hili yanapoeleweka, kila mshiriki anatakiwa:

- Kujua neno moja la tafsiri ya uongozi
- Kujua kanuni tano za misingi ya kibiblia ya uongozi

☞ **Ziada**

1A Mchanganuo wa uongozi

☞ **Ushauri kwa Wakufunzi**

Somo hili ni pamoja na shughuli tatu- katika darasa. Tumia kuamua kwako mwenyewe kwa mda uliotumika juu yake. Kwa nyongeza, ziada 1A inakupa nafasi ya kufikiri matokeo ya kanuni iliyoelezewa katika somo hili. Kama inawezekana kabisa, hii inaweza kufanyika vizuri zaidi darasani katika makundi madogo, au angalau katika utaratibu ambao utasisimua majadiliano.

## UTANGULIZI

Mara nyingi inasemekana kwamba hitaji kubwa la kanisa ni hitaji la viongozi bora walioandaliwa. Utafutaji wa viongozi au kuwaelimisha, unaweza ukamalizika vizuri zaidi mara tutakapokuwa tumetafsiri maana ya uongozi. Ni jinsi gani tunauelewa uongozi? “Uongozi” ni neno lenye maana nyingi. Tunapojadili uongozi katika mandhali maalumu ya kanisa, kisha maana yake hasa inaweza ikawa hata ngumu zaidi kuelewa. Wengi wetu tuna mawazo kadhaa juu ya uongozi, ambayo yanatokana na tamaduni zetu maalumu, mapokeo au uzoefu. Kanuni za uongozi pia zinatoka katika maandiko, ambazo zina ukweli halisi. Tunapojifunza kanuni za kibiblia, tunagundua uongozi wa kimungu ni tofauti kabisa na uongozi wa kidunia. Katika somo hili, tutakazia juu ya kile maandiko yanachofundisha juu ya uongozi.

## I. TAFSIRI YA UONGOZI

SHUGHULI: *Chukua dakika kutoa tafsiri ya neno “uongozi” kwa maneno machache iwezekanavyo. Shirikisha tafsiri yako wengine.*

Tambua tafsiri mbili hapo chini:

> *“Uongozi ni kuongoza” uwezo wa mtu mmoja kuongoza wengine” (Sanders, spiritual Leadership. P. 31).*
>
> *“Uongozi ni nguvu ya utaratibu ambao mwanaume au mwanamke alipewa uwezo-na Mungu wa kutawala watu wa Mungu kwenye kusudi lake katika kundi hilo.” (Clinton, making of a Leader, 14; cf. p. 127).*

Neno la msingi katika tafsiri zote ni “kuongoza.” Neno moja la tafsiri ya uongozi linaweza kuwa kwamba uongozi ni “kuongoza.” Watu wanapata kuongoza (na kwa hiyo uongozi) katika njia mbalimbali. Wakati mwingine watu wanaongoza kwa maadili katika nafasi walizopo. Wengeni wanaongoza kwa sababu ya ujasiri wao. Na bado wengine wanamvuto kwa sababu ya hadhi yao. Inaweza kuwa vigumu kuonyesha ni nini kinawapa watu uongozi, lakini kwa namna fulani hao wanaoongoza wanaweza kufanya hivyo kwa sababu wanaweza kuongoza.

> Neno moja la tafsiri ya uongozi linaweza kuwa kwamba uongozi ni “kuongoza.”

Tunapozungumzia juu ya uongozi katika somo hili, hatuzungumzii uongozi kama nafasi ya kawaida. Badala yake, tunapenda kusisitiza uongozi kama kazi, ili kwamba mtu mwenye kuongoza zaidi katika kikundi anaweza kutazamwa kama kiongozi halisi bila kujali nafasi yake. Kuelewa huku kunaweza kubadilisha sana mtazamo wa wenye majukumu ya kiuongozi. Kama kiongozi mzuri wa kanisa hivi karibuni alisema: “*Unaelewa kwamba uongozi ni kuongoza badala ya cheo, hilo linabadili kila kitu. Huhitaji kufanya bidii kuwa kiongozi; unajitahidi kuongeza thamani kwa watu, na watakufanya kuwa kiongozi*” (Maxwell, The Potential Around You. P. 25).

## II. KANUNI ZA UONGOZI WA KIBIBLIA

Mawazo yetu juu ya asili ya mwanadamu, kivutio na uongozi yanatoka ulimwenguni. Njia ya kidunia ya kushughulika na watu inaweza kuwa ya upotovu. Ulimwengu wa biashara wa kidunia unadhani kuwa “viongozi hawawezi kuwaamini wa chini yao kufanya yale wanayofanya, “na hiyo” kama unawaamini watu sana, watakudharau.” Viongozi wa kidunia wanaweza kuamini zaidi watu watafanya ambayo unataka wafanye endapo tu malipo yanakuwa ya kuvutia au kwa kutishiwa kwa adhabu. Matokeo ya jambo hili la kudhani kabla, viongozi wa kidunia mara nyingi wanatwaa mamlaka kwenye misingi ya cheo chao au kwa nguvu ya hadhi.

> SHUGHULI: *Katika makundi, chukua dakika kadhaa kujadili jinsi ulivyojisikia kukandamizwa na viongozi waliotenda kulingana na mawazo ya hapo juu.*

Kwa kuwa tunaishi katika ulimwengu ulopotoka ambapo tunaona hisia hizi zikifanya kazi mara nyingi, Zinaweza zikaleta maana kwetu. Lakini tumeitiwa katika njia nyigine kuhusu uongozi. Tambua kanuni za kibiblia juu ya uongozi.

### A. Mamlaka ya Kuongoza Yanatoka kwa Mungu

Akida katika Luka 7:1-10 alikuwa mkuu wa maasikali 100 wa Kiroma. Hata hivyo alijielezea mwenyewe kabla ya yote, siyo kama kiongozi wa wengi, lakini kama “mtu chini ya mamlaka.” Inaonekana kwamba alielewa kuwa ingawa alikuwa kiongozi, hakuwa huru kuongoza kwa njia yoyote anayochagua. Aliwajibika kwa hao waliokuwa juu yake.

Mungu ameanzisha mamlaka halali ya kisheria katika wizara mbalimbali kama vile serikali ya wananchi (Rum 13:17), familia (Kut 20:12, Efe 5:22-23, 6:1-4) na kanisa (Ebr 13:17). Kama vile maakida, hakuna kiongozi mwanadamu aliye na mamalaka kamili. Badala yake, kila mamlaka yanatoka kwa Mungu. Mungu peke yake ni mwenyezi, kwa hiyo wote walio katika uongozi lazima kila wakati wajitoe kwake. Anafanya kazi kupitia hao aliowaweka katika uongozi kwa kusudi lake (Mit 21:1). Yesu alitoa mfano wa kujitoa huku kwa Baba yake katika huduma yake ya kidunia (Yoh 8:28-29).

Tukiwa na hili akilini, tunaweza kuelewa kwamba viongozi wazuri ni wafuasi wazuri—wafuasi wa Bwana wao Yesu Kristo. Hakuna hata mmoja aliye huru kuongoza katika njia yeyote anayoitaka. Kwa hakika, viongozi wa Kikristo siyo viongozi kwa uchaguzi wao, badala yake, wamechaguliwa au kuitwa na Mungu (Yoh 15:16). Viongozi wa maana wa kikiristo wanajikuta wana majukumu makubwa kuongoza kama Mungu anavyoelekeza, na kwa hiyo wanajitahidi kufata Mungu anavyoongoza. Badala ya kukalia vyeo vyao, hadhi au uwezo wa mtu wa mamlaka, wanamwangalia Mungu, chanzo cha mamlaka yote.

> Viongozi wazuri ni wafuasi wazuri—wafuasi wa Bwana wao Yesu Kristo.

### B. Utumishi wa Unyenyekevu Unatakiwa Kuwa Tabia ya Viongozi wa Kikiristo

Kiongozi wa kikristo ni mtumishi wa kwanza na wa mbele . Utumishi unatakiwa kuwa na tabia ya yale yote kiongozi anayoyasema na kuyafanya. Pengine hakuna kilicho kibaya kwa kiongozi wa kikiristo kuliko kinyume cha utumishi—kiburi. Siyo tu kwamba kiburi kinaanzisha

mipaka kati ya viongozi na wafuasi, lakini ni moja ya vitu ambavyo Mungu anavichukia (Mit 6:16-17).

Kiongozi wa kikiristo siyo "mtawala" katika namna ya mabavu. Badala yake ni mtumishi. Neno "tawala" halikuwahi kutumika katika Agano Jipya kuelezea uhusiano kati ya wakristo. Kutafuta nafasi ya uongozi kutoshereza nafsi yake au kama msingi wa kufanyia majaribio ya mamlaka ni kinyume na wazo la kibiblia la kiongozi mtumishi (Flp 2:1-8).

Kiongozi wa kikiristo siyo "mtawala" katika namna ya mabavu. Badala yake ni mtumishi.

Yesu aliliweka wazi kwa wafuasi wake kwamba uongozi hautakiwa kujitumikia-binafsi (Mt 20:20-28); Yoh 13:1-16). Isipokuwa mara moja tu katika huduma ya Yesu alielezea kipekee kwamba alikuwa akifanya kitu fulani kama mfano kwa wafuasi wake, alipokuwa akiwahudumia kwa unyenyekevu kwa kuosha miguu yao (Yoh 13:15). Ingawa viongozi wengi wa kidunia wanatumia vitisho au ukubwa kuwafanya wafuasi kuwatii, vitu hivi havitakiwi kuwa tabia ya kiongozi wa kanisa (Mt 20:25-28, 1Pet 5:1-7).

Baadhi ya viongozi wa kanisa wanaanza kwa unyenyekevu, lakini baada ya mafanikio fulani katika huduma, wanaanza kiburi cha hila au kujisikia madaraka. Lakini mtume Paulo alikua katika utu katika kipindi cha huduma yake. Tambua kwamba mwanzo katika huduma yake anajielezea mwenyewe kama "mdogo kuliko mitume wote" (1Kor 15:9). Baadaye katika barua yake kwa Waefeso anajiita "mdogo kuliko watatkatifu wote" (Efe 3:8). Na mwishoni mwa maisha yake anajielezea mwenyewe kama "mkuu wa wenye dhambi" (1Tim 1:15

**C. Uongozi wa Kikristo Unahitaji Kuendelezwa kwa Mafunzo ya Uangalifgu na Kufanyia Mazoezi**

Mara nyingi tunashangaa kama viongozi wamezaliwa au wameundwa. Kunaweza kukawa hakuna mashaka kwamba baadhi ya watu wamezaliwa na uwezo wa kuongoza, lakini viongozi wa kikristo wameumbwa. Baada ya yote, nani amezaliwa na uwezo wa kufanya kazi zote hapo chini, ni zipi zinaweza kudhaniwa kuwa za kiongozi wa kikristo?

- Kuliongoza kanisa kwa neno la Mungu
- Kuwasaidia wengine kutambua na kutumia vipawa vyao, vipaji na uwezo
- Kuwatia moyo wengine kwa kazi njema
- Kupanga na kuatayaridsha kazi za watu wa Mungu
- Kuwatia moyo waliochoka
- Kuwashauri wadhaifu wa imani

Nyingi kati ya shughuli hizi ni za kimiujiza na za kigeni kwetu. Uongozi wa kikristo unakwenda kinyume na mwelekeo wetu wa kuzaliwa katika dhambi.; kwa hiyo, unatakiwa uendelezwe. Chunguza chati hiyo hapo chini ambayo inaonyesha tofauti nyingi za uongozi wa kidunia na uongozi wa kikristo.

**Kielezo 1.1 Uongozi wa Kiulimwengu Dhidi ya wa Kikristo**

| Uongozi wa Kidunia | Uongozi wa Kikristo |
|---|---|
| Ujasiri wa Binafsi | Ujasiri ndani ya Mungu |
| Kumwelewa mtu | Kumwelewa Mungu na mtu |
| Kufanya maamzi yake mwenyewe | Kutafuta kupata mapenzi ya Mungu |
| Tamaa ya madaraka | Mtumishi |
| Kuanzisha njia zake mwenyewe | Kutafuta na kufata njia za Mungu |
| Kufurahia kuwaamrisha wengine | Anayefurahia kumpendeza Mungu |
| Anayevutiwa na fikira zake mwenyewe | Anayevutiwa na upendo kwa Mungu na mtu |
| Anayejitegemea | Anayemtegemea-Mungu |

> Wote "kiongozi wa kawaida" na "asiyekiongozi" wanahitaji kufanya kazi sana kuwa "viongozi wa kikristo" wa kweli.

Pengine unamfahamu mtu ambaye anatabia kama "kiongozi wa kawaida." Pengine sifa zilizompatia cheo hicho ni zile zilizo kushoto katika chati 1.1. Kwa njia sawa, mtu bila sifa hizi pengeni hataelezewa kama "kiongozi." Katika hali halisi, wote "kiongozi wa kawaida" na "asiye kiongozi" pengine wanahitaji kufanya kwa juhudi sawasawa ili kuwa "viongozi wa kikristo." Kiongozi wa kawaida" lazima kujifunza kumtegemea Mungu, badala ya kujitegemea. "Asiye kiongozi" lazima ajifunze kwamba anaweza kumtegemea Mungu, hata kama mwenyewe ni mdhaifu.

Uongozi pia ni moja ya vipawa vya kiroho. Hao walio na kipawa hiki (na siyo wote wanakuwa nacho) wanaelekezwa kuvifanyia mazoezi kwa bidii (Rum 12:8). Roho Mtakatifu anaweza kutoa kipawa hiki cha uongozi kwa "kiongozi wa kawaida" au kwa "asiyekuwa kiongozi." Haitokani na uwezo wa kawaida. Kwa hiyo, ni muhimu kwa kila muumini kugundua kama hiki ni moja ya vipawa vyake au la. Hii ni bora kama ikifanyika kwa kuwahudumia wengine.

Kipawa cha uongozi kinaweza kulinganishwa na kipawa cha uinjilisti. Baadhi ya waumini wanacho, na wengine hawana. Kwa jinsi hiyo, wote wanatarajiwa kutumika katika uinjilisti na uongozi kama tukio na hitaji linaloibuka. Hao wenye kipawa cha uongozi wataona matunda mengi kutokana na kazi yao, lakini kila muumni anawajibika kutumia kanuni za kibiblia, uongozi wa kikristo katika maisha yake na huduma. Hii inaweza kuwa nyumbani, kazini, kanisani, katika kupanda kanisa jipya, katika kikundi kidogo, katika kikundi kiini au katika hali nyingine. Kwa sababu uongozi wa kikristo ni kazi (Kitu tunachofanya) badala ya madaraka, Bwana anatutarajia kukitumia.

### D. Biblia Inaeleza Utofauti wa Mitindo ya Uongozi

Uchunguzi wa karibu wa Biblia unaonyesha kwamba hakuna viongozi wawili ambao wako sawsawa kabisa. Viongozi wanatofautiana kutoa aina ya kitume (Paulo), aliye na tabia ya uwezo wa kuwavutia watu kumwitikia Mungu katika njia mpya katika hali mpya, mpaka kwenye aina ya uchungaji (Barnabasi), aliye na tabia ya kulisha neno na uwezo wa kusimamia. Hadhi na misukosuko inaongeza mapana ya mtindo wa uongozi. Kwa hakika Yoshua aliitikia tofauti kwenye changamoto ya uongozi wake kuliko alivyofanya Daudi. Mitindo tofauti inaeleweka kwa sababu hadhi na hali mara nyingi zinakuwa tofauti.

Waefeso 4:11-12 inaelezea taratibu mbalimbali za uongozi ambazo zilikuwepo kwenye kanisa la Agano jipya. Ingawa zilikuwa zinatofautiana sana, kila moja ilifanya kazi "kuwaandaa watu wa Mungu kwa ajili ya kazi ya huduma" au kwa maneno mengine, kuwaongoza kwenye huduma.

**Kielezo 1,2 Kazi za Uongozi Katika Agano Jipya**

| Wito | Fikira | Kazi |
|---|---|---|
| Mtume | Maono | Mwanzilishi |
| Nabii | Dhambi | Kuhubiri |
| Mwinjilisti | Wokovu | Kufikia watu nje |
| Mchungaji | Kulisha Neno | Kufikia watu wa ndani |
| Mwalimu | Ukweli | Kuelekeza |

Kazi zilizoorodheshwa katika kielelzo 1.2 zinahitajika katika kanisa leo. Mtindo mmoja wa uhusiano siyo lazima kwamba ni mzuri kuliko mwingine, lakini mmoja unaweza kuwa muhimu kulingana na mahitaji yaliyopo ya kundi kwa mda fulani. Kwa kipindi chote cha kudumu kwa huduma yako, unaweza kujitwalia mitindo mbalimbali kwa vipindi tofauti kwa sababu ya mahitaji maalumu.

> *Shughuli: Chukua dakika kadhaa kuangalia kwenye "Mzunguko wa Upandaji Kanisa" (Mwongozo1, somo la maono la 3). Katika vikundi vidogo au kama darasa, jadili mitindo ya uongozi kwa kila hatua ya mzunguko.*

**E. Kazi ya Kwanza ya Uongozi wa Kanisa ni Kuandaa**

Kimapokeo, Wachungaji na viongozi wa kanisa wamekuwa wakidhaniwa kama wale "wanaofanya" huduma—kama makuhani wa Agano la Kale, na wote tunapaswa kuhudumu. Waefeso 4:11-12 inaonyesha kwanza wajibu wa kwanza wa mchungaji anatakiwa kuwa na picha kichwani ya kuandaa waumini ili kwamba waweze kufanya huduma. Tabia yake inatakiwa kuwa: "vizuri kuweka watu 10 wa kufanya kazi kuliko kufanya kazi za watu 10." Kwa maneno mengine, Viongozi wa kanisa wanatakiwa kuwa wawezeshaji.

**Kielelezo 1.3 Kiongozi Anayeelekeza na Anayewezesha**

| KIONGOZI MWELEKEZAJI | KIONGOZI MWEZESHAJI |
|---|---|
| Ana asili ya kazi: Kufanya kazi kufanyika" | Ana asili ya watu: Anafanya watu kuhusika" |
| Mtendaji | Mwakilishi |
| Lengo- "Kufanya kazi ya huduma" | Lengo- "Kuwaandaa wengine kuhudumu" |
| Anayefanyia mazoezi cheo | Kuandaa, Kuwezesha, kufundisha |

Wazo la kuwezesha linaweza kuelezewa kwa msemo wa mwenyeji wa china mwenye busara aliyeitwa Lao Tse: *"wakati kazi ya kiongozi bora inapofanyika, kazi yake imekamilika, watu watasema, 'tumeifanya wenyewe.'"*

**MASWALI YA KUTAFAKARI, MARUDIO NA MATUMIZI**

- Ni nini maana ya kutafsiri uongozi kama "Kuongoza?" Ni nani viongozi katika kanisa lako au huduma ukiwa na tafsiri hii kichwani?
- Ni jinsi gani watu wanakuwa viongozi katika utamaduni wako?
- Kwa nini ni muhimu kwamba viongozi wote kwanza wawe wafuasi wazuri?
- Ni kwa jinsi gani kuelewa kwako kwamba mamlaka yako ya kuongoza yanatoka kwa Mungu kunabadilisha mtazamo wa uongozi wako?
- Ni nafasi zipi zinachukuliwa wakati muumini mpya mwenye uwezo wa kawaida wa kuongoza anapopewa uongozi katika kanisa?
- Ni ipi kati ya mitindo ya uongozi iliyoonyeshwa katika kielelezo 1.2 ni ya kawaida kwako?
- Ni kwa njia zipi mawazo haya ya uongozi yanatofautiana na kanuni za uongozi za kidunia?

**UTEKELEZAJI WA AZIMIO**

Jadili karatasi ya mazoezi 1A, "Mfano wa Kufanyia Utafiti wa Uongozi." Kwa kila mfano wa kufanyia utafiti, tambua kuwa kanuni za kibiblia zinatumika au hazitumiki. Kwa kila hali, jinsi gani unaweza kumshauri kiongozi kama ungekuwa umeitwa ili kusaidia?

**VYANZO**

- Clinton, J. Robert. *The Making of a Leader.* Colorado Springs, CO: NavPress, 1988.
- Sanders, J. Oswald. *Spiritual Leadership Chicago*, IL: Moody Press, 1980.
- Maxwell, John. "*The Potential Around You*," Leadership Journal. Fall, 1996.

UONGOZI
*ZIADA*

1A

# Mchanganuo wa Uongozi

## KANUNI ZILIZOTUMIKA

**Karatasi ya Maswali ya Mazoezi: Jibu maswali yanayohusiana na mchanganuo wa utafiti chini**:

1. Yuri amekuwa akiongoza mradi wa kupanda kanisa huko Yekatarinburg. Misha na Marina wamekuwa wajumbe wa timu kwa miezi mitatu. Hivi karibuni Misha na Mrina wameanza kujisikia hali ya kuchanganyikiwa kutokana na huduma. Wana baadhi ya hisia nzuri za uinjilisti lakini hawajisikii uhuru hata wa kuweza kuelezea hisia zao. Kiongozi wao, Yuri, anaonekana kutokuwa tayari kuwasikiliza ushauri wao. Badala yake anawaambia wanachotakiwa kufanya na jinsi gani wafanye. Matokeo yake, Misha na Marina wanafikiria kuiacha huduma na kuanzisha ya kwao**. Jinsi gani unaweza kutathimini uongozi wa Yuri**

2. Gennadi profesa anayejulikana wa chuo kikuu aliyempata Kristo wakati jirani yake Nic alipompatia Biblia kusoma. Alianza kuwa anahudhuria kanisa na Nic alikuwa amevutiwa na mafunzo ya Biblia ya watu wazima wanaokutana kila jumatano usiku. Katika wiki chache za kwanza, mtu mmoja alishauri kwamba Gennadi, mwalimu mzuri, aongoze mafunzo. Uongozi wa Gennadi ulikuwa ukileta wageni wengi kwenye kikundi kwa kuwa anajulikana na hasa kwa ualimu wake mzuri pia. **Je Gennadi aongoze mfunzo ya kikundi**?

3. Slava anaongoza timu ya familia tatu katika kupanda kanisa huko Rostov. Slava anatoa mahubiri mazuri zaidi wakati wa ibada kila jumapili na anaongoza kikundi kiini katikati ya wiki, ambacho kimekua kwa karibu ya wajumbe waaminifu 20. Kila mmoja anapenda uwezo wa Slava wa kufundisha na kuhubiri neno la Mungu, vilevile na uwezo wake wa kupanga shughuli. Kwa jinsi hiyo, Slava anaanza kujisikia kuchoka kutokana na mzigo wa kazi. Slava anamuuliza mwanakikundi Anatoli kuanza kikundi kingine kidogo na wachache kutoka katika kikundi cha Slava. Lakini, kuna haja ndogo ambayo inamkatisha tamaa Anatoli. **Tathimini jinsi Slava alivyochulia kuhamisha madaraka kwa Anatoli**

4. Kanisa mpya katika eneo la Smolensk linakua kwa kiwango cha haraka. Wengi wanahesabia ukuaji huu kwa uongozi bora wa Victor na Luba walioutoa. Walianza kanisa baada ya Victor kutoka Moscow chuo kikuu. Wengi wa hao wanaohudhuria ni waumini wapya wasiokuwa na uzoefu wa nyuma wa kanisa hata kidogo. Victor anafanya karibu mahubiri yote na Luba anapanga taratibu za madarasa ya jumapili. Kwa kuwa wamekua, Victor anaanza kutafuta viongozi wengine kutoka nje wa kumsaidia katika kazi za kanisa. Lakini hakuna hata mmoja anyeonekana kufaa kuongoza. Anajisikia angalau angepata vijana watatu ambao wanaweza kufundishwa kwa ajili ya uongozi wa kanisa. Victor alipata msaada wa kusomesha wawili wao kuingia chuo kikuu cha Moscow. Wanaondoka karibu mwezi wa nane kuanza kozi ya miaka 3. **Jinsi gani unaweza kutathimini njia hii ya maendeleo ya uongozi huu**

5. Boris anaisha katika mji mdogo wa kusini mwa Urusi ambao hauna makanisa ya kiinjili. Boris hivi karibuni amegundua waumini kadhaa katika kijiji chake wanaosafiri sehemu tofauti kuhudhuria kanisa-wengine umbali kama wa km 30. Chini ya uongozi wa Boris, waumini wamejipanga katika kanisa jipya. Waumini wanapokutana, wote wanahamasa ya kanisa jipya la mtaa na kila mmoja kwa shauku anashirikisha hisia juu ya jinsi kanisa linatakiwa kupangwa kutokana na uzoefu wao wa makanisa yao ya mwanzo. Lakini Boris anaweka wazi kwamba atakuwa mchungaji na kwamba watu wanatakiwa kusahahu juu ya mapokeo yoyote au walivyofanya katika makanisa waliyotoka, kwa sababu ni mkuu kama mchungaji wa kanisa hilo jipya. **Unafikiri ni nini itakuwa matokeo ya njia ya Boris?**

6. Keril amepanda makanisa matatu katika miji tofauti ya magharibi ya Urusi. Keril ni mpanda kanisa wa kawaida. Ana juhudi na mchangamfu, mwenye kipawa kama mwinjilisti. Anapiga gita na kuimba na anaweza kuburudisha umati kwa masaa. Anapenda kuanzisha vitu na kisha kuhamia kingine tena. Makanisa anayoanzisha yanaonekana kufanana na hadhi yake. Yanaonekana kuvutia mwanzoni lakini mara hufifia kitu kingine cha kuvutia kinapotokea. Keril anashikilia kauli kwamba hii ndiyo hadhi yake na kwamba hakuna kitu hasa anchoweza kufanya kuibadili. Anajua kuwa Mungu anamtumia bila kujali hilo. **Jinsi gani utatathimini uongozi wa Keril?**

7. Zhenya amekuwa anfanya kazi kwa juhudi katika kupanda kwake kanisa kwa miaka kadhaa. Kanisa linafanya vizuri sana. Limekua karibu kufikia 200 kwa miaka mitatu iliyopita. Mke wake na watoto wanne wakati mwingine wanamaliza siku kadhaa bila kumuona kwa sababu anaondoka asubuhi mapema na kurudi usiku sana. Zhenya hapendi kuishi hivi lakini watu wake ni wahitaji sana. Wengi wao ni wagonjwa na wanahitaji kutembelewa, jiko la mchuzi wa walala nje linahitaji kuangaliwa kwa karibu. Zhenya anajua kama akiacha kufanya yote anayoyafanya, huduma itayumba, watu hawataokoka na kanisa halitakua zaidi tena. **Unafikiri Zhenye ni kiongozi mzuri? Kwa nini na kwa nini siyo?**

UONGOZI

SOMO LA 2

# Sura ya Kiongozi

☞ **Kusudi la Somo**

Lengo la somo hili ni kusaidia mfunzwa kuelewa nafasi yake kama kiongozi katika mandhali maalumu ya upandaji kanisa

☞ **Wazo Kuu**

- Kuna tabia nane za kiongozi wa kikristo.
- Kiongozi wa kawaida na 'kiongozi asiye wa kawaida anaweza kuongeza ujuzi wake wa uongozi.

☞ **Matokeo Yanayotarajiwa**

Wakati yaliyoma katika somo hili yanapoeleweka, kila mshiriki anatakiwa:

- Kujua nafasi ya kiongozi katika hatua ya upandaji kanisa
- Kujua uwezo wake kama kiongozi
- Kujitoa kufanya kazi katika maeneo mawili maalumu anapokusudia kukua katika uwezo wa uongozi.

☞ **Ziada**

2A "Kiongozi"

☞ **Ushauri kwa Wakufunzi**

Ujue kwamba kila moja ya mawazo haya yameelezewa kwa upana katika masomo yajayo.

## UTANGULIZI

Kuna mitindo tofauti ya viongozi. Kwa jinsi hiyo, haijalishi ni mtindo upi ni kawaida kwa mpanda kanisa, lazima wakati wote awe mwezeshaji. Mwezeshaji ni yule anayewezesha wengine kutumia vipawa vyao na uwezo kwa ufanisi zaidi. Viongozi wa kanisa wanawajibika kuwaandaa watu wa Mungu kwa ajili ya huduma (Efe 4:12), badala ya kufanya sehemu ya kazi ya huduma peke yao. Ingawa mpanda kanisa lazima awe "mtendaji" Hata ni muhimu zaidi kwamba "anasababisha vitu kufanyika."

Chini kuna orodha ya baadhi ya tabia na ujuzi unaomwezesha kiongozi mpanda kanisa kuona kanisa limepandwa chini ya huduma yake.

## I. KUTUNZA TABIA –INAYOENDANA NA YA KRISTO

Mpanda kanisa, mwanzo wa yote, lazima awe na tabia inayoendana na ya kristo. Huduma inatiririka kutoka katika tabia. Fikiria msemo: "mafanikio ya binafsi yanazidi mafanikio ya uma." Labda Kristo awe ameununua moyo wako ili kwamba kufanana naye kuwe dhahili, jinsi gani unavyoweza kutarajia kuona kazi ya Kristo kupitia wewe katika taifa lako? Kama mpanda kanisa hakubadilishwa na Kristo, ni mashaka kwamba wengine wataweza kubadilishwa kupitia yeye.

Kufanana- na Kristo kunachanua kutokana na kuelewa upendo wa Mungu kwetu, na katika hitaji letu la kumuhitaji kufanya kazi katika maisha yetu. Huduma lazima iwe matokeo ya neema ya Mungu inayofanya kazi katika maisha yetu; hakuna kivutio kingine kitaheshimiwa na Mungu au kitanusuru wakati ambapo hali ni ngumu. Ufahamu wa neema ya Mungu katika maisha yetu unapatikana na kunusuriwa kwa kutafakari neno la Mungu, kuamini ahadi zake, maombi, na kuabudu.

Katika ushirika wa kila siku na Kristo, kuzingatia katika ahadi za Mungu, na maono aliyotoa kwa ajili ya huduma yako. Kiri utegemezi wako kwake kuweza kukamilisha kusudi lake katika maisha yako na huduma. Mtukuze Mungu kwa kile alichokwishafanya katika maisha yako tayari.

## II. FANYA KAZI VIZURI NA TIMU

Miradi mingi ya upandaji-kanisa inaanza kwa kuwepo uongozi wa timu mahali pake. Mara nyingine, mpanda kanisa anaanza akiwa mwenyewe na baadaye lazima aanzishe wengine ambao wataungana naye kadiri huduma itakavyokuwa inakua. Iwe hali yoyote, mara nyingi fanya ukielekea katika kuunda timu, zote, za uongozi na za huduma. Ifanye kuwa mfano wa kawaida kwa huduma yako na kwa ajili ya kanisa katika kuendelea kwake.

> Kufanya kazi kwa timu ilikuwa mfano wa kawaida wa huduma katika Agano Jipya.

Wapanda kanisa wanaofanikiwa hawafanyi kazi peke yao. Kwa kutofautishaWanakuwa na wengine, au wengine wanakuwa nao katika kazi ambayo Mungu amewaita kufanya. Mara nyingi kufanya kazi na wengine kama timu kunaweza kuwa kama chombo cha kuyeyushia ambacho tabia yetu ya kweli inaonekana na kuendelezwa. Uwe macho na viongozi ambao hawazungukwi na timu. Kama mmoja wao hawezi kufanya na timu, anawezaje kuongoza kanisa? Kufanya kazi katika timu ni kielelezo cha huduma katika Agano Jipya. Roho Mtakatifu alimtenga Paulo na Barnabas kama timu ya umishenari (Mdo 13:2). Ingawa Paulo na Barnabas walikwenda katika njia zao tofauti baadaye katika huduma, wote walianzisha timu mpya za wale waliowahudumia (Mdo 15:36-41). Kufanya kazi katika timu kulikuwa muhimu sana kwa Paulo kwamba hata alipopata mlango wazi wa huduma, aliacha kwa sababu alikuwa peke yake (2Kor 2:12-13).

“Timu” inaweza kutafasiriwa **kama kundi la watu walioungana pamoja kufanya kazi kwa ajili ya kusudio moja.** Timu nzuri ina thamani na falsafa ya huduma ya namna moja. Vipawa mabalimbali vya wajumbe wa timu vinapaswa kuwa vya namna mbalimbali wakati wakiheshimiana wao kwa wao, kuthibitika na utii lazima uwe wazi kwa mawasiliano wazi na ya kujenga kwenye timu. Ni kazi ya kiongozi kufanya kazi na timu siyo kama bosi au mfalme lakini kama mwezeshaji. Wajumbe wenzake siyo wafuasi, lakini wafanya kazi wenzake. Kujenga na kufanya kazi na timu kunaweza kukawa kugumu zaidi kwa hali ya juu na mkazo wa utaratibu wa mda lakini unaweza kuwa na hakika kuwa malipo yake ni makubwa.

## III. ENDELEZA VIPAWA NA UWEZO WA WENGINE

Kiongo wa kanisa lililopandwa anaongezeka mwenyewe kwa kujilinganisha na kuwaendeleza wafanya kazi wengine. Viongozi wengi wanajaribu kujenga huduma zao wao wenyewe na ukamilishaji wao wenyewe. Lakini Mungu ametuita kufuasa na kufundisha wengine (2Tim2:2). Mara zote ni vizuri kuweka watu 10 kufanya kazi kuliko kufanya kazi za watu 10.

> Mara zote ni vizuri kuweka watu 10 kufanya kazi kuliko kufanya kazi za watu 10.

Moja ya kazi kuu ya kiongozi wa upandaji kanisa lazima awe anawezesha wengine kujilinganisha vipawa vyao na kuwa wafanisi katika huduma. Hii inahusisha kufundisha wafanya kazi wa kanisa waliokomaa na wapya waliokata shauri kufanya kazi ya huduma, na kuoanisha watu wenye vipawa vinavyofaa kwenye nafasi ya huduma zinapotokea. Hii pia ina maana kwamba kiongozi ni, wa kwanza katika yote, mfundishaji. Hata kama hatumii mda mwingi akifundisha katika hali ya kiufundi, maisha yake ni kielelozo cha jinsi ya kufanya huduma. Watu wanaendeleza vipawa na uwezo wao kwa kuwa karibu na watu kama hawa.

Sehemu ya hatua ya kufuasisha waumini wapya ni kuwasaidia kufahamu na kutumia vipawa vyao. Kuwahusisha katika huduma ni njia nzuri ya kufanya hili. Hii ni njia yenye ufanisi kuwafundisha kwa ajili ya huduma.

## IV. JUA JINSI YA KUGAWA MAJUKUMU

Kiongozi mwenye hekima anafurahi kugawa wakati inapokuwa muafaka (Kut 18). Mgao unakamilisha zaidi kuliko kufanya peke yako, kwa kuwahusisha wengine katika huduma.

Kuna sababu nyingi za mgao. Mpanda kanisa anaweza kugawa majukumu katika sehemu ya huduma ambapo yeye hawezi na wengine wamejaliwa kupaweza. Katika hali zingine, anaweza kugawa ili na wengine wajisikie hali ya kuwa sehemu ya huduma. Watu wanapenda kuwajibika kwa vitu ambavyo na wenyewe wanashiriki.

Wakati mpanda kanisa kila mara anaangalia njia za kugawa, anafanya hivyo bila kuhitaji zaidi kwa wengine kuliko yeye alivyo tayari kutoa. Anaepuka kuwafanyisha wengine zaidi. Anapokuwa anawapangia watu kwenye majukumu ya huduma, anahakikisha pia kuwa wana vifaa vinavyohitajika kukamilisha kazi. Inapokuwa muafaka, kiongozi mwenye hekima anaandaa huduma kabla ya kuitarajia kutoka kwa wengine.

## V. WEKA MALENGO, MAAZIMIO NA MAKUSUDIO NA KUYAFANYIA KAZI

Kuweka malengo na kuazimia ni tendo la kawaida linalokubaliwa katika maandiko. Katika Mithali, tunajifunza kuwa tunatakiwa “Kila kusudi huthibitika kwa kushauriana; na kwa shauri la akili fanya vita” (Mit 20:18). Yesu alitumia maelezo ya mjenzi ambaye hakupanga kabla ya kujenga gorofa na mfalme ambaye hakujiandaa sawasawa kwa ajili ya mapigano kama mifano ya watu ambao wanawajibika kidhaifu kwenye kazi zao. (Lk 14:28-33). Kama kweli tunawajibika kwenye huduma zetu, kisha kuweka malengo wazi na mipango ianafaa pia kwetu.

Mpanda kanisa kwa maombi anaweka malengo, makusudio na mikakati katika kuwahusisha wengine kwenye timu yake. Mipango yake ni halisi. Anaepuka malengo yasiyohalisi ambayo hayawezekani. Mipango yake ni ya kunyumbulika,  ili kwamba aiweze kwa ufanisi na maana inayofahamika kuwili na mabadiliko. Anaweza kurithi mikakati na mipango kwa hali fulani. Inapokuwa lazima, anarekebisha vipao  mbele vyake na kusisitiza kutokana na hatua mbalimbali za kuzaliwa kwa kanisa na kukua.

**Kielelzo 2.1 Tabia za Kiongozi wa Kikristo**




## VI. KUELEZA WAZI MAONO KATIKA NJIA AMBAYO INAWAVUTA WENGINE

Kiongozi ni mtu wa maono. Ina maana, haoni tu wakati uliopo, lakini pia anaweza kufikiri jinsi mbeleni kutakavyokuwa. Kwa mpanda kanisa, hii ina maana kuwasiliana na Mungu kwa njia ya neno na maombi, kwa matokeo ambayo yatakuwa na hisia wazi za kile Mungu anachotaka kufanya kumtumia wakati ujao. Pia anatambua umuhimu wa kuwakilisha kwa kushawishi maono haya kwa kanisa na kwa waumini wengine watakaomsaidia kupanda kanisa jipya. Anaweza kuanzisha kisa au maneno yanayoweza kukumbukwa ambayo yanaeleza kwa ufupi maono na falsafa ya huduma. Mpanda kanisa mwenye maono anaweza kuyaweka maono kati ya kila kitu kilichofanyika katika kuanzisha kanisa jipya. Kwa kupitia juhudi hizi, hao waliohusika katika kupanda kanisa watabakia kujitoa kwenye maono, na kujisikia kuwajibika kwenye ukuaji na hatua ya huduma.

## VII. DUMU NA SHINDA VIKWAZO

Njia anazotumia kiongozi zinatia changamoto kama “Nafasi” badala ya “matatizo”.

Kiongozi wa kikristo lazima awe mvumlivu. Shetani atapinga kila jaribio la kujenga kanisa la Yesu Kristo. Matatizo yatatokea. Lazima awe tayari kufanya kazi kwa bidii na pamoja bila kukata tamaa. Anachukua maamzi na ni mwenye kuhakikisha mambo yamefanyika, bila kuwa bosi au kuchukiza. Ni mwanzishaji- wa pekee kama mdudu chungu katika Mithali 6:7 anayefanya kwa sababu ya maanzilishi yake mwenyewe, bila kusubiri kuelekekezwa. Anakabili changamoto kama “nafasi” badala ya “matatizo.” Anaamini kwamba Mungu atafanya mambo makubwa kwa utukufu wake.

Watu wengi ni wa kushituliwa; ikimaanisha shughuli zao zinatawaliwa na matukio yanapotokea kwao. Mtu wa kushtuliwa mara zote anaitikia kile kinachoendelea kwake na kuishia kuwa mwathirika wa misukosuko. Kiongozi wa kikristo au mpanda kanisa anatakiwa awe anafanya kwa matazamio. Anatakiwa kufikiri kabla na kujiandaa mwenyewe na hao anaowahudumia ili kwamba waweze kiushindi wayafanyie kazi matatizo wakati yanapotokea. Kwa mfano, kiongozo wa kikristo kufundisha ukweli mbele ya mashahidi wa yehova kuiba kondoo wake, na kushughulikia matatizo wakati yakiwa bado madogo na yanayowezekana. kiuwazi, kutakuwepo na nyakati ambapo kiongozi bora lazima akasirike kwenye tatizo. Lakini kiongozi mzuri ataweka msingi mzuri kabla, ili kwamba matatizo yawe rahisi kutatua. Hata katika nyakati ngumu, atabakia kuwa kiongozi, badala ya mwathirika.

**Jedwali 2.2 Mwathirika au Kiongozi**

| Mwathirika | Kiongozi |
|---|---|
| Anasema: “Hakuna tunaloweza kufanya” | Anasema: Ngoja tuangalie kwenye uwezekano mwingine” |
| Anang’ang’nia kwenye matatizo | Anakazania kwenye uwezekano |
| Anaishi katika wakati uliopita | Anaishi kwa ajili ya wakati ujao |
| Anayeona yote kuwa mabaya | Anayesadiki kuwa yanawezekana |
| Anasubiri mpaka wengine waanze | Ni mwanzilishi |

## VIII. GOZA KATIKA UINJILISTI

Haiwezekani kupanda kanisa bila uinjilisti. Kwa sababau uinjilisti ni kama sehemu muhimu ya upandaji kanisa, lazima iwe wazi kwamba ni kipao mbele cha kiongozi. Wengi katika mradi wa upandaji kanisa watakuwa na hali sawa kama ya kiongozi inapokuja kwenye uinjilisti. Kama kiongozi hakuhusika, hawataweza kuwa. Kama kiongozi anaongelea tu juu ya uinjilisti, na kamwe haufanyi, hata wala hautatokea. Kama kiongozi anashauku kama mwinjilisti, utatokea pia.

Uinjilisti ni kazi ya kimsingi iliyoamriwa kwa kurudiwa katika Agano Jipya (Mt 28:19-20). Yesu alifundisha 12 wa kuchukua nafasi yake. Kuwafundisha ilikuwa ndiyo fikira zake-lakini hakupoteza upeo wa sababu ya kuwafundisha. Alilifanya kuwa wazi kwa mafundisho yake na mfano wake kwamba fikira zake ilikuwa kwa umati wa waliohitaji wokovu. Wanafunzi wake walipata fikira sawa kupitia mfano wa Yesu vile vile na mafundisho yake wazi. Paulo pia alimwambia Timotheo kufanya kazi ya uinjilisti (2Tim 4:5). Uinjilisti unaweza kuwa haikuwa kipawa chake, lakini Paulo alijisikia kana kwamba Timotheo alihitaji kuupa kipao mbele uinjilisti.

Uinjilisti na huduma ya kufundisha vyote ni shughuli nyeti kwa mpanda kanisa. Mtu anaweza kuuliza jinsi kiongozi wa kupanda kanisa anavyoweza kukazania kila moja ya haya wakati mmoja. Hili ni swali zuri. Njia moja ya kulijibu ni kuhusisha viongozi unaowafundisha kwenye uinjilisti. Mara zote fanya kazi na mwingine na atakuwa wakati wote anajifunza.

**SULUHU**

Tabia na ujuzi wa mtu hapo juu zinamwezesha vizuri kiongozi mpanda kanisa kwa ufanisi kuona makanisa mengi yamepandwa chini ya huduma yake. Mpanda kanisa atakuwa na hekima kuendeleza ujuzi na tabia hizi. Hata hivyo lazima iwekwe kichwani kwamba wapanda kanisa wote hawafanani kabisa. Hadhi na mitindo inatofautiana kama ilivyo kwenye vipawa vingine vya huduma. Ni kwa njia ipi hapo juu una kipawa kama mpanda kanisa? Ni kwa njia ipi huwezi, kwa mawazo yako?

**MASWALI YA KUTAFAKARI, MARUDIO NA MATUMIZI**

- Kwa nini kiongozi agawe?
- Ni kazi ipi unayofanya ambayo unatakiwa kuwapa wengine?
- Ni nani mwezeshaji?
- Ni kwa njia zipi mpanda kanisa ni kama mkulima?
- Jinsi gani kiongozi anaweza kuwafanya wengine kuhusika katika kuweka malengo?
- Ni lipi ni muhimu zaidi, kuwafundisha viongozi au kufanya uinjilisti kwa bidii?
- Ina maana gani kuwa mtu anayepanga kabla na kwa nini mpanda kanisa awe na tabia hii?
- Una timu na kufanya nayo kazi?
- Una au timu yako ina malengo ya huduma yenu?

**UTEKELEZAJI WA AZIMIO**

Tazama ziada 2A: “Kiongozi.” Ni nini tabia za uongozi wa kikristo unazoona katika hesabu hii ya maisha ya Kristo? Ziorodheshe kwa ajili yako, na kisha zilinganishe kwenye tabia zilizojadiliwa katika somo hili. Zinakubaliana? Ni kwa jinsi gani unafikiri ni muhimu? Ni kwa jinsi gani maisha yako na huduma yako zinajilinganisha?

UONGOZI ZIADA

2A

# Kiongozi

Kiongozi alikuwa angalau na kazi ya kufanya. Misheni yake ilikuwa kuubadilisha ulimwengu. Mabadiliko ambayo kiongozi huyo alipanda hayakuwa tu mapambo, au kitu cha mda tu. Yalihusu kwa ujumla falsafa mpya ya maisha yanayotokana na utamaduni mpya kuwafikia kila kabila na taifa. Kusema machache, kiongoizi alikuwa na kazi ngumu zaidi mbele yake. Viongozi wengine mashuhuri walijaribu vitu kwa ufahari kidogo na kushindwa. Kusema kwa kibinadamu, kiongozi alikuwa peke yake kwenye misheni hii. Hakuna mtu mwingine tena aliyekuwa amejitoa kwa hilo, hata mmoja kuielewa. Ni kwa jinsi gani angeweza kukamilisha kazi yake? Ni jinsi gani angeweza kufikisha ujumbe wake nje? Ni kwa jinsi gani angeweza kuwavutia wengine kuishi kufuatana na hiyo?

> Kiongozi hakufanya mengi kati ya ambayo pengine tungetarajia.

Uchunguzi wa njia za kiongozi una mengi ya kushangaza. Kiongozi hakufanya mengi kati ya ambayo pengine tunatarajia. Hakutafuta ofisi za uma au kukusanya jeshi. Hakufungua wizara yoyote, au kuendesha semina za kawaida kufundisha katika falsafa yake mpya; hakuwavuta mbali wafuasi wake kwa kipindi kilichopangwa cha kiakili. Hakukabidhi maandishi kwenye uchapishaji kuzalisha vitabu na magazeti yanazolenga mpango wake. Badala yake, kiongozi alianza kwa kujikusanya kikundi kidogo cha wafuasi (Mt 10:2-4). Badala ya kukazania umati, alitumia mda wa miaka mitatu maalumu kuwafundisha watu hawa kwa njia yake inayobadilisha katika maisha kwa tumaini kwamba wangemsaidia kubadilisha umati.

Na watu 12 tu, hii ilionekana kama mwanzo mdogo wa kukatisha tamaa. Hata hivyo, aliishi kwa imani yake na kuwapenda hawa 12 kana kwamba ilikuwa sehemu ya familia yake. Waliishi pamoja, kula, kupumzika, kufanya kazi na kujilaza bila kizuizi wala mpaka wowote. Katika yote haya, kiongozi anaweka fikira zake katika matendo kwa kuishi kwa kuyaonyesha kwa wafuasi wake. Walisafiri pamoja kutoka kijiji hadi kijiji mahali alipozungumza na wengine, kukutana na mahitaji ya aina zote. Kiongozi kawaida alihubiri kwa makutano makubwa (Mk 4:1). Mahubiri yake hayakuwa ya kufafanua; alitumia vielelezo vingi kutoka katika maisha kama walivyokuwa wanaishi katika nchi hiyo na mda huo. Angeweza mara nyingi kurudi na wanafunzi wake peke yake kijijini alipofanya mahubiri yake kuwa ya maana kwa undani ikifuatiwa na majadiliano (Mk 4:34).

> Wafuasi aliochukua walikuwa zaidi, watu wa kawaida.

Wafuasi walikuwa wamejitoa na kuonekana wenye bidii ya kujifunza, lakini walionyesha ahadi kidogo. Wengi wao walikuwa wanakijiji wa nyuma, wanaoweza kusoma kidogo,; mmoja amekuwa mkusanya kodi, cheo kilicho dharauliwa na watu wa kawaida; wachache walikuwa katika biashara ya uvuvi. Kwa zaidi walikuwa watu wa kawaida, siyo ‘wapasuaji’ aina ambayo miongoni mwao mtu asingetarajia mambo makubwa. Hakuna mmojawao aliyemiliki maelezo kama karisma inayohitajika na viongozi wa harakati . Na ingawa kiongozi alikuwa na ujumbe wa kiroho, hakuna mmoja wao aliyemchukua aliyekuwa kiongozi wa kidini. Bila kujali haya yote ya kutokuwa na sifa, hawa wafuasi wasiotarajiwa walikuwa ndio aliochagua mwenyewe kusimama peke yao mstari wa mbele wa harakati kuu. Kiongozi alidhani kwamba sifa za watu hawa ingekuwa kwamba wamekuwa pamoja naye.

Kiongozi alikuwa na utu usio wa kawaida. Hakujali kwenye maneno ya uchungu yaliyokuwa wazi juu ya mji wake. Alikuwa ameridhika kujulikana kama kijana wa kwenye mji mdogo na mtoto wa selemala. Hakutafuta sifa wala heshima, lakini alitafuta kuwawezesha wengine na kukaa nje kwenye nuru yake nyeupe. Baadhi walidhani kwamba angeweza kuwa na matokeo makubwa kama uongozi wake ungekuwa zaidi wa kawaida, kama angelitumia mfumo uliokuwepo. Lakini kiongozi alikataa hadhi ya kawaida. Alikataa utawala wa moja kwa moja wa ufalme wa duniani hata ulipotolewa kwake (Mt 4:8-10). Badala ya kufanya kuelekea mageuzi ya mfumo uliokuwepo, kiongozi alijitahidi kuwasha harakati zote mpya.

Kwa kutazama yaliyopita, tunaweza kushangaa juu ya ujasiri wa kiongozi, Kufanya urafiki na wenye dhambi (Mk 2:15-17). Mahubiri yake na mafundisho yalikanyaga juu ya miguu ya wengi waliokuwa katika nafasi ya kusaidia chanzo. Kwa tofauti ya wachache, kiongozi hakuonyeha ujasiri kwa viongoizi wa kidini katika siku zake. Kiwango chake kilikuwa cha juu—alihitaji yote au hakuhitaji chochote kutoka kwa watakao kuwa wafuasi wake na wengi hawakuweza kujitoa (Mt 10:37-39).

Kiongozi alitathimini tamaduni na kawaida kulingana na matokeo ya kazi yao. Kwa mfano, kwa kiongozi, “anayefanya kazi nyingi” ingeweza kuwa mtego ambao ungewazuia watu kutokana na vitu muhimu halisi (Lk 10:41-42). Kuhusu sheria za kidini, kiongozi mara zote alikuwa mwenye heshima wakati pia akiwa mtendaji, bila kuzuiliwa na barua za sheria. Aliachilia kiwango cha hasira zake zote wakati alipoona hekalu linatumiwa kwa kazi ambayo haikukusudiwa. Kiongozi alikemea mapokeo na matambiko yaliyokuwa yamewalemea watu badala yake kuwapa uhuru wa ndani, Alikuwa na fikara za mabadiliko ya ndani kulingana na ‘roho ya sheria’ kuliko uthibitisho wa nje kutawala kwa kanuni na taratibu. (Mt 15:7-9).

Kiongozi aliwapenda watu kwa undani; misheni yake ilihusisha utumishi-kama huduma kwa watu wengine.

Kiongozi aliwapenda watu kwa undani; misheni yake ilihusisha utumishi-kama huduma kwa watu wengine. Pengine hii ndiyo sababu watu wengi hawamkumbuki kwanza na kuendelea kama ‘kiongozi,’ Kutoelewa vema uongozi kama ‘daraja’ ‘nafasi’ au ‘hadhi’ kunawafanya wengi kutomfikiria mtu huyo kama kiongozi. Badala yake, anakumbukwa kama mtumishi, mwalimu, mponyaji, mshauri, au cheo chochote kinachoweka wazi kwamba mtu huyu alisaidia na kuwaelekeza watu. Utu wake wa siku hadi siku ilikuwa mara kwa mara kuvutwa na mahitaji ya wengine. Mara zote alichukua mda kuongea na watu wa kawaida, kutimiza mahitaji yao kwa kuwaponya au kuwaelekeza kuelekea uhuru wa ndani. Wakati umati mkubwa ulipomjia, aliitikia kwenye haja zao na mahitaji na kwa kujali kudogo ratiba za kawaida au mahitaji yake mwenyewe. Hakujali usumbufu wa watoto (Mt 19:13-15). Alishughulikia kineema namna zote za usumbufu usio wa kawaida, hata paa lilipobomolewa juu ya kichwa chake. Hakuweza kutekwa katika mgawanyo usio muhimu wa wanadamu. Ndivyo watu walivyokuwa muhimu sana kwake kwa hiyo alifupisha sheria kiuhusiano.

Hakuwa amependezwa sana kwa ufahamu, utajiri, au utii uliojifunga kwenye sheria, kama alivyokuwa kwa imani. Kwa hakika, kama ulitaka kumfurahisha kiongozi, kuiweza imani ilionekana kama njia nzuri ya kuweza hilo. Imani pengine kilikuwa ndio kipimo cha kupimia wengine. Aliendelea kusisitiza wengine kuamini na alikuwa karibu azimie kwa kuonyesha mlipuko wa nje wa kukumbatia alipopata watu wa imani. Wakati fukara wa jamii alipoonyesha imani ndani yake, hata katika njia ya usumbufu, kiongozi alimpokea (Lk 7:36-38). Ingawa yeye mwenyewe alikuwa na uwezo wa asili, katika hatua mabalimbali alieleza kuwa alikuwa hasa anazuiliwa na kukosa kwa imani kwa watu wengine.

Karibu na mwisho wa kazi yake na wafuasi , ilionekana kana kwamba kulikuwa na kushindwa kwingi. Wafuasi wake mara nyingi hawakuweza kuelewa alichofundisha. Watu wote kwa ujumla walikuwa wamechanganyikiwa juu ya alikuwa nani. Wafuasi wake walikuwa wamejitoa kwake alipokuwa wa watu wengi lakini hawakusimama naye alipowahitaji zaidi. Hata mmoja wa wafuasi aliyekuwa karibu alikataa kuwa alimjua kiongozi wakati muhimu sana (Mt 26:69-74). Mfuasi mwingine alimsaliti kwa ajili ya vipande vya fedha vya kwanza kuvipata, lakini mara baada tu akajinyonga. Hatimaye kuanzishwa kuligeuziwa kwa kiongozi. Alikamatwa, akajaribiwa, akahukumiwa na kuwekwa katika kifo kama adui wa watu. Zaidi kwa kuubadilisha ulimwengu.

Kulikuwa hakuna shaka kwamba wafuasi wake walishangazwa na kuvunjwa moyo kwa kuondoka kwa kiongozi kusikokuwa kwa kawaida na kwa ghafla. Hawakujisikia kuwa tayari kwa kiongozi kuondoka. Ilionekana kana kwamba ndiyo alikuwa anaanza. Alikuwa ameshakuwa na matokeo ya ajabu, lakini ulimwengu, wakiwa wamemkataa kiongozi, walikuwa mbali na kubadilishwa. Kwa sababu kazi ilikuwa haijamalizika, kiongozi, katika kuondoka kwake, aliwapa wafuasi wake maagizo kuendeleza kama alivyofanya (Mt 28:18=20). Alikuwa kwa kikamilifu amewaandaa ili kwamba kama watatumia walichojifunza kutoka kwake, wangeweza kuwa na matokeo (hata makubwa zaidi) ya yake.

Na kuongoza wafuasi hawa kulifanyika. Waliibuka kama watu wa imani kubwa na maono ya mabadiliko aliyotaka kiongozi. Kwa jitihada za ajabu na shauku waliendeleza misheni. Walipokuwa wakifanya hivyo walifanya kitu kimoja wazi—kiongozi hakuondoka hasa. Ilionekana hivyo kwa kitambo kidogo tu. Kwa hakika, uwepo wake wa kiroho ulikuwa ndio ufunguo wa mabadiliko aliyotaka. Yeye, kiongozi, alikuwa nao walipopanga kueneza ujumbe wake kwa kila kabila na taifa. Uwepo wake ulikuwa ndio ujumbe wao na mvuto wa Mungu!

Wafuasi wake waliishi kulingana na ujumbe na kuwapenda wengine kwa undani.

Wafuasi hawa, kwa kuonyesha wenyewe kuwa wafuasi wazuri baada ya yote, hawakuacha umaana kutoka katika mfano ambao kiongozi alikuwa ameanzisha. Waliendeleza majadiliano yenye nguvu na watu wa kawaida katika sehemu za masoko, vile vile na majumbani). Wafuasi wake waliishi kulingana na ujmbe na kuwapenda wengine kwa undani, wakati wakiendelea kuwakusanya wafuasi wengine kufanya wanayofanya. Watu walipokubali ujmbe, ushirika wa mtaa ulishangilia uwepo wa kiongozi kuanzishwa. Kama kiongozi, wafuasi hawa na washirika wao wa mitaa walikuwa na matokeo ya ajabu kiasi kwamba serikali na dini zilitishika vibaya sana—mpaka kwenye hatua ya kufanya malipizi.

Wizara za kawaida na vipindi vya mkazo vilifunikwa na uwepo wa kiongozi.

Siyo vizazi vingine baadaye, wafuasi waliendeleza zaidi njia ya“kutatanisha” ya kumfata kiongozi. Mara nyingine kwa kudhani “kufanya kama Waroma wanavyofanya’ kuliko kufanya kama kiongozi alivyofanya, walitumia utawala wa mtindo wa kidunia unavyofanya. Harakati za hiari zisizo za kawaida zilizosisitiza uwepo wa kiongozi zilitoa njia kwa wizara na vipindi vigumu vya kawaida. Mashirika ya kuvutia, majengo makubwa, na vipindi vya ‘ncha ya kukatia’ vilikuwa badala ya sherehe za kawaida na kutangaza hisia za moyo ambazo ni utii upasao kwa kiongozi alioonyesha. Mwelekeo huu ulitoa usalama fulani na ulinzi, lakini uwepo wa kiongozi ulifunikwa na kile alichosimamia kiongozi kilikataliwa. Kwa kuanzisha na kuheshimu mifumo kwa gharama ya utendaji, matokeo halisi ya misheni yake ilipotea.

Mvuto wa kiongozi unaendelea. Hao wanaomfata kiongozi wameamriwa kufanya kazi kama alivyofanya. Kama maelezo ya azimio kwa kubadilisha ulimwengu kwa vipindi na wizara zinaonyesha ahadi kidogo kuliko ambavyo haijawahi kuwa, wafuasi wake wanatakiwa tena wakumbushwe njia ya pekee ya kiongozi. Hisia ya msingi ni rahisi kiajabu: kiongozi, anayeishi kufuatana na anachoamini, kwa undani akiwapenda wafuasi wake ambao anachangia nao njia ya maisha—huu ni uongozi kwa kiwango cha juu. Huyu ni kiongozi mkuu anayegusa maisha na kubadilisha ulimwengu.

**VYANZO**

Adopted from *The Teacher*, an unpublished manuscript by Ted Ward and Lois McKinney.

# VIKUNDI KIINI

VIKUNDI KIINI

SOMO LA 1

# Kazi na Faida za Vikundi Kiini

☞ **Kusudi la Somo**

Lengo la somo hili ni kuonyesha faida za kutumia vikundi kiini kwa ajili ya huduma.

☞ **Wazo Kuu**

- Vikundi kiini ni tofauti na vikundi vidogo kwa sababu vinazidisha.
- Kazi nne za msingi za vikundi kiini ni: ushirika, kuabudu, kufuasisha, na uinjilisti.

☞ **Matokeo Yanayotarajiwa**

Wakati yaliyomo katika somo hili yanapoeleweka, kila mshiriki anatakiwa:

- Kuweza kueleza jinsi vikundi kiini vinavyotofautiana na vikundi vidogo.
- Kuweza kujadili faida za kutumia vikundi kiini katika uinjilisti, kuanzisha mahusiano, kuinjilisha na upandaji kanisa.

☞ **Ushauri kwa Wakufunzi**

Somo hili lina marejeo kwa maono ziada 3A (Kutoka mwongozo wa 1) "Mitindo ya Upandaji Kanisa." Unatakiwa kurudia ziada hii kabla ya kumaliza na uwe nayo unapokuwa unafundisha.

## I. MISINGI YA KIKUNDI KIINI

### A. Utangulizi

Makanisa zaidi na zaidi ulimwenguni kote yanatambua umuhimu wa ajabu wa vikundi kiini. Kwa kupitia vikundi hivi makanisa yanakua na watu wanatumia vipawa vyao. Mwili wa Kristo unahamasishwa kwa ajili ya huduma, na matokeo yake ni kwamba waliopotea wanapata ukweli na upendo wa Yesu Kristo.

Je vikundi kiini ni kitu fulani kipya, kisichojulikana au huduma ya kimtindo mpya katika kanisa? Siyo kabisa. Matumizi ya vikundi kiini kanisani yalianza na kanisa la Agano Jipya ilivyoelezwa katika kitabu cha Matendo. "Viini" vya kanisa walikutana katika nyumba za watu kuabudu, kushirikiana, katika kukua katika imani yao mpya, na kwa kushirikisha majirani na marafiki habari hii njema waliyoipata. Vikundi hivi pia walikutana pamoja kwa ajili ya mikutano mikubwa hekaluni kwa ajili ya kuabudu, kufundisha na kuinjilisha.

> Tofauti kubwa kati ya vikundi kiini na vikundi vidogo ni kwamba vikundi kiini **vinazidisha**, wakati vikundi vidogo vinaweza visizidishe.

Kwa nini tunatumia neno Vikundi "kiini"? Kwa nini tusiviite vikundi "vidogo"? Makanisa mengi yana vikundi vidogo vinavyokutana kwa ajili ya aina mbalimbali za huduma ya kanisa, mara nyingi kwa ajili ya kujifunza Biblia. Kuelewa tofauti kati ya vikundi vidogo na vikundi kiini, tunaweza kutumia mfano kutoka kwenye sayansi. Katika somo la biolojia, kiini ni kitu hai, kiumbe kinachokua ambacho kinaongezeka chenyewe zaidi na zaidi. Tofauti kubwa kati ya vikundi kiini na vikundi vidogo ni kwamba vikundi kiini **vinazidisha,** wakati vikundi vidogo vinaweza visizidishe. Hii ni tofauti yenye maana sana. Unaweza kufanya aina nyingi za huduma katika makundi, lakini kama moja ya lengo la kikundi siyo kukua na kuzidisha chenyewe kwenye kikundi kipya, kisha hakiwezi kuitwa kikundi kiini.

### B. Utofauti

Badala ya kutoa tafsiri ngumu ya kikundi kiini katika somo hili, tutaanzisha “kuelewa “kunakoendelea” kwa nini kikundi kiini ni na kinafanya nini tunapofanyia kazi somo hili la kikundi kiini katika mwongozo huu. Kwa jinsi hiyo, Ni muhimu kutoka mwanzo kuelewa tofauti za kimsingi za kikundi kiini chochote. Kila kikundi kiini kina:

1. ***Kujitoa kwenye uinjilisti***
2. ***Kujitoa kulisha neno na kufuasisha waumini***
3. ***Kujitoa kuanzisha viongozi***
4. ***Kujitoa kwenye kuzidisha, ili kutimiza Utume Mkuu***

## II. KAZI ZA VIKUNDI KIINI

Kuna njia nyingi za kutumia vikundi katika hatua ya upandaji kanisa. Hata hivyo, vikundi kiini ambavyo vinatumika katika upandaji kanisa vinaonekana kuwa na baadhi ya viungo vya kawaida—kazi za kawaida—miongoni mwao. Viungo hivi ni ushirika, kuabudu, kufuasisha, na kuijilisha. Kazi hizi sawa zinaweza kupatikana kutoka kwenye mfano wa kanisa la kwanza la Agano la Kale. Hakika, hizi siyo kazi pekee zinzoonekana katika kanisa la Agano Jipya, lakini hizi ni maeneo ambapo vikundi kiini na kanisa la kwanza vinachangia kikawaida katika kazi. Majedwali yafuatayo yanalinganisha kazi hizi katika kanisa la Agano Jipya na katika vikundi kiini.

| **Kazi ya Ushirika** | |
|---|---|
| ***Katika Kanisa la Agano Jipya*** | ***Katika Vikundi Kiini*** |
| Ushirika ambao waumini waliufurahia ulikuwa moja ya tabia inayotofautisha ya kanisa la kwanza (Matendo 2:42,).<br><br>Walitiana moyo (Ebr 10:25, 1The 5:11) na mara nyingi kuumega mkate kwa pamoja (2:42, Ac 20:7, 11) | Katika kikundi kiini, ushirika ni kutiana moyo wao kwa wao, kushirikishana, na urafiki katika Kristo, ili kutimiza hitaji la upendo, kukubaliana, umoja na kusaidiana.<br><br>**Kazi zinazowezekana**<br>• Kushirikisha matatizo mmoja kwa mwingine<br>• Kubebeana mizigo<br>• Kuombeana katika maombi<br>• Kula chakula pamoja<br>• Kufurahia pamoja kama familia<br>• Kutiana moyo mmoja kwa mwingine |

| **Kazi ya Kuabudu** | |
|---|---|
| ***Katika Kanisa la Agano Jipya*** | ***Katika Vikundi Kiini*** |
| Maombi na kutukuza ni kisa kinachojirudia katika kanisa la Agano Jipya (Mdo 2:47, Mdo 1:14, Mdo 6:4, Col 4:2).<br><br>Kuabudu kwao kulitoka kwenye mioyo iliyokuwa na “furaha na shangwe.” Ilikuwa kitu cha kawaida kumuitikia Mungu kwa furaha waliyopata katika Kristo na katika uwepo wa waumini wengine. | Katika kikundi kiini, kuabudu ni kusifu na kutukuza Mungu kwa kuzingatia asili yake, matendo, na maneno, ili kumletea Mungu furaha.<br><br>**Kazi zinazowezekana**<br>• Kuimba nyimbo<br>• Kumtukuza Mungu kwa ajili ya ukuu wake<br>• Kumshukuru Mungu kwa mambo yote<br>• Kumwabudu Mungu kwa jinsi alivyo<br>• Kuomba kwa sauti au polepole<br>• Kusoma vifungu vya kuabudia (Mf. Zaburi)<br>• Kuandika/au kusoma mashairi ya kikristo |

| Kazi ya Kuinjilisha | |
|---|---|
| ***Katika Kanisa la Agano la Jipya*** | ***Katika Vikundi Kiini*** |
| Kulikuwa na kuwajibika kwa hali ya juu katika kanisa la kwanza kwenye "huduma ya neno" (Mdo 6:4).<br><br>Waumini wa kwanza walijitoa kwenye mafundisho ya mitume (Mdo 2:42), na kanisa lilipoenea, mafundisho haya yakawa katika mfumo wa barua kutoka kwa mitume kwenda kwenye kanisa (Col 4:16, Flp 1:1, Gal1:2). | Katika kikundi kiini, ni hatua ya kusaidiwa, kufundishwa na kushauriwa na wengine, ili kukua katika akili na katika roho kuelekea kivuli cha Kristo.<br><br>**Shighuli zinazowezekana**<br>• Kukariri maandiko<br>• Kujifunza mafungu ya Biblia kama kikundi<br>• Kujifunza kutumia Biblia katika maisha ya kila siku<br>• Kutumia mda pamoja kwa akina dada na kaka waliokomaa<br>• Kushiriki katika huduma na kikundi<br>• Kujifunza na kutumia vipawa vya kiroho |

| Kazi ya Uinjilisti | |
|---|---|
| ***Katika Kanisa la Agano Jipya*** | ***Katika Vikundi Kiini*** |
| Kushirikishana habari njema ya Yesu Kristo ilikuja kiasilia kwa waumini wa kanisa la kwanza. Uinjilisti hakikuwa "kipindi" ambacho walitakiwa kukianzisha, wala kuwa kitu fulani ambacho ilikuwa wafundishwe kwa ajili yake—ilikuwa upendo wa Kristo uliokuwa ukijionyesha wenyewe kupitia maisha yao na maneno kwa wanaowazunguka (Mdo 5:42, 4:20). Ilikuwa Roho Mtakatifu aliyekuwa akifanya kazi ndani yao (Mdo 4:31), walipokuwa wakimtangaza Kristo kote katika majumba na katika sehemu za jumuia (Mdo 20:20). Matokeo yake ilikuwa watu kuamini katika jina la Bwana Yesu na waliookoka (Mdo 8:12, 16:31-34). | Katika kikundi kiini, uinjilisti ni kuwafikia nje kwa habari njema za upendo wa Kristo kwa watu wenye mahitaji, ili kuwasaidia kumjua Mungu kama Baba na Kristo kama Mwokozi.<br><br>**Kazi Zinazowezekana**<br>• Kuomba na watu wengine wawili katika maombi ya utatu kwa ajili ya marafiki ambao hawajaokoka<br>• Kuwakaribisha wasioamini kwenye kikundi<br>• Kusaidia mahitaji ya watu nje ya kikundi<br>• Kufanya urafiki na wasioamini<br>• Kushirikisha Kristo kwa wasioamini |

## III. FAIDA ZA VIKUNDI KIINI

### A. Faida kwa Uinjilisti

Mara nyingi, makanisa yetu yana mipaka inayoonekana na isiyoonekana ambayo inawazuia watu nje. Tuna mapokeo, tuna namna tunavyovaa na kutenda, na pengine kuwa na matarajio kwa hao ambao wangetutembelea. Mapokeo yanaweza kuwa mazuri kutoa maana ya jamii na mwendelezo, lakini inaweza kufanya vigumu hasa kwa watu kuja makanisani kutoka "nje."

> Asili isiyo ya kawaida ya vikundi kiini vinatoa "daraja" ya kawaida zaidi kwa wasioamini.

Utafiti umeonyesha kwamba ni vigumu kwa watu kuvuka mipaka ya tamaduni zao kwenda kanisani. Kama wanatambua kuwa watatakiwa kuvaa tofauti, au kujifanya kuwa vile amabavyo sivyo walivyo, hawatahudhuria kanisa. Wanajisikia kana kwamba kuna ghuba pana kati yao na kanisa.

Vikundi kiini vinatoa zaidi "daraja" la kawaida kwa wasioamini. Kwa kuwa wajumbe katika kikundi kiini wanaanzisha mahusiano na marafiki wasioamini, ni hali ya kwawaida kwao kuwakaribisha kwenye mkutano wa kikundi. Na kwa asiyeamini, kuja kwa wachache, kukutana kusikokuwa kwa kawaida hakutishi zaidi kuliko kwenda sehemu ambayo hawajui mtu yeyote na hawana uhakika wa "taratibu" zilivyo.

Katika Yohana 13:35, Yesu alisema, “kwa hili watu wote watajua kuwa ninyi ni wanafunzi wangu, kama mnapendana ninyi kwa ninyi.” Wageni wanapokuja kwenye kikundi kiini, moja ya ushuhuda wenye nguvu watakaokuwa nao ni kujali na kulisha neno ambako kunatokea katika kikundi. Waanatakiwa waone tofauti katika tabia zetu, maneno na matendo , na kuanza kushangaa kwa nini tuko tofauti. Wanapoona upendo katika kikundi na kuona kujaliwa huko na kujipenda wao wenyewe, watavutwa kwa Yesu, chanzo cha upendo huo.


**B. Faida kwa Kuanzisha Mahusiano**

Tunapoangalia huduma ya Yesu hapa duniani, ni muhimu kutambua kuwa alichagua kuishi katika jamii na wafuasi wake. Watu hawa kumi na wawili waliomba pamoja, walimwabudu Mungu pamoja, walijifunza kwa neno la Yesu na mfano, walikula pamoja, walitiana moyo, kutangaza habari njema ya wokovu kwa pamoja. Hakika, haikuwa ajali kwamba Yesu alichagua kutumia kikundi kuwaandaa wafuasi wake kwa ajili ya huduma. Kikundi chao kilikuwa ni kikundi “kiini” cha kwanza chenye uhai ambacho, kama mfano wa mbegu ya haradali katika Mathayo sura ya 13, ilianza ikiwa kidogo na kwa haraka ikakua kuwa kubwa sana.

Huduma inayofanywa katika vikundi kiini ina faida nyingi, na moja ya faida ni maendeleo ya kawaida ya mahusiano katika kikundi. Kikundi kinapokutana katika ushirika, kuabudu, kufuasisha, na uinjilisti, kila moja ya shughuli hizi inachochea hali ya pekee ya uhusiano. Mahusiano haya, pia yameonyeshwa katika kielelezo 1.1, ni”

- Ushirika: mtu kwa mtu
- Kuabudu: Mtu kwa Mungu
- Kufuasisha: Mungu kwa mtu
- Uinjilisti: Mwili wa Kristo kwa waliopotea

**Kielelezo 1.1 Aina Nne za Mahusiano ya Kikundi Kiini**




Katika kikundi kiini, Wajumbe wanatumia mda pamoja, kushiriki katika huduma pamoja, kutiana moyo na kuombeana, na kusaidiana mmoja kwa mwingine katika masumbufu na mahitaji. Kuna nguvu na mkazo kwenye upendo wao na sala kwa Mungu na kwa mmoja kwa mwingine. Wanajisikia kuwa shehemu, kuwa sehemu ya jumuia ambayo inawajali. Wajumbe wa kikundi wanapokua katika upendo wao wa mmoja kwa mwingine, kuna kitu maalumu sana juu ya mda waliotumia pamoja katika kuabudu, wanapoonyesha upendo pamoja walionao kwa Mungu.

Kikundi kiini pia kinatoa mazingira kamili ya maendeleo ya kushauri au mahusiano ya kufuasisha. Waumini waliokomaa zaidi wanaweza kuja bega kwa bega na waumini wachanga kuwatia moyo, kuwafundisha, na kufanya huduma pamoja nao.


Kwa kuwa moja ya lengo la kikundi kiini ni kukua na kuongezeka, wajumbe mara zote wataendelea kuangalia njia za kuwafikia nje waliopotea. Wataweza kushirikishana hisia na kujifunza kutoka kwa kila mmoja njia tofauti wanazoweza kushirikisha Kristo kwa familia zao na marafiki. Kuna kujitoa katika kikundi kiini kujenga mahusiano na wasioamini, ili kuweza kuwashirikisha habari njema ya Yesu.

### C. Faida za Kufuasisha

Warumi 14:19 inasema, "Basi kama ni hivyo, na mfuate mambo ya amani na mambo yafaayo kwa kujengana." Vikundi kiini vinatoa nafasi ambapo waumini wanaweza kuhudumiwa, na ambapo wanaweza kuhudumia wengine. Biblia inadokeza wazi wajibu ambao waumini wanao mmoja kwa mwingine. Yote haya yanatokea kikawaida katika kikundi kiini, wakati kila mtu anapohudumu kulingana na kipwa chake.

Huduma kati ya waumini ni kipengele muhimu cha kanisa la kikundi kiini. Waumini watajaribu kupita katika vipawa vinavyojenga kanisa (1Kor 14:12). Vipawa vya kiroho vilitolewa kuandaa watu wa Mungu kwa kazi za huduma, Ili kwamba mwili wa Kristo uweze kujengwa (Efe 4:12). Tunatakiwa kutiana moyo mmoja kwa mwingine (1The 4:18) na kuongea maneno ambayo yatawajenga wengine kulingana na mahitaji yao (Efe 4:29). Hii inamaanisha kwamba tunashirikishana mizigo mmoja kwa mwingine (Gal 6:2) ili kwamba tuweze kusaidiana. Haja yetu kubwa zaidi inatakiwa iwe kuheshimiana katika upendo wa kindugu (Rum 12:10) na kupendana kwa undani, kutoka moyoni (Pet 1:22). Nguvu ya kikundi kiini inatoa njia ya kawaida na ya ufanisi kwa waumini kutimiza agizo la kibiblia la kujengana, kama ilivyoonyeshwa katika kielelezo 1.2.

**Kielelezo 1.2 Kufuasishana Wao kwa Wao**




Vikundi kiini pia ni mahali ambapo vipawa vya kiroho vya kila mjumbe vinagunduliwa, kuendelezwa na kutumika. Katika maandalizi ya kikundi kiini, watu wanalishwa neno na kutiwa moyo kuvitambua vipawa vyao kiroho kwa kujihusisha kwao kwenye huduma ya kiini. Kwa njia hii, wanakua katika imani zao na kukomaa, na kupata nafasi ya kufuaswa na wakristo waliokua zaidi. Katika kipindi, watakapoanza hatua hii na kuanza kufuasisha hao walio katika kikundi ambao hawajakomaa kiroho.

Wakristo wengi wapya watakuwa na matatizo mengi na mahitaji ambayo kikundi kinaweza kusaidia. Kikundi kiini kinaweza kwa ufanisi kuwatunza na kukidhi mahitaji ya watu kimwili, kiroho, kijamii na kihisia. Wajumbe wa kikundi wanakua kujua na kupendana kwa kushirikishana mahitaji haya na kwa kufanya kazi pamoja kuyatimiza. Kwa walio wengi, itakuwa mda wao wa kwanza kujifunza kwamba ukweli kutoka kwenye Biblia unaweza kulinganishwa kwenye maisha yao ya kila siku. Watajifunza jinsi ya kusoma Biblia wao wenyewe, na jinsi ya kutumia wanayojifunza kwenye matatizo na magumu wanayokutana nayo.

### D. Faida kwenye Kuendeleza Viongozi

Kipengele kingine cha hakika cha kuanzisha makanisa kwa kutumia vikundi kiini ni swala la uongozi. Robert Logan, katika toleo lake "Kuzaliana kwa Vikundi Kiini," inasema, "Ni watu wangapi ambao mtu mmoja aliyejazwa na roho anaweza kuhudumia au kufundisha? Kristo mwenyewe aliishia kumi na wawili. Hata hivyo hapa tu, wachungaji, na viongozi wasio na ujuzi, wanaojaribu kujiingiza katika zizi na kisha kwa mkono mtupu kutunza mahitaji ya watu katika vikundi vya 50, 100, 250, 500 na wakati mwingine watu 1000! Je sisi ni wakuu zaidi ya Bwana wetu? Ingawa kwa jinsi fulani kutegemea tofauti za tamaduni, kumi wanaonekana kuwa idadi ya kati ya watu ambao kwa utoshelevu wanaweza kuhudumiwa na mtumishi ambaye amejazwa na Roho ambaye hana ujuzi." Faida za vikundi kiini ni kwamba viongozi wanawajibika kwa maendeleo ya kiroho ya watu walio wa kwenye kiganja, na siyo kumi au mamia. Hii inawaondoa viongozi wanaojaribu kuhudumu mpaka kufikia hatua ya kuishiwa nguvu.

Njia ya kikundi kiini pia inahusisha watu wengi zaidi kama inavyowapa viongozi wasio na ujuzi nafasi ya kuendeleza vipawa vyao vya kiroho vya uongozi. Badala ya kuwa na "wenye daraja la ujuzi" wanaopewa nafasi za uongozi kutokana na yale wanayoyajua, viongozi wa vikundi kiini wanastahili kwa ukomavu na uwezo walioonyesha kupitia huduma zao katika kikundi kiini.

### E. Faida kwa Upandaji Kanisa

Matumizi ya vikundi kiini yana faida nyingi katika hatua ya upandaji kanisa. Ili kuanzisha makanisa mapya, unahitaji kuinjilisha, kuwajenga waumini wapya katika imani zao, kuendeleza viongozi wapya na kuhakikisha kuwa kila kazi za kanisa zipo. Vikundi kiini vinatoa njia za kukamilisha malengo yote haya. Viini pia vinaweza kutoa hali ya kujisikia kushiriki katika kanisa jipya.

> Vikundi kiini vinaweza kutumika kwa faida ya wapanda kanisa, haijalishi ni aina gani ya mtindo kanisa linaofanyia kazi.

Kuna njia nyingi za kuanza kanisa. Fikiria nyuma kwenye maono ziada 3A "Mitindo ya Upandaji Kanisa" kutoka katika mwongozo wa 1. Baadhi ya makanisa mapya yanaanza kutoka kwenye kusanyiko lililopo (mtindo wa kanisa binti). Mengine yanaanzishwa na timu ya wapanda kanisa wanaopelekwa kwenye eneo mpya kutoka kwenye kanisa lililpo (mtindo wa ukoloni). Bado mengine yaanzishwa kwa kujitegemea kwa muundo wa kanisa lililopo (mtindo wa timu ya misheni). Mengine yanaanzishwa katika majengo ya kawaida ya kanisa, na mengine yanakutana isivyo kawida katika miji ya watu. Moja ya faida kubwa zaidi za vikundi kiini ni kwamba vinaweza kutumika kwa faida ya wapanda kanisa, haijalishi ni aina gani ya mtindo kanisa linaofanyia kazi.

Katika mkakati wa kueneza upandaji kanisa, ni haja ya mpanda kanisa kujaza maeneo kwa makanisa ambayo yanazaa na kunzisha makanisa mapya mwenyewe. Ni nini baadhi ya vizuizi vya mapokeo kwa ukuaji wa kanisa na kuzaliana? Uinjilisti usio wa mafanikio, kukosa kufuasa, kukosa fedha za kutosha, ukosefu wa viongozi wa kutosha walioelimishwa, na mara nyingi, kukosa maono ya kuwafikia waliopotea kwa ajili ya Kristo. Vikundi kiini vinatoa njia ya kawaida na ya ufanisi kuinjilisha, kufuasa waumini wapya na kuendeleza viongozi wapya. Kama vikundi vinakutana katika majumba ya watu, kunaweza kukawa hakuna hitaji la jengo la kawaida. Kuondoa gharama hii kunawezesha kanisa kuanzisha makanisa mengine mapya wakati ambapo vikundi kiini viko tayari, siyo wakati ambapo fedha ipo. Kwa maneno mengine, kukosekana kwa fedha siyo kizuizi kwa ukuaji wa kanisa kawaida.

Vikundi kiini vinatoa uwezo wa kuendeleza mkakati ambapo ujirani mzima, mji, au nchi inaweza kuenezwa kwa ushuhuda wa mafanikio kwa ajili ya Kristo. Bila kuwa na vizuizi vya mapokeo kwa ukuaji, vikundi kiini vinaweza kutapakaa. Kwa kifupi inaelezwa, utumiaji wa vikundi kiini unarahisha uanzishaji wa makanisa mapya.

## MASWALI YA KUTAFAKARI, MARUDIO NA MATUMIZI

- Ni nini tofauti ya msingi kati ya vikundi kiini na vikundi vidogo?
- Huduma ya "mmoja kwa mwingine" inaweza kufanyika kwenye ibada ya mapokeo ya asubuhi jumapili? Nini itakuwa matokeo kwa wakristo kama mahitaji haya hayatatimizwa? Wakristo wapya watakua na kukomaa kama mahitaji haya hayakutimizwa?
- Kuna vizuizi vyovyote kanisani kwako ambavyo vinaweza kumzuia asiyeamini ambaye hajawahi kuwa kanisani asije katika moja ya ibada zenu? Ni jinsi gani vikundi kiini vinaweza kutumika kama "daraja" kwa wasioamini?
- Kwa ujumla, jinsi gani vikundi kiini vinaweza kutumiwa kama sehemu ya mafanikio ya kueneza mkakati wa upandaji kanisa?

## UTEKELEZAJI WA AZIMIO

Tafuta rafiki wa kikristo au unayemfahamu ambaye hajui juu ya vikundi kiini. Elezea kwake faida za njia ya vikundi kiini kwenye huduma, na muulize akupe sababu kwa nini anakubaliana au kutokubaliana na wewe. Kama inawezekana, jadili majibu yake na wafunzwa wengine wanaojifunza nyenzo hii.

## VYANZO

Logan, Robert. *Multiplication of Cell Groups*. Old Tappan, NJ: Fleming H. Revell Co.. n.d.

VIKUNDI KIINI

SOMO LA 2

# Kanuni za Uongozi wa Kikundi Kiini

☞ **Kusudi la Somo**

Kusudu la somo hili ni kutoa mtazamo kwa ujumla wa kazi na wajibu wa kiongozi wa kikundi kiini.

☞ **Wazo Kuu**

- Kazi kuu nne za kikundi kiini lazima ziwekwe katika mzani
- Ni muhimu sana kuanzisha kiongozi mwanafunzi

☞ **Matokeo Yanayotarajiwa**

Wakati yaliyoma katika somo hili yanapoeleweka , kila mshiriki anatakiwa:

- Kuelewa nafasi ya pekee ya kiongozi wa kikundi kiini katika huduma ya kikundi kiini kwa ujumla
- Kuelewa wajibu wa kiongozi wa kikundi kiini kwa kila shughuli za mkutano wa kikundi kiini.
- Kujua kanuni za kupanga kwa mafanikio kwa ukuaji wa kikundi kiini na kuongezeka.
- Kukamilisha mfano wa mpango wa mkutano wa "kwanza"wa kikundi kiini kukutana.

☞ **Ziada**

2A Kikundi kiini kivunja barafu

2B Mfano wa shughuli katika mkutano wa kikundi kiini

## I. WAZO LA UONGOZI KWA UJUMLA

### A. Kueleleza Maisha ya Kikristo

Kwa kuwa uinjilisti ni kipande muhimu cha huduma ya kikundi kiini, inaonekana zaidi kutakuwa na baadhi ya waumini wapya, au waumini wasiokomaa kiroho katika kikundi kwa kipindi fulani. Wengi wa watu hawa hawaelewi ina maana gani kuwa mkristo au ina maana gani kumtumikia Mungu katika huduma. Kiongozi wa kikundi kiini ana nafasi ya kuwafundisha vitu hivi kwa mfano wa jinsi anavyosema na anavyotenda. Anahitaji kuwa wazi na kundi lake juu ya baraka katika maisha yake vilevile na mizigo. Anatakiwa kushirikisha kundi lote mafanikio na mahangaiko katika kutembea kwake na Bwana , na jinsi anavyofanya kwenye misukosuko tofauti tofauti inayomzunguka. Hii haitatia moyo tu wajumbe wa kikundi kiini, lakini pia itasaidia kuwafundisha jinsi ya kuishi nje wanachoamini kwa njia ya vitendo.

Wakati kiongozi anapofundisha kwa "kuonyesha mitindo" wajumbe wa kikundi wataweza kuelewa zaidi maisha ya kikristo na kufundisha wengine. Nini njia mojawapo kati ya njia za kufundishia Yesu alizotumia kwa wanafunzi wake. Walivyotumia mda kuwa na Yesu, walijifunza kwa kifupi tu kwa kuangalia na kusikiliza. Katika 1Wathesalonike 1:6-7, Paulo, Silasi na Timotheo inaeleza jinsi Wathesalonike walivyogeuka kuwa "wa kuigwa" kwao, na kisha wakawa "kielelezo kwa waumini wote katika makadonia na Akaya." Paulo, katika 1Wakorintho 11:1, anawaelekeza waumini" kufata mfano wangu, kama ninavyofata mfano wa Kristo." Kiongozi wa kikundi kiini anahitaji kuweka mfano katika jinsi anavyoishi na huduma ambayo kundi lake litafata.

### B. Endeleza Viongozi Wapya

Moja ya kusudi la msingi la kila kikundi kiini ni kwamba kuzidisha chenyewe. Wakati kundi linapokuwa tayari kuzidisha, mtu aliyefundishwa na kuandaliwa anahitaji kuwa tayari kushikilia kama kiongozi wa kikundi kipya.

> Moja ya kipao mbele cha kwanza cha kiongozi wa kikundi kiini ni kuchgua mtu kwa maombi kutoka kwenye kikundi kuwa "mwanafunzi" kiongozi.

Moja ya faida za vikundi kiini ni kwamba vinatoa njia bora za kuendeleza viongozi wapya wa kikristo. Moja ya kipao mbele cha kwanza cha kiongozi wa kikundi kiini ni kuchagua mtu kwa maombi kutoka kwenye kikundi kuwa "mwanafunzi" kiongozi. Mtu huyo anatakiwa aonyeshe ujuzi fulani na utayari wa uongozi, Lakini hata kwa njia yoyote atakuwa na sifa zote za kiongozi mfanisi. Moja ya jukumu la kiongozi wa kikundi kiini ni kuwa mshauri kwa kiongozi mwnafunzi. Mwanafunzi hatakiwa kusikiliza tu na kuona yale kiongozi wa kikundi kiini anayofanya, lakini pia lazima achukue wajibu katika huduma ya uongozi. Somo la kikundi kiini la 9 "Kuwafundisha Viongozi wa Kikundi kiini kipya" (katika mwongozo 3) tutaona kwa undani hatua ya maendeleo ya uongozi mpya. Kitu muhimu zaidi cha kukumbuka wakati kundi jipya linapoanzishwa ni kwamba Mungu anahitaji kuinua mmoja au zaidi katika kundi hilo kuwa viongozi wa kikundi kiini wenyewe.

### C. Andaa na Toa Kwa Ajili ya Huduma

Wakristo wote wanatakiwa kuelewa ni vipawa gani vya kiroho ambavyo wamepewa na Roho Mtakatifu, na kujifunza jinsi ya kutumia vipawa hivyo. Hata hivyo, waumini wengi wana nafasi ndogo ya kutumia vipawa vyao vya kiroho, hata kama wanaelewa ni nini (na wengi wao hawaelewi). Asili ya kikundi kiini inawezesha wakristo siyo tu kugundua vipawa vyao vya kiroho, lakini pia kuviendeleza na kuvitumia vipawa hivyo katika huduma.

Kiongozi wa kikundi kiini anatakiwa kutoa njia kusaidia wajumbe kujua vipawa vyao vya kiroho. Kuna "majaribio" mbalimbali au "orodha ya vipawa vya kiroho"viliyopo kusaidia mtu kuelewa vipawa vya kiroho kwa ujumla, na kuwasaidia kuona ni kipawa gani ambacho pengine Roho Mtakatifu amewapatia. Mara nyingi, kipawa cha mtu kinaweza kudhihirishwa wanapoanza kujihusisha katika aina mbalimbali za huduma.

Kiongozi wa kikundi kiini lazima atoe nafasi zote kutambua vipawa vy kiroho na kutumia vipawa hivyo katika huduma. Hii inafanyika kimsingi kwa kudumu na kuongeza ugawaji wa huduma kwa wajumbe wa kikundi. Kiongozi ataweza tu kugawa kazi kidogo mwanzoni, lakini kadiri kikundi kinavyokua na kukomaa, anatakiwa aenmdelee kukazana kuhusisha kila mjumbe katika shughuli na huduma ya kikundi.

## II. KUONGOZA MKUTANO WA KIKUNDI KIINI


Hakuna mfumo "sahihi" wa mkutano wa kikundi kiini. Ni wajibu wa kiongozi kuamua jinsi gani mkutano utapangwa na kuendeshwa. Kwa jinsi hiyo, kila mkutano unatakiwa uwe na mda kwa ajili ya kila moja ya kazi za kikundi kiini (Ushirika, kuabudu, kuadilishana, na uinjilisti).

Mkutano wa "aina" ya kikundi kiini unaweza kuwa na utaratibu huu:

- Kuanza kwa mda wa ushirika na kushirikisha kati ya wajumbe wa kikundi.
- Kufuatiwa na mda wa kuabudu kwa maombi, kuimba na kumtukuza Mungu.
- Baada ya hili, Kuna mda wa kujadili na kujifunza Biblia
- Kisha kikundi kinahamia katika mda wa huduma ya kutafakari, ambapo wajumbe wanajadili kazi za binafsi na za kikundi kuwafikia marafiki, majirani na pengine kundi kubwa kwa injili. Hii inatakiwa ihusishe mda wa maombi kwa ajili ya mtu pekee ambaye hajaalikwa kwenye kikundi.

Kiasi cha mda uliotumika katika kila shughuli unategemeana ni kwa kipindi gani kikundi kimekuwa kikikutana. Mwishoni, kundi linatakiwa kutumia mda mwingi katika kushirikiana na kiasi katika kujadili Biblia. Katika mda, msisitizo zaidi utawekwa katika kujifunza Biblia na uinjilisti. Uwiano huu unaobadilisha unaonyeshwa katika kielelezo 2.1.

**Kielelezo 2.1 Kuwianisha Kazi za Kiini**




Kusema kwa ujumla, mkutano wa kikundi kizima cha kiini unatakiwa usizidi dakika 90. Kwa mfano, kikundi kinaweza kutumia dakia 20 za kushirikiana, dakika 20 katika kuabudu, dakika 30 katika majadiliano ya Biblia, na dakika 20 katika mda wa uinjilisti.

Kiongozi ana wajibu wa kuanza mkutano katika mda kamili, huku akihamisha kikundi kutoka shughuli moja hadi nyingine, na kumalizia mkutano katika wakati unaotakiwa. Kila moja ya kazi nne za kiini ni muhimu kwa ukuaji na ukomaavu wa wajumbe, kwa hiyo kiongozi anatakiwa kuhakikisha kuwa kikundi kinatumia mda kwa kila moja ya kazi.

Kiongozi wa kikundi anawajibika katika upangaji na uelekezaji wa kila moja ya mkutano wa kiini. Kadiri kiini kinavyokua na kukomaa, kiongozi ataweza kugawa shughuli mbalimbali kwenye mkutano kwa wengine katika kikundi. Kila kipengele cha mkutano kinahitaji aina fulani ya maandalizi:

**A. Mahali**

Kiongozi anahitaji kuamua wapi kikundi kitakutana na nani atakayekarimu kikundi. Karibu mara nyingi kiongozi pia anakarimu. Mkarimu anahakikisha kuwa chumba kimeandaliwa kwa viti ambavyo kila wajumbe wataweza kuonana (mduara unaruhusu kiwango kikubwa cha kuwasiliana miongoni mwa wajumbe). Kwa uchaguzi, mkarimu pia anaweza kufanya maandalizi ya vinywaji (ambavyo vinaweza kuwa rahisi kama vile chai na/kahawa).

**B. Ushirika**

Mda wa kuabudu unaweza kuwa kawaida au si kawaida kulingana na kiongozi anavyohitaji. Kama kuna mjumbe mpya au mgeni katika kikundi, inashauriwa kwamba unatumia aina fulani ya shughuli (kivunja barafu"kuwafanya kujisikia kukaribishwa, na kusaidia kila mtu katika kikundi kujifunza zaidi juu ya wengine. Mda wa kushirikiana ni kipindi ambacho wajumbe wanapata kujua kilichokuwa kinaendelea katika maisha ya wajumbe wengine, kuwatia moyo, kuwashirikisha furaha na huzuni, na kujengana.

Kwa mifano ya baadhi ya shughuli zitakazosaidia wajumbe wa kikundi kiini kuweza kujuana zaidi, tazama Ziada 2A "Kikundi Kiini Kivunja Barafu."

**C. Kuabudu**

Kuongoza kuabudu katika kikundi kiini kunawaandaa wajumbe kwa ajili ya mda uliobaki wa mkutano, hasa wanapomwangalia Mungu kuzungumza nao kupitia mda wa majadiliano ya Biblia. Kama kiongozi au mtu mwingine katika kundi ana uwezo wa mziki, kisha gita, au kinanda au chombo kingine cha mziki kinaweza kutumika kuongozana na mda wa kuabudu. Kama siyo, Mungu anafurahishwa kusikia sifa zinazoimbwa kutoka kwenye mioyo yenye furaha na shukurani.

### D. Maombi

Maombi yatakuwa sehemu ya kila shughuli ya mkutano wa kikundi kiini. Kiongozi anatakiwa kuanza na kumalizia kwa maombi. Kiongozi anatakiwa kufikiria kwamba kuomba kwa sauti hakutawapendeza wajumbe wapya, na anatakiwa aweke wazi kuwa hili ni la uchaguzi. Wanapotumia mda mwingi katika kikundi na wamethibitishwa na wajumbe, wataanza kufanya hili wao wenyewe.

Kuomba kutakuja kiasili wakati wa kipindi cha kuabudu, lakini kiongozi lazima apange kuwa na maombi wakati wa kipindi cha uinjilisti na wakati wa kushirikiana pia. Maombi ya utatu ni watu watatu wanaoomba pamoja hasa kwa wokovu wa marafiki watatu au wanaowafahamu kila mmoja (hii ni waumini watatu kuombea wasiomini tisa) na hii inaweza kuwa sehemu ya mda wa uinjilisti. Wakati wa mda wa kushirikiana, maombezi yanaweza kushirikishwa na kuombewa na kikundi. Nia nyingine ni kuomba katika makundi ya wawili, ambayo inaweza kutumika kuwatia moyo wakristo wachanga kuomba (mbao pengine wanaweza kuwa wanaona haya sana mbele za kikundi), vilevile kushirikishana mahitaji zaidi ya binafsi.

### E. Majadiliano ya Biblia

Ni wajibu wa kiongozi wa kikundi kiini ama kuanzisha somo kwa ajili ya mda wa kujadili Biblia, ama kugawa hili kwa mtu mwenye kipawa cha kufundisha. Njia ya kujifunza Biblia kwa kuongozwa na neno ni njia moja ambayo inatakiwa kutumika na kufundishwa kwa wajumbe wa kikundi kiini, ili kwamba wajifunze kujilisha wenyewe kutoka kwenye neno la Mungu. Wakati njia ya kujifunza Biblia siyo tu njia pekee inayoweza kutumika, kusudio la mda wa majadiliano ya Biblia inatakiwa iwe ugunduzi wa ukweli wa Biblia na jinsi ya kuutumia katika hali halisi ya maisha.

> Kusudio la mda wa majadiliano ya Biblia unatakiwa kuwa mda wa kugundua ukweli na jinsi ya kuutumia katika hali halisi ya maisha, siyo wakati wa mda wa kuhubiri.

Neno la tahadhali: Vikundi vingi vinaweka msisitizo mkubwa kwenye kujifunza Biblia, kwa kuwa hili limekuwa mtindo waliochunguza katika uzoefu wa kanisa lililopita. Wakristo wapya wana mahitaji maalumu. Msisitizo kupita kiasi juu ya mda wa kujadili Biblia unaibia mda kutoka kwenye shughuli zingine za kiini. Ni muhimu kiongozi kutunza uwiano wa kazi nne za kikundi kiini.

### F. Kufuasa

Kufuasa kunatokea wakati tunapomsaidia mtu fulani kwa uangalifu kufanana zaidi na Yesu katika tabia na kuwa mwaminifu katika huduma. Mkristo mpya ana mahitaji maalumu anapokuwa anashughulika na mashaka, kukatishwa tamaa, kutokufahamu mambo ya kiroho, vipingamizi vya kiroho na hali ya kujisikia “kutokutulia” katia makazi asiyofahamu. Mkristo mpya anahitaji kuwa na mtu fulani ambaye anaweza kujadiliana naye maswali, na ambaye anamjua kuwa anamjali. Kwa sababu ya ukaribu wa asili wa uhusiano wa kufuasa, wanaume wanatakiwa kufuasa wanaume na wanawake wanatakiwa kufuasa wanawake.

Kiongozi wa kikundi kiini anatakiwa kukabidhi “mzazi”wa kiroho kwa mkristo mpya kwenye kikundi. Kunatakiwa kusiwe na wakati amabapo mkristo mpya anakosa mtu wa kumfuasa na kumtunza. Kikundi kitasaida pia utaratibu, lakini kama Kristo alivyojihusisha kwa wanafunzi mmoja kwa mmoja, kwa hiyo kila mkristo mpya anatakiwa awe na mtu ambaye anaweza kujilinganisha mmoja kwa mmoja.

Usisahau kwamba kiongozi wa kikundi kiini lazima pia kwa maombi achague mtu fulani kutoka kwenye kikundi kuwa mwanafunzi kiongozi, mtu fulani ambaye kiongozi atafuasa kuwa kiongozi wa kikundi kiini kingine. Mwanafunzi anatakiwa kushirikishwa kwenye maswala ya huduma na kiongozi wa kikundi kiini, ili kwamba aweze kuona na kuzoea uongozi wa kikundi kiini mara moja.

### G. Uinjilisti

Kuanzisha maono ya huduma kwa wajumbe wa kikundi kiini ni wajibu wa kiongozi wa kikundi kiini. Kiongozi anawapatia wajumbe maono ya hitaji la kuinjilisha na kuanzisha mahusiano ambayo yatatoa njia ya kawaida ya kushirikisha Kristo. Anawasaidia kuona jinsi juhudi zao za binafsi kufika nje na kujiingiza kwenye juhudi za kiinjilisti za kikundi kiini kwa ujumla. Hii pia inaweza kufanyika kwa kusoma vifungu kutoka kwenye maandiko yanayohimiza wakristo

kushirikisha habari njema, na kisha kuwapa changamoto wajumbe kutumia vifungu hivi katika maisha yao.

Mda wa uinjilisti wa mkutano wa kikundi kiini ni mda mzuri sana kushirikishana shuhuda juu ya jinsi Mungu anavyofanya kazi katika na kwa maisha ya wajumbe wa kikundi kiini kuwafikia nje kwa upendo wa Kristo. Ni wakati pia ambao kiongozi wa kikundi kiini anaweza kukumbusha kikundi chote hitaji la kuzidisha na utaratibu wa vikundi vyao katika vikundi kiini viwili.

## III. UTAWALA WA KIKUNDI KIINI

Ingawa hakuna anayefurahia kazi za makaratasi, kuna sababu mbalimbali kwa nini kiongozi wa kikundi kiini anatakiwa kufanya kazi na kikundi chake kuandaa mpango wa malengo na makusudio ya kiini:

- **Uwajibikaji:** Kama wakristo lazima tuwe mawakala wema wa yale Mungu aliyotupatia, ikiwemo mda na juhudi tunazotumia kuongoza kikundi kiini. Kupanga kunatusaidia kufanya uwezekano wa matumizi ya machache tuliyonayo.
- **Ukuaji:** Kama unalinganisha kikundi kiini na meli safarini, kuwa na mpango kunaweza kufanya tofauti kati ya kikundi kiini kinachofata dazeni ya mwendo na kujikuta kikiwa kinazaa matunda sana na kingine ambacho kinashangaa bila kuwa na dhumuni kwenda kila mahali upepo unapokivutia. Mungu anahitaji kwamba viini katika kanisa vinakua na kuzidisha, vinapofanya kazi kuelekea agizo la Utume Mkuu. Kuwa na mpango kamili, kikundi kiini kitadumu katika kusudio na kufikia lengo hili la kukua, kuendelea na kuongezeka.

Upangaji unahusu sehemu tatu rahisi-za utaratibu.

1. Ya kwanza, Omba na muulize Mungu kukupa hekima unapokuwa unapanga (Yok 1:5).
2. Ya pili, Jaribu kupanga malengo yanayowezekana na makusudio kwa ajili ya kikundi chako, Na anzisha mda wenye tarehe kwa kila lengo na kusudio.
3. Ya tatu, Kwenye mda weka na mda wa kipindi kwa ajili ya tathimini ya maendeleo yako.

Unapoendelea na utaratibu huu wa kuomba, kupanga na marudio, utaanza kuona maeneo ambayo yanayohitaji uangalizi na hatua ambazo zinzazotakiwa kuchukuliwa kuyafikia malengo uliyopanga. Mara chache kikundi kiini chako kinaweza kutaka kurekebisha malengo yake na tarehe, lakini hii ni sehemu ya kawaida ya hatua ya upangaji.

## MASWALI YA KUTAFAKARI, MARUDIO NA MATUMIZI

- Kiongozi wa kikundi kiini anatakiwa kugawa shughuli na majukumu kwa wajumbe wote wa kikundi kiini, na siyo tu kwa mwanafunzi kiongozi? Kwa nini na kwa nini siyo?
- Kwa nini ni muhimu kwamba kila mjumbe mpya wa kikundi akabidhiwe kwa “mzazi” wa kiroho wa kumfuasa?
- Ni mda gani baada ya kikundi kuanza kiongozi wa kikundi kiini anatakiwa asubiri kabla hajachagua kiongozi mwanafunzi? Ni aina gani za shughuli kiongozi wa kikundi kiini anaweza kufanya na mwanafunzi kumuandaa kuongoza kikundi chake?
- Kwa nini kiongozi wa kikundi kiini ajisumbue kuanzisha mpango wa kikundi kwa ujumla, na kwa kila moja ya mkutano? Kwa nini asiache kundi kuhusika “kiasili” katika mwelekeo wowote kinaotaka?

## UTEKELEZAJI WA AZIMIO

Rudia Ziada 2B, “Mfano wa Shughuli katika Mkutano wa Kikundi Kiini.” Ziada hii ina ushauri wa nini kifanyike katika wakati wa mkutano wa kikundi kiini kwa kila moja ya kazi. Kiongozi wa kikundi kiini anaweza kutumia ushauri huu, au kuzikarabati kadiri inavyohitajika kwa hali yake maalumu.

## VYANZO

Trinity Christian Center, *Cell Groth and Evangelism Strategy Seminar*, N.p., n.d.

VIKUNDI KIINI ZIADA

2A

# Vikundi Kiini Vivunja Barafu

*"Vivunja barafu" vinachekesha, njia zisizotisha za kuwajua watu zaidi. Hizi zinatumika mara nyingi wakati wa mda wa ushirika wa kikundi kiini kipya. Baadhi ya nukuru:*

- Kivunja barafu lazima kifae kwa ajili ya kikundi kiini. Ni ya kitoto zaidi, watu hawatajisikia kuridhika. Kama inatisha zaidi, watu watarudi nyuma.
- Weka wazi kwamba kila mmoja anatarajiwa kushiriki.
- Baadhi ya vivunja barafu vinaweza kutumika mara nyingi.
- Uwe na hali ya kuwafahamu watu ambao wanaonekana kutoridhika na mchezo au shughuli.
- Vivunja barafu vinageuka kuwa vifupi na umuhimu mdogo wakati kikundi kinaposongamana kwa nguvu kwa kipindi cha mzunguko wa maisha ya kikundi kiini. Unaweza kutumia nusu ya mda kwenye vivunja barafu wakati wa mikutano miwili ya kwanza, lakini unahitaji tu kutumia dakika 10 au 15 baada ya miezi michache.

**Maswali ya Kufungulia**

Ulipokuwa kati ya umri wa miaka 7-12….

1. Uliishi wapi? Ulikuwa na dada na kaka wangapi?
2. Ni aina gani ya usafiri familia yako walitumia?
3. Ni mtu gani ulijisikia kuwa karibu sana naye?
4. Ni lini Mungu alikuwa wazi zaidi kwako kuliko maneno?

**Mimi ni Nani?**

Andika majina ya wanaojulikana/ au wahusika katika Biblia kwenye karatasi. Zigundishe kwenye mgongo wa kila mmoja. Mtu hawezi kusoma karatasi yake. Watakwenda nyuma ya chumba wakiuliza swali moja baada ya mda juu ya wao ni nani mpaka watakapohisi wao ni nani.

**Nitabahatisha Wewe Hujui Hili**

Kila mtu kwenye kikundi anaandika kwenye kipande wazi cha karatasi kitu fulani anachodhani kwamba hakuna mtu kwenye kikundi atakayejua juu yake. Vipande vya karatasi vinakunjwa, na kuchanganywa vizuri, na kuwekewa namba kwa kufuatana. Kisha mtu aliyechaguliwa anaanza kuzisoma, kwa kusema namba kwanza. Kila mjumbe wa kikundi anaanza kubuni orodha ya watu ambao anajisikia zaidi kwamba wanaoana na kila muhusika. Baada ya kidokezo cha mwisho kusomwa, mtu mwenye kuoanisha kwa usahihi anakuwa mshindi.

**Utangulizi**

Kila mtu katika kikundi anaambiwa kuwa wana dakika kadhaa za kufikiri swali na kuliuliza watu wengine kwenye kikundi. Baada ya kila mmoja kufikiria swali, wanatakiwa kuanza kuzichanganya na za wengine, wakiuliza maswali yao. Andika jina la kila mtu na jibu. Baada ya kama dakika 10, kikundi kinakwenda kwenye mzunguko na kueleza walichopata juu ya kila mtu. Kadiri swali linavyokuwa zuri, ndivyo utakavyopata majibu yenye ubunifu na ufahamu.

### Aina Mbili za Ukweli na Uongo

Kila mtu aandike ukweli wa mambo mawili juu yake na uongo mmoja. Kila mmoja kisha anaamua ni kipande gani cha karatasi kiende na mtu gani, ni yapi maelezo yake yalikuwa uongo. Unaweza kuacha sehemu ya kwanza yaani (kila mtu anashikilia kipande chake cha karatasi na watu wanabuni tu ni maelezo yapi ni uongo). (siyo halali kama mtu fulani anachukua uongo karibu na ukweli).

### Kutoa Taarifa ya Hali ya Hewa

Nenda katika mzunguko, anza na kiongozi, na eleza jinsi unavyojisikia kwa sasa kwa maana ya kutoa taarifa ya hali—kuwa na mawingu kidogo, jua, n.k. Washiriki wanaweza kuelezea kwa nini wamechagua aina hiyo ya hali ya hewa. Kiongozi anaweka mfano kwa undani.

### Kutembea kwa Tumaini

Unda vikundi katika jozi. Mfunge kitambaa mtu mmoja usoni katika kila jozi. Kila mtu ambaye hakufungwa kitambaa usoni anamwongoza aliyefungwa kitambaa usoni kuzunguka kwenye ujirani wa sehemu ya mkutano kwa ujumla. Jaribu kutoa tofauti nyingi za uzoefu—zichukue mpaka kwenye ngazi fulani, nenda nje na ndani, wasaidie kugusa vitu mbalimbali (majani, sakafu, uchafu) lakini usiseme kitu baada ya kuwa mmeanza kutembea. Unaweza bila kuongea kuwakilisha kila ujumbe. Baada ya kama dakika tano badilisha sehemu. Baada ya dakika zingine tano kikundi kinakutana tena. Shirikisha ni aina gani ya hisia ulizokuwa nazo ulipokuwa umefungwa na ulipokuwa ukigusa vitu, n.k. Umejisikiaje juu mtu mwingine? Ilikuwaje kutokuwa na udhibiti wa yaliyokuwa yakitokea? Umejifunza nini juu yako mwenyewe? Hii inahusianaje na uhusiano wako na Mungu? Na wengine?

### Mchezo wa senti

Kama una watu wapya katika mkutano wako wakati mwingine, Unaweza kutunza mchezo wa senti kichwani kwa ajili ya kivunja barafu. Mpe kila mmoja senti kumi. Kila mtu lazima aandike jina la kitu kimoja juu yake mwenyewe ambacho kinatofautiana na cha kila mtu mwingine. (Kwa mfano, mjumbe jasiri wa kikundi anaweza kusema, “Nimepanda vilele vya mkuki.”) Msemaji anaweka senti katikati. Kama mchezaji mwingine pia amepanda kilele cha mkuki, anaweza kuweka senti pia. Mtu wa kwanza kumaliza senti zake zote anashinda.

### Kutegua Kwa Timu

Kwa shughuli hii unahitaji timu mbili na vyumba viwili. Gawanya kikundi katika timu mbili. Timu A inafikiri juu ya aina ya mwendo au shughuli kwa ajili ya kuigizwa na timu B (mf. Kunywa chai asubuhi) bila kutumia maneno yoyote. Timu A inamwambia mtu mmoja tu (tutamwita “Laura”) kutoka timu B shughuli ni nini, na Laura haruhusiwi kumwambia mtu mwingine yeyote katika timu yake. Timu B inasubiri katika chumba cha kwanza, wakati Laura akichukua mtu mwingine kutoka kwenye timu yake (Tutamwita “Michael”) kwenye chumba cha pili. Katika chumba cha pili, timu A inaangalia wakati Laura anaigiza shughuli kwa ajili ya Michael (kumbuka, hakuna maneno!) Kisha Laura anarudi kwenye chumba cha kwanza na kumpeleka mwingine mmoja kutoka timu B. Kisha Michael anaigiza shghuli kwa mtu mwingine, na Michael anarudi kwenye chumba cha kwanza na kumpeleka mwingine kutoka kwenye timu yake. Utaratibu huu unarudiwa, mpaka mtu wa mwisho kutoka timu B anaangalia shughuli. Mtu wa mwisho kwa hiyo lazima abuni shughuli ni nini. Kisha timu zinabadilishana wajibu na timu B inafikiri juu ya shughuli kwa ajili ya timu A kuigiza.

### Majibu na Waandishi

Kwenye vipande vya karatasi, andika maswali yanayotisha au yasiyotisha ambayo yanaweza kudhihirisha kitu fulani juu ya mtu (mf. Ni nini mali unayopenda zaidi? Ni nini ungependa kufanya ambacho huwezi kufanya kwa sasa? Ni yapi mapumziko yako ya maana? Watu wanatakiwa kujibu kila moja, au angalau matatu, lakini waelekeze wasiweke majina yao kwenye karatasi. Kisha kiongozi anakusanya karatasi na kusoma majibu yake, na kila mmoja anajaribu kubuni nani ametoa majibu hayo.

### Majirani Zangu Wote

Kila mmoja anaanza kukaa kwenye viti vilivyoandaliwa katika mduara, kasoro mtu mmoja ambaye anaanza kusimama katikati. Mtu wa katikati anahitaji kutafuta baadhi ya "majirani." Kufanya hili anahitaji kufanya maelezo ya kweli juu yake mwenyewe, ambayo pengine yatakuwa kweli juu ya majiarani zake (Mf. "Majirani zangu wote wanapiga kinanda"). Kila mtu ambaye atasema maelezo haya kiukweli lazima asimame na kutafuta kiti kipya. Hawezi kurudi kwenye kiti alipokuwa amekaa. Mtu wa katikati pia anatafuta kiti. Kwa hiyo kila wakati kutakuwa na mtu atakayekuwa katikati bila kiti. Lazima atoe maelezo ya kweli na kutafuta baadhi ya "majirani" ambao kwao maelezo hayo pia ni kweli.

### Majadiliano ya Kikundi

Chini kuna maswali machache ambayo yanaweza kutumika wakati wa mda wa kushirikiana. Tambua kuwa baadhi ya maswali haya yanafaa kwa vikundi vichache, na baadhi ya maswali ni vizuri yakiwekwa kwenye vikundi ambavyo wajumbe wameshajuana kidogo. Kawaida, swali moja tu litatumika katika kila mkutano wa kikundi kiini.

1. Ni wakati gani ulikuwa wa furaha katika maisha yako?
2. Unaweza kutuambia nini kuhusu tarehe yako ya kwanza?
3. Ni nini majuto makubwa kuhusu maisha yako?
4. Ni kitu gani kilikuwa kigumu katika vitu ambavyo umewahi kufanya?
5. Ni sifa gani kubwa ambayo umewahi kupata?
6. Ni nani rafiki yako sana wa hapa duniani? Mwelezee
7. Ni chumba kipi katika nyumba yako unachopenda zaidi?
8. Ni kitu gani kimoja unataka kukitimiza wiki ijayo?
9. Ni wapi ulijisikia uvuguvugu na usalama ulipokuwa mtoto?
10. Kama ulikuwa na mashine ya mda ambayo ingefanya kazi mara moja tu, ni hatua gani ya mbeleni au katika historia ungetembelea?
11. Ni lini mara ya mwisho umefanya kitu kwa mara ya kwanza?
12. Wakati wa chakula marafiki zako wanaaza kukuumbua kawaida ya kirafiki. Unafanya nini?
13. Kama ungeweza kunywa vidonge ambavyo vitakuwezesha kuishi mpaka kufikia miaka 1000, unaweza kunywa? Kwa nini?
14. Unapofanya kitu fulani kiupumbafu, ni kwa kiasi gani inakuudhi kuona watu wengine wamejua na kucheka?
15. Ungependa kujua tarehe kamili ya kifo chako?
16. Kama ungeweza kubadilisha mambo mawili ya jinsi ulivyolelewa, yangekuwa ni yapi, kama umetoka katika familia iliyoachika, ni kwa jinsi gani imekuathiri?
17. Ni yupi ndugu yako unayempenda zaidi? Kwa nini?
18. Ni kumbukumbu gani ya mda uliotumia, kama mtoto, na baba yako? Na mama yako?
19. Ni nani Mungu alimtumia kukuweka katika hatua ambayo ulijua kwamba ulimuhitaji Yesu?
20. Kama ungebadilisha sehemu na wahusika wa Biblia, Ni yupi ungechagua? Kwa nini?
21. Ni kitabu gani cha Biblia unachokipenda zaidi? Kwa nini?
22. Kama ungekwenda sehemu yoyote ulimwenguni, ni wapi ungekwenda?
23. Fikiria nyumba yako iko inawaka moto na una mda tu wa kuchukua kitu kimoja (familia yako iko salama). Ni nini utachukua?
24. Ni kipindi gani katika TV unachopenda zaidi?
25. Ni nani amekuwa na mguso mkubwa katika maisha yako tangu tulipokaa kwa mara ya mwisho?
26. Ni kitu gani kizuri kimekutokea wiki hii iliyopita?
27. Fikiria mda ambao ulishindwa hivi karibuni?
28. Taja mtu fulani unayemtamani ambaye ameweza kushinda vipingamizi vikubwa kufikia alipo sasa?
29. Ni kitu gani unathamini zaidi katika uhusiano wa kibinadamu? Katika uhusiano wako na Kristo? Na wazazi wako?





30. Unafanyaje unapokuwa hukushukuriwa kwa kutoa mda wako kwa ajili ya mtu fulani?
31. Ni mda gani mzuri zaidi kwako katika siku?
32. (Bachela) Aina ya msichana /mvulana ninayetaka kuoa/kuolewa… (Wliooana) Nini kilinisababisha kuolewa au kuoa mwenzi wangu?
33. Ni nini kilikuwa cha kukatisha tamaa katika maisha yako?
34. Ni vipawa gani (mbali na kukata shauri kwako) ambavyo hutasahau?
35. Ni nini ilikuwa tukio muhimu katika maisha yako wiki hii iliyopita?
36. Kama ungechagua kwenda sehemu yoyote duniani kwa siku tatu, wapi ungekwenda na kwa nini?
37. Kama ungechagua kukutana na mtu yeyote ambaye amewahi kuishi katika nchi yako, angekuwa nani huyo, na kwa nini ungependa kukutana naye?
38. Kama ungechagua kuishi kokote ulimwenguni, ni wapi ungeishi, na kwa nini?
39. Ni kipawa gani (kiroho, kihisia, kiakili n.k.)unaamini unakileta kwenye mkutano huu? (kwa maneno mengine, Ni nini unadhani unaleta ambacho kinaweza kuchangia kwenye kutia moyo kwa wengine?
40. Ni uzoefu gani ulikuwa wa maana katika maisha yako ambao ulibadilisha utaratibu wa thamani yako kabisa kabisa?
41. Ni nini baadhi ya malengo yako kwa miaka ijayo?
42. Ni nani wazazi wako, ni nini wanafanya na nini ungependa kubadilisha juu yao?
43. Kama ingekuwa kwamba uchague cheo chako tena, ungefanya nini?
44. Kama unakuwa kiongozi wa nchi yoyote ulimwenguni ingekuwa ipi na kwa nini?
45. Ni nini ulikuwa uzoefu wako mzuri na mbaya zaidi wa wiki yako?
46. Kama ungechukua safari ya bure ya wiki-mbili kwenda sehemu yoyote ulimwenguni, ingekuwa wapi na kwa nini?
47. Kama ingekuwa kwamba uongee na mtu yeyote anayeishi sasa, angekuwa nani na kwa nini?
48. Mpe kila mmoja kipande cha karatasi na waambie kuchora picha ya kazi zao au chochote wanachofanya kila siku. Elezea michoro yako.
49. Kwa nini una furaha kuwa katika kikundi kiini hiki jioni ya leo?
50. Ni nini baadhi ya hatua imara na dhaifu katika uhusiano wako na mtoto wako mkubwa au wazazi wako-mashemeji au mme wako?
51. Mjulishe kila mmoja kwamba wamepewa dola milliono moja. Ruhusu kila mmoja kusema ni jinsi gani angetumia kipato chake kipya.
52. Una jina la utani na kama ndiyo ni lipi? Ni majina gani ya utani uliyonayo kwa ajili ya mme wako na watoto?
53. Kuna kipindi cha wakati ambacho ungependa kuwa ungeishi humo? Kama ndiyo kwa nini?
54. Kikundi kiini kimekuwa msaada kwako? Tumia mda kukiongelea na kushukuriana.
55. Kiambie kikundi kiini vitu vitatu ambavyo unashukuru juu ya familia yako na njia tatu ambazo unakuta ugumu juu yake katika nyakati.
56. Ni kitu gani kimoja ungependa kuona kinatokea mda huo katika familia yako? katika kanisa lako? Katika kikundi kiini chako? Katika ulimwengu?
57. Ni rafiki gani wa karibu uliyenaye kwa kipindi hiki katika maisha yako?
58. Umekuwa na maombi yaliyojibiwa hivi karibuni? Shirikisha historia.
59. Ni nini kazi yako? Ni nini unachoofurahia juu yake?
60. Ni nani amekuwa msukumo mkubwa katika maisha yako ya kikristo na kwa nini?
61. Ni kitabu gani, senema, video umeona/kusoma ambavyo ungevishauri kwa wengine? Kwa nini?
62. Ni nini unadhani kinamfurahisha Mungu kuliko vitu vyote katika maisha yako?
63. Ni kitu gani cha kutia moyo kimesemwa kwako wiki hii?
64. Ni tendo gani la kutia moyo umefanya kwa mwingine wiki hii?
65. Ni nini kilikufanya kuhudhuria kanisa hili?
66. Ni nini bado unapenda kukamilisha katika maisha yako?
67. Ni nini uzoefu wako unaotia aibu zaidi?

68. Ni kwa lipi unashukurani?
69. Ni tukio gani la kukumbukwa katika maisha yako na kwa nini?
70. Shirikisha andiko lenye kuleta maana kwako na kwa nini linamaanisha hivyo?
71. Ni jinsi gani wewe na mwenzi wako mlikutana na nini kiliwafanya muanze kwenda nje pamoja au ni mtu wa aina gani ungependa kuwa naye kama mwenzi wako?
72. Maisha yako yangekuwaje kama ungejua kuwa Yesu angerudi katika kipindi cha wiki moja?
73. Ni mtu yupi wa kuvutia zaidi umekutana naye?
74. Ni siku zipi za kupumzika unazopenda zaidi?
75. Shirikisha uzoefu wa kiroho ambao umewahi kuwa nao.
76. Ni nini kinakuudhi juu ya mwenzi wako au rafiki?
77. Ni jinsi gani unavyopumzika?
78. Ni aina gani ya mziki/wimbo unaopenda zaidi n.k.?
79. Ni nini kimetokea kwako wiki hii ambacho ungependa kuwaambia kikundi chote?
80. Ni lini mara ya mwisho ulipokasirika hasa?
81. Kama usingeshindwa, ungependa kufanya nini?
82. Kama ungeishi tena maisha yako ni nini ungebadilisha?
83. Ni nini unataka kiandikwe kwenye jiwe lako la kaburi?
84. Ni nini unataka kisemwe kwenye msiba wako?
85. Ni nini hutaki kisemwe kwenye msiba wako?
86. Kama ungekwenda kuishi kwenye mwezi na kuweza kubeba kitu kimoja tu, ni nini kingekuwa?
87. Ni nini ungefanya kama ungeliona (1) Mtu akiwa ameibiwa (2)Mtu anayezama (3)Nyumba inayoungua moto?
88. Ni kitu gani kimoja kilianzisha taabu katika maisha yako wiki hii?
89. Ni nini kitu kimoja kinachokufanya kujisikia hatia?
90. Ni kitu gani kimoja ambacho hujui juu ya jinsia tofauti?
91. Kama ingekuwa kwamba uirudie wiki hii tena, ni kitu gani ungefanya tofauti?
92. Elezea kundi jingine dogo ambalo ulikuwa mjumbe nje ya kanisa lako. Kwa nini unadhani kundi lilifanyika (halikufanya)? Hauzuiliwi na makundi ya “dini”. Wengi wetu tunakutana katika vikundi vidogo kazini.
93. Ni Biblia gani ya kukumbukwa uliyowahi kupata? (Mf. Katika ubatizo wako, ndoa, kukata shauri, n.k.) Tuambie kwa nini ina maana kwako.
94. Ni kitu gani kinachokuja akilini mara ya kwanza unapofikiri juu ya Mungu?
95. Ni swali gani kubwa ulilonalo juu ya uhusiano wako na Mungu?
96. Ni katika misukosuko ipi unajisikia upweke zaidi? Upweke kidogo? Kwa nini?
97. Ni katika eneo gani la maisha yako ni vigumu kumutumaini Mungu? Watu wengine? Wewe mwenyewe?
98. Kwa nini unaamka asubuhi? Kusudi ni kutafuta nini nguvu ya mvuto iko katika maisha ya mtu huyo. Ni sawali rahisi lakini linachukua mawazo hasa kulijibu kwa uaminifu.
99. Ni lini ilikuwa mara ya mwisho ulipokubari umekosa? Kwa nini ni vigumu kufanya hivyo?
100. Nini uliyojifunza hivi karibuni kutoka kwa muumini?

**VIKUNDI KIINI**
***ZIADA***
**2B**

# Mfano wa Shughuli Katika Mkutano wa Kikundi Kiini

*Ifuatayo ni mfano wa shughuli kwa kila moja ya sehemu nne za mkutano wa kikundi kiini. Mda ulioorodheshwa kwa kila kazi ni makadilio:*

| Ushirika | Kuabudu | Kuadilishana | Uinjilisti |
|---|---|---|---|
| Mtu kwa mtu | Mtu kwa Mungu | Mungu kwa mtu | Mwili wa Kristo kwa ulimwengu |
| "Kwa ndani" | "Kwa juu" | "Kwa chini" | "Kwa nje" |
| Dakika 20 | Dakika 20 | Dakika 30 | Dakika 20 |
|  |  |  |  |
| • Furahia shughuli za kufurahisha pamoja<br>• Kula chakula pamoja<br>• Pata kujuana zaidi<br>• Kutiana moyo<br>• Shirikishana furaha<br>• Shirikishana matatizo<br>• Ombeaneni | • Imba nyimbo za sifa<br>• Mshukuru Mungu kwa ukuu wake<br>• Mshukuru Mungu kwa yote aliyofanya<br>• Omba kwa sauti au kimya kimya<br>• Soma vifungu vya kuabudu (kwa mfano, Zaburi).<br>• Soma mithali za kikristo | • Jifunze vifungu vya maandiko kama kikundi<br>• Tumia ukweli wa kibiblia katika hali za kila siku<br>• Husika katika huduma na kikundi<br>• Gundua na tumia vipawa vya kiroho<br>• Kariri mistari ya Biblia | • Unda “maombi ya utatu” na waombee marafiki wasiookoka<br>• Wakaribishe wasioamini kwenye kikundi<br>• Kama kikundi, timiza mahitaji ya watu wanaowazunguka<br>• Anzisha urafiki na wasioamini<br>• Shirikisha habari njema za Kristo kwa watu wengine |

VIKUNDI KIINI

SOMO LA 3

# Kuanzisha kikundi Kiini

☞ **Kusudi la Somo**

Kusudi la somo hili ni kutoa hatua za vitendo za kuanza kikundi kiini kipya.

☞ **Wazo Kuu**

- Msaada wa maombi ni muhimu zaidi.
- Inaweza kuchukua mda kuanzisha anwani za awali.
- Kikundi kiini cha mafanikio lazima kiwe kimepangwa

☞ **Matokeo Yanayotarajiwa**

Wakati yaliyomo katika somo hili yanapoeleweka, kila mushiriki anatakiwa:

- Kuelewa kinachohitajika kutokea ili kuanzisha kikundi kiini kimoja au zaidi.
- Kuanzisha mpango wa kuanzisha kikundi kiini kipya.

☞ **Ziada**

3A Karatasi ya kupangia

☞ **Ushauri kwa Wakufunzi**

Somo hili karibu linakamilishwa na somo la 2 “Kanuni za Uongozi wa Kikundi Kiini.” Masomo yote yanatakiwa kumalizika kabla ya mfunzwa kuanza kundi lake la kwanza.

## I. ANDAA KWA AJILI YA KIKUNDI KIINI

### A. Unda Timu ya Maombi

<u>Hatua muhimu zaidi katika kuanzisha kikundi kiini kipya ni maombi.</u> Kiongozi wa kikundi kiini anatakiwa kuunda timu ya waombaji watakaomuombea na kikundi kiini mara kwa mara. Hawa wanaweza kuwa watu kutoka katika kanisa lake la mtaa, marafiki wa kikristo na jamaa ya familia, au waumini kutoka makanisa mengine katika eneo ambapo kikundi kiini kitaanzishwa.

Omba kwa ajili ya uongozi wazi wa Mungu na omba kwa ajili ya hekima kuhusu kuwahi mda, eneo, n.k. Omba kwa ajili ya uamusho wa mioyo ya waumini waliopo katika eneo linalolengwa. Omba kwa kila kikundi kiini kipya kinachotakiwa kuanza. Paulo, katika huduma yake ya upandaji kanisa, maalumu aliomba maombezi (Efe 6:19, 1The 5:25, Rum 15:30). Mpanda kanisa anatakiwa kuwa mtu wa maombi, na lazima azungukwe na maombi.

### B. Unda Timu ya Uongozi

Ingawa inawezekana kwa mtu mmoja kuanzisha kikundi kiini, ingependeza kuwa na timu ya uongozi ya watu wawili mpaka wane. Wajumbe wa timu ya uongozi wanaweza kufanya utafiti kwa ufanisi zaidi,uinjilisti na mwanzo wa kuanza kikundi kiini. Kwa nyongeza, wanaweza kuombeana, kumfanya kila mmoja kuwajibika na kufuasa waumini wapya ambao wanaletwa katika kikundi. Yesu mwenyewe alionyesha hili alipowatuma 72 katika jozi kwa ajili ya uzoefu wao wa kwanza wa huduma (Lk 10:1). Mtu mmoja kutoka kwenye timu ya uongozi lazima achaguliwe kuwa kiongozi wa kikundi kiini kipya.

### C. Tafiti Eneo Lako Unalolenga

Ili kujifunza jinsi gani na wapi pa kuanzisha vikundi kiini kama sehemu ya mkakati wa upandaji kanisa, utafiti lazima ufanyike katika eneo linalolengwa. Katika mwongozo wa kwanza kuna somo linaloitwa, “Kanuni za Utafiti” (Maono ya KUM somo la 4). Kama utafiti huu haukumalizika, timu ya uongozi inatakiwa ifanye marudio ya somo hili na kufanya utafiti. Utafiti ambao umefanyika kulingana na kanuni zilizoorodheshwa katika somo utadhihirisha kigezo nyeti juu ya jinsi gani kikundi kiini kitaanzishwa.

## II. FANYA MAWASILIANO

Amua nani ni wasikilizaji unaolenga, na fikiri juu ya mahitaji yao dhahiri (kama ilivyoanishwa katika utafiti uliofanya baada ya kumaliza mwongozo wa kwanza). Ombea juu ya jinsi kikundi kiini chako kitakavyoanza kutimiza mahitaji haya. Omba kwamaba Mungu akuonyeshe watu wenye mvuto katika eneo lako unalolenga. Hawa ni watu wenye mvuto katika jamii zao, na walio na maono, heshima na nguvu. Mara nyingi, watu mashuhuri wamekuwa katika nafasi za aina fulani ya uongozi. Wana uwezo kama wakristo kuwa mashahadi wenye uwezo katika maisha ya wengi walio na uhusiano nao.

> Haijalishi kundi lako unalolenga ni lipi, anza kuomba kwa ajili ya wokovu wao hata unapokuwa unaanzisha uhusiano nao.

Kama eneo lako unalolenga ni majirani zako, kisha utaratibu wa kuleta familia, marafiki na watu unaowafahamu katika kundi sio mgumu. Umeshakuwa na uhusiano na watu hawa. Omba kwamba Mungu atatumia uhusiano wako kukupa nafasi ya kuwakaribisha kwenye kikundi kiini. Katika kipande cha karatasi, weka orodha ya watu ambao unaongea nao au kukutana nao katika kipindi cha wiki. Anza kumuombea kila mtu katika orodha yako, kwamba utakuwa na nafasi ya kuwashirikisha Kristo na kuwakaribisha katika kikundi kiini.

Kama eneo unalolenge siyo majirani zako wa karibu, kisha utaratibu wa kuanzisha uhusiano ni wa taratibu. Ni lazima uwafahamu kwanza hao ambao utawakaribisha, kuanza kuanzisha uhusiano nao. Tumia mda pamoja nao, angalia njia za kuwasaidia na kuwahudumia. Uwe “chunvi na nuru” kwao hata kabla hujaanza kikundi. Haijalishi kundi lako unalolenga ni lipi, anza kuomba kwa ajili ya wokovu wao hata unapokuwa unaanzisha uhusiano nao. Kama kuna tofauti ya ngazi ya kijamii au kundi la watu katika eneo lako unalolenga unaweza kuhitaji kuwa na kikundi kiini cha kulenga moja ya jamii hii au vikundi hivi, lakini fanya mpango wa kuanza vikindi kiini vingine kufikia ngazi za jamii katika eneo lako unalolenga.

Unatakiwa pia kuwasiliana na kanisa lolote katika eneo lako unalolenga kuongea nao juu ya mpango wako wa kuanzisha kanisa la kikundi kiini. Kama inawezekana, tafuta kujua uongozi katika makanisa haya na waombe baraka zao kwenye huduma yako. Hakikisha kuwa wanakuelewa kuwa hutakuwa (unaiba” moja ya kondoo zao, kwa kuwa kikundi kiini chako kitakua kwa matokeo ya uinjilisti uliofanyika kwa wasio-waumini, ambao wengi wao hawaendi kanisani.

Hata kama eneo lako unalolenga halina makanisa na halina wakristo, utaratibu ni uleule. Wafahamu watu katika kundi lako unalolenga, tumia mda pamoja nao, jifunze juu yao, jaribu kuwahudumia na kuonyesha kupitia maneno yako na matendo upendo wa Mungu. Kama unahusika katika aina hii ya kazi ya uvumbuzi, weka kipaombele kutumia mda katika maombi kuvunja vizuizi vya kiroho. Tarajia upinzani mwingi kutoka kwa Shetani, ambaye hataachilia kirahisi eneo ambalo halijawahi kushuhudiwa.

## III. CHAGUA ENEO

> Eneo lako la kawaida zaidi kwa ajili ya kikundi kiini kukutana mwanzoni ni nyumbani kwako au unakopanga.

Eneo lako la kawaida zaidi kwa ajili ya kikundi kiini kukutana mwanzoni ni nyumbani kwako au unakopanga. Kama hili haliwezekani, uwezekano wa pili utakuwa kwenye mji wa mmoja katika timu ya uongozi. Uwezekano unaofata utakuwa kwenye mji wa mtu ambaye unaanza naye uhusiano. Kama hili ndilo uchaguzi tu uliopo, ombea kwanza jinsi ya kuwaendea kwa ombi lako.

Jaribu kuepuka eneo la mkutano ambalo utatakiwa kulipia. Ni gharama ambayo haihitajiki kwa kikundi kiini, na ina uwezo wa kusababisha matatizo mengi sana. Baada ya hapo tu kikundi kitahitaji kushughulikia jinsi watakavyolipia eneo, na mkazo wa mkutano unaweza kuwekwa pembeni. Watu wapya wanaweza kujisikia kusukumwa kusaidia kifedha, hasa kama wajumbe wengine wamekuwa wakifanya hili. Hii inaweza kuwa kizuizi chenye nguvu ambacho kinaweza

kuzuia watu wengi kutokuja kwenye kikundi, au kutorudi kwenye kikundi mara wanapokuwa wamekitembelea.

Baada ya kuamua wapi pa kukutana, unahitaji kuamua lini. Unatakiwa kuchagua siku na mda kulingana na ratiba ya kazi, shughuli za kawaida za siku ya mapumziko na shughuli za jioni siku za kazi za watu unaolenga. Kama kila mmoja kwenye kikundi chako unacholenga anatakiwa kununua chakula na mahitaji jumapili asubuhi, usiweke ratiba ya kukutana kwa hiyo. Jaribu kuchagua mda ambao watu wengi wanaweza kuja. Tumia utafiti wako wa sehemu iliyolengwa kuonyesha mda gani unaweza kuwa mzuri zaidi, na waulize hao ambao utakuwa unawakaribisha ni mda gani mzuri kwao.

## IV. ANDAA KWA AJILI YA MKUTANO WA KWANZA

Mkutano wako wa kwanza unatakiwa uwe umeombewa vizuri na kuandaliwa vizuri. Fanya marudio ya timu yako ya uongozi wako nini kitatokea wakati wa mkutano. Hakikisha mkarimu (kama siyo wewe) anaelewa ni watu wangapi wamealikwa, jinsi ya kuandaa eneo la mkutano, na (kama inafaa) ni vinywaji gani vitakavyokuwepo wakati wa mda wa ushirika. Fanya maandalizi ya vitabu vya nyimbo mapema au kopi za mashairi kwa wimbo utakaokuwa unafundisha na kuimba. Uwe na Biblia za ziada mikononi kwa hao ambao hawana au hawakuleta za kwao.

Kwa kuwa wengi wa watu wanaokuja kwenye mkutano wa kwanza hawajuani, ni muhimu kuwa na shughuli ya “kivunja barafu” ya kuanza nayo. Shughuli hizi kwa kifupi zinazowaruhusu wajumbe wa kikundi kujuana kimchezo, njia isiyo ya kutisha (tazama Ziada 2A “kikundi Kiini Kivunja Barafu”).

> Usianze kwa maombi ya dakika ishirini, Na usifanye mafunzo ya Biblia ambayo yatachanganya na kuwachosha wageni!

Fanya mambo kuwa ya bila utaratibu na ya kawaida. Usianze kwa maombi ya dakika ishirini, Na usifanye mafunzo ya Biblia ambayo yatachanganya na kuwachosha wageni (Mf. Usifanye mafunzo ya ufunuo kwenye mkutano wa kwanza). Badala yake, kiongozi wa kikundi kiini anatakiwa kuongoza kikundi kwenye mda wa kujifunza Biblia ambao unafaa kwa kikundi. Hii inaweza kuwa majadiliano ya kifungu katika Biblia, njia ya kujifunza Biblia kwa kufata neno, au mafundisho yanayokubalika. Tambulisha Biblia kama neno la Mungu, ambalo lina majibu kwa maswali na matatizo ya kila siku.

Wafundishe wimbo mmoja au mbili na tumia kitabu cha nyimbo/kopi kuwasaidia kuimba. Fanya majadiliano yako ya kwanza ya Biblia na kikundi. Usitegemee mchango zaidi au kuhusika katika hatua hii kwenye kikundi. Jaribu kuonyesha matumizi kwa vitendo kwa mahitaji dhahiri ambayo yalionekana katika utafiti wa eneo linalolengwa..

Jadili makusudi ya kukutana pamoja kwenye kikundi kiini. Amua pamoja na kikundi kama mda na saa ya mkutano huo wa kwanza ulikuwa mzuri karibu kwa kila mmoja wao, au kama inahitaji kubadilishwa. Waulize kama wana kitu ambacho utakuwa ukiwaombea. Andika hilo mahali ili kwamba ukumbuke kuwauliza juu yake kwenye mkutano unaofata. Funga mkutano kwa maombi. Usiwaharakishe sana kila mmoja kuondoka! Mara nyingi wageni watakuwa wanajipumzisha baada ya “mkutano” kwisha, na unaweza kutumia mda huu kuwajua zaidi.

Baada ya wageni kuondoka, tathimini pamoja na timu yako ya uongozi ni nini kimekwenda vizuri na nini kirekebishwe kwenye mkutano unaofata. Ni bora kufanya hili mara tu baada ya mkutano, wakati mambo bado ni mapya katika akili ya kila mmoja. Andika mapendekezo yoyote kwa ajili ya mabadiliko au marekebisho.

## MASWALI YA KUTAFAKARI, MARUDIO NA MATUMIZI

- Ni vipengele gani vya msingi utavihusisha katika mpango wa kuanza kikundi kiini kipya?
- Ni nini baadhi ya matatizo ya kipekee unayoweza kukutana nayo unapofanya “uvumbuzi” wa upandaji kanisa katika eneo lisilo na ushuhuda wa kikristo? Ni nini kinatakiwa kufanyika kushinda vipingamizi hivi?
- Ni nini unachoweza kusema kwa muumini ambaye ni sehemu ya kikundi kiini chako lakini anayeogopa kutoa nyumba yake kwa wageni ambao hawafahamu?

**UTEKELEZAJI WA AZIMIO**

- Ngoja tuseme kwamba utakuwa na mkutano wa kikundi kiini chako katika mda wa wiki moja. Tumia ziada 3A, “Karatasi ya Kufanyia Mpango, mkutano wa kikundi kiini,” kufanya mpango wa mkutano huu wa kwanza. Ingia kwa undani zaidi iwezekanavyo. Kuna vipengele vingine vya mkutano ambavyo utaviweka kwenye mpango pia? Unapomaliza, shirikisha mpango wako kwa mmoja wa wafunzwa na muombe autathimini. Na wewe utathimini mpango wake pia.
- Kama hujamaliza utafiti wa eneo lako unalolenga, unahitaji kufanya hili sasa. Baada ya kufanya utafiti wa eneo lako unalolenga, tumia kanuni na hatua za vitendo katika somo kuanzisha mpango wa kuanza kikundi kiini kipya. Weka na majina ya timu ya uongozi, majina ya wanaowaombea, jinsi utakavyofanya mawasiliano, ni hitaji gani dhahiri kikundi kiini chako kitajaribu kulitimiza, lini na wapi kundi litakutana, na kitu gani kingine unadhani kinatakiwa kuwa sehemu ya mpango. Baada ya kukamilisha mpango huu, Mpatie mkufunzi wako au msimamizi aufanyie marudio.

**KIKUNDI KIINI**
***ZIADA***

# 3A

# Karatasi ya Kupangia

## MKUTANO WA KIKUNDI KIINI

Tarehe na mda wa mkutano: ______________________

Eneo na Mkarimu: ______________________

**Ushirika**

Vinywaji: ______________________

Shughuli, Mchezo: ______________________

**Kuabudu**

Kiongozi wa wimbo: ______________________

**Maombi**

Shughuli za maombi: ______________________

**Majadiliano ya Biblia**

Kiongozi wa majadiliano: ______________________

Kifungu cha maandiko: ______________________

**Makusudio ya huduma**

Mda wa kushirikishana: ______________________

Shughuli za kikundi: ______________________

Shughuli za mtu binafsi: ______________________

Vifaa vingine vya kupangia: ______________________

**Ya kufikiria:**

- Ni yupi kiongozi wako mwanafunzi?
- Ni nani anafuasa kila mjumbe wa kikundi chako? (Ni nani unayemfuasa?)
- Ni nini unachofanya kumsaidia kiongozi mwanafunzi kuendeleza ujuzi wa uongozi? Ni jinsi gani unavyogawa huduma kwake? Ni jinsi gani unavyokuwa kielelezo cha huduma kwake?
- Unamuombea kila mjumbe katika kikundi kiini chako?

VIKUNDI KIINI

SOMO LA 4

# Uinjilisti wa Kikundi Kiini

☞ **Kusudi la Somo**

Kusudi la somo hili ni kuelezea utaratibu wa uinjilisti katika vikundi kiini.

☞ **Wazo Kuu**

- Uinjilisti wa *Oikos* unawafikia hao ambao umeshakuwa na uhusiano nao.
- Uinjilisti wa kusudio unawafikia hao walio nje ya mzunguko wa karibu.
- Kuna aina mbili za wsioamini: Aina A na B.

☞ **Matokeo Yanayotarajiwa**

Wakati yaliyomo katika somo hili yanapoeleweka, kila mshiriki anatakiwa:

- Kuwa na kuelewa kwa jumla ambako, wasioamini wanaweza kutengwa katika aina mbili (Aina A na Aina B), na kwamba aina tofauti za uinjilisti zinahitajika kufikia kila aina hii ya watu.
- Kuelewa wazo la *Oikos*—mtandao wa uhusiano wa kila mtu.
- Kufanya ordha ya kila mtu ya uhusiano wa *Oikos*
- Kuelewa utaratibu wa uinjilisti wa *Oikos* na uinjilisti wa kusudio katika kikundi kiini.

☞ **Ziada**

4A "Juu ya *Oikos*"

☞ **Ushauri kwa Wakufunzi**

Somo hili linaelezea njia moja ya kutazama hali ya kiroho ya wasioamini kwa kuwatenga katika makundi mawili—kimsingi, hao walio na shauku ya injili na hao wasio na shauku ya injili. Tafsiri hii rahisi inamsaidia mfunzwa kuelewa vizuri jinsi uinjilisti unavyoweza kufanya kazi kwenye vikundi kiini. Tambua kuwa wazo la hali ya kiroho la asiyeamini na kuelewa kwake juu ya Mungu imeendelezwa kikamilifu kwenye mwongozo huu katika somo la uinjilisti la 6,7 "Hatua ya Kukata Shauri."

Hakikisha unaacha mda wa kutosha wakati wa somo hili ili wafunzwa "kuweka alama ya orodha yako ya mahusiano ya zoezi la Oikos"

## I. AINA MBILI ZA WASIOAMINI

Ili kwa kikundi kiini kuweza kuwafikia waliopotea wanaokizunguka kwa ufanisi, lazima kwanza kuwe na kuelewa jinsi ya kuwahudumia vizuri zaidi watu hao. Katika ukurasa wa pili wa Waefeso, Paulo anaandika juu ya jinsi Kristo alivyokuja kuvunja mipaka kati ya Wayahudi na Mataifa na kufanya wokovu kupatikana kwa wote watakaoamini. Waefeso 2:17 inasema kwamba Yesu alikuja na kuhubiri amani kwa hao waliokuwa **mbali sana** (Mataifa) na amani kwa hao waliokuwa **karibu** na (Wayahudi).

Tunaweza kutumia kuhitilafiana sawa tunapowaangalia hao ambao hawajampokea Kristo kama mwokozi. Baadhi ya watu wako mbali sana na kujitoa huku, na wengi wako karibu zaidi. Ralph Neighbour amewatenga waumini hao walio **karibu** kama "Aina A" ya wasioamini, na hao walio **mbali sana** kama Aina B" ya wasioamini. Migao hii ni ya kubuni , na tungeweza kuwaita vyovyote tunavyotaka. Maana ni kwamba makundi haya ya watu yanatofautiana, kikundi kiini kitakwenda kutumia njia tofauti kuinjilisha kila mmoja wao.

### A. Aina za Wasioamini: Hao Walio na Haja

Aina A ya wasioamini ni watu ambao tayari wanamwamini Mungu, na kujua kuwa Yesu ni mwana wa Mungu. Wanaweza kuwa na mwanga fulani wa Biblia, kuelewa kuwa Yesu alikufa msalabani. Wanaweza kuwa wanahudhuria kanisani au hawahudhurii, au pengine wanahudhuria mara chache (Mf. Wakati wa krismasi na Pasaka).

Hawa ni watu waliotayari kumsikiliza Mungu kwa ajili ya maisha yao na wanatafuta kupata majibu ya kiroho kwenye matatizo yao na maswali. Aina A ya wasioamini wanatakiwa wasipingwe kuja kwenye mafunzo ya Biblia kujifunza zaidi juu ya Mungu na neno lake. Mara nyingi, Aina A ya wasioamini wako karibu ya kujitoa kwa Kristo. Mara kwa mara, ni kwa sababu tu hawajasikia ujumbe wa injili ukiwa imeelezwa waziwazi.

### B. Aina B ya Wasioamini: Hao Ambao Hawataki Kujua


Aina B ya wasioamini wanahudhuria mara chache au ambao hawajawahi kuhudhuria kanisani, na wanaweza kuamini au kutokuamini katika Mungu. Hawaikubali Biblia kama kitabu chenye mamlaka, na pengine hawajui chochote juu ya Biblia. Yesu pengine si kitu zaidi ya umbo la kihistoria au wanaweza wakawa hawajawahi kusikia juu yake.

Aina B ya watu pengine wana furaha na aina ya njia yao ya maisha, na hawako wanatafuta kusudi la Mungu kwa ajili yao. Hawataweza kusikiliza wanapofikiwa kwa uinjilisti, na hawawezi kuhudhuria aina yoyote ya shughuli za "kanisa". Kwa hakika, Baadhi ya aina B ya wasioamini wanauhasama kwenye ujumbe wa injili. Hawataki kuhudhuria mafunzo ya Biblia, Na hawaoni jinsi "dini" ilivyo na mahusiano na maisha yao ya kila siku.

## II. KUIELEWA *OIKOS*

*Oikos4* ni neno la Kiyunani ambalo linaonekana mara kwa mara katika Agano Jipya. Ni neno linaloelezea uhusiano wa jamii ya watu uliopo kwa kila mtu. Kamusi ya Kiyunani ya Strong ya Agano Jipya inatafsiri *Oikos* *k*ama"nyumba" ambayo watu wote wanaounda familia moja, na/au watu wa nyumbani." Kwa mfano, Katika Matendo 16:15, imetumika kuelezea familia ya Lidia: "Wakati yeye na wote katika nyumba yake walipobatizwa, alitukaribisha sote nyumbani kwake."

**Kielelezo 4.1 Uhusiano wa *Oikos***




Kila mmoja wetu ana *Oikos,* mzunguko wa watu katika maisha yetu ambao tuna uhusiano nao. Mauhusiano haya ni pamoja na familia, marafiki, watu tunaofanya nao kazi majirani na wengine ambao tumetumia mda pamoja mara moja moja. Kielelezo 4.1 kinaonyesha uhusiano wa makundi haya ambayo yanafanya *Oiko*s ya utu wetu binafsi.

> Uinjilisti wetu binafsi wenye ufanisi zaidi kawaida ni wa watu ambao wameshakuwa katika maisha yetu, watu ambao tuna uhusiano nao.

Kuna njia nyingi za kufanya uinjilisti, kutegemeana na hali na nani unayejaribu kumfikia. Tunaweza na lazima wakati mwingine tumwambie mtu ambaye ni mgeni kabisa kwetu juu ya Yesu Kristo, Roho Mtakatifu anapotupa nafasi. Lakini uinjilisti wetu binafsi wenye ufanisi zaid kawaida ni kwa watu ambao wameshakuwa katika maisha yetu, watu ambao tuna uhusiano nao. Katika hekima yake, Mungu ametupa njia ya kushirikisha Kristo kwa wengine kutokana na matumaini na kujali kunakotokana na kuwa na uhusiano binafsi nao. Siyo "kipindi" cha kutokujuana na watu usiowajua; badala, ni njia inayofaa kumuonyesha rafiki kwamba unajali juu yake.

Kuwa "mfano hai" ni ushuhuda wenye nguvu kwa watu katika *Oikos*. Roho Mtakatifu anatumia matatizo yetu na mafanikio yetu kuwaonyeha wengine kwamba Kristo analeta *tofauti hasa* katika maisha yetu ya kila siku, kwamba Biblia ina majibu ya matatizo ya maisha, na kwamba furaha na amani inaweza kupatikana katika ulimwengu wenye matatizo mara kwa mara.

**Zoezi: Kufanya Orodha ya Uhusiano Wako wa *Oikos***

Kwenye kipande cha karatasi, chukua dakika chache kuandika majina ya watu ambao unazungumza nao au unaongea nao mara kwa mara katika kipindi cha wiki au kwa mwezi. Andika jina moja kwa kila mstari. Fanya orodha yako isizidi watu 20 (kama kuna zaidi, chagua 20 ambao umekuwa na uhusiano nao wa karibu zaidi).

Sasa, chunguza majina  yako katika orodha. Kwa kila mtu unayemjua kuwa ni muumini, weka alama ya msalaba mbele ya jina lake. Inayofata, fikiria juu ya watu ambao siyo waumini. Kwa watu wote wa “aina ya A” weka alama ya A mbele ya majina yao. Hawa ni watu unaodhani wanaweza kuwa wazi kwa mambo ya kiroho, kwa kujifunza Biblia, au kujifunza zaidi juu ya kusudi la Mungu katika maisha yao.

Mwishoni, Agalia majina yaliyobaki. Kama hawa ni watu unaowajua kuwa hawana mpango na Mungu au mambo ya kiroho, ambao hawatapenda kuja kujifunza Biblia, na ambao hawamuoni Mungu kuhusiana katika njia yoyote katika maisha yao ya kila siku, weka B mbele ya majina yao. Hawa ni “aina B” ya wasioamini.

Tunza orodha hii, pengine ndani ya Biblia yako. watu wenye alama ya msalaba mbele ya majina yao ni waumini ambao pengine inawezekana wangekusaidia kuanza kikundi kiini kipya. Watu wenye alama ya A mbele ya majian yao ni hao ambao unaweza kuwa unawaombea na kuwaalika kwenye kikundi kiini chako. Watu wenye alama ya B mbele ya majina yao ni watu ambao unaweza kuwa unawaombea juu ya kupata mda zaidi wa kuwa pamoja nao.

Unaweza kushangazwa kuona jinsi wachache (kama wapo!) wasioamini wako kwenye *Oikos* yako bianafsi. Wakristo wenge wana uhusianom kidogo na wasioamini. Muumni mpya atakuwa na uhusiano zaidi na asiyeamini. Kwa jinsi hiyo, kadiri wakristo wanapoanza kushirikiana na wakristo wengine, wanagundua mara moja kwamba wanatumia mda kidogo au hakuna tena na marafiki zao wasiowakristo.

## III. VIKUNDI VYA KUSHIRIKISHA

Tuanpofikiria juu ya kazi na shughuli za kikundi kiini, tunaona kwa haraka kwamba aina hii ya kikundi inaweza kukimbilia kwenye aina A ya wasioamini. Pengine wamejisikia kufarijika kikundi kinapoomba, kuabudu na kujifunza kutoka kwenye Biblia. Kwa jinsi hiyo, Ni kama ilivyo rahisi kuona aina ya B ya wasioamni kutokujisikia sana faraja kwenye kikundi kiini. Aina B ya watu hawataweza pengine kuja kabisa kwenye mkutano wa kikundi kiini mwanzoni, au kama watahudhuria, pengine hawataweza kurudi tena.

> Tuanpofikiria juu ya kazi na shughuli za kikundi kiini, tunaona kwa haraka kwamba aina hii ya kikundi kinaweza kukimbilia kwenye aina A ya wasioamini.

Ili kumfikia aina ya B ya wasioamini, tunahitaji kutumia kitu fulani ambacho Raph Neighbour anakiita “Makundi ya Kushirikishana.” Unaweza kuita vyovyote unavyopenda, lakini kanuni ya msingi ni hiyo ya aina B ya wasioamini, mahusuiano lazima yajengwe kabla injili haijaelezewa. Kuanzisha mahusiano haya kunachukua mda na juhudi, lakini ni njia bora kuwafikia watu ambao hawajali au wapinzani wa Mungu.

**Kundi la Kushirikisha** kwa kifupi ni wakristo wawili au watatu wanaoanza kutumia mda na aina B ya wasioamini kutoka kwenye mzunguko wa uhusiano wao. Mwishoni, huu hautakuwa mda wa kufanya mafunzo ya Biblia, maombi,  au hata kuongea juu ya Mungu. Badala yake, ni mda wa kuanzisha uhusiano, ili kwamba wasioamini waweze kuona kwamba wakristo wana nia nao kweli, kwenye matatizo yao na katika familia zao. Kwa mda, Roho Mtakatifu atatoa nafasi kwa wakristo kushirikisha jinsi Mungu anavyofanya kazi katika maisha yao, jinsi anavyowasaidia katika matatizo, na jinsi Biblia ilivyo na majibu ya maswali ya maisha.

## IV. UTARATIBU WA UINJILISTI WA KIKUNDI KIINI

### A. Uinjilisti wa *Oikos*


Kikundi kiini kipya kawaida kinaanza na aina A ya wasioamini kadhaa. Hawa ni watu ambao wakristo wamekuwa wakiwaombea na ambao wamekuwa wakiwashuhudia. Majadiliano ya kwanza ya Biblia na kikundi ni ya kiinjili kiasili, na yanatakiwa yawe yameandaliwa kuwakaribisha wajumbe wapya kwenye kikundi

> Kikundi kiini kipya kawaida kinaanza na aina A ya wasioamini kadhaa.

kwa Kristo. Roho Mtakatifu anapothibitisha mioyo, wasioamini watatoa maisha yao kwa Kristo, na kuanza kukua katika imani zao. Kama waumini wapya, watu hawa watakuwa na mawasiliano ya kawaida na wasioamini katika *Oikos* zao. Wanapojijenga katika imani zao na kuanza kukomaa, watawafikia pia aina A ya watu wanaowajua, kwa kuwaombea na kuwakaribisha kwenye kikundi. Kwa njia hii utaratibu wa kuombea, kujitoa na kukua katika Bwana unarudiwa katia kikundi. Kukata shauri na kukua kunatokea pamoja bega kwa bega na mistari ya uhusiano wa *Oikos* ambayo Mungu anatoa kwa kila mmoja wetu.

Wakati huo huo aina ya A ya wasioamini wanaletwa katika kikundi na kuyatoa maisha yao kwa Kristo, wakristo waliokomaa katika kikundi wanaanza kuomba juu ya nani katika aina B ya wasioamini wamfikie . Wanachagua watu kadhaa tu kwa aina hii ya huduma, kwa kuwa mda mwingi na juhudi vinahitajika. Angalau wawili au pengine watatu wa wakristo wanaanza kuombea na kutumia mda na kila aina B ya wasioamini. Huu siyo mda wa kujifunza Biblia, maombi, au mambo ya“dini”. Mwishoni, huu ni mda unaotumiwa kwa kifupi kujenga uhusiano wa kutumaini. Kielelzo 4.2 kinaelezea jinsi kundi linaloshirikisha la kikundi kiini wanavyosaidia kutoa injili kwa wote aina A na B ya wasioamini.

**Kielelezo 4.2 Kuwafikia Aina A na B ya Wasioamini**




Kadiri uhusiano unavyozama, Roho Mtakatifu anatoa nafasi ya kushirikisha jinsi Mungu anavyofanya kazi kwa juhudi katika na kupitia maisha ya waumini. Wanaweza kuwajulisha wasioamini kuwa wananawaombea katika mda wa matatizo, na kumpa sifa Mungu kwa ajili ya majibu ya maombi hayo. Kujifunza Biblia kidogo kunaweza kuanza kati ya wajumbe wa "kikundi cha kushirikisha," lakini bado siyo kwenye kikundi kiini. Katika wakati, Roho Mtakatifu ataleta mtu wa aina B (ambaye kwa wakati huu yuko karibu na kuwa aina A) anajisikia faraja kwenye kikundi kiini, kwa watu walewale waliokuwa wakitumia mda pamoja kabla wakiwa kwenye kikundi kiini. Kisha anakwenda nao katika njia ya uvumbuzi, kuthibitishiwa, kujitoa na kukua. Katika mda, mkristo huyu mpya ataanza kuwafikia watu nje katika *Oikos* yake wanaohitaji kujifunza juu ya upendo wa Kristo

**B. Uinjilisti wa Kulenga**

Uinjilisti wa *Oikos* ni moja ya kawaida na wenye mafanikio ya kuwafikia waliopotea wanaotuzunguka. Hii ni njia ya kwanza ya uinjilisti ya kutumia kwa waumini wapya katika kikundi kiini. Baada ya kuwa kundi limehusika kwenye uinjilisti wa *Oikos*, aina ya pili ya mkakati (ambao Raph Neighbour anaita "kukusudia") unaweza kuanzishwa. **Uinjilisti wa kulenga** unawafikia nje watu ambao ni wapya, lakini wenye mahitaji sawa, upendeleo na matatizo. Uinjilisti wa kukusudia unatakiwa utumike tu katika vikundi kiini ambavyo vimehusika katika uinjilisti wa *Oikos.*

> Uinjilisti wa *Oikos* unawafikia marafiki na wanaofahamika. Uinjilisti wa kulenga unawafikia wapya wenye nia sawa.

Uinjilisti wa kulenga ni sawa na kundi la kushirikisha kwa sababu watu wanaowafikia haijalishi kuwa wana nia na injili. Wanakutana kujadili mahitaji yao, matatizo au nia moja. Kiini au kisa cha makundi haya kinatofautiana kwa mapana, kutoka kujiheshimu mwenyewe, kujenga

ndoa, kulea watoto na kuponya majeraha ya kuvunjika kwa ndoa kwa kikundi kinachokutana kujadili muziki, wanyama au matengenezo ya gari! Njia nzuri ya kuamua ni kundi gani la kutoa ni kuzungumza na wajumbe wapya wa kikundi cha kushirikisha wanapokuwa wanafikia nje watu kwenye *Oikos* . Hitaji la aina fulani ya kundi linalolengwa mara nyingi linaonyeshwa na maumivu au nia ya watu ambao wajumbe wapya wanajenga nao uhusiano.

Makundi yanapokutana kujadili mahitaji, maumivu, nia na matatizo, wakristo wana nafasi ya ajabu kushirikisha jinsi Mungu na Biblia inavyotoa majibu, kutia moyo na mapumziko ya maeneo haya ya maisha. Hao wanaoonyesha nia ya ndani wanaweza kukaribishwa kwenye mkutano wa kiini, ambapo wanaweza kuanza kuonja uhusiano na faraja ya kikundi. Uinjilisti wa kulenga mara kwa mara ni njia inayofaa kuwafikia nje kwenye maeneo ambako mstari wa kawaida wa *Oikos* haupo, kama ilivyo kwenye "kuvumbua" huduma.

### C. Ukubwa wa Kikundi na Kuzidisha

Tofauti hasa ya ukubwa wa kikundi kiini kati ya watu 6-12, na kinatakiwa kisikue zaidi ya watu 15. Mara kikundi kinapokua kupita watu 15, Namna ya mawasiliano na mwingiliano unabadilika, na hakiwezi tena kutoa hali ya kujisikia kuwa pamoja na ukaribu ambao kikindi kiini kiasili kitakuwa nao.

Kikundi kinapoanza kuwafikia nje kwa kutumia uinjilisti wa *Oikos* na uinjilisti wa kukusudia, Roho Mtakatifu atathibitisha mioyo na watu wataanza kujiunga na kikundi. Fikiria kiwango cha ukuaji wa kikundi kushinda kukomaa kwa kiongozi mwanafunzi ambaye unafanya naye kazi. <u>Usiruhusu kikundi kukua sana kwa haraka kiasi kwamba ongezeko linatokea kabla mwanafunzi kuwa tayari.</u> Mara kikundi kinapoanza kukaribia watu 15, shirikisha kikundi kwamba ni lazima wabakie katika idadi hiyo tu mpaka kiongozi mwanafunzi atakapokuwa ameandaliwa kiroho, kiakili, na kihisia kushika nafasi ya uongozi kwenye kikundi kipya.

Mara ongezeko linapotokea, kiongozi wa kila kikundi ataanza kufanya kazi na mwanafunzi, na uinjilisti utaendelea kwa uaminifu katika vikundi vyote.

## MASWALI YA KUTAFAKARI, MARUDIO NA MATUMIZI

- Katika Luka 5:32, Yesu alisema, "sikuja kuwaita wenye haki, lakini wenye dhambi wafikie toba." Ni mda kiasi gani Yesu alitumia na wenye "dhambi" wakati wa kipindi cha huduma yake duniani? Toa mifano miwili au mitatu ya watu Yesu aliokutana nao ambao wangedhaniwa kuwa aina A na aina B ya watu.
- Ni aina gani ya shughuli unaweza kudhani kuwa unaweza kujengea uhusiano na aina B ya watu kutoka kwenye orodha yako binafsi ya Oikos? Ni wakristo gani wengine wanaweza kwenda na wewe unapofanya mahusiano haya?
- Ni mda kiasi gani unadhani inachukua kujenga uhusiano wenye maana na watu wasioamini? Ni nini vipao mbele, kama kuna chochote, unachoweza kubadilisha katika maisha yako ili kuweza kutumia mda zaidi na wasioamini?

## UTEKELEZAJI WA AZIMIO

Kama kikundi kiini chako, kinaanzisha mkakati wa kuwafikia nje kwa kutumia uhusiano unaojengwa wa kila mjumbe. Kama wengine katika kikundi chako hawajafanya orodha ya uhusiano kwenye *Oikos* yao, wafanye hivyo kwenye mkutano ujao. Wanakikundi waamue ni yupi kweye aina A wa kuombea na kuwasilana naye, na watu gani wa aina B wa kuombea na kuanza kutumia mda pamoja nao. Kiongozi wa kikundi kiini lazima atunze orodha ya majina haya, ili kwamba kikundi kiweze kujiwajibisha kuwafikia.

## VYANZO


- Neighbour, Raph. A *Guidebook for cell Group Churches.* Houston, TX: Touch Publications, 1990.
- Neighbour, Raph. *Knocking on Doors, Opening Hearts.* Houston, TX: Touch Outreach Ministries, 1990
- Trinity Christian Center, *Cell Growth and Evangelism Strategy Seminar*, N.P., n.d.

**VIKUNDI KIINI**

***ZIADA***

**4A**

# Kuhusu *Oikos*

Kuelewe kikamilifu umuhimu wa vikundi kiini katika mkakati wa upandaji kanisa, tunatakiwa kufikiri juu ya neno Oikos, kama neno la kibiblia linaloelezea msingi wa kawaida wa matofali ya kujengea katika jamii yoyote. Inaonekana katika Biblia nzima na inarejeza kwenye jamiii iliyopo kwa ajili yetu sote. Imetafsiriwa katika kiingereza kama "nyumba" au "watu walio katika nyumba." Kwa mfano, katika Matendo 16:31, Paulo na Sila walilitumia waliposema, "*Amini katika Yesu, na utaokoka—wewe na nyumba yako."*

### *OIKOS:* NJIA YA ULIMWENGU YA KUUNDA VIKUNDI KIINI KWA AJILI YA WOTE

> Kwa hao tu tunaotoa kwao mda wa kutosha wanaweza kusemekana kuwa sehemu ya *Oikos* yetu.

*Oikos* ya kila mmoja wetu inayoishi ndani siyo kubwa. Tunaweza kuwa tunajua jozi kadhaa, hata mamia kadhaa, ya watu, lakini mda wa kutosha unaotumika na wengine kwa kiwango cha juu ni mfupi—na kwa hao tu tunaotoa kwao mda wa kutosha wanaweza kusemekana kuwa sehemu ya *Oikos* yetu, utu wetu binafsi wa jamii. Kila mmoja wetu ana kikundi cha kwanza ambacho ni pamoja na baadhi ya jamaa yetu na baadhi ya marafiki zetu wanaohusiana nasi kwa kupitia kazi, burudani, mapendeleo, na majirani. Hawa ni watu tunaozungumza nao, tunaohusiana, na kushirikishana, angalau kwa saa moja kwa juma.

Katika hali ya juu isiyo ya kawaida kupata mtu mwenye watu 20 katika *oikos* yake. Kwa miaka mingi, nimechunguza ukubwa wa *oikos* kwa hao wanaohudhuria semina zangu na madarasa. Mkristo kawaida ana wastani wa watu tisa, na asilimia yao kubwa kati yao hawajaanzisha uhusiano wa *oikos* mpya kati yao kwa kipindi cha miezi sita iliyopita!

Maisha yanajengwa na mnyororo wa muunganiko wa *oikos* usio na mwisho. Kila mmoja ameshafanywa pacha katika mahusiano haya. Kama watu wamekubalika katika oikos, wanajisikia usalama ambao hawawi nao wanapokutana na watu wasiowajua.

Katika kila utamaduni wa ulimwenguni, Uhusiano wa karibu wa kuunganika katika *oikos* unadhaniwa kuwa wakfu. Wachina wana neno maalumu kwa urafiki wa karibu, na aina ya umoja huo inadhaniwa kuwa kitu wakfu. Huko Argentina, nilionyeshwa mulija wa kibuyu wa chuma wenye tundu mwishoni kwa ajili ya kunywea "chai ya wenzi." Kawaida ya ukaribu wa *oikos* katika jamii zao ni kushiriki na rafiki kwa kunywea mulija mmoja. Mara nyingi, sherehe inakuwa ya jamaa ya familia tu.

### *OIKOS* INATOFAUTIANA KULINGANA NA UWEZO WA HISIA

Tangu ulimwengu ulipoanza, watu wamekuwa wakiishi kwenye *oikos* mara zote. Kila utaduni mmoja, bila kuwa na tofauti, wanazo. Usalama wa binafsi ni katika hakikisho linalopokelewa na hao walio na umuhimu katika oikos. Katika kipindi cha utotoni, mama ndiye anayetoa uthibitisho kwa uwepo wake na kwa kujali kwake. Mtoto anapokua, uthibitisho huu unapokelewa, au kutokupokelewa, na wajumbe wa nyumba nyingine. Kisha mwalimu wa shule anakuwa sehemu ya oikos, na baadaye inakuwa *Oikos* ya kundi la waliokomaa ambao lazima wamukubali. Katika sehemu ya kazi, uthibisho unaungana na kupewa madaraka na kuongezwa mshahara.

Kila *oikos* inakuwa sehemu ya mfumo wa jami kubwa. Kitu muhimu kwetu kuchukua ni kwamba kila kiumbe hai kinaishi katika, ulimwengu mwembamba, mara kwa mara kinalazimika kuhusiana na watu wanaolazimika juu yake kwa muundo wa oikos. Leo, Maumivu ya kusukumwa katika mji ambako mama ni mlevi au baba ni mbakaji wa watoto kunataka huduma muhimu ya kanisa la vikundi kiini.

Unaposoma hili, fikiri matokeo ya hili katika maisha yako mwenyewe. Chukua mda kuandika majina ya watu wote unaotumia nao saa nzima kila wiki mkiongea ana kwa ana, katika tabia ya mtu kwa mtu.

(Saa hii inaweza kukusanywa dakika chache chache kwa kipindi, kwa mda wa siku saba, lakini lazima iwe kila mara—na lazima iwe uso kwa uso). Matokeo ya kuzidi kwa mguso wa wachache juu ya kila maisha yetu lazima kufikiriwe. Kwa mfano: Ni nani wengine wenye maana katika maisha yako? Ni nani ambaye kuruhusu au kutoruhu kwake ni muhimu kwako? (Nimewashauri hao ambao bado wanajaribu kuwaridhisha baba wasioridhisha waliokwisha kufa miaka mingi). Nani unamhofia atakukataa, nani unamwangalia kukuthibitisha? Kutafakari juu ya *oikos* ya mtu kunaweza kuleta ufahamu mkubwa.

**WAFANYA KAZI WA KIKRISTO WANA *OIKOS* ZINAZOKOSA WASIOAMINI**

Uchunguzi wangu mwenyewe juu ya somo hili miongoni mwa wafanya kazi wakristo imedhihirisha ukweli wa ajabu. Nina uhakika nimehesabu vichwa zaidi ya 5,000 vya wachungaji, wake wa wachungaji, jamii ya wafanya kazi wa kanisa na wamishenari angalau katika nchi therathini. Ni kitu cha mara chache kukuta hao walio katika “kazi ya kudumu ya kikristo” ambao wana wasioamini katika *oikos* zao za mwanzo.

> Ni kitu cha mara chache kukuta hao walio katika “kazi ya kudumu ya kikristo” ambao wana wasioamini katika *oikos* zao za mwanzo.

Labda awe ameajiliwa katika ulimwengu wa kawaida mke wa mfanya kazi wa kikristo ana angalau kidogo ya kuwasiliana na mmoja asiyekuwa wa kanisa. *Oikos* yake imejazwa na watu wa kanisa. Katika tukio moja kiongozi wa elimu wa kanisa kubwa aliinamisha kichwa chake mikononi na kulia kwa aibu alipogundua ametumia ujuzi wake wote akiwa amefungiwa kwenye kazi za kanisa. Hakuweza kukumbuka akiwa na oikos ya wasioamini ndani tangu alipomaliza chuo.

**YESU MARA KWA MARA ALIVAMIA OIKOS ZA WAPAGANI**

Wakati kanisa likiwavuta watu kutoka kwenye *oikos* zao na kuwapa uanachama kwenye mashirika ambayo yanawakubali, Agano Jipya linadhihirisha tofauti ya namna tofauti ya uhusiano wa watu. Yesu wakati wote alifanya kazi yake kwa kuvamia vikundi vya oikos. Alijua hapakuwa na njia nyingine ya kushirikisha injili isipokuwa kupenya kwenye kundi dogo la watu hawa. Ni wazi kwamba kila oikos inatokana na nyumba, siyo jengo la kiwizara. Kwa hiyo, Bwana alitumia mda wake kwenda nyumba moja hadi nyingine.

Katika Luka 19:2-5, tunaona Yesu akiwasiliana na Zakayo. Anamwambia, “Zakayo…*ninataka kukaa nyumbani mwako leo.”* Wakati akiwa ameegemea meza kahaba anakuja na kumumwagia marashi miguuni mwake. Ni mfano gani huu wa kushangaza wa kupenya kwa *oikos!*

Katika Mathayo 8:14, Anaingia nyumbani mwa Petro na kumponya mmoja wa wajumbe wa *oikos* wanaoishi pale. Katika Mathayo 9:10, Anakula chakula cha jioni na wanafunzi wake na wakusanya kodi wengi na wenye dhambi katika nyumba ya Mathayo. Tena, anapenya oikos katika Mathayo 9:23 anapoingi katika nyumba ya mtawala na kuona wapiga zeze na umati wenye fujo. Katika Mathayo 17:25, Petro anamkuta katika nyumba ya Kapernaumu, ambapo Yesu anazungumzia kuhusu yeye kulipa kodi. Tunasoma katika Marko 3:20 kwamba Yesu aliingia katika nyumba na umati wakiwa wamekusanyika, “*mpaka yeye na wanafunzi hawakukuweza hata kula.”* Katika Marko 7:17, Anaingia katika nyumba ambapo wanafunzi wake wanambishia juu ya mfano. Katika Marko 7:24, anaingia katika nyumba peke yake, ili tu kufunikwa na umati ambao wamejifunza alipokuwa anakaa.

**KANISA LA KWANZA LILIPENYA *OIKOS,* PIA!**

Katika Matendo 5:42, tunasoma kwamba kanisa la kwanza walikwenda nyumba kwa nyumba. Katika Matendo 8:3, Wakati Sauli alipotaka kuchoma kanisa, alijua ni wapi pa kuwapata watu wa Mungu. Tunaambiwa kuwa, “*kwenda nyumba kwa nyumba, aliwaswaga wanaume na wanawake kwenda jela.”*

Inafurahisha kuona katika Matendo 10 jinsi Roho Mtakatifu alivyopangilia kwa Paulo kutoka katika nyumba ya Simoni mchuna ngozi kwenda kwenye makao ya Corneli, ambapo Korneli alikata shauri. Mpenyo wa *oikos* ni sehemu ya huduma katika karne ya kwanza.

> Mpenyo wa *oikos* ni sehemu ya huduma katika karne ya kwanza.

Kukata shauri kumeandikwa mara kwa mara kama kusukuma *oikos* yote kwenda kwenye ufalme. Katika Matendo 6, Wote Lidia na mfungwa wanabadilishwa pamoja na jamaa yao ya *oikos*. Tendo la kwanza la Lidia baada ya kukata shauri kwake ilikuwa kumkaribisha Paulo kukaa nyumbani mwake.

### KUKATALIWA NA *OIKOS* YA MTU KWA KUWA MKRISTO INAUMIZA

Yesu anatukumbusha katika Mathayo 10:36 kwamba kumfuata kunaweza kukawa kwa gharama kubwa: "*Adui wa mtu ni wale wa oikos yake*" Kukata shauri kumfata kunaweza kusababisha kuchanganyikiwa katika uhusiano na watu wa kwanza. Hii ndiyo sababu alisema katika Mathayo 10:35, *"Kwa maana nalikuja kumfitini mtu na babaye, na binti na mamaye, na mkwe na mkwe wake…"* katika mstari wa 37, anawaita kwa ajili ya uamzi kati *ya oikos* na ufalme: "*Apendaye baba au mama kuliko mimi, hanistahili; Wala apendaye mwana wala binti kuliko mimi hanistahili…"*

Huko Singapore leo, kuna mchungaji wa kanda anayefanya mazoezi kwa watu ninaofanya nao kazi anayetoka katika nyumba ya kihindi. Baada ya kujitoa kumfata kristo, *oikos* ilimuondoa kwenye ukoo kwa laana. Mjomba wake alisubiri mpaka atakapokuwepo kusema kwa baba yake, "kwa nini unamruhusu kijana wako kututia aibu sote kiasi hiki?" katika Asia ya kusini mashariki ya wakati ule, Doctor kijana wa mwili alimfuata Bwana kwa gharama ya familia yake ya kiislamu kumtangaza kuwa amekufa na kuzikwa*. Oikos* inaweza kukosa huruma wakati mmoja anapochagua njia nyingine ya maisha.

### MWILI WA BWANA WETU UNAITWA *"OIKOS"*

Kwa jinsi hiyo, kuna oikos maalumu kwa hao ambao wamekutana na kukataliwa kwa mwisho. Waebrania 3:6 inasema, "Bali Kristo kama mwana, juu ya oikos ya Mungu. Ambaye oikos yake ni sisi, na kama tukishikilia sana kwenye ujasiri wetu na faraja ya taraja letu mpaka mwisho." Fikiria mistari hii ya nyongeza ambayo inazungumzia ukweli, unaopatikana katika 1Petro 4:17, Timotheo3:15, Waefeso 2:19; na 1Petro 2:5:

> "*Ni wakati wa hukumu kuanzia katika oikos ya Mungu; na kama inaanzia kwetu, nini yatakuwa matokeo kwa hao ambao hawaitii injili ya Mungu?"*
>
> *"Kama nikikawia, ujue iwapasavyo watu kuenenda katika oikos ya Mungu, iliyo kanisa la Mungu aliye hai, nguzo na msingi wa kweli."*
>
> *"Basi tangu sasa ninyi si wageni wala wapitaji, bali ninyi ni wenyeji pamoja na watakatifu, watu wa kwenye oikos ya Mungu."*
>
> *"…nanyi, kama mawe yaliyo hai mmejengwa muwe oikos ya roho, ukuhani mtakatifu, mtoe dhabihu za roho, zinazokubaliwa na Mungu, kwa njia ya Yesu Kristo."*

Wazo la oikos likielezea kanisa linatakiwa kutufanya kutambua umuhimu wa viini kama msingi wa jamii ya wakristo. Maandiko yanaelekeza kwa wakristo wa kwanza kama wajumbe wa oikos hii ya kiroho kwa kuongea na hao waliokuja kwenye imani kwa muungano wa familia, badala ya kujitoa kwa mtu:

> *"Krispo, mtawala wa sinagogi, na oikos yake yote ilimwamini Bwana…Salimia pia kanisa linalokutana nyumbani kwao… Salimia hao walio wa oikos ya Aristbuolo… Salimia hao walio wa oikos ya Narkiso walio katika Bwana… wengine kutoka oikos ya chloe wamenitarifu kuwa kuna ugomvi kati yenu… Ndiyo, nimebatiza pia Oikos ya Stefano… Unajua kwamba Oikos ya Stefano walikuwa wakata shauri katika Akia… Akwila na Prisila wanawasalimia kwa shangwe katika Bwana, na hivyo hata kanisa linalokutana kwenye nyumba yao… watakatifu wamewatumia salamu, hasa hao walio wa Oikos ya kaisari… Toa salamu zangu kwa… Nimfa na kanisa katika nyumba yake… Bwana na aijalie rehema Oikos ya Onesfo… Msalimie Prisila na Akwila na Oikos ya Onesfo."*

> Kanisa la kwanza lilifikiri juu ya mnyororo wa *oikos* kushindiwa.

Amini, kanisa la kwanza lilifikiri juu ya mnyororo wa *oikos* kushindiwa wakati wakifurahia sawia kwamba Mungu amewaunda katika msingi wa jamii ya wakristo. Kwa kanisa kuishi katika ngazi ya *oikos* ulikuwa mpango hakika wa Mungu. Moyo wa maisha ya wakristo hauhusiani na neno "hekalu," au "sinagogi," au "jengo la kanisa." Kama kitambaa cha msingi wa wanadamu maisha yamefunikwa kwenye *oikos,* hata maisha ya mwili wa Kristo pia yanatakiwa kutokana na *oikos.*

*Na R. W. Neighbour, edited by J. Geske*
*Wapi "Tunakwenda Kutoka Hapa?"- imetumiwa kwa ruhusa.*

VIKUNDI KIINI

SOMO LA 5

# Kuonyesha Mfano wa Kikundi Kiini

☞ **Kusudi la Somo**

Lengo la somo hili ni kutoa onyesho (kutumia kushiriki-darasa) kwa baadhi ya shughuli halisi za mkutano wa kikundi kiini, ili kuzoeza wafunzwa na baadhi ya uzoefu wa "mkono juu yake " wa kutenda.

☞ **Wazo Kuu**

- Washiriki kwa uzoefu wa "kutenda" na utaratibu wa kikundi kiini utakuwa umeandaliwa vizuri kuongoza vikundi kiini vyao.

☞ **Matokeo Yanayotarajiwa**

Wakati yaliyomo katika somo hili yanapoeleweka, kila mshiriki anatakiwa:

- Kuchunguza na kushiriki katika kipengele kimoja au zaidi cha kikundi kiini halisi.
- Kutathimini kazi na mwitikio wa wajumbe wanapofanya majaribio ya kuongoza na kushiriki katika shughuli.

☞ **Ushauri kwa Wakufunzi**

Somo hili linahitaji mpango na maandalizi ili kuwa lenye faida. Mkufunzi lazima afikiri mbele kabla ya mda ni shughuli ipi atapenda kufanya na kundi la wafunzwa, na kupanga kufuatana. Kama aina yoyote ya mda wa mafunzo ya Biblia itakuwa sehemu ya shughuli za ndani ya darasa, mfunzwa anatakiwa apewe siku moja au mbili kabla ya somo hilo ili kujiandaa.

Kuna aina nne za kimsingi za shughuli za kuchagua kutoka, na zinahusiana na sehemu nne halisa za mkutano wa kikundi kiini: ushirika, kuabudu, kuadilishana, na uinjilisti. Labda kuwe na zaidi ya saa moja ya kutumia katika somo hili, inahofisha kwamba mkufunzi atakuwa na mda wa kutosha kufanyia mazoezi sehemu zote nne. Uwezekano mkubwa wa mtiririko wa matukio ni kwa wakufunzi kuchagua shughuli moja au mbili za kufanyia majaribio. Uchaguzi huu utakuwa upande wa idadi, aina, uzoefu na maswali.





Mifano na mapendekezo yaliyotolewa katika somo hili ni maelekezo ya utaratibu. Kama mkufunzi anafahamu sehemu fulani zenye matatizo au maswali yanayohusiana na mandhali maalumu, anatakiwa kwa njia zozote kurekebisha shughuli za somo hili kujibu matatizo hayo au maswali.

Kama kundi la wafunzwa ni kubwa, wanatakiwa wagawanywe katika makundi madogo ya wasiozidi watu 8-10 kwa zoezi la darasani. Mkufunzi anatakiwa amwagize "kiongozi" wa kikundi kiini kwa kila makundi yanayofanya kazi. Kutegemeana na shughuli, mkufunzi anaweza kutaka kuwa na watu kadhaa kushikilia nafasi ya uongozi wakati wa mda wa zoezi hili.

## I. KUONYESHA MFANO WA KIKUNDI KIINI

Kusudi la somo hili ni kutoa nafasi ya kuchunguza na kushiriki katika vipengele mbalimbali vya mkutano wa kikundi kiini. Kumbuka kuwa mkutano wa kikundi kiini una sehemu nne: ushirika, kuabudu, kuadilishana, na uinjilisti. Somo limeandaliwa kuwapa wakufunzi uhuru wa kuchagua ni ipi kati ya shughuli hizo nne za kufanyia maonyesho. Kama kundi litafaidika kutokana na kufanya majaribio mda wa kushiriki na kuabudu, mkufunzi anaweza kuchagua kukazia katika maeneo hayo. Kama kundi litapenda kutumia mda fulani katika kufuasa, wanaweza kufanya majaribio ya kujifunza Biblia kwa kuongozwa na neno. Shughuli kwa somo hili zitakuwa kidogo tu kwa ukubwa wa kikundi na mda uliopo.

**Kielelezi 5.1 Kazi Nne za Mkutano wa Kikundi Kiini**

| Ushirika | Kuabudu | Kuadilishana | Uinjilisti |
|---|---|---|---|
| Mtu kwa mtu | Mtu kwa Mungu | Mungu kwa mtu | Mwili wa Kristo kwa ulimwengu |
| "kwa ndani" | "kwa juu" | "Kwa chini" | "Kwa nje" |
|  |  |  |  |

Yafuatayo ni mapendekezo ya kila moja ya maeneo manne ya mkutano wa kikundi kiini. Mkufunzi anatakiwa kuamua ni eneo gani lifanyiwe mazoezi, na kwa njia gani  au zipi hasa. Kama kuna mda, baadhi ya tathimini inatakiwa ifanyike baada ya kila shughuli. Kama inahitajika, Rejea nyuma kwenye kikundi kiini 2B “Mfano wa Shughuli katika Mkutano wa Kikundi Kiini” kwa marudio ya shughuli halisi ya kila moja ya kazi nne.

**A. Ushirika**

*Mtiririko wa matukio:* Kikundi kiini kinakuwa na mkutano wake wa kwanza. Marafiki na wanaojulikana na waumini wamealikwa, na kwa ujumla, watu kwenye kikundi hawajuani. Kiongozi wa kikundi angependa kikundi kutumia mda fulani katika shughuli ambazo zitawafanya wajuane vizuri zaidi. (chukua mda fulani wa kufanya kadhaa ya vivunja barafu katika ziada 2A “Kikundi Kiini Kivunja Barafu.” Au, Kama anapenda, mkufunzi anaweza kutumia shughuli zake mwenyewe ambazo zitasaidia wajumbe wa kikundi kujuana zaidi).

**B. Kuabudu**

*Mtiririko wa matukio:* Kikundi kiini kimekuwa kikikutana kwa wiki kadhaa. Mpaka hapo, mda wa kuabudu kwa kifupi umeendelea kuwa na kuimba nyimbo chache ambazo kikundi kimejifunza. Kiongozi wa kikundi atapenda kushirikisha njia zingine ambao kikundi kinaweza kumwabudu Mungu kwa pamoja. Hii inaweza kuwa ni pamoja na kuomba katika au kusoma baadhi ya zaburi (kila mmoja ana soma zaburi anayoipenda, au kila mtu anasoma mistari kadhaa ya zaburi moja), kuimba wimbo mpya au ambao haujulikani, kuomba katika vikundi vya watu wawili au watatu, n.k.

**C. Kuadilishana**

Kuna shughuli kadhaa ambazo zinaweza kusaidia kujua ambacho kimetokea wakati wa kipindi cha kuadilishana cha mkutano wa kikundi kiini.

- *Ufuasaji wa mmoja kwa mmoja.* Mtiririko wa matukio: Kikundi kiini kimekuwa kikijifunza Luka 14:26, “Kama mtu akija kwangu naye hamchukii baba yake na mama yake, mke wake na watoto, kaka zake na dada zake—ndiyo, hata maisha yake mwenyewe—hawezi kuwa mwanafunzi wangu.” Wakristo wachanga katika kikundi wamechanganyikiwa, na kiongozi wa kikundi kiini ameuliza wakristo waliokomaa kutumia mda fulani wakati wa mkutano wa kikundi kiini kusaidia kwa kueleza maana ya kifungu kwao. (Kiongozi anatakiwa kugawanya kundi linalofanya kazi katika sehemu mbili. Nusu ya kwanza ya sehemu ya wafunzwa watashika nafasi ya wakubwa, wakristo waliokomaa zaidi. Nusu nyingine watashika nafasi ya wakristo wapya).
- *Kujifunza Biblia kwa kufata neno.* Mtirirko wa matukio: Kikundi kiini kitajifunza kifungu katika Biblia kwa kutumia njia ya kijifunza kwa kufata neno. (Mkufunzi anatakiwa awaulize darasa kuandaa mafunzo mapema kwa kifupi ya kujifunza kwa kufata neno ya kifungu

anachopenda. Kadiri mda unavyoruhusu, kila mtu ataongoza kundi katika mda wa kujifunza kwa kufata neno akitumia kifungu na maswali yaliyoandaliwa na kila mtu).

- *Mafundisho yenye mamlaka.* Mtiririko wa matukio: Kiongozi wa kikundi kiini anataka kuwapa watu kadhaa katika kikundi chake kiini nafasi kushirikisha baadhi ya mafundisho kutoka kwenye maandiko. Kwa jinsi hiyo, anawataka kufanya mazoezi ya utambuzi badala ya mahubiri. Amewaomba kutayarisha baadhi ya mawazo ambayo wanaweza kushirikishwa kati ya dakika 4-5 na kundi. Kiongozi wa kikundi anawajibika kuhakikisha kila mtu anakaa kati ya mda uliotolewa. Kama kuna mda, watu wengine kwenye kikundi wanaweza kuuliza maswali juu ya maelezo au mawazo ambayo hayakuwa wazi kwao. (Mkufunzi atahitaji kuwauliza wafunzwa kuandaa kabla ya shughuli hii)

**D. Uinjilisti**

Mda wa uinjilisti unaweza kufanyiwa majaribio kwa njia kadhaa:

- *Ushuhuda wa binafsi.* Mtiririko wa matukio: Kikundi kiini kimewaalika wageni kadhaa ambao siyo waumini. Kiongozi amewaomba mtu mmoja au wawili kutoka kwenye kikundi kushirikisha shuhuda zao <u>kwa dakika 2-3</u> akitumia “lugha ya “kawaida” ambayo itakuwa ya kueleweka kwa wasio wakristo. Watu kadhaa wanatakiwa washike nafasi ya hao wanaotoa ushuhuda, na wengine kadhaa wanatakiwa washike nafasi ya wasio wakristo ambao wanasikia kitu kama hicho kwa mara ya kwanza. Kama “wageni” wanasikia kitu fulani ambacho hakiko wazi au kinachochanganya, wanatakiwa wamsimamishe mtu anayetoa ushuhuda na kuomba kikundi kuweka wazi. (Kwa ajili ya shughuli hii mkufunzi anahitaji kuuliza wafunzwa kabla ya kuanza kuandaa ushuhuda mfupi wa binafsi).
- *Maazimio ya huduma ya mbeleni*. Mtiririko wa matukio: Kikundi kiini kiko kwenye eneo ambalo lina viwanda na ambapo kawaida baba na mama wote wanfanya kazi. Mpaka hapo, jaribio la uhusiano katika majumba na kuwakaribisha watu katika kikundi limekuwa siyo la mafanikio. Siku ambayo watu hao wana mapumziko ni siku za jumapili tu. Kuna watoto wengi katika eneo. Kikundi kiini kinahitaji kujadili jinsi ya kuweza kuwafikia kundi la watu hao wanaolengwa. (mkufunzi anatakiwa kumwagiza mtu mmoja kuwa wa kikundi kiini).
- *Kikundi cha “Kushuhudia*”. Mtiririko wa matukio: Kikundi kiini kina maono na mzigo wa kuwafikia nje wanaume katika jamii zao. Hata hivyo, wanaume wengi hawana haja ya mambo ya kiroho na wanakataa kuja kwenye mkutano wa kikundi kiini. Kikundi kiini wanaamua kuanzisha “kikundi cha kushuhudia” ambacho kwa namna fulani kitawahusisha wanaume wa jamii katika shughuli au majadiliano ya aina wanayoyapendelea. Itatoa pia nafasi ya kujenga uhusiano nao ili hatimaye kuwashirikisha Kristo. Katika jamii kama hii, wanaume wanaonekana kupenda kucheza mpira wa miguu, na kushughulikia magari yao siku ya mapumziko. Kikundi kiini wanahitaji kujadili njia imara ambazo wanaweza kuanza kikundi cha kushirikisha baadhi ya wanaume hawa. (Mkufunzi anahitaji kumwagiza mtu mmoja kuwa kiongozi wa kikundi kiini).

## II. TATHIMINI

Wafunzwa wanatakiwa watathimini shughuli mbalimbali za “kikundi kiini.” Ni nini ilikuwa uwezo wao na udhaifu? Jinsi gani “kiongozi” wa kikundi kiini alivyoyachukulia matatizo mbalimbali na maswali? Ni nini kingekuwa kimefanyika tofauti?

## MASWALI YA KUTAFAKARI, MARUDIO NA MATUMIZI

- Kwa nini ni muhimu kupanga kwa kila sehemu ya mkutano wa kikundi kiini?
- Ni kwa njia zipi kiongozi wa “kikundi kiini” katika zoezi hili amekuwa na ugumu wa wajibu walioshika? Kutakuwa na ugumu sawa katika mkutano wako halisi wa kikundi kiini?

## UTEKELEZAJI WA AZIMIO

Kumbuka mambo uliyojifunza kutoka katika somo hili utakapokuwa unaongoza kikundi kiini chako, au utakapokuwa unawafundisha wengine jinsi ya kuongoza vikundi vyao.

VIKUNDI KIINI

SOMO LA 6

# Falsafa ya Huduma ya Kikundi Kiini

☞ **Kusudi la Somo**

Kusudi la somo hili ni kuchunguza wajibi wa vikundi kiini katika hali ya ujumla ya harakati za kueneza upandaji kanisa.

☞ **Wazo Kuu**

- Vikundi kiini vinawezesha kueneza upandaji kanisa.
- Kuna njia nyingi za kutumia vikundi kiini katika huduma.

☞ **Matokeo Yanayotarajiwa**

Wakati yaliyomo katika somo hili yanapoeleweka, kila mshiriki anatakiwa:

- Kujifunza kwamba vikundi kiini ni msingi wa matofali ya kujengea kwenye mkakati wa huduma kubwa.
- Kuelewa mzunguko wa maisha ya kikundi kiini.
- Kuelewa nafasi ya vikundi kiini katika harakati za kueneza upandaji kanisa.
- Kuweza kuanzisha mkakati wake wa kikundi kiini.

## I. FALSAFA YA KIKUNDI KIINI

Kila kikundi kinatakiwa kifanye kazi kama "jumuia" ya wakristo wanaoshiriki mmoja kwa mwingine, wanaomwabudu Mungu pamoja, wanaofuasana, na wanaotiana moyo na kusaidiana wanapokuwa wanawafikia nje waliopotea karibu nao. Katikati ya kikundi kiini, kuna maeneo mengi ya wajibu na shughuli nyingi za kupanga na kufanya. Kiongozi wa kikundi kiini,vilevile na wajumbe wa kikundi kwa hakika watakuwa na kazi nyingi za kutimiza mahitaji na kukamilisha malengo ya kikundi.

Vikundi kiini ni msingi wa matofali ya kujengea kwenye mkakati wa huduma kubwa.

Kwa jinsi hiyo, katikati ya shughuli zote za kikundi kiini peke yake, ni muhimu kuelewa kwa ujumla wazo la huduma ya kikindi kiini. Tunahitaji kwa makini kurudi nyuma kutoka kwenye kikundi kiini pekee na kuchunguza kwa ujumla jinsi vikundi kiini vinavyofaa katika mpango wa huduma kubwa. Kwa kifupi imeelezwa, vikundi kiini ni msingi wa matofali ya kujengea kwenye mkakati wa huduma kubwa. Katika hali ya kuanzisha makanisa mapya, vikundi kiini vinatoa msingi ambao juu yake makanisa mapya "yanajengwa."

### A. Viini Vina Mzunguko wa Maisha

Kila kikundi kiini kinapitia katika ngazi za desturi zinazoeleweka za maendeleo.

Kikundi kiini kinapokuwa kimeanzishwa na kukua, kitapitia katika hatua mbalimbali za "maisha," karibu katika njia sawa watu wanvyobadilika wanapokua na kuzeeka. Kila kikundi kiini kinapitia katika ngazi za desturi zinazoeleweka za maendeleo. Kiongozi wa kikundi kiini anatakiwa afikirie juu ya hatua iliyopo ya kikundi chake anapopanga shughuli za kila mkutano, na lazima atarajie nini kinaweza kutokea au kutokutokea wakati wa mkutano huo. Kwa kuelewa ni hatua gani kikundi chake kilipo, kiongozi wa kikundi kiini anaweza kuhakikisha kwamba kikundi chake kiko kwenye kusudio la kuzidisha chenyewe.

Katika aina ya kikundi **kidogo** hasa, kuzidisha hakutokei. Kwa hakika, uzoefu umeonyesha kwamba mwelekeo wa kikundi kidogo ni kuacha kukua au hata kufa baada ya kama miaka miwili. Wajumbe wa wakati huo wanaridhika katika mahusiano yao, na watu wapya hawakaribishwi kwenye kikundi. Hali ile ile, bila kuwa na mpango kamili na maono, kikundi

kiini kinaweza pia kudumaa na kamwe hakitazidi. Ili kufikia lengo la kuzidisha, lazima kuwe na uinjilisti katika kikundi ili kwamba watu wapya waletwe kwenye kikundi, na kiongozi wa kikundi kiini kwa makini lazima alielekeze kundi kupitia hatua za maisha ya mzunguko ili kwamba kundi lisipate “kukwama”na kubakia katika hatua mojawapo yoyote.

Vikundi kiini vinaweza tu kuwa sehemu ya mkakati kuona kuwa makanisa mapya yameanzisha kama wako makini kujua wapi walipo katika maisha ya mzunguko, na nini wanatakiwa kufany ili kuenedelea kusogea katika hatua tofauti za mzunguko wa maisha. Michoro ifuatayo inaelezea hatua za maisha ya mzunguko ambayo kila kikundi kiini kinatakiwa kipitie. <u>Tambua kuwa mda uliotolewa wa kudumu ni makadilio tu, na utatofautiana kutokana na eneo fulani na mandhali ya kikundi kiini</u>. Kiongozi wa kikundi kiini anatakiwa kurejea kwenye mchoro huu katika kipindi kuona ni wapi kikundi kilipo katika maisha ya mzunguko, na nini anatakiwa kufanya ili kwamba kikundi kihamie kwenye hatua inayofata.

**Jedwali 6.1 Hatua za Kikundi Kiini**

| Hatua | Kudumu | Maelezo |
|---|---|---|
| **Mazoezi** | Juma 1 – 4 | Watu wanafahamiana. Kuna hatua nyembamba ya kushirikishana na hatua ndogo ya kuaminiana. Kiongozi wa kikundi kiini anaelekeza karibu huduma yote. |
| **Mpito** | Juma 5 – 10 | Wajumbe wanapata kujuana na kukubaliana. Wanajilinganisha na kile kinachosemekana kama tabia “kawaida” kwenye kikundi. Kuna ongezeko la kuaminiana, na mwanzo wa mahusiano ya kweli. |
| **Jumuia** | Juma 11 – 15 | Wajumbe wanaendana wenyewe kutokana na matarajio ya kikundi. Kuna kuongezeka kwa kujitoa, uwazi, na kuhusika katika kusudi la kikundi. Wajumbe wa kikundi wanapata kutambulika kwenye kikundi. Kiongozi anaweza kugawa shughuli zaidi na maeneo ya wajibu kwa wajumbe wa kikundi. |
| **Matendo** | Juma 16 – 35 | Kuna mwingiliano mkubwa wa kikundi, na watu wanatumia ukweli wa Biblia kwenye hali-halisi ya maisha. Karibu mara kwa mara, kikundi kinajihusisha katika huduma kwa pamoja. Kuaminiana kunakuwa kwa ndani kati ya kikundi cha wajumbe, na uhusiano unaendelea kuongezeka na kukua. |
| **Kuongezeka** | Juma 36 - 40 | Kikundi kinafikia mda ambao ni muhimu kugawanyika katika vikundi viwili. Kiongozi (vi) mwanafunzi anaanza kikundi (vi) kipya, na kundi la mwanzoni linaanza kupanga kwa ajili ya kurudia mzunguko wa kuongezeka. |

## B. Viini Vinafanya Kazi Kuelekea Lengo Moja

Vikundi kiini, karibu sawa na viini katika miili yetu wenyewe, kila kimoja kina “kazi” ya kufanya. Katika mji fulani, kikundi kimoja cha kiini kinaweza kuwafikia nje kwenye hali fulani ya eneo la kijogorafia, wakati kiini kingine kinafanya na pingili la watu. Viini vyote viko vinafanya kazi kwa ajili ya malengo ya pekee, lakini wakati huo huo, vinafanya pamoja kusaidia kuinjilisha mji ambamo wanaishi.

Utafiti unatuambia kwamba kikundi cha watu wanaofanya kazi pamoja kinaweza kukamilisha zaidi kuliko mkusanyiko matokeo ya kila mtu aliyefanya peke yake. Kwa njia hiyo hiyo, vikundi kiini vinavyofanya kazi pamoja pia vinaweza kukamilisha malengo makubwa kuliko ambavyo mmoja wao angefanya peke yake.

Kabla ya kikundi kiini cha kwanza kuanza, Wazo linahitaji kutolewa kwenye lengo kwa ujumla la kikundi. Anza na matokeo ya mwisho akilini, na fanya kazi kwa kurudi nyuma kutoka kwenye lengo hilo. Ni aina gani ya vikundi vinahitajika, na wapi? Ni makundi mangapi yatahitajika kutimiza malengo? Kila kiini kipya kitakuwa na kutambulika kwa pekee, lakini pia kitakuwa sehemu ya mwili “mkubwa’ wa viini uaofanya kazi pamoja kwa kusudi moja.

### C. Viini ni Sehemu Muhimu ya Mkakati wa Kueneza Upandaji Kanisa

> Harakati za makanisa mapya zinahitaji njia ambazo ni rahisi, nyepesi, zinazonyumbulika na zinazozaa.

Mkakati wa kueneza upandaji kanisa kiasili ni "msingi wa chanzo" cha harakati za makanisa yanayozaliana. Harakati za makanisa machache zinahitaji njia ambazo ni rahisi, nyepesi, zinazonyumbulika na zinazozaa. Bila sifa hizi, harakati haziwezi kupatikana au kutengemezwa. Karibu haiwezekani kuwa na harakati za makanisa machache ambazo zinahitaji mchungaji wa kulipwa "mwenye kuisomea" na nyumba ya kanisa yenye thamani.

Vikundi kiini vinatoa urahisi na kunyumbulika ambako harakati zinahitaji. Ni mtindo ambao ni rahisi kuanza na kuzalishwa. Kuna mahitaji kidogo ya fedha au hakuna. Vinatoa huduma ya kiutendaji katika kufundisha na matumizi. Vinatoa jumuia na ushirika miongoni mwa waumini. Mkazo wa huduma ya vikundi kiini ni kwa watu na mahitaji, siyo kwenye vipindi na taratibu. Kikundi kiini kinafanya kazi katika ngazi ya kukidhi hitaji la msingi la binadamu la upendo. Kukubalika na kumaanisha.

Muhimu zaidi, Kwa ajili ya harakati za kueneza upandaji kansia, vikundi kiini vinatoa harakati za yote maono ya kuwafikia waliopotea na maono ya kuzidisha. Bila maono ya kuwafikia ambao hawajafikiwa kwa ajili ya Kristo, hakuna hitaji la harakati za upandaji kanisa. Bila maono na uwezo wa kuzidisha makanisa, harakati haziwezi kuwepo.

Agizo la Utume Mkuu linaweza kutimizwa vizuri zaidi kwa harakati za kueneza upandaji kanisa. Harakati za kueneza upandaji kanisa zinaweza kutambulika zaidi kwa kutumia vikundi kiini kama msingi ambapo kuzalisha makanisa kunaanzia.


## II. VIELEZO VYA HUDUMA YA KIKUNDI KIINI

Moja ya faida za vikundi kiini ni kwamba vinaweza kutumika kwa njia tofauti tofauti, na hasa katika huduma ya mpanda kanisa. Ifuatayo ni mitindo mbalimbali inayoweza kutumika katika huduma ya kikundi kiini. Kila mtindo una faida zake, na mpanda kanisa anatakiwa awe huru kuchagua mtindo (au mchanganyiko wa mitindo) ambao utafanya kazi vizuri katika hali yake.

### A. Kielezo 1: Vikundi Kiini Vinavyoanza Kanisa la Mapokeo kwa Viini

Katika hali hii, moja au zaidi ya kiini cha kwanza kinakua na kuzidisha. Wakati idadi kadhaa ya watu wanakutana katika vikundi (Pengine jumla ya watu 50), uamzi umefanywa kuanzisha kanisa mpya, la mapokeo. Kanisa hili litakutana katika eneo la kati na ibada ya mapokeo inayofaa kwa mandhali ya hapo na utamaduni. Kanisa litaendelea kutumia huduma ya vikundi kiini kwenye uinjilisti, kushirikiana, kufuasa na kukua kwa kanisa kunakoendelea. Linaweza pia kuchagua kuanzisha huduma za "vipindi" vya mapokeo kama vile darasa la jumapili, huduma ya wanawake, kuwafikia watoto siku za mapumziko n.k. Kielelezo 6.1 kinaonyesha aina hii ya mtindo.


**Kielelezo 6.1 Viini Vinaanzisha Kanisa**



**B. Kielezo 2: Kanisa Lililopo Linaanza Kutumia Vikundi Kiini**

Inawezekana kwa kanisa lililopo kuanza kutumia vikundi kiini kwa ajili ya kushirikiana, uinjilisti na kufuasa. (Somo la 12 la Vikundi kiini "Kutumia Vikundi Kiini katika Kanisa Lililopo" katika Mwongozo wa Tano tutazungumzia hili kwa undani). Uongozi uliopo katika kanisa lazima uamue ni vikundi vingapi vinahitajika/vinavyowezekana kutokana na idadi ya watu kanisani na idadi ya watu ambao wangeweza kufundishwa kuwa viongozi wa kikundi kiini. Kwa wakati huo, Kanisa litaanza kukua kadiri vikundi kiini vitakavyokua na kuongezeka. Mpangilio huu umeonyeshwa katika kielelezo 6.2.


**Kielelzo 6.2 Viini Vilivyoongezwa Kwenye Kanisa**




**C. Kielezo 3: Vikundi Kiini Vinavyoanzisha Kanisa la Kikundi Kiini**

Kanisa la kikundi kiini linatofautiana na kanisa la mapokeo kwa maana kwamba hakuna jengo la kanisa, hakuna ibada ya kawaida ya jumapili, na kanisa halipo kutunga na kuendeleza"vipindi" kanisani. Kanisa linaundwa na viini vyenyewe, na kazi zote za kanisa zinatokea katika kila kiini, ikiwa ni pamoja na ubatizo na ushirika wa meza ya Bwana. Viini vinakutana mara moja moja (Mf. Mara moja kwa mwezi) kwa ajili ya "kusherehekea" mkutano. Huu ni mda wa kutiana moyo, kushirikiana, kuabudu na/mafundisho. Katika maeneo ambapo harakati za vikundi kiini zimekua sana, wakati mwingine majumba ya maonyesho na majumba makubwa ya senema yanahitajika kuweza kuchukua watu wote hawa kutoka kwenye vikundi kiini kwa ajili ya mkutano wa sherehe hizi. Viini vinajifikiria kwa ujumla kuwa sehemu ya mmoja, kanisa kubwa. Kielelezo 6.3 kinaelezea mtindo huu.


**Kielelezo 6.3 Viini Kuanzisha Kanisa la Kiini**



**D. Kielezo 4: Aina Kadhaa ya Vikundi Kiini Kukua, Kuzaliana na "Kulisha" Makanisa ya Mtaa Yaliyopo**

Siyo hitaji kwamba vikundi kiini vianzishe makanisa mapya moja kwa moja. Inaweze ikawa zaidi kimkakati kujenga na kuimarisha makanisa ya mtaa yaliyopo, ambayo kwa mda yataanza makanisa mapya, makanisa binti. Vikundi kiini vinaanzishwa kwa kujitegemea kwa makanisa yaliyopo. Kadiri watu wapya wanavyoletwa katika vikundi kiini, wanatiwa moyo kuanza kuhudhuria kanisa la mtaa vilevile. Mara nyingi wataendelea kuwa sehemu ya kikundi kiini chao na vilevile kuhudhuria kanisa. Utaratibu huu umeonyeshwa katika kielelezo 6.4.

**Kielelezo 6.4 Viini Vinalisha Makanisa**




**E. Zoezi la-Darasani: Michanganuo**

Ifuatayo ni baadhi ya mifano ya kufanyia uchunguzi wa mikakati ya upandaji kanisa ambayo wengi wanaweza au wasiweze kutumia kanuni kutoka kwenye mitindo ya vikundi kiini iliyoorodheshwa hapo juu. Darasani, jadili (1) ni mtindo gani wa mtiririko wa matukio unatokana (kama upo) na (2) faida na hasara za mtiririko wa matukio haya kama mkakati wa upandaji kanisa.

**Mchanganuo 1**

Kanisa la ufufuo linahitaji msaada fulani. Kanisa lina zaidi ya miaka hamsini, na lina karibu watu 25 wanaokutana katika ibada. Mashemasi watatu walimwendea mchungaji wakiwa na wazo la kuwaweka wajumbe 25 katika makundi matatu ya vikundi kiini. Vikundi kiini vitaongozwa na mashemasi, na watakuwa na mkazo kwenye uinjilisti, kufuasa, kukua na kuongezeka.

**Mchanganuo 2**

Mpanda kanisa anahamia kwenye mji ambao hauna kanisa na kuweza kuanzisha vikundi kiini kadhaa vipya. Vikundi kiini vina mafanikio makubwa, na kuanza kukua na kuongezeka vyenyewe. Watu katika viini wanajisikia ukaribu wa mmoja kwa mwingine, na kuamua kuwa wataanza kanisa moja kutoka kwenye vikundi. Kila kikundi kiini kipya kilichoanzishwa kitaendelea kuwa sehemu ya kanisa hili moja kubwa.

**Mchanganuo 3**

Kanisa la Babutisti ya kwanza lina wajumbe 1000. wana ibada kadhaa za jumapili na ibada nyingine jumatano. Mchungaji kiongozi wa kanisa anaamua kuwa wajumbe wanatakiwa wawe wanakutana pamoja katika makundi madogo. Viongozi wa kanisa wanagawanya wajumbe katika makundi kumi, na kuwaweka wajumbe kwenye vikundi maalumu.

**Mchanganuo 4**

Wapanda kanisa kadhaa wanaanza kuanzisha vikundi kiini. Kundi lina maono ya kufanya uinjilisti na kuongezeka, lakini halitaki kuanzisha makanisa mapya. Badala yake, wanaelekeza waumini wapya katika moja ya makanisa yaliyopo katika mji. Baadhi ya vikundi vina wajumbe ambao wanaendelea kukutana katika vikundi, vilevile na kuhudhuria makanisa ya mtaa ya madhehebu mengine.

**Mchanganuo 5**

Miaka michache iliyopita huduma kutoka magharibi ilileta wamishenari ambao walianzisha baadhi ya vikundi vodogo vya kujitegemea kutoka kwenye makanisa ya mtaa yaliyopo. Makundi haya yanakutana mara moja kwa wiki na kufanya mafunzo ya Biblia kwa kufata neno.

**Mchanganuo 6**

Kanisa la kiinjili lina vikundi vidogo vingi ambavyo vinakutana kujifunza Biblia. Watu walewale wameshawahi kukutana katika vikundi hivi miaka kadhaa iliyopita, na vikundi havikukua. Vikundi kadhaa vina watu wanaoisha karibu, lakini wanaoishi mbali kutoka kanisani. Vikundi hivi vinaamua kuwa vingependa kuanzisha kanisa mpya karibu na wanapoishi.

**Mchanganuo 7**

Mpanda kanisa anahamia kwenye mji mpya na anaanza kufanya uinjilisti. Watu ni wapokeaji, na mara ameanza vikundi kadhaa vidogo, ambavyo kila kimoja kina maono ya kuinjilisha na kuzidisha. Vikundi vinakutana jumapili kwa ajili ya mda wa kuabudu na mafundisho, na jumatano jioni wanaalika marafiki wasio-amini kwa mda wa burudani na kushirikiana. Hakuna mpango wa kujenga jengo la kanisa, na mara moja kila baada ya wiki sita kikundi kinakodi ukumbi kwa ajili ya jioni ya ibada ya pamoja na mafundisho.

Hakuna njia moja “sahihi” ya kutumia vikundi kiini katika huduma la upandaji kanisa, lakini kila mpanda kanisa lazima afikirie mtindo bora wa kutumia katika mandhali yake. Haijalishi msisitizo wa vikundi kiini ni nini, kuzidisha mara zote litakuwa ni lengo la kikundi hicho.

## III. KUANZISHA MKAKATI WA HUDUMA YA VIKUNDI KIINI

Kwa kuwa vikundi kiini ni matofali ya kujengea kwenye mkakati wa huduma kubwa, mawazo lazima yatolewe kwa ujumla kwenye mkakati wa kujenga kanisa na jinsi vikundi kiini vinaweza kutumika ili kufanikisha lengo lililowekwa. Katika kila ngazi ya kikundi kiini, inasaidia kutafakari juu ya hatima ya lengo la kikundi.

Yafuatayo ni mawazo kadhaa ya kufikiria:

1. Tambua lengo la huduma kwa ujumla. Unaanzisha harakati za kueneza upandaji kanisa? Kanisa moja? Makanisa ya kutosha kueneza , mji au eneo la kijografia? Matokeo yako ya mwisho yataonyesha aina, idadi, na mkazo wa huduma ya kikundi kiini chako.
2. jinsi gani viini vinahitaji kufanya kazi kwa kujitegemea na kwa pamoja ili kuona malengo yanakamilika? Jinsi gani kazi hii itapangwa na kufanyiwa tathimini?
3. Ni nini eneo linalolengwa, na ni watu gani wanaolengwa? Utafiti unatakiwa ufanyike ili kuweza kuelewa vizuri aina za shughuli zinazohitajiwa katika vikundi kiini (Tazama somo la maono “Kanuni za Utafiti” katika Mwongozo 1).
4. Ni aina gani ya uinjilisti inafaa kwa eneo /watu wanaokusudiwa? Ni jinsi gani utashirikisha hili katika vikundi kiini vipya?
5. Ni viongozi gani wa mstari wa mbele katika eneo linalolengwa? Jinsi gani itawezekana kwa kikundi kiini kimoja au zaidi kuanzisha uhusiano na watu hawa na pengine kuwaleta kwa Kristo?
6. Ni aina gani ya “mitindo” ya kikundi kiini unayohitaji ili kukamilisha malengo yako? (Mf. Viini vingi vinavyounda kanisa moja, viini vinavyotumiwa na makanisa yaliyopo, viini vinavyoanzisha kanisa la kikundi kiini, n.k.). Zaidi ya ilivyo, utahitaji kutumia aina kadhaa ya mchanganyiko wa mitindo ya kikundi kiini iliyoonyeshhwa katika somo hili ili kukamilisha malengo yako kwa ujumla.

## MASWALI YA KUTAFAKARI, MARUDIO NA MATUMIZI

- Kikundi kiini chako kitakuwa katika moja ya ngazi ya mzunguko wa maisha (majaribio, mpito, jumuia, matendo au kuzidisha). Kwa nini hili linamaanisha unapokuwa unapanga kwa ajili ya shughuli zako za mkutano? Kwa nini inamaanisha kutoka kwenye mtizamo wa mkakati wa kikundi kiini kwa ujumla?
- Kwa nini vikundi kiini ni sehemu muhimu katika mkakati wa kueneza upandaji kanisa?
- Ni upi kati ya mitindo (Kama upo) kutoka kwenye "Mitindo ya Huduma ya Kikundi Kiini" sehemu inaweza kufanya kazi katika eneo lako unalolenga?

## UTEKELEZAJI WA AZIMIO

- Katika sentensi kadhaa, andika tafafsiri ya vikundi kiini kwa kifupi lakini yenye mambo mengi. Mpatie hii mkufunzi.
- Kulingana na unachojua juu ya eneo lako unalolenga na malengo uliyoweka kwa ajili ya eneo hilo, andika msingi wa mkakati wa jinsi unavyoweza kutumia vikundi kiini ili kuyatimiza malengo hayo. Weka pamoja na vigezo kutoka kwenye "Fikira za mkakati wa kikundi kiini" sehemu katika mpango wako. Shirikisha mpango wako na mfunzwa mwingine, na kila mmoja wenu atathimini mpango wa mwingine. Kwa kusudi la somo hili, mpango wako unatakiwa usiwe zaidi ya uefu wa vifungu vichache

# NJIA ZA KUJIFUNZA BIBLIA

NJIA ZA KUJIFUNZA BIBLIA

SOMO LA 8

# Njia Tofauti Tofauti za Kutumia Mafunzo ya Biblia Kwa kufata Neno

☞ **Kusudi la Somo**

Kusudi la somo hili ni kutia moyo utumiaji wa njia za kujifunza Biblia kwa kufata neno katika aina tofauti za mafunzo kwa nyongeza ya mafungu mafupi.

☞ **Wazo Kuu**

- Lengo la mafunzo yoyote ya Biblia linatakiwa liwe kuchunguza nini Biblia inasema, na hili ni vizuri lifanyike kwa njia ya kujifunza kwa kufata neno.
- Aina ya mafunzo ambayo yanaweza yakafaidisha kutoka kwenye njia ya kujifunza kwa kufata neno ni pamoja na kujifunza historia ya maisha, kujifunza vitabu, na kujifunza kuhusu kisa.

☞ **Matokeo Yanayotarajiwa**

Wakati yaliyoma katika somo hili yanapoeleweka, kila mshiriki anatakiwa:

- Kushawishika kuwa njia ya kujifunza kwa kufata neno inatakiwa itumike katika mafunzo yoyote ya kujifunza Biblia anayofanya au kuongoza.
- Kujua jinsi ya kukabili kujifunza wahusika wa Biblia, kitabu au kisa kutoka kwenye mtazamo wa kujifunza kwa kuongozwa na neno.

☞ **Ziada**

8A Kujifunza historia ya maisha ya Barnabas

**UTANGULIZI**

Mwongozo uliopita umeelezea jinsi njia ya kujifunza kwa kufata neno inavyokazia kwenye kugundua na kutumia maana ya neno la Mungu. Msisitizo ni kwenye maandiko badala ya kuelewa kwetu kwa kwanza kwa kifungu. Kwa tumaini kuwa tayari imeshazidisha kujifunza kwako kwa neno.

Mpaka hapo, Tumetumia njia ya kujifunza kwa kufata neno kuangalia katika vifungu vifupi kwa sababu ya mda usiotosha uliopo wakati wa somo. Kwa jinsi hiyo, Njia ya kujifunza Biblia kwa kufata neno inaweza kutumika kujifunza kipande kikubwa zaidi cha Biblia au kulinganisha mistari kutoka sehemu tofauti—kama ambavyo itakuwa muhimu katika kiini au katika historia ya maisha ya mtu. Katika somo hili, tutajadili baadhi ya mipaka ya kutumia njia ya kujifunza kwa kufata neno kwa aina ya mafunzo hayo tofauti.

## I. FANYA MARUDIO YA KANUNI ZA NJIA ZA KUJIFUNZA BIBLIA KWA KUFATA NENO

Kabla ya kutumia njia ya kujifunza Biblia kwa kufata neno, unatakiwa uangalie nyuma kwenye sehemu ya njia za kujifunza Biblia katika Mwongozo wa kwanza


### A. Sababu ya Njia ya Kujifunza Kwa Kufata Neno

Njia ya kutumia upunguzaji inaanza kwa kuelewa-kulikopo au ukweli unaoonyesha maana ya hali iliyosomwa. Tunapotumia njia hii kujifunza Biblia, Tunaishia kujaribu kufanya mstari kusema kile ambacho tumekwisha kuelewa juu yake baadala ya kujifunza kutokana nao. Kinyume chake, Tunapotumia njia ya kujifunza kwa kufata neno katika kujifunza Biblia, tunakuja kwenye fungu kujifunza na kuruhusu neno kusema kwetu.

### B. Hatua za Njia ya Kujifunza Kwa Kufata Neno

Hatua tatu za njia ya kujifunza kwa kufata neno—uchunguzi, ufafanuzi, na matumizi—yameonyeshwa katika kielelezo 8.1. Njia ya kujifunza kwa kufata neno inatuongoza katika hatua ya kuuliza nini Biblia inasema, ina maana gani, na nini nifanye juu yake. Inaanza kwa kuchukua mda kuchunguza kwa karibu mandhali ya maandiko, na kumalizia kwa kuyaweka katika matumizi ya maisha yangu na huduma.

**Kielelezo 8.1 Hatua Tatu**




Ni muhimu kuzifanyia kazi hatua kwa utaratibu, bila kurukia mbele. Utaratibu ni kama piramidi, ambapo ilikuwa lazima kujenga msingi mkubwa na imara wa uchunguzi kabla ya kuanza kujenga ufafanuzi wetu juu yake, na kuutumia katika maisha yetu.

### C. Msisitizo wa Njia ya Kujifunza kwa Kufata Neno

Njia ya kujifunza Biblia kwa kufata neno inaweza kutumika katika aina nyingi za mafunzo ya Biblia, vilevile kama utakavyoona hapo chini. Kuna idadi ya kanuni ambazo kwa ujumla ni muhimu, bila kujali ni aina gani ya mafundisho unafanya. Haya ni pamoja na:

- Kuuliza maswali mengi kama Nani?, Nini?, Wapi?, Lini?, Jinsi gani?, na Kwa nini?
- Kuangalia vigezo vikuu
- Elewa kusudi la mwandishi
- Ruhusu ufunuo wa kuendelea
- Elewa mandhali
- Eleza kanuni ya kibiblia
- Linganisha mandhali ya kibiblia na ya kisasa
- Omba

Rejea kwenye somo lililopita kwa taaarifa zaidi za kanuni hizi.

## II. MAFUNZO YA HISTORIA ZA MAISHA YA WATU

Mafunzo ya historia za maisha ya watu, au mafunzo ya wahusiaka, yanahusu kujifunza kila kitu kilichoandikwa juu ya mtu fulani kwenye Biblia. Kama hii inahusisha idadi ya vifungu vingi, vinavyoweza kusaidia kujifunza tukio maalumu au mda wa karibuni katika maisha ya muhusika. Kwa mfano, unaweza kujifunza juu ya Paulo wakati wa safari zake za kimishenari au Daudi wakati wa kukimbia kwake kutoka kwa mfalme Sauli. Kwa jinsi hiyo, hata katika hali hiyo, fikiria maisha yote ya mtu, na jinsi sehemu iliyochaguliwa inavyotosheleza kwa jumla.

### A. Kwa nini Kufanya Mafunzo ya Historia ya Maisha ya Mtu

Kila mmoja anapenda historia. Ni rahisi kulinganisha kwenye matatizo, changamoto, majaribu, furaha, na mafanikio ya wengine wakati haya yanapoonekana katika umbo la historia. Biblia imejaa mifano mizuri na mibaya inayoonekana katika historia za maisha ya watu.

> Kwa kujifunza masisha ya watu muhimu kibiblia na uwezo wao na udhaifu wao, tunaweza kujifunza masomo mengi ya kutusaidia kujilinganisha na sura ya Kristo.


Kwa kujifunza maisha ya watu muhimu kibiblia na uwezo wao na udhaifu wao, tunaweza kujifunza masomo mengi ya kutusaidia kujilinganisha na sura ya Kristo. Zaidi Biblia inahusika na Mungu kufanya kazi na mmoja mmoja kurejeza utaratibu huu. Kwa mfano, kutoka kwa Ibrahimu tunajifunza juu ya imani; Kutoka kwa Yusufu tunajifunza juu ya kukabiliana na majaribu; kutoka kwa Esther tunajifunza juu ya kutenda kwa utakatifu kwa Mungu; kutoka kwa Danieli tunajifunza juu ya maombi; kutoka kwa Yona tunajifunza juu ya kinachotokea kwa mtu anayejaribu kumkimbia Mungu; kutoka kwa Paulo tunajifunza juu ya misheni. 1Wakorinthi 10:11 ni msitari wa ufunguo: “Mambo haya yaliwatokea kama mifano na kuandikwa kama maonyo kwetu.” Ni mifano ipi tena inayokuja akilini mwako?

Kwa kutumia historia ya maisha ya wahusika katika Biblia, wapanda kanisa lazima waweze kuwakilisha ukweli mwingi kwa hao wanaotafuta kuinjilisha na kuwafundisha. Lakini ili kuitumia kwa usahihi zaidi, ni muhimu kuelewa ni nini Biblia inafundisha kupitia maisha ya mtu. Kanuni nzuri za kujifunza Biblia lazima zitumike kwenye mafunzo ya historia ya maisha ya watu sawa na aina yoyote ya kujifunza Biblia.

### B. Jinsi ya Kufanya Mafunzo ya Historia ya Maisha ya Watu

Mafunzo ya kufata historia za maisha ya watu inafata mfano unaofanana na wa uchunguzi, ufafanuzi, na matumizi kama somo moja linavyofanya, kwa tofauti moja ya maana. Kielelezo 8.2 kinaelezea jinsi uchunguzi unavyofanywa kwa kila fungu. Hata hivyo, kufafanua kunahitaji hatua nyingine. Kwanza, kanuni ya kibiblia kwa kila fungu imeonyeshwa. Kisha, kanuni ya kawaida inaundwa kutoka kwenye kanuni ya pekee. Mwisho, matumizi ya kawaida yanayofupisha vifungu vyote yanatungwa na kuwekwa katika matumizi. Sehemu ya chini itapanua mawazo haya.

**Kielelezo 8.2 Mafunzo ya Historia za Maisha**



1. *Uchunguzi*

Uchunguzi unahusu kuangalia kabisa katika vifungu vyote vinavyoendana—kila kimoja baada ya kingine. Kila fungu linafundisha ukweli fulani katika mandhali fulani. Unahitaji kugundua ukweli ni nini kwa kila fungu kabla ya kuendelea kwenye ufafanuzi. Tumia hatua hapo chini kama kiongozi:

- Chagua mtu katika Biblia unayetaka kujifunza juu yake
- Fanya orodha ya malejeo YOTE ya kibiblia kwa mtu huyo. Kama ipo, tumia kamusi ya Biblia.
- Ipange mistari kwa utaratibu wa mfuatano.
- Unda na uliza maswali mengi ya uchunguzi iwezekanavyo (Nani?, Nini?, Wapi?, Lini?, Jinsi gani?, na Kwa nini?)
- Fanya uangalifu wa pekee kwenye dalili kama ilivyo kwa muhusika, hadhi, mawazo, au matendo ya mtu unayejifunza. Kwa mfano:
  - Nini tunachoweza kujifunza kutoka kwa mababu na familia?
  - Maana ya jina lake ni muhimu? Ililibadilishwa? Kama ni hivyo, nini ilikuwa maana ya mabadiliko hayo, mf. Abramu kuwa ibrahimu, Yakobo kuwa Israeli, Simoni kuwa Petro n.k.
  - Lini na wapi aliishi? Ni nini tunachojua kutoka kwenye vyanzo vingine, vyote vya kibiblia na visivyo vya kibiblia, juu ya maisha katika siku zake?
  - Ni matukio gani ya maana yaliyotokea katika maisha yake: misukosuko, aliyokamilisha, kuitwa kwenye kazi maalumu matatizo aliyokutana nayo, n.k.
  - Mahusiano: Ni nini ilikuwa uhusiano wake na Mungu? Ni jinsi gani alivyopatana na wengine?
- Andika na weka kwa kifupi maandishi yako kwa kila mstari.

2. *Ufafanuzi*

> Kila moja ya vifungu ambavyo unachagua kujifunza vina kusudi maalumu na mafundisho ya pekee.

Ufafanuzi ni utaratibu wa-sehemu mbili unapohusisha zaidi ya fungu moja la maandiko—kama ilivyo mara nyingi kwenye swala la kujifunza historia ya maisha. Kila moja ya vifungu ambavyo unachagua kujifunza vina kusudi maalumu na mafundisho ya pekee. Kwa sababu ya umoja wa maandiko, makusudi haya hayatapingana, lakini yanaweza kuwa tofauti. Kawaida, yanaongeza habari zaidi. Kila moja ya makusudi haya inatakiwa igunduliwe na kuelezewa kama kanuni ya kibiblia, kwa kutumia uongozi uliotolewa kwenye majadiliano ya awali ya njia ya kujifunza kwa kufata neno.

Mara kanuni hizi za kila fungu pekee zinapokuwa zimeelezwa, inawezekana kumalizia utaratibu wa kutafsiri kwa kuziunganisha kwa uangalifu na kimawazo kwenye kanuni moja ambayo inajumlisha mchango wa kila sehemu. Kwa mfano unachagua kujifunza kipande cha maisha ya Daudi. Fungu moja limefundisha kuwa alikuwa amejitoa kwenye neno la Mungu. Nyingine lilikazia maisha yake ya kuomba. La tatu linasisitizia kumtumaini kwake Mungu nyakati za matatizo. Kanuni ya kawida inayofaa inaweza kuwa, “Tunatakiwa kujitoa kwenye neno na maombi tunapomtumaini Mungu katika nyakati za matatizo.” Kanuni inafupisha mafunzo ya mafungu yote matatu.

3. *Matumizi*

Mara mafunzo yako ya mhusika yanapokuwa yametafsiri kanuni ya kawaida ya kibiblia, unaweza kulinganisha hali yako na yake na kuonyesha nini unatakiwa kufanya. Hii ni kwamba, utaangalia njia ambazo zipo kwenye mandhali yako na ya mhusia kibiblia inafanana, na kuitikia kulingana na mafundisho uliyoyaona katika neno. Unapofanya hatua hii, unaweza kuhitaji kurejea kwenye baadhi ya vifungu Roho Mtakatifu anapovileta akilini, na kumruhusu kukufundisha na kukuongoza katika utaratibu.

Kuna maswali mengi ya ufafanuzi ambayo unaweza kuuliza kukusaidia kugundua matumizi yako muhimu zaidi. Haya ni pamoja:

- Ni kwa jinsi gani uzoefu wangu ni sawa na wake?
- Nina uwezo kama wake? Udhaifu?
- Kwa nini Mungu alimuhusisha mtu huyu katika maandiko?
- Ni vitu gani maalumu Mungu anataka kunifundisha kwa kujifunza maisha yake?

*Tambua: Mfano wa mafunzo ya historia ya maisha ya Barnabas yanapatikana katika ziada 8A.*

## III. MAFUNZO YA VITABU

Wasomi wengi wa Biblia wana kisa kimoja—ingawa wanabishana jinsi ya kukieleza kiusahihi. Kila kitabu cha Biblia kinaanzisha kisa hicho cha wote kwa kuchangia kitu fulani cha kipekee. Mfano mzuri wa hili unaonekana katika vitabu vya injili. Waandishi wa injili nne waliandika juu ya maisha ya Kristo. Kuna kufanana kwingi kwenye vitabu vya injili na pia kutofautiana kwingi. Kila kimoja kimeandikwa kutoka kwenye mtazamo wa kipekee.

- Mathayo—anamuonyesha Kristo kama Masiya wa Wayahudi (wa kifalme)
- Marko—anamuonyesha Kristo kama mtumishi (mnyenyekevu)
- Luka—anamuonyesha kristo kama mwana wa mtu (mwanadamu)
- Yohana—anamuonyesha Kristo kama mwana wa Mungu (asili)

> Vitabu vyote sitini na –sita vya Biblia vinafanya kazi pamoja kutoa ujumbe kamili Mungu alionao kwa ajili yetu.

Kila moja ya picha ya Kristo ni kweli, na bado, kila moja ni tofauti. Kila injili inaelezea kipengele muhimu cha mtu au cha muhusika wake vizuri zaidi kuliko nyingine. Injili zote nne zinafanya kazi pamoja kumwelezea Bwana kikamilfu. Katika njia sawa, vitabu vyote sitini na –sita vya Biblia vinafanya kazi pamoja kutoa ujumbe kamili Mungu alionao kwa ajili yetu. Kitabu kimoja kinaelezea upendo wake vizuri zaidi, kingine uvumilivu wake, kingine gadhabu yake. Kitabu kimoja kinasisitizia hali ya kupotea ya anguko la mwanadamu, wakati kingine kinaelezea wokovu wetu wa utukufu kupitia kumwagika kwa damu ya Kristo.

### A. Kwa nini Kufanya Mafunzo ya Kitabu?

Kwa kuwa vitabu vyote sitini na-sita vinafanya kazi pamoja kutoa ujumbe wa Mungu kwetu, tunahitaji kuchunguza kila kitabu kwa uangalifu kama tunataka kuelewa kwa usahihi mchango wake kwenye ujumbe huo. Kuna faida nyingine pia. Tunapoelewa kisa cha kila kitabu, tunajua wapi pa kugeukia kutafuata jibu kwa ajili ya tatizo fulani. Kuna mtu fulani anahangaika na uhalali? Nenda kwa Wagalatia. Tuna mashaka na wokovu wetu? Soma Warumi. Tuna maswali na uungu wa Kristo?. Soma Yohana. Kama tuna mashaka na uzito wa dhambi, tunatakiwa kusoma Waamuzi. Kila kitabu kina msisitizo na ujumbe maalumu.

### B. Jinsi ya Kufanya Mafunzo ya Kitabu

Mafunzo ya kitabu yanatumia hatua sawa kama za njia ya kujifunza kwa kufata neno ambazo tumekuwa tukijifunza. Kawaida, kujifunza kitabu kutahitaji mda wa kutosha kufanya kiusahihi. Faida, kwa jinsi hiyo, itafanya kiurahisi mda wako kuwa wa faida. Mfunzo ya kitabu yana hatua nne:

1. *Soma Kitabu Mara Kadhaa*

> Chukua mda wa kukisoma kitabu kwa kurudia kabla ya kujaribu kukifafanua.

Vitabi vingi vya Biblia kwa kifupi ni barua fupi au ujumbe mfupi. Vilikuwa vimekusudiwa kusomwa kuanzia mwanzo hadi mwishoni bila ufafanuzi. Njia nzuri ya kujifunza ni kuvisoma mara kadhaa mpaka unapoanza kugundua kisa na wazo lililorudiwa au kukaziwa. Baadhi ya vitabu virefu (kama vile Isaya na Yeremia) viliandikwa miaka mingi iliyopita, lakini pia vimekusudiwa kwa aina moja ya watazamaji na vitawasilisha zaidi waziwazi kama tukivisoma vyote. Mara inapokuwa haitoshi—ama ni kuangalia tu uchaguzi kutoka kwenye kitabu. Chukua mda kukisoma kwa kurudia kabla hujajaribu kuanza kukifafanua.

2. *Soma 'mpangilio' wa kitabu*

   Kuna idadi ya vigezo muhimu ambavyo tutaviita 'mpangilio' wa kitabu. Unaweza kupata baaadhi ya habari hizi kwenye kitabu chenyewe au kwenye maandishi kwenye Biblia yako. Maswali mengine yatahitaji matumizi ya kamusi, vitabu vidogo vya Biblia, au msaada mwingine. Unapoanza mafunzo yako, punguza matumizi ya misaada hii kupata utangulizi wa ukweli juu ya kitabu, na siyo kutoka kwenye mawasilisho ya mfasiri. Tunza hilo kwa ajili ya baadaye, mara unapokuwa umepata mda wa kuruhusu neno kuzungumza kwako kwanza. Unapoanza mafunzo yako, angalia ukweli wa 'mipangilio' ifuatayo:

   - *Mwandishi*—Kama inawezekana, amua ni nani aliyeandika kitabu, na kisha jifunze zaidi uwezavyo juu ya mtu huyo. Kwa nini Mungu alimchagua yeye kama mwandishi mwanadamu? Ni nini ilikuwa hali yake ya nyuma na uzoefu? Alikuwa mtu wa namna gani? Ni akina nani walikuwa familia yake? Lina na jinsi gani aliokoka? Alikuwa na umri gani? Alikuwa na cheo gani? Jibu maswali mengine mengi juu ya mtu huyo uwezavyo.
   - *Mpokeaji*—Ni akina nani waliandikiwa kitabu? Nini ilikuwa hali yao kwa wakati huo? Ni kwa nini unadhani kitabu kiliandikwa? Jinsi gani kilitolewa kwao (kuhubiriwa, kutolewa unabii, barua iliyobebwa- mkononi, n.k.)? Ni nini ulikuwa uhusiano wao na Mungu? Kwa mwandishi mwanadamu? Nini ilikuwa hali yao ya kisiasa? Hali yao ya kidini?
   - *Tarehe*—Ni lini kitabu kiliandikwa? Ni nini matukio yaliyokuwa yanatokea kihistoria katika wakati huo? Ni wapi kitabu hiki kinafaa Mungu kuendeleza ufunuo kwa mwanadamu? Ni nini ulikuwa mda wa kitambo wa kuandika kitabu?
   - *Mtindo wa maandishi*—Ni aina gani ya maandishi yalitumika (Mashairi, unabii, kihistoria, ya kujulisha, n.k.)? Angalia njia za kujifunza Biblia Ziada 2A: "Lugha ya Biblia" kwa habari zaidi juu ya mitindo. Ni kwa jinsi gani mtindo huu utaathiri kufafanua kwako? Ni kwa jinsi gani inaweza kuwa imemwathiri mpokeaji?


3. *Jifunze Yaliyomo Katika Kitabu*

   Kuna mambo mawili ya kutafakari katika kujifunza kitabu. La kwanza ni kisa na la pili ni jinsi gani kisa kimeendelezwa. Kwa maneno mengine, mwandishi alitaka kuwakilisha wazo maalumu kwetu, na alifanya hivyo kwa njia maalumu. Yote ni muhimu.

   a. Kisa cha Kitabu

      Sasa unajua ukeweli mwingi juu ya kitabu, jifunze yaliyomo katika kitabu. Kitabu kitakuwa na kisa kimoja kikubwa au inaweza kuwa si rahisi kukigundua. Kwa mfano, Yohana anaeleza wazi wazi kisa cha injili yake (Yoh 20:31). Hata Yuda (Yd 3). Waandishi wengine hawako wazi sana.

**Kielelezo 8.3 Sehemu za Kitabu**



b. Maendeleo ya Kisa

Yaliyomo katika kitabu yatafanya kazi pamoja kuwakilisha kisa cha kitabu kwa mpokeaji (na kwetu). Unapokuwa unasoma na kuuliza maswali, tambua jinsi mwandishi anavyokamilisha kazi. Ni aina gani ya hali anayoonyesha (mamlaka, upole, upendo, hasira,n.k.)? Ni lugha ya aina gani anayotumia- lugha ya wazi, lugha ya uchungu, lugha yenye ufasaha, au lugha ya kushawishi, n.k? Ana mkazo kwenye mawazo au hisia? Jinsi gani? Kwa nini unadhania anatumia njia hizo?

4. *Wekajedwali la Maendeleo ya Kisa cha Kitabu*

Msaada mmoja katika kujifunza kitabu ni kutengeneza chati ya kisa kikuu, wahusika, sehemu, n.k ambao wamejadiliwa katika kitabu. Kila mara Biblia ya kujifunza au kamusi itakuwa pamoja na chati kama hiyo. Kuna vyanzo vingine pia vya chati hii, kama vile Jensen (angalia vyanzo). Kwa jinsi hiyo,unaweza kutengeneza vyako mwenyewe. Kwa hakika, kujifunza kwako kutakuwa kwa faida zaidi kama unajaribu kuweka chati ya mtiririko wako mwenyewe kabla hujatafuta msaada kwa vyanzo vingine. Michoro hii haihitaji kuelezewa—inakusudiwa kukusaidia kuona asili kwa ujumla ya kitabu. Kielelzo 8.3 ni mchoro wa mfano wa kitabu cha Matendo.

**Kielelezo 8.3 Mchoro wa Kitabu cha Matendo**

<table>
<tr><th colspan="7">Kitabu cha Matendo</th></tr>
<tr><td>Kisa:</td><td colspan="6">"Mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalemu, na Yudea yote na Samaria, na miisho ya dunia" (Mdo 1:8)</td></tr>
<tr><td>Sura:</td><td>1-7</td><td>8-12</td><td colspan="4">13-28</td></tr>
<tr><td>Sehemu:</td><td>Yerusalemu</td><td>Yudea & Samaria</td><td colspan="4">Miisho ya dunia</td></tr>
<tr><td>Huduma kwa:</td><td>Wayahudi</td><td>Wayahudi & Mataifa</td><td colspan="4">Mataifa</td></tr>
<tr><td>Watu Muhimu:</td><td>Petro<br>Yohana<br>Stefano</td><td>Petro<br>Filipo<br>Saul/Paulo<br>Barnabas</td><td colspan="4">Paulo<br>Barnabas<br>Sila</td></tr>
<tr><td>Matukio Muhimu:</td><td>Mpao<br>Pentekosti</td><td>Eunich<br>Korneli</td><td>(13-14) 1st Safari ya Kimishenari</td><td>(15-18) 2nd Safari ya kimishenari</td><td>(19-20) 3rd Safari ya Kimishenari</td><td>(21-28) Paul Kwenda Urumi</td></tr>
<tr><td>Kanuni:</td><td>Kukua</td><td>Mateso</td><td colspan="4">Misheni</td></tr>
</table>

5. *Tumia Kisa cha Kitabu Kwenye Hali Yako*

Katika kiwango hiki, unatakiwa kuwa na kuelewa kuzuri kwa nini Biblia inasema kutoka kwenye uchunguzi wako. Unatakiwa pia uwe umechunguza kisa na maendeleo yake—ina maana kwamba nini kitabu kinamaanisha. Hatua ya mwisho ni kufikiri juu ya nini unatakiwa kufanya. Kama ilivyokuwa kwenye somo lililopita, hii inahusu kuchunguza maisha yako mwenyewe na hali kuona ni ulinganifu gani uliopo kati yake na mandhali ya kwanza ya kitabu. Swali unaloweza kutaka kujiuliza mwenyewe kusaidia utaratibu huu ni pamoja na:

- Ni kitu gani katika maisha yangu kinafanana na hali iliyo katika kitabu?
- Ni kitu gani katika maisha yangu kinafanana na mwandishi wa kitambu?
- Ni kwa jinsi gani ningekuwa nimechukulia hali hii?
- Ni nini hasa kimesema kwenye moyo wangu hasa niliposoma kitabu?

## IV. MAFUNZA KISA

Mara nyingi, tunataka kujifunza kichwa cha somo maalumu. Aina hii ya mafunzo inasemekana kama kujifunza‘kisa’. Sheria ya kawaida ya kujifunza kwa kufata neno inatumika.

### A. kwa Nini Kujifunza Kisa

Vichwa vingi au ukweli unaanzishwa katika sura zote za Biblia. Vipindi vingi katika Agano zote. Mafunzo ya kitabu yataonyesha sehemu tu ya visa hivi. Kwa mfano, mafundisho juu ya maombi yako kila mahali kwenye maandiko. Njia pekee ya kujifunza kwa ukamilifu ni kufanya mafunzo ya visa.

### B. Jinsi ya Kufanya Mafunzo ya Kisa

Mara unapokuwa umeamua ni kisa gani utajifunza, utataka kufanya kazi katika hatua zote hizi:

- *Tafuta mistari inayoendana*—nukuru na mtajo wa kitabu katika ukurasa kwenye ukingo wa Biblia yako inaweza kukusaidia kutafuta mistari inayohusiana na kisa chako. Tafuta mstari unaofahamu kuwa unahusiana, na kisha anza kufata kiungo kutoka mstari mpaka mstari. Kwa jinsi hiyo,. Njia kamili zaidi inatumika kutumia kamusi kuangalia mistari yote ambayo inajadili kichwa chako. Uwe mwangalifu, ingawa—mistari ambayo ina neno sawa haimanishi kwamba inahusiana na kisa chako.
- Ipange mistari katika mfuatano—Kisa ulichochagua kinaweza kuendelezwa hatimaye kupitia Biblia. Soma mistari ambayo iliandikwa zamani kabla ya mistari ya hivi karibuni. Kwa njia hiyo utagundua ukweli kwa njia sawa na ile ambayo Mungu mwanzoni aliidhirisha.
- Jifunze na fupisha kila mstari katika mandhali—epuka kuwa na hatia kwa kuondoa mstari katika mandhali yake na kujaribu kuufanya kusema kile unachotaka useme. Muruhusu Roho Mtakatifu kuzungumza kupitia huo. Chunguza na fafanua kila mstari kwa uangalifu. Fupisha inachofundisha juu ya kisa.
- Weka kwa kifupi mafundisho ya kisa—baada ya kuwa umejifunza mistari ya pekee na kujua inasemaje na inamaanisha nini, Weka kwa kifupi mafundisho yake katika maelezo wazi ambayo ni pamoja na mchango wa kila mstari. Utaratibu huu una umuhimu sawa na njia za kujifunza historia ya maisha ya mtu zilizoonyeshwa katika kielelezo 8.2. Tofauti kubwa ni kwamba kila fungu linahusu kisa badala ya mtu.
- Tumia ukweli—kwa maombi na kwa kufikiri muombe Mungu kukuonyesha jinsi ukweli huu unavyotakiwa kubadili maisha yako na huduma. “umeangalia kwenye kioo”—sasa nenda nje fanya kile ulichojifunza (Yak 1:22-25).

Mfano wa kujifunza kisa na mistari yake ya ufunguo imeorodheshwa katika njia za kujifunza Biblia Ziada 10A: “Vifungu vya Kujifunza Biblia kwa Kufata Neno.”

## UFUPISHO

Njia ya kujifunza Biblia kwa kufata neno inasaidia katika mafunzo ya aina mbalimbali ya kujifunza Biblia. Ina nguvu sana kwa sababu inatukumbusha katika kila hatua kuruhusu maandiko kuzungumza kwetu, badala ya kulazimisha kuelewa kwetu juu yake. Hata wakati tunajifunza kitabu au vifungu vingi (kama katika kisa au kujifunza historia ya maisha) tunahitaji kuwa waangalifu kujifunza kila mstari katika mandhali yake ili kwamba iweze kuzungumza wazi kwetu.

## MASWALI YA KUTAFAKARI, MARUDIO NA MATUMIZI

- Ni nini kipo kwenye faida za kufanya mafunzo ya historia ya maisha?
- Ni nini tofauti kati ya ‘mpangilio’ na ‘yaliyomo’ kwenye kitabu cha Biblia?
- Kwa nini ni muhimu kuchanganua mistari kwa ajili ya historia ya maisha au mafunzo ya kisa katika utaratibu wa mfuatano?

## UTEKELEZAJI WA AZIMIO

- Fanyia kazi mafunzo ya historia ya maisha kwenye maisha ya Barnabas katika Ziada 8A. Fikiria kwenye nafasi yake katika utaratibu wa upandaji kanisa katika Matendo. Ni matumizi yapi unayoona kwa ajili ya maisha yako mwenyewe na huduma?
- Chukua mda kutumia njia ya kujifunza kwa kufata neno na kwa kujifunza kisa. Chukua kitabu kidogo au kisa kinachowezekana kwa ajili ya jaribio lako la kwanza. Tathimini ufanisi wa njia hii katika kukusaidia kugundua vitu ambavyo hujawahi kuviona katika neno.

KUJIFUNZA BIBLIA
*ZIADA*

8A

# Kujifunza Juu ya Maisha ya Barnabas

Tumia njia ya kujifunza Biblia kwa kufata neno unapofanyia kazi mafunzo ya historia ya maisha ya Barnabas. Unapokuwa na maswali juu ya utaratibu, rejea nyuma kwenye wazo namba 11. "Mafunzo ya Historia ya Maisha" ya njia za kujifunza Biblia somo la 8: "Njia Tofauti za Kutumia Kufanya Mafunzo ya Biblia kwa Kufata Neno."

## I. KUJIFUNZA VIFUNGU VINAVYOENDANA

Mistari ambapo Barnabas ametajwa kwa jina imeorodheshwa kwa ajili yako. Soma kila mstari au kifungu katika orodha ifuatayo, na andika uchunguzi wako. Kisha weka fungu kwa kifupi. La kwanza limefanywa kwa ajili yako.

### A. Matendo 4:36,37

1. *Uchunguzi:*
   - Alikuwa mlawi
   - Alitoka Kipro
   - Jina lake alilopewa ni Yusufu
   - Mitume walimpatia jina la "Barnabas"
   - Mwana wa kutia moyo
   - Aliuza ardhi yake kusaidia kufadhili kazi ya kanisa
   - Alitoa zawadi yake kwa utii ("chini ya miguu ya mitume")
2. *Ufafanuzi/Ufupisho:*

   Barnaba alikuwa 'mtia moyo' kwa asili yake—hata kwa kiasi cha kutoa mali yake kutia moyo na kuwezesha waumini wengine.

### B. Matendo 11:19-24

1. *Uchunguzi*

2. *Ufafanuzii/ufupisho*

**C. Matendo 11:25-26**

*1. Uchunguzi*

*2. Ufafanuzi/Ufupisho*

**D. Matendo 11:27-30**

*1. Uchunguzi*

*2. Ufafanuzi/Ufupisho*

**E. Matendo 12:25**

*1. Uchunguzi*

*2. Ufafanuzii/Ufupisho*

**F. Matendo 13:1-13; 42-43**

*1. Uchunguzi*

*2. Ufafanuzi/Ufupisho*

**G. Matendo**

*1. Uchunguzi*

*2. Ufafanuzi/Ufupisho*

**H. Matendo 15:2-4, 12, 22, 25, 35-39**

*1. Uchunguzi*

*2. Ufafanuzii/Ufupisho*

**I. Wakolosai 4:10**

1. *Uchunguzi*

2. *Ufafanuzi/Ufupisho*

**J. Wagalatia 2:11-13**

1. *Uchunguzi*

2. *Ufafanuzi/Ufupisho*

## II. FUPISHA MAFUNDISHO

Sasa umeshaangalia katika vifungu vya pekee, ni muda wa kuangalia katika matokeo na kuweka kwa kifupi kile Biblia inachofundisha juu ya Barnabas. Unapofanya hivyo, tafakari maswali haya:

- Barnabas alikuwaje nyuma?
- Kwa nini unafikiri kwamba mitume walimpatia Yusufu jina la utani la"Barnabas?"
- Ni uthibitisho gani unauona kutoka katika vifungu hivi kwamba Barnabas alikuwa mfariji?
- Ni nini maana ya agizo ambalo Paulo na Barnabas (au Barnabas na Paulo) wametaja?
- Ni jinsi gani Barnabas alipokea badilikoa la uongozi kwa Paulo?
- Ni jinsi gani alifanya wakati wa migogoro? (Mdo 15:1-4 na Mdo 15:36-40)
- Kwa nini unafikiri kuwa aliitikia kama alivyofanya katika Wagalatia 2:11-13?

Sasa andika maelezo kufupisha ulichojifunza juu ya maisha ya Barnabas. Hakikisha yanakuwa na aina zote za mawazo uliyoyaona katika kila kifungu:

## III. AMUA NINI CHA KUFANYA JUU YAKE

Kujifunza maandiko kuna thamani kidogo mpaka tunapoamua jinsi gani tunahitaji kuyatumia katika maisha yetu. Fikiri katika mafundisho ya maisha ya Barnabas unapoangalia maswali yafuatayo:

- Umewahi kuwa na “akina Barinabas” katika maisha yako? Walikuwa akina nani na jinsi gani walivyokutia moyo?
- Unamfahamu mkristo yeyote anayehitaji kutiwa moyo? Ufanye nini ili kumtia moyo?
- Katika Mdo 9:26ff na 11:26-26, Barnabas alihatarisha sifa yake njema kwa kuwatia moyo wengine. Uko tayari kufanya sawa naye kwa ajili ya injili?
- Barnabas alihamia pembeni na kumuruhusu Paulo kujitwalia nafasi ya kwanza katika uongozi. Uko tayari kuwafundisha viongozi wapya na kuwaruhusu kujitwalia uongozi hata kama ni lazima uchukue nafasi ya juu?
- Ni somo gani hasa Bwana amekuwa akikufundisha ulipojifunza maisha ya Barnabas?

Kwa maombi fikiri jinsi gani Mungu angekufanya uishi tofauti kwa matokeo ya mafundisho haya. Katika nafasi chini, andika unachokusudia kufanya juu yake, na kisha muulize Mungu kukusaidia kwa uaminifu ukamilishe hilo.

NJIA ZA KUJIFUNZA BIBLIA

SOMO LA 9

# Kuongoza Mafunza ya Biblia Kwa Kufata Neno

## KUWAONGOZA WENGINE KWENYE UGUNDUZI

☞ **Kusudi la Somo**

Kusudi la somo hili ni kuelezea jinsi ya kuongoza kikundi cha kujifunza Biblia kwa kufata neno katika namna kwamba wajumbe wanaweza kugundua maana na matumizi ya maandiko wanayojifunza.

☞ **Wazo Kuu**

- Ugunduzi una nguvu zaidi kuliko "kuambiwa."
- Swali zuri linawezesha ugunduzi.

☞ **Matokeo Yanayotarajiwa**

Wakati yaliyomo katika somo hili yanapoeleweka, kila mshiriki anatakiwa:

- Kujua tofauti kati ya "kufundisha" na "kuongoza katika ugunduzi."
- Kuweza kutunga swali linalofaa ambalo linapelekea kwenye ugunduzi.

☞ **Ziada**

9A Mafunzo ya Biblia kwa kufata neno katika Mathayo 20:17-28

9B Mafunzo ya Biblia kwa kufata neno katika Luka 15:1-7

☞ **Ushauri kwa Wakufunzi**

Somo la 10, 11 litakuwa la warsha ya masaa -2 kuwapa wafunzwa mazoezi ya kuongoza mafunzo ya Biblia kwa kufata neno. Wafunzwa wanatakiwa angalau kuwa na jioni moja ya kufikiri juu ya jinsi ya kutumia ujuzi wa majadiliano yaliyotolewa katika somo hili kabla ya warsha.

### I. TABIA ZA KUNDI LA KUJIFUNZA BIBLIA KWA KUFATA NENO

Kujifunza Biblia kwa kufata neno ni ya kwanza na ya mwanzo kuliko njia zote kwa ukuaji wa binafsi wa mkristo. Kwa jinsi hiyo, pia ni mfumo wenye ufanisi sana wa huduma kwa wengine. Unaweza kutumika kwa uinjilisti, au kwa kufuasa. Hii kawaida inatokea katika mandhali ya kikundi.

> Kikundi cha kujifunza Biblia kwa kufata neno ni kikundi kidogo cha watu wanaokutana kwa kusudi la kujifunza Biblia.

Kikundi cha kujifunza Biblia kwa kufata neno ni kikundi kidogo cha watu wanaokutana kwa kusudi la kujifunza Biblia. Wajumbe wanaweza kuwa waumini au siyo waumini—ingawa, hata hivyo kiongozi anatakiwa awe muumini. Njia ya kujifunza Biblia kwa kufata neno ni njia nzuri kwa wasioamini kugundua ujumbe Mungu alionao kwa ajili yao—hii ni, kutubu na kumtumaini Kristo kwa ajili ya wokovu. Kama wajumbe siyo waumini, kiongozi atataka kuchagua kipande cha maandishi kwa mafunzo yanayoelezea injili waziwazi. Kama wajumbe ni waumini, kichwa cha habari kinaweza kuwa chochote ambacho wanakifurahia.

Kuna idadi ya tofauti kati ya kujifunza Biblia kwa kufata neno katika kikundi na mahubiri. Matatu muuhimu zaidi kati ya tofauti hizi yameorodheshwa hapo chini.

#### A. Maandiko ni Mamlaka

Katika mahubiri, chanzo cha mamlaka mara nyingi sana kinachukuliwa kama kuegemea ya mwalimu. Matokeo yake, kama msemaji ana uwezo, watu wanasikiliza anachosema, na wanaweza au wasiweze kutambua kuwa ujumbe unatoka kwa Mungu. Katika hali ya

kinyume, ujumbe wa neno unaweza kusongwa au kupotoshwa na asiye na uwezo wa kuzungumza. Katika hali zote, mtu anasimama kati ya msikilizaji na neno la Bwana.

Kujifunza Biblia kwa kufata neno, kwa kutofautisha, kunamruhusi kila mjumbe wa kikundi kukazia kwenye maandiko. Neno la Mungu hai na lenye nguvu lina uwezo wa kugusa undani zaidi wa mtu, kuleta uthibitisho au faraja. Hakuna kinachosimama kati ya neno na msikilizaji. Hakuna mwanadamu anayejipenyeza. Roho Mtakatifu anautumia ujumbe moja kwa moja kwenye moyo wa msomaji.

> Mafundisho mara zote yanatakiwa yawe na uwiano na mtu binafsi anayejifunza maandiko.

Kiuwazi, kuna mda na sehemu ya mafundisho. Wakati mwingine inasaidia kumsikiliza mwalimu wakati watu wanapokuwa hawako tayari kusoma neno wenyewe, au wakati mwalimu anapokuwa na ufahamu maalumu wa kifungu au somo maalumu. Kwa jinsi hiyo, mafindisho lazima yawianishwe mahali popote na wakati wowote inapowezekekana kwa kujifunza kwa mtu maandiko. Mafundisho yanatakiwa yaongeze kwenye kile tunachojifunza wenyewe—hayatakiwa kuwa *badala yake.*

### B. Lengo ni Uvumbuzi

Maelezo ya kielimu kwa nguvu na kwa kurudia yamehakikisha kwamba tunajifunza na kukumbuka zaidi kitu fulani tunapokigundua wenyewe. Kuwa na mtu anayetuambia kuwa uvuaji wa samaki unakuwaje ni tofauti mbali sana na kwenda wenyewe na kupata kujua uvuaji unavyokuwa. Ina ukweli sawa na katika ukweli wa neno. Tunapogundua ukweli katika kifungu cha Biblia, tunakaribia kuuelewa, kuuamini, na kuutendea kuliko mtu anapotuhubiri huo. Ili kuwezesha ugunduzi huu, kikundi cha kujifunza Biblia kwa kufata neno kinatakiwa kiwe kidogo vya kutosha kuwezesha urahisi wa kuchangia miongoni mwa wajumbe. Chini ya watu 10 wanaweza kutosha, ingawa baadhi ya viongozi wa kikundi wanweza kuvutia uchangiaji hata katika kundi kubwa.

### C. Kiongozi ni Mwezeshaji

> Njia nzuri zaidi ya kujifunza ukweli wa kiroho ni kuugundua wenyewe.

Kwa kuwa njia nzuri zaidi ya kujifunza ukweli wa kiroho ni kugundua wenyewe, kiongozi wa kujifunza Biblia kwa kufata neno lazima awasaidie wajumbe kugundua ukweli kwenye kifungu—na siyo kuwaambia. Hii inakamilishwa kwa kutumia maswali ya kiujuzi. Maswali ni njia ya kuelekeza usikivu wa mjumbe kwenye kweli muhimu katika kifungu, bila kuwaambia hasa. Inawaongoza, lakini inawaruhusu kugundua. Hili ndilo lengo.

Inatakiwa iwe dhahiri, kwa hiyo, swali unalochagua kuuliza kikundi ni muhimu sana. Hakutakuwa na mda wa kutosha wakati wa kipindi cha mafunzo ya kikundi kuuliza maswali yote waliyonayo wana kikundi. Badala yake, majukumu ya kiongozi wa kikundi ni kujifunza kifungu kabla ya mda, na kutambua ni swali lipi lilikuwa la msaada kwake. Hii ni pamoja na maeneo yote—uchunguzi, ufafanuzi, na matumizi. Idadi ya maswali yanayohitajika inategemeana na urefu wa kipindi cha mafunzo, lakini hutahitaji zaidi kwa kuwa utahitaji kuruhusu mda wa kutosha kujadili majibu. Pia, unatakiwa kabisa kuruhusu wajumbe wa kikundi kuuliza na kujibu maswali yao—hasa wanapopata uzoefu katikati ya utaratibu.

## II. MAANDALIZI YA MAFUNZO

Kabla ya mafunzo, kiongozi wa kikundi anatakiwa aandae mafunzo kwa uangalifu.

### A. Jifunze Fungu Mwenyewe

Ni muhimu kwamba kiongozi anagundua ukweli wa kati na matumizi ya fungu. Kiongozi anatakiwa kuchunguza, kufafanua, na kutumia fungu peke yake kulingana na maelekezo ya kujifunza Biblia kwa kufata neno yaliyotolewa katika Mwongozo wa kwanza.


### B. Andika Kusudi la Mfunzo

Kiongozi anatakiwa kuamua mwelekeo kwa ujumla ambao kikundi kidogo cha kujifunza Biblia kitachukua. Mwelekeo huu unatakiwa usiwe maalumu sana. Kumbuka kwamba Roho Mtakatifu anaweza kufundisha kikundi katika njia ambazo hukutarajia.

### C. Tayarisha Maswali Juu ya Fungu Kwa Ajili ya Kikundi Ambayo Yanagusia Sehemu Zote Tatu za Mafunzo

Kiongozi anatakiwa ajiandae kuongoza kikundi **kutumia ufafanuzi** sahihi kutokana na **uchunguzi** wa uangalifu kwa kukiongoza kikundi kupitia utatratibu sawa wa ugunduzi ambao ameshauchukua. Maswali ya—mawazo ya kuchochea yanatakiwa yajengwe juu ya moja kwa jingine ili kwamba majadiliano yakutanike kwenye kusudi kuu na matumizi ya kifugu. Swali linatakiwa lisiwe linalohitaji majibu rahisi ya "ndiyo au hapana." Badala yake, yanatakiwa yaongoze kikundi kutafuta mstari kwa ajili ya kupata uhakika, maana, na matumizi. Kama inachukua dakika chache na majaribio kadhaa kujibu swali kikamilifu, hiyo ni sawa. Swali linatakiwa liwasaidie wajumbe kugundua—siyo kutukana utambuzi wao.

**Kielelezo 9.1**




Mwongozo uliopita umekuonyesha jinsi ya kuandaa aina hii ya maswali, na kukuuliza kuandaa mfano wa kujifunza. Katika mafunzo yote ya mbeleni ambayo unaongoza, unatakiwa kuyafanya katika utaratibu sawa. Unapojiandaa, utafikiria sana maswali ya mbali ya kutumia katika kikundi. Baada ya kumaliza mafunzo ya kifungu kwa ajili yako, utahitaji kuchambua katika maswali yako kufahamu ni lipi swali la msaada au lenye habari za kutosha, na kutumia hayo tu katika kuwaongoza wengine katika somo la kujifunza.

Hakikisha unaweka maswali kadhaa kwa kila hatua—ya uchunguzi, ufafanuzi, na matumizi. Kumbuka mfano wa kujenga piramidi kwa msingi imara. Inapendekezwa kuwa na maswali zaidi ya uchunguzi kuliko ya ufafanuzi. Hii haimanishi kwamba kufafanua kuna maana kidogo—ni kitu muhimu zaidi. Kwa jinsi hiyo, itahitaji maswali kadhaa kuwaongoza wajumbe wa mafunzo ya kikundi kwenye hatua ya kugundua tumizi moja ambalo linahitajika katika maisha yao. Kuwaongoza watu kwenye ugunduzi kwa maswali ya kiujuzi ni vigumu, lakini ina malipo.

### D. Fanya Marudio ya Maswali

Wakati maswali yanapokuwa yameandaliwa, kiongozi anatakiwa kuuliza:

- Maswali yangu ni wazi?
- Kila moja limefupishwa vya kutosha kuwa limeshaeleweka?
- Je maswali yanakifanya kikundi kulitafiti fungu?
- Je maswali ya uchunguzi yanatoa msingi imara ambao juu yake yanaulizwa maswali ya kiufafanuzi na matumizi?
- Je maswali yanakihamisha kikundi kutoka kwenye fungu zima?
- Je maswali ya matumizi yanakiongoza kikundi kwenye utendaji maalumu?

### E. Tayarisha Swali la Kiutangulizi Kuwatia Wajumbe Hamasa Juu ya Mafunzo ya Biblia

Swali la kiutangulizi linaweza kukazia juu ya jinsi fungu hili linavyoongea juu ya hali maalumu ambayo wajumbe wanaifahamu. Kwa mfano, 1Petro ilikuwa imeandikiwa kanisa lililokuwa linateswa. Kujifunza kitabu hiki, unaweza kuuliza: Unafanyaje unapokuwa unateswa kwa ajili ya kuwa mkristo? Jinsi gani watu aliokuwa anawaandikiwa Petro walivyoitikia kwenye mateso?

## III. KUONGOZA MAFUNZO

### A. Mfunzo Yanatakiwa Kuanza Kwa Maombi na Kumalizika kwa Maombi

Kujifunza Biblia siyo kitu kama utaratibu wa kiufundi. Inahitaji usaidizi wa Roho Mtakatifu kufungua macho yetu kwenye ukweli ambao Mungu anataka kuwasilisha kwetu. Tunatakiwa kuomba kwa ajili ya uelevu kabla ya kujifunza, na kisha kumuuliza Bwana kutusaidia kutumia tuliyojifunza baada ya masomo.

**B. Kiongozi Anatakiwa Kujiandaa Kujifunza Kutoka Kwenye Kikundi**

Kuwepo kwa ‘mjuaji’ kunaweza kuua majadiliano ya uaminifu.

Kumbuka kwamba Roho Mtakatifu yuleyule anayesema na kiongozi ndiye anayesema na watu wengine. Wengine wanaweza kuwa na ufahamu ambao kiongozi anaukosa. Kama kiongozi hakujiandaa kujifunza, kisha ataonekana kuwa ‘mjuaji.’ Kuwepo kwa ‘mjuaji’ kunaweza kuua majadiliano ya uaminifu. Mara nyingi, watu hawatapenda kushirikisha maoni yao mbele ya mjuzi ambaye anaweza kuwasahihisha.

**C. Kiongozi Anatakiwa Asijibu Maswali Yake Mwenyewe Au Maswali Yanayoweza Kutokea Kwenye Kikundi**

Kiongozi anatakiwa kuepuka kujibu maswali yake mwenyewe. Itapunguza kufikiri kwa kikundi. Kama kiongozi anajibu maswali yake mwenyewe, maswali yanaanza kuwa kama maswali ya mtihani yenye majibu sahihi. Watu wengi hawatapenda kujibu maswali kwamba wanaweza “kukosa.” Kunapokuwa na kusita kwingi baada ya swali fulani, kiongozi anatakiwa kuwa tayari kurirudia swali kama kuna hali ya kikundi kutoelewa. Kadhalika, swali linalotoka katika kikundi linatakiwa lilinganishwe na nyuma kwa ajili ya kutafakariwa na kikundi. Kwa mfano, “Sasha ana swali juu ya ______. Unafikiri nini juu yake?” Au, Unaweza kulielekeza swali la Shasha kwa mtu mmoja kwenye kikundi: “Tanya, unawezaje kujibu swali la Shasha?”

**D. Usiogopeshwe na Ukimya**

Kiongozi anatakiwa aruhusu mda wa kutosha kujibu maswali. Kunaweza kukawa na wakati kidogo wa ukimya—ambao hakika ni sawa. Watu wanahitaji kufikiri. Ukimya ni msukumo unaofanya kazi badala ya kiongozi.

**E. Kiongozi Mara Zote Hatakiwi Kuridhika Na Jibu la Kwanza Lililotolewa**

Kama kiongozi anakubaliana na jibu mara kwa mara na kuhamia swali linalofata, kisha kikundi kinaweza kuangukia kwenye namna ya swali/jibu, swali/jibu. Ingekuwa vizuri kwa kikundi kuwa na majadiliano, siyo chemsha bongo. Kwa kubembeleza majibu kadhaa kwenye swali, kunaonekana kuwa na majadiliano ya kawaida. Vilevile, jibu la kwanza lililotolewa mara nyingi siyo kamili zaidi au lenye ufahamu. Wakati mwingine kunaweza kukawa na jibu zaidi ya moja. Kwa kuchukua mda kujadili majibu mengine, ndivyo kuelewa zaidi kwa kifungu kunavyopatikana.

**F. Swali Ambalo Halikujibiwa na Kikundi Linaweza Kuachwa Bila Kujibiwa**

Kiongozi anatakiwa ajiepushe na kujibu maswali ambayo kikundi hakikuweza kuyafanyia kazi. Kufanya hivyo kunaweza kuwa kukatiza mtu pekee au kikundi kufikiri na kutoa jibu. Pia, Kama tunamtumaini kiongozi kuwa mwalimu hasa, kisha tunatakiwa kutumaini kuwa swali ambalo halikujibiwa ni kitu ambacho kikundi hakiko tayari kuliweza kwa mda huo. Swali ambalo halijajibiwa linaweza kushika udadisi wao na kulileta wiki ijayo.

**G. Jibu Lisilo Sahihi au Lisilotoshereza Linatakiwa Lisahihishwe kwa Maandiko na/au Kikundi, Siyo Kiongozi**

Kutakuwa na majibu yasiyo sahihi na maelezo. Hali ya kawaida ni kwa kiongozi kusahihisha na kukemea. Lakini kufanya hivyo kunaweza kukatisha tamaa wajumbe na kutokuwa wazi. Hii baadaye itaua majadiliano ya uaminifu. Badala ya kusahihisha jibu lisilo sahihi au lisilotoshereza, kiongozi anaweza kufanya moja ya haya:

- Kumuomba mtu anayejibu kurudia kusoma maandishi, au kuyarejeza kwenye maneno mengine.
- Kuuliza kikundi kama kinakubaliana na jibu au la.
- Kuwauliza wajumbe wa kikundi mstari mwingine wa maandiko unaoendana kusaidia au kusahihisha jibu.

**H. Tunza Majadiliano Kuwa Kwenye Kisa Kikuu cha Fungu**

Shetani ni bwana wa kuwafanya watu kuhamisha mawazo yao kutoka kwenye ukweli. Majadiliano ya Yesu na mwanamke msamaria (Yohana 4) ni mfano mzuri wa jaribio la kumhamisha Kristo kutoka kuzungumzia hitaji hasa la mwanamke. Inawezekana swali kama hilo zuri, hata la maana zaidi, kutokea kutoka kwenye majadiliano. Kama hayahusiani na kisa

kikuu, kisha kiongozi anatakiwa kusema kama ifuatavyo: “Sasha, hili ni swali linalofurahisha. Lakini kwa kuwa haliendani na kisa cha jioni ya leo, tutalitunza mpaka baada ya mafunzo kulijibu.” Au, “Sasha, swali lako ni muhimu sana, lenyewe tu linahitaji somo zima. Tutaandaa mafunzo juu yake baadaye. Jioni ya leo tunahitaji kukazia juu ya kisa chetu cha fungu hili.”

**I. Usisahau Kuuliza Maswali ya Matumizi**

Lengo la mfunzo siyo tu kupata ufahamu juu ya neno la Mungu, lakini kugundua jinsi ya kulitii neno la Mungu kwa matumizi. Kiongozi anatakiwa asiogope kutumia maswali ya hekima yaliyo ya moja kwa moja yanayowaweka tayari watu kwenye utendaji. Wana kikundi hawatapenda kuwa kama mtu katika Yakobo 1:22-24 ambaye hakufanya kulingana na alivyojifunza. Kiongozi anatakiwa kusaidia kila mmoja kuwa maalumu iwezekanavyo katika matumizi ili aweze kuangalia nyuma baada ya wiki na kuona maendeleo aliyofanya katika matumizi ya maandiko katika maisha yake.

**J. Dhibiti Michango ya Hao Wanaoongea Sana au Kidogo**

Vikundi vidogo vingi vinakuwa na jozi ya watu wenye shauku ya kutaka kujibu kila swali, na walio wengi watakaojibu mara chache, na jozi ya watu wanaohitaji kutiwa moyo kushiriki. Kwa hao ambao mara nyingi wanajibu, kiongozi anahitaji kusema kitu kama hiki: “Sasha, tunaweza mara zote kukutegemea kujibu. Ngoja tusikilize kile Tanya anachofikiria juu ya ______.” Kwa hao ambao wanashiriki mara chache, kiongozi anaweza kuwaomba kusoma maandishi au kujibu swali la uchunguzi na kwa urahisi wa kuona jibu katika maandishi. Ujasiri unapojengwa, wanaweza kushauriwa kushiriki katika ufafanuzii rahisi na maswali ya matumizi.

**K. Mwishoni Mwa Mafunzo, Kiongozi Anaweza Kufupisha Kile Ambacho Kikundi Wamejifunza na Kuonyeshwa**

Kiongozi anatakiwa kuepuka kuongeza habari mpya ambazo kikundi hakikudhania. Kuongeza habari mpya hakumuweki tu kiongozi kama “mjuaji,” Kunaonyesha pia kukosekana kwa uaminfu katika kumruhusu Roho Mtakatifu kudhihirisha alichotaka kikundi kigundue. Ni vizuri kuthibitisha walichojifunza kikundi na kuendelea.

## MASWALI YA KUTAFAKARI, MARUDIO NA MATUMIZI

- Kwa nini ugunduzi ni muhimu katika kukua kwa mkristo? Kwa nini mahubiri peke yake hayatoshi?
- Ni nini kitakuwemo kwenye maswali ya majadiliano?

## UTEKELEZAJI WA AZIMIO

- Katika Mwongozo uliopita, ulielekezwa kuandaa mafundisho mafupi ya kueleweka ya kujifunza Biblia kwa kufata neno katoka moja ya vifungu vifuatavyo:

Matendo 13:4-12 (Pafo)
Matendo 13:13-5 (Antiokia)
Matendo 14:1-7 (Ikonio)
Matendo 14:8-20 (Lstra na Derbe)
Matendo 16:11-40 (Ufilipi)
Matendo 17:10-15 (Beroya)
Matendo 17:16-34 (Athene)
Matendo 17:16:34 (Athene)
Matendo 18:1-17 (Korintho)

- Katika maandalizi ya somo linalofata, unatakiwa kuwa na mafunzo hayo yaliyomalizika, ikiwemo uchunguzi wako, ufafanuzi, na maswali ya matumizi. Katika somo lijalo (10, 11), utaongoza baadhi ya wafunzwa wengine katika mafunzo kwa kutumia kanuni katika somo hili. Chukua mda kufanya marudio ya mafunzo hayo, na yatafakari jinsi utakavyoongoza majadiliano.
- Kama, kwa baadhi ya sababu, huna mafunzo yaliyoandaliwa, unaweza kutumia mojawapo ya mfano wa mafunzo katika Ziada 9A au 9B, lakini inashauriwa hasa kwamba utumie yako. Kuongoza mafunzo yako mwenyewe kutakusaidia zaidi kutathimini uandaaji wa maswali yako na ustadi wako katika kutumia njia ya kujifunza Biblia kwa kufata neno.

MAFUNZO YA BIBLIA *ZIADA*

9A

# Mafunzo ya Biblia Kwa Kufata Neno Mathayo 20:17-28

*Tambua: Mafunzo haya yametolewa kama mtindo wa mafunzo ya Biblia kwa kufata neno. Ni muhimu kabisa, kama ni lazima kabisa , yanaweza kutumika kwa Warsha katika Somo la 10, 11. Kwa jinsi hiyo, inashauriwa sana kwamba hii inatumika tu kama mwongozo, na kwamba unafanya mafunzo yako mwenyewe katika moja ya kifungu kilichoagizwa katika Mwongozo wa kwanza.*

**UTANGULIZI**

Somo la uongozi katika kozi hii ya upandaji kanisa litakuwa linaangalia katika huduma ya Yesu kama kielelezo kwa uongozi. Kuna aina nyingi za 'uongozi' ulimwenguni, lakini Yesu alitoa tofauti kubwa ya kuelewa nini inamanisha kuwaongoza wengine. Kama tunavyoona katika Mathayo 20:17-28, hata wafuasi wake walikuwa na wakati mgumu wa kukabili matokeo ya aina hii mpya ya uongozi wa kikristo. Tunataka kujibu swali la: Nini maana ya uongozi wa kikristo?

**I. KUOMBA**

Anza mafunzo kwa kumwomba Mungu kuondoa vipingamizi vingine kutoka akilini mwako, na kukuruhusu kukazia juu ya kujifunza ukweli wa kifungu ili kwamba uwe kiongozi mkristo mzuri.

**II. SOMA MATHAYO 20:17-28**

Soma fungu kwa uangalifu na kwa kufikiri. Mtu mmoja anaweza kusoma lote, au unaweza kugawanya usomaji miongoni mwa wanakikundi

**III. UCHUNGUZI**

Kazi yetu ya kwanza ni kugundua kile Biblia inachosema. Angalia kwa karibu kwenye kifungu kisha jibu maswali yafuatayo"

*Kutoka kwenye mandhali ya (Mt 19:27-20:16)*

- Ni kwa njia ipi inawezekana mafundisho ya Mathayo na Yohana yamechochea haja ya kutawala katika ufalme?

- Ni nini kiini kikuu cha mfano wa Mathayo 20:1-15, Kama ilivyofupishwa na Yesu katika mstari wa 16?

*Kutoka kwenye kifungu (Mt 20:17-28)*

- Ni wapi Yesu na wanafunzi walipokuwa wanakwenda, na nini kilikuwa kinakwenda kutokea pale?

- Ni upendeleo gani mrs Zebedayo anaomwuliza Yesu?
- Ni jinsi gani wanafunzi wengine walivyofanya kwenye ombi lake, na kwa nini?
- Ni nani anaamua nani anakaa wapi kwenye ufalme, na nini kipimo cha mpangilio huu?
- Ni kwa jinsi gani vipimo, hivi vinatofautiana kutoka kwenye utaratibu wa kidunia (mataifa)?

## IV. UFAFANUZI

Na sasa tuko tayari kuangalia maana ya kifungu hiki. Fikiria kwa uangalifu juu ya maswali yafuatayo unaporejea nyuma kwenye uchunguzi wako:

- Ni kwa jinsi gani unaweza kufupisha nia ya Mrs. Zebedayo na wanafunzi walipokwenda Yerusalemu? Ni nini walitarajia kuwa kingekuwa pale (fikiria juu ya maana ya ("mkono wa kulia na mkono wa kushoto"). Ni nini hii inadokeza juu ya sababu zao za kumfuata Yesu?
- Ni nini Yesu alimaanisha kwa "kikombe?" (Tambua: tuna faida ya matokeo yake! ) Ni nini kilihusisha katika maisha ya Yesu na kwa jinsi gani baadaye kilitimizwa katika maisha ya mitume? Ni aina maalumu ya huduma, matendo, nia, au kitu kingine?
- Ni SAWA kwangu kuwa na haja ya kuheshimiwa katika ufalme wa Mungu? Ilikuwa ni tatizo kwamba wanafunzi walitaka kuheshimiwa , au kwamba walitaka waheshimiwe sasa badala ya wakati Yesu atakaporudi?

Weka kwa kifupi katika sentensi au katika kiini kikuu cha mistari hii. Lielezee katika misingi ya kibiblia kama inawezekana. Liandike katika nafasi hapo chini.

*Kanuni ya kifungu:*

## V. MATUMIZI

Sasa unahitaji kufikiri jinsi kanuni hii inavyoweza kutumika katika maisha yako na huduma yako leo. Fikiria kwa uangalifu juu ya maswali haya:

- Ni nini mvuto wangu wa kumtumikia Kristo kama mpanda kanisa? Ni nini ninachotumaini kupata, na lini?

- Kama haja yangu ni kumpendeza Kristo, ni jinsi gani uongozi wangu utofautiane na huo wa wengine wanaonizunguka? Ni nini hasa ninatakiwa kuwa nafanya ili kuongoza kama mtumishi na kutoa maisha yangu kwa hao Yesu aliowanunua?

## UFUPISHO

Kama ulivyofanya kazi katika kifungu hiki, unatakiwa uwe umejibu maswali, “Ni nini maana ya uongozi wa kikristo?” Umefikiria pia kwamba hiyo ingekuwa na maana gani kwako mwenyewe katika maisha yako na huduma. Na sasa ni wakati wa kuanza kuomba kwa Mungu msaada wa kuishi maisha ya aina hiyo. Hasa kumuuliza kusaidia maeneo hayo ambayo sasa unaona kwamba una udhaifu au nia mbaya.

MAFUNZO YA BIBLIA
*ZIADA*

9B

# Mafunzo ya Biblia Kwa Kufata Neno Luka 15:1-7

*Tambua: Mafunzo haya yametolewa kama mtindo wa mafunzo ya Biblia kwa kufata neno. Ni muhimu kabisa, kama ni lazima kabisa , yanaweza kutumika kwa Warsha katika Somo la 10, 11. Kwa jinsi hiyo, inashauriwa sana kwamba hii inatumika  tu kama mwongozo , na kwamba unafanya mafunzo yako mwenyewe katika moja ya kifungu kilichoagizwa katika kipindi cha kwanza cha mafunzo .*

**UTANGULIZI**

Umewahi kupoteza kitu fulani muhimu? Ni nini ulifanya kujaribu kukitafuta? Kama ulikipata, ulijisikiaje? Katika Luka 15, Yesu alielezea jinsi Yeye na Baba yake wanavyojisikia juu ya watoto wa Mungu “waliopotea.”

**I. MAOMBI**

Anza mafunzo kwa maombi ukimuuliza Mungu akusaidie kuelewa jinsi mistari hiyo inavyoweza kugusa maisha yako, na huduma yako ya upandaji kanisa.

**II. SOMA LUKA 15:1-7**

Soma kifungu kwa uangalifu na kwa kutafakari. Mtu mmoja anaweza kusoma lote, au unaweza kugawanya usomaji miongoni mwa wanakikundi.

**III. UCHUNGUZI**

Angalia kwa ukaribu katika kifungu na jaribu kugundua nini inachosema kwa kujibu maswali yafuatayo”

*Kutoka katika mandhali ya Luka (14:13, 23)?*

- Ni aina gani ya watu ambao Yesu amekuwa akisema tunahitaji tuwaalike waje na kushirikiana nasi na Bwana pia (14:13, 23)?

- Jinsi gani kielelezo cha “chumvi” isiyofaa katika mstari wa 34 kinavyohusu hao ambao wanaowaalika na wasiowaalika waliopotea kuja kwa Mungu?

*Kutoka katika kifungu (Lk 15:1-7)*

- Ni kwa akina nani mfano huu ulikuwa umetolewa—wenye dhambi au mafarisayo wenye dini na walimu wa sheria (v.3)? Unajua nini kuhusu kundi hili?

- Ni nini yalikuwa malalamiko ya mafarisayo na walimu wa sheria dhidi ya Yesu?

- Ni kondoo wangapi waliopotea kulinganisha na kondoo wangapi waliomo zizini?

- Nini walichofanya wachungaji kwa kondoo mmoja aliyekuwa amepotea?

- Nini Yesu anachosema katika wazo kuu la mfano huu (V. 7)?

## IV. UFAFANUZI

Sasa tunahitaji kufikiri juu ya hadithi hii ya kondoo waliopotea ina maana gani. Hii kwa namna fulani ni rahisi kuliko kawaida, Kwa kuwa Yesu alikielezea kisa katika mstari wa 7. Maswali yafuatayo yanaweza kukusaidia kufikiri katika kanuni alizokuwa anafundisha:

- Kumbuka ni kwa nani Yesu alitolea mfano huu. Ni kwa jinsi gani wazo “kufurahia juu ya mmoja anayetubu” linavyohusiana na kisa hasa? Kwa nini unafikiri Yesu alichagua kutumia mfano badala ya kueleza tu ukweli?

- Kwa nini unafikiri kuwa walihitaji kusikia mfano huu? Nini kingekuwa tofauti katika maisha yao?

Weka kwa kifupi katika sentensi au katika wazo kuu la mistari hii. Lielezee katika misingi ya kibiblia kama inawezekana. Liandike katika nafasi hapo chini.

*Kanuni ya kifungu:*

## V. MATUMIZI

Sasa tunahitaji kuamua jinsi ya kutumia mafundisho haya kwenye maisha yetu wenyewe. Fikiria kwa uangalifu kwenye maswali yafuatayo kukusaidia kufanya hayo:

- Unaamini kabisa kwamba mmoja mwenye dhambi aliyepotea anayemwamini Kristo ni muhimu zaidi kuliko kanisa lililojaa, tuseme, waumini 99 wanaoishi kwa haki, maisha ya utakatifu na uaminifu? Kama ni hivyo, nini maana ambayo hii inaweza kuwa nayo katika huduma yetu?

- Jinsi gani ninavyofanya wakati mtu fulani anapojiunga na watu wenye dhambi ili kuwaleta kwa Yesu? Tunaweza kufanya hivyo na kubakia "watakatifu?" Inawezekana kujenga uhusiano wa karibu na wasioamini ili kutoa ushuhuda wetu wa maisha kwao (1Kor 5:9-12)?

- Ninafanya nini wakati mwenye 'dhambi' anapotubu, lakini 'hajasafisha maisha yake' ili kwamba awe mtakatifu kama mimi nilivyo? Ninafurahia naye na kumsaidia kukua, au ninamlaaumu kwa vitu ambavyo bado havijawa sawa katika maisha yake?

## UFUPISHO

Katika historia yote ya ulimwengu, kama ilivyoandikwa katika maandiko, Mungu amekuwa akiwatafuta watu waliopotea kutubu na kumrudia yeye. Kristo aliacha utukufu wa mbinguni na kuwa mtu ili kulipa deni kwa ajili ya ukombozi wetu na kufanya upatanisho wetu kwake kuwezekana. Ametuachia amri ya kutimiza utume mkuu kwa kuchukua ujumbe wa injili kwa kila mmoja. Nini utakuwa mchango wangu? Bwana ananiita kupanda kanisa jipya ambapo waliopotea wanaangamia kwa kukosa injili? Nini ninachotakiwa kufanya?

NJIA ZA KUJIFUNZA BIBLIA

SOMO LA

10,11

# Warsha Juu ya Kuongoza Mafunzo ya Biblia kwa Kufata Neno

☞ **Kusudi la Somo**

Kusudi la somo hili ni kuwapa wafunzwa uzoefu wa “kutenda” uliosimamiwa kwa kuongoza mafunzo ya Biblia kwa kufata neno.

☞ **Wazo Kuu**

- Mkazo unatakiwa uwe kwenye kugundua
- Hatua zote—Uchunguzi, Ufafanuzi, na Matumizi—yanatakiwa yafanyike.

☞ **Matokeo Yanayotarajiwa**

Wakati yaliyoma katika somo hili yanapoeleweka, kila mshiriki anatakiwa:

- Kujua jinsi ya kuongoza mafunzo ya Biblia kwa kufata neno.
- Kujua uwezo wake na udhaifu katika kuongoza mafunzo.

☞ **Ziada**

10A Vifungu vya mafunzo ya Biblia kwa kufata neno

☞ **Ushauri kwa Wakufunzi**

Kipindi hiki cha masaa mawili chote kimetolewa kuwaruhusu wafunzwa kufanya mazoezi ya kuongoza mafunzo ya Biblia kwa kufata neno, na kufanyaina tathimini wanapofanya hivyo. Kazi yako kama mkufunzi ni kupanga makundi, na kisha kuyazungukia kati yao kusikiliza mawakilisho, na kuhakikisha wafunzwa wanafanya kazi ya haki na kamilifu na kufanyia kazi yote yaliyoorodheshwa baada ya kila moja. Watie moyo wafunzwa kuwa waaminifu, lakini wazi.

## MFUMO WA WARSHA

Kila mfunzwa anatakiwa kuwa ameandaa kwa kifupi na wazi mafunzo ya kujifunza Biblia kwa kufata neno kwenye kifungu cha uchaguzi wake mwenyewe. Kikamilifu, mfunzwa anatakiwa achukue karibu dakika 20 kuelezea mafunzo yake, yakifatwa na dakika 7 za kutathimini kwa kutumia orodha iliyotolewa katika somo hili, hii ina maana kwamba kila kikundi kinatakiwa kuwa na watu wanne, ili kwamba kila mmoja aongoze mafunzo yao. Gawanyika katika vikundi vingi vya watu wanne kama inavyohitajia na idadi ya wafunzwa. Linaweza kuwa wazo zuri kuchukua dakika 5 za mapumziko kati ya masaa mawili.

Wakati kila mfunzwa anapoendesha mafunzo yake, anatakiwa akumbuke kwamba huu siyo wakati wa mahubiri. Lengo ni ugunduzi. Mfunzwa anatakiwa aongoze kikundi kwa kuuliza maswali ambayo yanawasaidia wafunzwa wengine kufunua ukweli, maana, na matumizi yao wenyewe. Kwa sababu hii, mfunzwa anayeongoza anatakiwa awe ameshachagua maswali machache ya msaada katika kila moja ya maeneo haya—**uchunguzi, ufafanuzi**, na **matumizi.** Baada ya kila swali kuulizwa, ruhusu mda wa kutafuta jibu, na majadiliano. Tia moyo majadiliano, lakini punguza idadi ya maswali unayouliza ili kwamba uwe na mda wa kwenda mpaka kwenye matumizi.

Hili siyo tu zoezi. Kikundi kinatakiwa kijifunze kutoka kwenye mafunzo.

Kumbuka kuomba kwa ajili ya werevu. Hili linatakiwa lisiwe tu zoezi. Kikundi kinatakiwa kione kifungu waziwazi, na kijifunze kutokana kama mafunzo yameongozwa kiusahihi. Huku ni kujifunza halisi kwa maandiko, na kila mmoja anatakiwa atiwe moyo nako. Tofauti kati ya mafunzo ya Biblia kwa kufata neno ya ‘kawaida’ yana mda mwisho dakika 20 kawaida, mafunzo ya binafsi ya kujifunza Biblia kwa kufata neno yataweza kuchukua masaa, au ikiwezekana siku kadhaa

kumaliza kabisa. Mafunzo ya kikundi kawaida yatahitaji saa, kutegemeana na urefu wa kifungu walichochagua. Dakika ishirini ni kwa kifupi, kwa hiyo hamtaweza kufanya yote mliyojifunza wakati wa maandalizi. Itakuwa kwa hiyo, inakupa wazo zuri la nini kilihusika kwenye mafunzo kama hayo.

Hata mfunzwa aliyeandaa mafunzo anatakiwa apate kuelewa wazi kupitia macho ya wafunzwa wengine. Usikatishwe tamaa kama kikundi kinafikia katika kutokuelewa ambako ni tofauti na kwa kiongozi wa mwanzo. Hii ni kawaida na asili. Hatutaweza kamwe kubwaga neno kikamilifu. Mara zote kuna zaidi ya kujifunza.

**ORODHA YA KULINGANISHA**

Kuna orodha nne ziliwekwa hapo chini, moja kwa kila wafunzwa wanne katika kikundi chako. Usijaze orodha wakati wa mafunzo ya Biblia. Badala yake, husika kikamilifu kwa moyo katika majadiliano ya kikundi. Kisha, baada ya kila mfunzwa kumaliza mafunzo yake, zungushia majibu ya kila swali katika upande wa kulia wa orodha kwa mfunzwa huyo.

Baada ya kumaliza orodha kwa mfunzwa wa kwanza, chukua ukumbusho wa dakika hizo 30 za mkato kushirikisha tathimini yako na mtu huyo kama kikundi wakati zikiwa motomoto akilini mwako. Uwe mwaminifu, lakini pia kumbuka kwamba hili ni jaribio lao la kwanza, na kwa hiyo, uwe mtiaji moyo.

Kuna maeneo makuu mawili ya kuzingatia. La kwanza ni kama mafunzo yalifata au hayakufata hasa njia ya kujifunza kwa kufata neno na kama umejifunza kitu fulani kutokana na mafunzo. Eneo la pili ni vizuri kiasi gani kiongozi wa mafunzo ameweza kuongoza kikundi kwenye ugunduzi kwa kutumia maswali mazuri na majadiliano yenye nguvu yanayofaa. Kama una mapendekezo ya kusaidia ambayo hayakufanyika kwenye maswali kumi na mawili kwenye orodha, ongeza taarifa hiyo kwenye sehemu ya "mapendekezo" chini kwenye orodha.

Hamia kwa mfunzwa wa pili na mafunzo ya Biblia wakati tu kikundi kinapokuwa kimemaliza tathimini ya kwanza. Kwa jinsi hiyo, jaribu kutumia dakika 30 tu ili kwamba na mfunzwa wa nne aweze kupata dakika 30 kamili kwa mafunzo ya mwisho.

**Orodha ya 1: Jina la Mfunzwa________________**

| Maswali ya Kutathimini | Tathimini |
|---|---|
| 1. Mafunzo yamefata njia ya kujifunza kwa kufata neno—uchunguzi, ufafanuzi, na matumizi? | Ndiyo Hapana |
| 2. Maswali yalikuwa wazi na ya kueleweka? | Ndiyo Hapana |
| 3. Maswali yamekusaidia kuelewa fungu zaidi? | Ndiyo Hapana |
| 4. Kiongozi ameruhusu kikundi kujibu maswali, badala ya kujibu mwenyewe? | Ndiyo Hapana |
| 5. Kiongozi amechochea maswali yaliyoulizwa tena kwenye kikundi? | Ndiyo Hapana |
| 6. Kiongozi amerudia kusoma maswali yaliyo magumu kueleweka? | Ndiyo Hapana |
| 7. Kiongozi ameweza kuwasaidia wajumbe wote kuhusika katika majadiliano? | Ndiyo Hapana |
| 8. Kiongozi ameweza kufanya mtu yeyote asitawale majadiliano? | Ndiyo Hapana |
| 9. Kiongozi amefupisha mambo ambayo kikundi kimegundua kwenye mafunzo? | Ndiyo Hapana |
| 10. Kiongozi ameruhusu kikundi na maandiko kusahihisha jibu lolote lisilo sahihi? | Ndiyo Hapana |
| 11. Kiongozi ameweza kukamilisha mafunzo yote katika mda uliotolewa? | Ndiyo Hapana |
| 12. Kiongozi ameanza na kumaliza mafunzo kwa maombi? | Ndiyo Hapana |
| Maoni: | |

**Orodha ya 2: Jina la Mfunzwa___________________**

| Maswali ya Tathimini | Tathimini |
|---|---|
| 1. Mafunzo yamefata njia ya kujifunza kwa kufata neno—uchunguzi, ufafanuzi, na matumizi? | Ndiyo Hapana |
| 2. Maswali yalikuwa wazi na ya kueleweka? | Ndiyo Hapana |
| 3.Maswali yamekusaidia kuelewa fungu zaidi? | Ndiyo Hapana |
| 4. Kiongozi ameruhusu kikundi kujibu maswali, badala ya kujibu mwenyewe? | Ndiyo Hapana |
| 5. Kiongozi amechochea maswali yaliyoulizwa kwenye kikundi? | Ndiyo Hapana |
| 6. Kiongozi amerudia kusoma maswali yaliyo magumu kueleweka? | Ndiyo Hapana |
| 7. Kiongozi ameweza kuwasaidia wajumbe wote kuhusika katika majadiliano? | Ndiyo Hapana |
| 8. Kiongozi ameweza kufanya mtu yeyote asitawale majadiliano? | Ndiyo Hapana |
| 9. Kiongozi amefupisha mambo ambayo kikundi kimegundua kwenye mafunzo? | Ndiyo Hapana |
| 10. Kiongozi ameruhusu kikundi na maandiko kusahihisha jibu lolote lisilo sahihi? | Ndiyo Hapana |
| 11. Kiongozi ameweza kukamilisha mafunzo yote katika mda uliotolewa? | Ndiyo Hapana |
| 12. Kiongozi ameanza na kumaliza mafunzo kwa maombi? | Ndiyo Hapana |
| Maoni: | |

**Orodha ya 3: Jina la Mfunzwa______________________**

| Maswali ya Tathimini | Tathimini |
|---|---|
| 1. Mafunzo yamefata njia ya kujifunza kwa kufata neno—uchunguzi, ufafanuzi, na matumizi? | Ndiyo Hapana |
| 2. Maswali yalikuwa wazi na ya kueleweka? | Ndiyo Hapana |
| 3.Maswali yamekusaidia kuelewa fungu zaidi? | Ndiyo Hapana |
| 4. Kiongozi ameruhusu kikundi kujibu maswali, badala ya kujibu mwenyewe? | Ndiyo Hapana |
| 5. Kiongozi amechoche maswali yaliyoulizwa tene kwenye kikundi? | Ndiyo Hapana |
| 6. Kiongozi amerudia maswali yaliyo magumu kueleweka? | Ndiyo Hapana |
| 7. Kiongozi ameweza kuwasaidia wajumbe wote kuhusika katika majadiliano? | Ndiyo Hapana |
| 8. Kiongozi ameweza kufanya mtu yeyote asitawale majadiliano? | Ndiyo Hapana |
| 9. Kiongozi amefupisha mambo ambayo kikundi kimegundua kwenye mafunzo? | Ndiyo Hapana |
| 10. Kiongozi ameruhusu kikundi na maandiko kusahihisha jibu lolote lisilo sahihi? | Ndiyo Hapana |
| 11. Kiongozi ameweza kukamilisha mafunzo yote katika mda uliotolewa? | Ndiyo Hapana |
| 12. Kiongozi ameanza na kumaliza mafunzo kwa maombi? | Ndiyo Hapana |
| Maoni: | |

**Orodha ya 4: Jina la Mfunzwa____________________**

| Maswali ya Tathimini | Tathimini |
|---|---|
| 1. Mafunzo yamefata njia ya kujifunza kwa kufata neno—uchunguzi, ufafanuzi, na matumizi? | Ndiyo Hapana |
| 2. Maswali yalikuwa wazi na ya kueleweka? | Ndiyo Hapana |
| 3.Maswali yamekusaidia kuelewa fungu zaidi? | Ndiyo Hapana |
| 4. Kiongozi ameruhusu kikundi kujibu maswali, badala ya kujibu mwenyewe? | Ndiyo Hapana |
| 5. Kiongozi amechochea maswali yaliyoulizwa tena kwenye kikundi? | Ndiyo Hapana |
| 6. Kiongozi amerudia maswali yaliyo magumu kueleweka? | Ndiyo Hapana |
| 7. Kiongozi ameweza kuwasaidia wajumbe wote kuhusika katika majadiliano? | Ndiyo Hapana |
| 8. Kiongozi ameweza kufanya mtu yeyote asitawale majadiliano? | Ndiyo Hapana |
| 9. Kiongozi amefupisha mambo ambayo kikundi kimegundua kwenye mafunzo? | Ndiyo Hapana |
| 10. Kiongozi ameruhusu kikundi na maandiko kusahihisha jibu lolote lisilo sahihi? | Ndiyo Hapana |
| 11. Kiongozi ameweza kukamilisha mafunzo yote katika mda uliotolewa? | Ndiyo Hapana |
| 12. Kiongozi ameanza na kumaliza mafunzo kwa maombi? | Ndiyo Hapana |
| Maoni: | |

**UFUPISHO**

Hili limekuwa zoezi la kukusaidia kuonja nguvu ya kujifunza Biblia kwa kufata neno. Huu unatakiwa uwe mwanzo badala ya mwisho. Kujifunza Biblia kwa kufata neno ni njia bora ya kujifunza kutoka kwenye maandiko. Utaratibu unakuruhusu kufikia ngazi mpya ya ukweli na kuelewa, kwa msaada wa Roho Mtakatifu. Hii njia ina thamani kwa:

- Mafunzo ya binafsi
- Kuandaa mahubiri
- Madarasa ya jumapili
- Vikundi vidogo
- Vikundi kiini
- Mafunzo ya uinjilisti kwa wasioamini
- Huduma za katikati ya wiki za kanisa
- Ufuasishaji wa mmoja kwa mwingine
- Na matumizi mengine mengi

**MASWALI YA KUTAFAKARI, MARUDIO NA MATUMIZI**

- Ni jinsi gani mafunzo haya yalikuwa tofauti kuliko mafunzo mengine ya Biblia uliyowahi kuhudhuria nyuma?
- Njia hii imekusaidia binafsi kujifunza? Unafikiri itakuwa yenye ufanisi kwa hao unaowafundisha au kuwaongoza? Kwa nini na kwa nini siyo?

**UTEKELEZAJI WA AZIMIO**

Ni juu yako kuchukua zana ulizonazo sasa, pamoja na tathimini ya wafunzwa wengine wenye uwezo wa kuongoza mafunzo, na kuzitumia kukamilisha yote kukua kwako kiroho na huduma yako.

KUJIFUNZA BIBLIA *ZIADA*

10A

# Vifungu Vya Mafunzo Ya Biblia Kwa Kufata Neno

*Vifungu vifuatavyo vinaweza kuendeleza mafunzo ya Biblia kwa kufata neno juu ya mawazo ya msingi ya maisha ya kikristo na imani. Mfunzwa anaweza kuvitumia kwa muumini mpya, Vikundi kiini, mmoja kwa mwingine, n.k.*

| | | |
|---|---|---|
| **Mamlaka ya Biblia** | **Uinjilisti** | **Msamaha** |
| Uf 1:1-3 | Mk 5:1-20 | Mwa 45:4-15 |
| Lk 24:27-48 | 1Pet 3:15-16 | Zab 103:2-18 |
| Zab 119:94-118 | 2Kor 3:1-3 | Mt 6:12-15 |
| Zab 119:159-168 | Mdo 22:1-21 | Lk 15:11-32 |
| 2Pet 1:19-21 | Mdo 4:1-20 | Efe 4:31-32 |
| 1Pet 1:24-25 | Mdo 18:24-28 | Mk 11:24-26 |
| 2Tim 3:14-17 | Mk 16:9-20 | Mt 18:21-35 |
| **Maombi** | **Utoaji** | **Maisha Mapya ndani ya Kristo** |
| Zab 55 | 2Kor 8:1-5 | 2Kor 5:16-21 |
| Mt 26:36-44 | 2Kor 9:6-11 | Yoh15:5-8 |
| Mt 6:5-13 | Mk 10:17-23 | Gal 3:26-28 |
| Mt 5:44-48 | 1Yoh 3;16-18 | Rum 8:1-11 |
| Yak 5:13-18 | Mk 4:24-25 | Flp 3:7-11 |
| Mk 11:20-26 | Mt 6:1-4 | Rum 6:3-11 |
| Rum 8:26-28 | 1Kor 16:1-2 | Col 3:1-4 |
| **Mafunzo ya Biblia** | **Majaribu** | **Kujilinda Mwenyewe** |
| Kum 17:17-20 | Rum 6:1-14 | Mit 6:6-11 |
| Zab 1 | Lk 4:1-13 | 1Pet 1:13-16 |
| Lk 4:1-13 | Hes 2:17-18 | Yoh 14:21 |
| Lk 4:14-21 | 1Kor 10:13 | Rum 12:1-3 |
| Yos 1:7-9 | Gal 6:1-11 | Col 3:15-17 |
| Mit 2:1-5 | Uf 3:7-11 | Yak 1:19-25 |
| Mit 4:20-22 | Yak 1:12-15 | Lk 6:47-49 |
| **Mpango wa Mungu wa Maisha** | **Toba** | **Ushirika wa Wakristo** |
| Flp 4:6-7 | Lk 5:29-32 | IThe 5:11-15 |
| Mit 3:5-6 | Lk 13:1-92 | Lk 22:24-27 |
| Mit 16 | Pet 3:8-9 | Hes 10:24-25 |
| Omb 2:1-26 | Isa 1:10-20 | Efe 1:15-23 |
| Mt 4:18-23 | 1Yoh 1:8-10 | Rum 12:3-16 |
| Lk 22:39-42 | Mdo 26:20 | Mdo 12:5-19 |
| Yak 4:1-10 | Yoh 3:1-10 | Mdo 2:38-47 |

# UINJILISTI

UINJILISTI

SOMO LA 4

# Uinjilisti na Upandaji Kanisa

## KUKIMBIA MBIO ZOTE

☞ **Kusudi la Somo**

Kusudi la somo hili ni kuonyesha kwamba uinjilisti unatakiwa ufanyike katika namna ya mahusiano ili kuwasaidia waumini wapya kiasilia kuendelea katika uhusiano wa kufuasa.

☞ **Wazo Kuu**

- Uinjilisti ndio mguu wa kwanza wa mbio za kikristo—ufuasishaji ni ya pili
- Mahusiano ya mtandao wa kawaida na "mlinda malango" yanawezesha ufanisi, uinjilisti wa mahusiano.
- Wakristo wapya pengine ndio wainjilisti wenye thamani.

☞ **Matokeo Yanayotarajiwa**

Wakati yaliyomo kwenye somo hili yanapoeleweka, kila mshiriki anatakiwa:

- Kuelewa kwa nini uinjilisti wa uhusiano unawezesha kushiriki kwa waliokata shauri wapya kwenye kanisa.

☞ **Ziada**

4A Kutathimini Mkakati wa Uinjilisti

☞ **Ushauri kwa Wakufunzi**

Ziada 4A Inaweza kutumika kama chombo cha majadiliano wakati wa somo hili.

### UTANGULIZI

Haiwezekani kupanda kanisa bila uinjilisti, lakini uinjilisti peke yake hautoshi. Wapanda kanisa wanahitaji kutumia njia inayofaa ya kiuinjilisti mbayo itapelekea kwenye kuanzishwa kwa makanisa yanayokua—siyo tu wokovu wa mtu mmoja.

Tunapofikiria kiasi kikubwa sana cha vifaa na njia zilizopo kwa uinjilisti na kujaribu kuona ni ipi ya kutumia, lazima tujikumbushe wenyewe lengo letu. Kama wapanda kanisa, lengo letu siyo tu kuwaonyesha watu injili, au tu kwa kifupi kuwasaidia kukata shauri kwa Kristo. Lengo letu ni kufanya wanafunzi watakaokuja pamoja kuabudu na kukua pamoja na watu wa Mungu.

### I. HITAJI LA NJIA MPYA


Vipindi vingi vinavyofahamika vya uinjilisti leo havifanani kabisa na uinjilisti wa kanisa la kwanza. Msisitizo leo mara nyingi ni wa mkazo, ulioandaliwa, hali ya mmoja kwa mwingine. Vipindi vingi vina nguvu katika kuanzisha yaliyomo katika injili na namna ya kuishirikisha, lakini hawasisitizii nguvu ya uhusiano wa kuja kwa Kristo na hivyo hawaandaliwi kwenye kuwaweka watu katika kanisa la mtaa. Matokeo yake ni kwamba mara nyingi watu wanaletwa kwa Kristo, na kamwe hawawekwi kanisani. Huduma moja kubwa ya CIS ilitafiti matokeo ya juhudi za kiuinjilisti na kupata kwamba "5-10% wanabakia kanisani baada ya uinjilisti. 90-95% wanaondoka kwa sababu wanakuta kwamba hakuna msaada na majibu kwa mahitaji yao." Wazi, hii haipendezi. Agizo letu siyo kufanya watu wakate shauri, isipokuwa *wanafunzi,* na wanafunzi wanaungana na mwili (Mt 28:19; Ebr 10:25).

Mpanda kanisa anatakiwa kutumia njia ya uinjilisti inayowaleta watu kanisani. Anahitaji mkakati ambao asilia unapelekea ufuatiliaji, na kiasili kufuasa na ukuaji katika kanisa.

## II. MBIO ZA KUPOKEZANA

Kuna aina nyingi za mbio za binafsi, lakini mbio za kupokezana ni juhudi za timu. Tabia muhimu ya mbio za kupokezana ni kwamba mkimbiaji wa kwanza anamaliza sehemu yake ya mwendo katika mda uliowekwa, lakini kama hakabidhi kifimbo kwa mkimbiaji mwingine, ameshindwa. Utaratibu wa uinjilisti unaweza kulinganishwa na mguu wa kwanza wa mbio za kupokezana, na ufuasishaji unaweza ukalinganishwa na mguu wa pili. Baada ya mwinjilisti kumuuongoza mtu kumtumaini Kristo (uinjilisti), lazima afuaswe na kusaidiwa kukua kwenye ukomavu katika Kristo (kufuashwa).

**Kielelezo 4.1 Kukabidhi kifimbo**




Miguu yote ya mbio lazima ikamilishwe ili asiyeamini aweze kuokoka na pia kuwekwa katika kanisa la mtaa. Mguu wa kwanza unahusu kuelewa msingi wa yaliyomo (ukweli wa kitheolojia) wa injili ambao unapelekea kwenye uhusiano na Mungu. Mguu wa pili zaidi ni wa kijamii au kimahusiano. Hata hivyo maana- nzuri wakristo mara nyingi wanakimbilia kuwakilisha yaliyomo katika injili bila kuchukua mda kuanzisha uhusiano na mtu aliyepotea ambaye wanamshuhudia. Wakati aliyepotea anapotubu, hana uhusiano wa maana ambao kiasili utamchukua kwenye uhusiano wa ufuasishaji, na kwa hiyo utaratibu wa kufanya wafuasi unarudishwa nyuma.

**Kielelezo 4.2 Miguu Miwili ya Mbio za Kupokezana**

| Mguu wa Kwanza | Mguu wa Pili |
|---|---|
| Uinjilisti | Kufuasa |
| Uhusiano na Mungu | Uhusiano kwenye mwili |
| Wokovu | Utakaso |
| Kuzaliwa Upya | Kukua Kufikia Kukomaa |

Zana nyingi za kiuinjilisti zinachukulia tu mguu wa kwanza. Injili inawakalishwa katika namna ambayo itaeleweka na kupokelewa. Mungu asifiwe kwa zana hizi za kiuinjilisti. Kwa jinsi hiyo, kama wapanda kanisa, ni lazima tuchukulie miguu yote hii. Kwa jinsi fulani, hao tunaowashuhudia lazima wasikie injili na kuona jinsi inavyobadilisha watu.

Tutakifanya kichwa kuanza kwanza kwenye mguu wa pili wa mbio kama waliopotea wanaona uhusiano miongoni mwa waumini ambao unawakilisha upendo, furaha n.k. Watu wanatakiwa waangalie katika maisha yetu na kujua kuwa tuko tofauti. Wakati –wasioamini wanapoanza kusema, “sijawahi kamwe kuhisi upendo kama huu nyuma,” hivyo uinjilisti utakuwa unafanyika namna ulivyotakiwa (Yoh 13:35).

Inatakiwa isitushangaze kuona kwamba wakala aliyepata asilimia 5-10 tu ya matunda yake yaliyobakia kanisani alifikia suluhu hii “Katika maoni yetu, jibu lenye ufanisi zaidi katika ufuatiliaji ni muundo wa vikundi vya nyumbani katika kanisa.” Huduma ya vikundi kiini ni sehemu nzuri ya kukazia kwenye miguu yote ya mbio. Yaliyomo katika injili yanaweza kuwekwa wazi pamoja na nafasi ya maswali ya marejesho. Kwa kuongeza, vikundi kiini ni vidogo na vya ukaribu, vikiwa na nafasi ya uhusiano hai wa kukua na kuonekana.

## III. KANUNI ZA UINJILISTI

Maoni yafuatayo ni mazuri kwa kanuni za kiuinjilisti katika kiwango chochote kwa ujumla. Yameorodheshwa hapa kwa sababu ni ya faida hasa katika utaratibu wa upandaji kanisa. Kama tulivyosema hapo juu, watu wengi watafanya uamzi wa binafsi kwa Kristo lakini hawataendelea katika uhusiano wa kufuasa. Mpanda kanisa lazima awe anaweza kusaidia waliopotea kukamilisha mwendo wote ili kwamba waokolewe na kuwa washiriki hai katika mwili wa Kristo.

### A. Tumia Mitandao ya Kawaida

Kila mtu ana mtandao wa marafiki, jamaa, wafanya kazi wenzake, na wengeine anaowajua vizuri na alio na mawasiliano nao ya mara chache. Uhusiano huu wa kawaida unatoa nafasi huru ya mtiririko wa mawazo (kunapokuwa na majadiliano na mtu usiyemjua yanaweza kujazwa na kutoelewana na upinzani). Mara nyingi maongezi “yanasafiri” kupitia mitandao hii, kwa sababu injili, kama umeme ulivyo, inafata njia ya upinzani mdogo.

Yesu alikuwa na ufahamu wa mitandao hii ya kawaida na alikuwa na uwezo wa kufikia siyo watu pekee tu, lakini mitandao vilevile. Katika Mathayo 9:9-10 Yesu alimwita Mathayo na mara moja alikuwa katika nyumba ya Mathayo na mtandao wote wa wakusanya kodi wamekusanyika. Baada ya Yesu kukutana na Anderea mvuvi, ghafla kulikuwa na kundi zima la wavuvi wakimfuata Yesu (Yoh 1:40-41). Yesu alikaa kisimani na mwanamke msamaria na baadaye, alileta kijiji chake kizima kuja kumuona Yesu (Yoh 4:28-30). Yesu aliposhirikisha injili mtu mmoja alimuomba mtu huyo kushirikisha injili kwa hao walio katika mtandao wake (Lk 8:38-39). Kitabu cha Matendo vilevile kimejawa na historia za familia nzima (Mdo 11:14; 16:31) na vijiji vyote (mdo 9:35) wanaokuja kwa Yesu kwa sababu ya kukata shauri kwa mtu mmoja.

Watu walio wengi wanafanya vizuri katika kushuhudia hao wanaowajua vizuri. Baadhi ya wakristo wana moyo wa kuinjilisha, wanataka kwenda “mlango kwa mlango” kwa watu wasiowajua wakati hawajashirikisha injili kwenye familia zao, marafiki wa karibu au wanaoshirikiana nao. Kwa jinsi hiyo, kanuni ya “mtandao wa kawaida” unatakiwa uwekwe akilini. Wakati watu kutoka katika mtandao ule ule wanafanya uamzi wa kumfata Kristo, inaonekana zaidi kwamba wataendelea katika mguu wa mbio za ufuasishaji.

### B. Wafanye Waumini Wapya kushuhudia Mara Moja

Ni watu wa aina gani unaodhani kuwa wainjilisti wenye ufanisi? Pengine wengine watajibu “wachungaji” au “wanatheolojia.” Hakuna jibu lisilo sahihi hapa. Mtu yeyote anaweza kuwa mwenye ufanisi kama mwinjilisti wanapofata maelekezo ya Roho Mtakatifu. Lakini mara nyingi tunashindwa kutambua kuwa **waumini wapya kwa namna fulani ni wainjilisti wenye ufanishi zaidi**. Kwa nini? Chini sababu mbili zimeorodheshwa.

1. *Imani yao ni “motomoto.”*

Imani mpya iliyopatikana inaambukiza. Hata bila kuwa na kuelewa kwa ndani kwa theologia, aliyekata shauri mpya kwa shauku atatoa ushahidi wa mabadiliko yaliyotokea katika njia ya ajabu zaidi. Wengine wanaweza kuona mabadiliko baada tu ya kukiri kuliko ambavyo wanaweza kuona katika kipindi cha kukua kama mkristo.

2. *Muumini mpya anakuwa bado na Marafiki wasioamini ambao wanaweza kuona mabadiliko*

Injili inasafiri kupitia uhusiano. Inasemekana kwamba mara muumini wa wastani anapokuwa mkristo kwa miaka miwili au zaidi, marafiki zake wote wa karibu wataokoka vilevile. Kumbuka, uinjilisti ni mgumu zaidi kati ya usiowajua. Yohana 4:29 anatoa mfano wa muumini mpya ambaye ni mshuhudiaji mwenye ufanisi zaidi. Wakati msamaria mwenye dhambi alipokutana na Yesu, alikuwa na ushuhuda rahisi lakini wa maana sana “*Njoo, mtazame mtu aliyeniambia mambo yote niliyoyatenda, huyu anaweza kuwa*

*Kristo?"* Huyu mwanamke asingejibu swali gumu la kitheolojia, lakini alijua kilichokuwa kimemtokea. Na nani angebishana naye? Alielezea kilichotokea kwake. Hicho ndicho alichotaka kujua kuwavuta wengine kwa Kristo. Watu wa mji huo wakakimbia kwenda kukutana na Yesu. Ushuhuda wake ungekuwaje kama angesubiri mwaka mzima ndipo ashuhudie historia yake?

Muumini mpya ni shahidi mwenye nguvu. Kama mpanda kanisa unaweza kutaka kuanzisha mpango ili kwamba kila aliyekiri mpya ataweza kushuhudia familia yake na marafiki. Inapokuwa haiwezekani kutumia mpango waombe waumini wapya kwenda na wewe kuzitembelea familia zao na marafiki na kuanza uhusiana nao na kuwashirikisha habari za Yesu vilevile.


### C. Nenda kwa "Mlinda Mlango"

Kila kikundi cha watu ni pamoja na wachache mashuhuri zaidi kuliko wengine. Wakati badiliko linapotokea katika kikundi, kawaida wanakuwa wao ndio wanaoanzisha mabadiliko au angalau kuyaruhusu kutokea. Wakati hawa "mashuhuri" wameletwa kwa Kristo, wengine itawezekana kufata. Wakati mwingine tunawaita watu wenye mvuto wa aina hii "walinda mlango" kwa sababu ya umashuhuri wao kwenye kikundi na kwa sababu ndio wanaokuruhusu wewe kufikia waliosalia katika kikundi.

Ni nani mlinda mlango? Mtu

- Aliye na sifa njema miongoni mwa wanaoochipuka
- Yuko tayari kufanya urafiki na wewe
- Yuko wazi kwa Bwana

**Kielelezo 4.3 Mlinda Mlango**




Paulo, mpanda kanisa mkuu, aliuelewa ukweli huu. Alitarajia hasa kuwalete watu mashuhuri. Kwa kuelewa wafalme wakuu mashuhuri (Mit 16:15; 19:12), aliwalenga wao! (Mdo 9:15). Alitangaza injili mbele ya liwali Felix, Festo na mfalme Agripa (Mdo 23-26).

**Mkakati wa Paulo wa kawaida wa upandaji kanisa ilikuwa kufundisha katika sinagogi na kisha nyumbani kwa "mlinda mlango."** Kwa mfano, Huko Filipi mlinda mlango alikuwa Lidia (Mdo 16:11-15), na Thesalonike alikuwa Yasoni (Mdo 17:1-9), na Korintho alikuwa Tito Yusto (Mdo 18:7). Wakati Paulo alipomuongoza mtu fulani kwa Kristo wengine walifuata.

*Mifano mingine ya walinda milango*

- **Mfilipi mlinzi wa jela:** "Kisha wakamwambia neno la Bwana na kwa wengine wote katika nyumba yake. Katika saa hiyo ya usiku mlinda jela akawachukua na kuosha majeraha yao; kisha mara moja yeye na nyumba yake wakabatizwa. Mlinzi wa jela aliwaleta katika nyumba yake na kisha akawaletea chakula; alikuwa amejawa na furaha kwa sababu amemwamini Mungu-yeye na nyumba yake yote" (Mdo 16:32-34).

- **Krispo:** “Krispo mkuu wa sinagogi akamwamini Bwana yeye na nyumba yake yote; na Wakorintho wengi waliosikia waliamini na kubatizwa” (Mdo 18:8).
- **Stefano**: “Unajua kwamba nyumba yote ya Stefano ilikuwa ya wakata shauri wa kwanza huko Akaya, na wakajitoa kwenye kazi ya watakatifu. Ninawahoji ndugu zangu, kujitoa kwenye haya na kwa kila mtu anayejiunga katika kazi…” (1Kor 16:15-23).
- Ingawa haikuwa wazi kabisa, tazama pia: 2Tim 1:16; 4:19), **Nimfa** (Col 4:15), **Koroneli** (Mdo 10:7-24), **Akwila na Prisila** (1Kor 16:3-5), **Gayo** (1Kor 1:14; 16:23).

Katika tamaduni nyingi “walinda mlango” ni wanaume vichwa vya nyumba. Kama wakija kwa Kristo, inawezekana familia yote ikafuata. Katika hali yoyote, “walinda mlango” wanapoletwa wataleta na wengine pamoja nao.

Wakati mwingine “walinda mlango” watakuwa kama samaki mkubwa. Saamaki mkubwa kawaida anakuwa kwenye maji yenye kina, mbali kutoka kwenye ukingo. Inaweza ikahitaji baadhi ya juhudi kumwendea samaki mkubwa, na wanaweza kuwa wapinzani. Wanaweza wakapinga injili njia yote, lakini kumkamata samaki mkubwa kunaweza kukawa faida ya juhudi!

### D. Fikiria Vizuizi Vya Kiutamaduni

Watu mara chache wanavuka vizuizi vya utamaduni kwenda kanisani. Watu wanaweza kufanya uamzi wa binafsi kwa ajili ya Kristo lakini wakasita kwenda kanisani—kuvuka daraja la pili—kwa sababu ya vizuizi vya kiutamaduni au kijamii. Watu ni viumbe wa kijamii, kwa sababu iwayo yote, wanapenda kuungana na hao walio kama wao.


Waliokata shauri wapya wanaonekana zaidi kujiunga kwenye kanisa kama kwa kufanya hivyo, hawatatakiwa kubalisha tamaduni zao sana. Fikiria njia za kuandaa kanisa lako ili kwamba livute tofauti za utamaduni na jamii ya watu unayojaribi kupata bila kupatanisha ukweli wa kitheolojia. Paulo waziwazi alitumia mkakati huu: “kwa Wayahudi, nalikuwa kama myahudi ili niwapate Wayahudi. Kwa hao walio chini ya sheria nalikuwa kama chini ya sheria… Kwa wanyonge, nalikuwa mnyonge, niwapate wanyonge” (1Kor 9:20-23). Paulo alikuwa tayari kurekebisha utamaduni wake ili kupunguza vizuizi kati yake na wasioamini. Mara nyingi, tunafanya kinyume. Tunageuka kuwa magogo ya kuwakwaza katika njia zao badala ya kuwasaidia kukimbia mbio za ushindi.

### E. Angalia ‘Kianzio cha Kawaida’

Wakati mwingine njia ya ‘msingi wa kuelewana” ndiyo tu inayotakiwa kuanzisha uhusiano na kuwaleta watu kwa Kristo. Kwa “msingi wa kuelewana”, tunaanzisha shughuli ambazo ni za kawaida zinazofanana kwa waumini na wasio waumini. Msingi wa kuelewana unaweza kutumika kama njia ya kuanzisha uhusiano na kuwakilisha injili.

Chukua mda kuandika shughuli kadhaa za msingi wa kuelewana zinazohusiana na maisha yako ya kikristo. Orodhesha shughuli hizi katika nafasi iliyotolewa hapo chini ya herufi “A” katika mchoro wa “msingi wa kuelewana”. Inayofata, Orodhesha shughuli zinazofanana katika wastani wa siku ambazo hazikubaliwi kwako kama mkristo lakini ni za kawaida kwa asiyeokoka katika kundi unalolenga. Andika majibu haya katika duara lililowekewa alama “C.” Mwisho, Katika sehemu “B,” orodhesha shughuli unazooshughulika nazo zinazokubalika kwako na ambazo zinaweza kukubalika kwa wasiookoka wanaokuzunguka.

**Kielelezo 4.4 Msingi wa Kuelewana**




## MASWALI YA KUTAFAKARI, MARUDIO NA MATUMIZI

- Fikiria watu wawili unaowajua waliofanya uamzi wa kumfuata Kristo, lakini ambao hawahudhurii kanisani. Kwa nini hawajajihusisha katika mwili wa waumini? Orodhesha sababu hasa iwezekanavyo.
- Mwelezee mtu fulani anayefaa kama “mlinda mlango” katika kundi lako unalolenga. Jinsi gani unaweza kumfikia?
- Ni mifumo ipi kiutamaduni inayofaa kuvutia watu katika kanisa lako?
- Ni kwa njia zipi unaweza kutumia msingi wa kuelewana uliopata kama njia ya kuwakilisha injili?

## UTEKELEZAJI WA AZIMIO

Chukua dakika kadhaa kusoma mkakati wa uinjilisti ulioelezewa kwenye Uinjilisti katika ziada 4A. Tathimini mikakati hii kulingana na kanuni za kiuinjilisti katika somo hili. Mikakati hii itapelekea kwa ufanisi wa makanisa mapya? Ni kwa jinsi gani kila moja ya mikakati hii inavyoweza kurekebishwa kuhakikisha upandaji kanisa wenye afya?

## VYANZO


- Zunkel, C. Wayne. *Strategies for Growing Your Church.* Elgin, IL: David C. Cook Publishing Co., 1986.
- Jenson, Ron, and Jim Stevens. *Dynamics of Church Growth*. Grand Rapids, Mi: Baker, 1986.

UINJILISTI
*ZIADA*
4A

# Kutathimini Mkakati wa Uinjilisti

Chukua dakika kadhaa kusoma mikakati ifuatayo ya kiuinjilisti. Tathimini mikakati hii kulingana na kanuni za kiuinjilisti katika somo hili. Baada ya kusoma kila mkakati zungushia namba kuanzia 1 (ya chini) mpaka 5 (ya juu) ambazo unafikiria zinaelezea vizuri jinsi unavyotimiza vipimo vilivyoorodheshwa katika visanduku. Mikakati hii itapelekea kwa ufanisi makanisa mapya? Ni kwa jinsi gani kila moja ya mikakati hii inavyoweza kurekebishwa kuhakikisha upandaji kanisa wenye afya?

## I. MKAKATI WA UINJILISTI 1—MAFUNZO YA BIBLIA YA KIUINJILISTI

Sasha na Tanya wanaishi katika mji wa watu 100, 000 pasipo na makanisa ya kiinjili. Wakiwa na haja ya kupanda kanisa, wanaanzisha mfunzo ya Biblia ya kiuinjilisti nyumbani kwao. Baada ya mwaka mmoja watu 15 wanahudhuria kwa uaminifu na wanavyoona 9 kati yao ni waumini. Wanatambua kuwa kwa watu 15 kikundi kinakuwa kikubwa kuweza kujisikia kila mmoja anahusika, wanaanzisha kikundi kingine kinachokutana katika usiku mwingine katika nyumba ya familia nyingine. Sasha anatumaini kwamba watakapokuwa na watu wa kutosha katika makundi haya, watakodi ukumbi na kuanza kuabudu kila jumapili kama kanisa.

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watu unaowasiliana nao binafsi:** | **1** | **2** | **3** | **4** | **5** |
| **Kutimiza hitaji linalogusa la waliopotea:** | **1** | **2** | **3** | **4** | **5** |
| **Tumia Mtandao wa kawaida wa uhusiano:** | **1** | **2** | **3** | **4** | **5** |
| **Kazania kwenye upokeaji:** | **1** | **2** | **3** | **4** | **5** |
| **Kazania kwa “mlinda mlango:** | **1** | **2** | **3** | **4** | **5** |
| **Kutoa ufuatiliaji wa ufuasishaji:** | **1** | **2** | **3** | **4** | **5** |

## II. MIKAKATI YA UINJILISTI 2—UINJILSTI WA MIKUTANO YA NJE

Alexander ana mpango mkubwa wa kupanda kanisa katika mji mkubwa. Alexander amemaliza chuo cha Biblia hivi karibuni. Wakati akiwa chuoni Alexander alifanya mawasiliano na kikundi moto moto cha kimisheni kilichojitoa kumsaidia katika mradi huo. Kwa pamoja, Alexanda na Wamarekani wanapanga kuanzisha mambo mwezi wa sita wakati wanafunzi 20 wa chuo cha Kiamerika watakapokuja kusaidia katika uinjilisti. Mpango ni kwa wiki watakayokuwa na wamarekani wakazane sana. Ukumbi utakodishwa na mkutano wa wazi pamoja na mziki, shuhuda, na kuwakilisha injili vitafanyika kila jioni. Wakati wa mchana Mmarekani na Mrusi wataungana na mkarimani kuzungukia mji wote, wakitoa vijitabu vya maandishi na kwenda mlango kwa mlango kutangaza mkutano wa jioni. Alexanda anatarajia kuwa matokeo ya uinjilisti wa wiki hiyo watu wa kutosha watakuwa wameokoka tayari kufungua kanisa lake mara moja.

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watu unaowasiliana nao binafsi:** | **1** | **2** | **3** | **4** | **5** |
| **Kutimiza hitaji linalogusa la waliopotea:** | **1** | **2** | **3** | **4** | **5** |
| **Tumia Mtandao wa kawaida wa uhusiano:** | **1** | **2** | **3** | **4** | **5** |
| **Kazania kwenye upokeaji:** | **1** | **2** | **3** | **4** | **5** |
| **Kazania kwa “mlinda mlango:** | **1** | **2** | **3** | **4** | **5** |
| **Kutoa ufuatiliaji wa ufuasishaji:** | **1** | **2** | **3** | **4** | **5** |

## III. MKAKATI WA UINJILISTI 3—MEZA YA VITABU VYA KIKRISTO

Andre na Luba wamekuwa wakristo kwa kipindi kirefu. Wakiwa na hitaji la kuanzisha kanisa jipya litakalofikia kikundi kipya cha watu wanaanzisha mkakati ufuatao. Wakigundua ni watu wangapi katika eneo lao wanapenda kusoma, wanakusanya vitabu vingi vya kikristo wawezavyo kupata na kuanzisha meza ya vitabu ikiwa na vitabu vya kikristo tu karibu na eneo la soko. Kila siku Andre na Luba wanaandaa meza yao ikiwa na vitabu vya kikristo kwa ajili ya kuviuza kwa bei ya chini sana. Baadhi ya vijitabu vya injili vinatolewa bure kwa kila mmoja anayepita kuuliza. Wana baadhi ya karatasi za kufanyia mafunzo ya Biblia pia ambazo watu wanazichukua kwenda nazo nyumbani na kuzifanyia kazi. Imeandaliwa ili kwamba watu wajadili karatasi za mazoezi pamoja na Andre au Luba kila mwishoni mwa kila moja kumalizika na kabla ya inayofata kupokelewa. Karasi hizi za kufanyia mazoezi ni za kiuinjilisti na Andre na Luba wanaomba kwamba watu wampate Kristo matokeo ya masomo hayo na hatimaye waanzishe kanisa.

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watu unaowasiliana nao binafsi:** | **1** | **2** | **3** | **4** | **5** |
| **Kutimiza hitaji linalogusa la waliopotea:** | **1** | **2** | **3** | **4** | **5** |
| **Tumia Mtandao wa kawaida wa uhusiano:** | **1** | **2** | **3** | **4** | **5** |
| **Kazania kwenye upokeaji:** | **1** | **2** | **3** | **4** | **5** |
| **Kazania kwa “mlinda mlango:** | **1** | **2** | **3** | **4** | **5** |
| **Kutoa ufuatiliaji wa ufuasishaji:** | **1** | **2** | **3** | **4** | **5** |

## IV. MKAKATI WA UINJILISTI 4—VIDEO ZA KIKRISTO

Vladima anajaribu kupanda kanisa katika mji mkuu. Ili kuinjilisha, Vladima anatumia video za kikristo. Anawaalika watu katika ujirani wake na katika kiwanda anapofanya kazi waone video hizo. Sasa, kikundi cha vijanya wenye shauku wasio wakristo wanakusanyika katika nyumba yake ya kupanga kila jumanne jioni. Mkutano kawaida unakuwa wa saa moja na nusu. Kwa dakika 30-45 washiriki wanaangali video na kufuatiwa na majadiliano yanayoendeshwa na Vladima akitumia mwongozo wa majadiliano unaoendana na video. Kwa kutumia njia hii, Vladima anatumaini kuwa watu wa kutosha watakuja kwa Kristo na kwamba ataweza kuanzisha kanisa.

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watu unaowasiliana nao binafsi:** | **1** | **2** | **3** | **4** | **5** |
| **Kutimiza hitaji linalogusa la waliopotea:** | **1** | **2** | **3** | **4** | **5** |
| **Tumia Mtandao wa kawaida wa uhusiano:** | **1** | **2** | **3** | **4** | **5** |
| **Kazania kwenye upokeaji:** | **1** | **2** | **3** | **4** | **5** |
| **Kazania kwa “mlinda mlango:** | **1** | **2** | **3** | **4** | **5** |
| **Kutoa ufuatiliaji wa ufuasishaji:** | **1** | **2** | **3** | **4** | **5** |

UINJILISTI

SOMO LA 5

# Vizuizi Kwenye Uinjilisti wa Mafanikio

## MADARAJA BADARA YA VIZUIZI

☞ **Kusudi la Somo**

Kusudi la somo hili ni kujadili mtu binafsi wa kwaida na vizuizi vya kiroho kwenye uinjilisti na jinsi ya kuvishinda.

☞ **Wazo Kuu**

- Vizuizi vya nje kwenye uinjilisti vinaweza kuwa vya kiutamaduni, lugha, dini au kiroho.
- Vizuizi vya ndani ni pamoja na mapokeo, athari, hofu au tabia za mtu.

☞ **Matokeo Yanayotarajiwa**

Wakati yaliyoma katika somo hili yanapoeleweka, kila mshiriki anatakiwa:

- Kuweka mpango wa kuzuia vizuizi vya ndani na nje kwenye uinjilisti

☞ **Ziada**

5A “Kanisa kwa Watu Wote: Maongezi ya Unyoofu juu ya Somo Gumu”

5B Kujibu Upinzani wa Kawaida: Tumia Maandiko Kama Mamlaka Yako

☞ **Ushauri kwa Wakufunzi**

Ruhusu mda wa watu kugawanyika katika vikundi vidogo kujadili maswali ya kutafakari, marudio na matumizi.

Badala tu ya kufanya marudio ya maandishi ya somo, fikiria kuchukua mda wa kuangalia katika mazungumzo ya Yesu na mama msamaria kisimani katika Yohana 4 kama mfano wa kushinda vizuizi katika kuwasilisha injili. Kama hili halikufanyika kama sehemu ya somo lenyewe, linaweza kuandaliwa kama mpango wa matumizi kufanyika kati kati ya miongozo.

Waulize wafunzwa kusoma na kujiandaa kujadili toleo katika Ziada 5A kabla ya kipindi.

### I. MATATIZO YA VIZUIZI NA HITAJI LA MADARAJA

Kwa karne nyingi, waumini wanaoishi katika eneo hili walikuwa kihalali wamekataliwa haki ya kushirikisha imani zao kwa uwazi katika jamii zao. Makanisa yalishawishi mitaa ya kidini—karibia miji ya maboma ya kidini —kuanza karibu nao, na hasia ya kujisikia, kujitenga, kutengwa, na kutoaminiwa kwa hao walio kwenye “serikali” ya kidunia ilikuwa inapenye kote. Mara nyingi eneo pekee la halali kushirikisha Kristo ilikuwa kwenye jengo la kanisa. Karne hizi ziliacha alama ya kudumu katika mkao wa akili na mapokeo ya hao wanaompenda Kristo. Vizuizi hivi vimesimamishwa. Vizuizi hivi lazima vigunduliwe na kuangushwa chini.

Mara nyingi, Kanisa limeelewa vibaya nafasi ya asiyeokoka katika mafarakano ya kiroho. Kwa kujua kwamba Ibirisi anaweza kutumia wasiookoka kuwalaghai waumini, waumini walikuwa wameonywa kujitenga kutoka kwa marafiki na majirani wasiookoka. Kwa jinsi hiyo, waliopotea siyo maadui. Ni dhamana katika vita vya kiroho. Ni walengwa katika juhudi zetu za kiroho. Wako kama tulivyokuwa kabla hatujawa na Kristo—vipofu kiroho, waliokufa kiroho, na wasio na kitu kiroho. Siyo maadui wa kushambulia. Badala, ni dhamana wa kufunguliwa. Wanaangamia bila kujua, juhudi za kijasiri zimechukuliwa na kanisa kuwaleta kwenye imani.

Ili kukamilisha kazi hii ya ukombozi na kurudisha, waumini lazima wajenge madaraja kwa wasio wakristo ulimwenguni wanaotuzunguka. Mara nyingi kukutana kwetu kwa ukristo na tamaduni ni kwa kigeni sana na kitu cha ajabu kwamba waumini hawatafanya juhudi kuungana nasi. Kama watafikiwa, lazima tuwafikie kwa kujenga madaraja ya unyoofu, rehema, huruma, ukweli na upendo.

Ngoja tuelewe hili. Tutaeleweka vibaya. Tutasikitishwa na juhudi zetu. Tutachoka kimwili, kihisia na kiroho. Tunahitaji kurejeza nguvu zetu kwa kuishi maisha yenye uwiano. Lakini juhudi lazima zifanyike kufikia kizazi hiki na kila kizazi kwa injili. Ni kazi yetu, wito wetu na changamoto yetu maalumu. Kizazi kingine cha waumini hakiwezi kufikia kizazi chetu na hatutakuwa hapa kufikia vizazi vyao. Ni wakati wa kuangusha vizuizi vyao.

## II. KUELEWA VIZUIZI VINAVYOZUIA UINJILISTI

Mmarekani anayejulikana vizuri Raph Winter amefanya baadhi ya uchunguzi muhimu juu ya uinjilisti. Kwa kutumia Matendo 1:8 kama msingi, anapendekeza kwamba maneno ya Yesu kwenye Utume Mkuu hayakutupa sababu tu za kugawanya ulimwengu kijogorafia (mji wangu, eneo langu, nchi yangu, na ulimwengu) lakini pia kugawanya ulimwengu kwa kutazama makundi ya watu kiutamaduni. Katika kifungu Yesu anarejea Yerusalemu, Yudea, Samaria na miisho ya ulimwengu. Kikawaida kwa wanafunzi, ingekuwa rahisi kwao kufanya uinjilisti Yerusalemu, na Yudea ambako kila mmoja alisema lugha sawa na kukulia katika utamaduni sawa. Kwa Petro au Yohana, Kufundisha na kuhubiri Samaria ingekuwa vigumu zaidi. Siyo tu kwamba kulikuwa baadhi ya tofauti za kiutamaduni, lakini kulikuwa na kuhukumiwa bila kusikilizwa kunakotokana na sheria ya kuabudu ambayo ingetakiwa kuondolewa. Mwisho, Kwa mmishenari au mwinjilisti kwenda “miisho ya dunia” kutahitaji kiasi kikubwa cha maandalizi (kujifunza lugha n.k.). Hili tunaliewa kirahisi. Kwa jinsi hiyo, Raph Winter anasema kwamba kama tunauangalia ulimwengu kwa mtazamo wa tofautu za tamaduni, kisha “*miisho ya dunia” mara nyingi siyo mamia ya kilometa za umbali, lakini kwa kweli, inaweza ikawa kwenye mji wako au jiji.* Kuna kundi la watu wote katika mji wako wanaoishi katika mila tofauti au mila ndogo. Kwa hakika, Mara nyingi wakristo wanazama katika maisha ya kundi lao kiasi kwamba wanazama katika tamaduni kidogo na hawawezi tena kuelewa au kujilinganisha na marafiki zao wa utotoni, jamaa ya familia au majirani.

Aina ya huduma maalumu na uinjilisti unaweza kuhitajika ili kuvuka mipaka ya vizuizi vya mila na kwa ufanisi kushirikisha injili. Tambua jinsi Yesu alivyoongea na mwanamke kisimani katika Yohana 4. Vilevile, tambua mtindo wa kuhubiri na yaliyomo aliyotumia Paulo alipokuwa anaongea na Wayahudi (Mdo 9:20-22) ikilinganishwa na alipokuwa akiongea na wasio Wayahudi (mdo 17:16-31). Wote Yesu na Paulo ilibidi washinde vizuizi vya mila ili kuweza kuhudumu kwa watu kwa ufanisi.

Chukua mda fulani kusoma toleo “*Kanisa Kwa Watu Wote: Maongezi Mroro Kuhusu Somo Gumu*” na Doanald McGavran (Ziada 5A). Unaposoma, fikiria kiwango ambacho MacGavran ameshawishika kwamba tofauti za mila zitazuia uinjilisti. Fikiria mandhali ambayo unafanya kazi. Onyesha katika akili zako mwenyewe kwa kiasi gani unajua mila za watu ambao unajaribu kupanda kanisa miongoni mwao.

Uinjilisti wa mafanikio zaidi unatokea mahali ambapo kuna “vizuizi” kidogo vya kuvunja. Uinjilisti unakuwa wa mafanikio unapokuwa unaongea na mtu fulani ambaye unafanana naye, anayefikiria kama wewe, anayependa kufanya yale unayopenda kufanya, anayeweza kuhusika kwenye furaha yako, anayeweza kufahamu matatizo yako, na zaidi.

Lakini kuna mila nyingi na mila ndogo zinazoingiliana za watu ambazo kuna waumini wachache au hakuna kabisa waumini. Ni lazima tujiandae kufanya juhudi za ziada kushinda “vizuizi” vilivyopo. Fikiria vizuizi vilivyoorodheshwa kwenye ukumbusho wa somo katika mwanga wa eneo la huduma yako ya hivi karibuni. Kumbuka kwamba hata tofauti ya vikundi vya umri, shughuli, na uwezo wa kiutendaji unaweza kuwa msingi wa kutokea kwa mila zinazoingiliana. Bila kujali hali, ni lazima tushinde vizuizi hivi ili injili iweze kusikiwa kwa uwazi.

## III. VIZUIZI VYA NJE KWENYE UINJILISTI WA UFANISI

### A. Vizuizi vya Kiutamaduni

Wafanya kazi wa kikristo kutoka nchi nyingine, mabara mengine, au hata eneo jingine la nchi moja kubwa kawaida lazima wajifunze kuelewa na kuendana na tofauti za kimila ili kupunguza pengo kati yao na hao ambao wangewafikia kwa injili. Paulo aliandika “Nimekuwa hali zote kwa watu wote ili kwa njia zote nipate kuwaokoa watu” (1Kor 9:22). Alikuwa tayari kuweka tofauti za kiutamaduni ambazo angeweza kuzichagua kwa madhumuni makubwa ya kuwaleta wengine kwa Kristo. Kwa jinsi hiyo, tatizo la kimila siyo kwa wamishenari tu.

Katika kila mila, kanisa limeanzisha mapokeo ambayo yanaweza kuwa bora na ya ufanisi yalipowekwa mwanzo, lakini ambayo kwa mda yamepitwa na wakati na kutofaa. Mila hizi za mapokeo ya kanisa zinaweza kudhihirika katika mziki wetu, mavazi, na maarifa ya ujenzi, kuorodhesha machache. Kama hatuna mzaha kuwafikia waliopotea kwa injili, mila hizi zinatakiwa kutazamwa upya na kurekebishwa.

| Kiutamaduni | |
|---|---|

### B. Vizuizi vya Lugha

Kwa hao wanaotoka katika mila ya pili, mpaka wazi zaidi katika kuwakilisha injili kwa ufanisi ni katika kutoweza kuongea lugha. Kwa jinsi hiyo, mawasiliano yanaweza kuwa tatizo kati ya wakristo na wasio-wakristo wanaoongea lugha moja. Maneno ya kipekee mara nyingi yanatumika katika ushirika wetu. Mara nyingi hata hatuna habari nayo.

Ninakumbuka uinjilisti wa kufikia nje miongoni mwa watu wa Yugoslavia. Walipokuwa wakiachana, ilikuwa ni kitu cha kawaida kufanywa kanisani kusema “Gospod s tobom”, ikiwa na maana “Nenda na Bwana.” Nilitumia fungu na mtu aliyekuwa mwaminifu kuhudhuria mikutano yetu. Jibu lake lilikuwa “Hapana, ninakwenda na mulani!” Hakujua wazo la ujumbe wangu wala makusudi yake. Aliyajua maneno, lakini yalikuwa tupu, na wote yeye na mimi tulichanganyikiwa kidogo na kujisikia vibaya..

Salamu yetu maalumu na maneno ya kiroho yanaweza kutatiza wasioamini ambao hatujaanzisha miongoni mwetu. Tunahitaji kutafuta njia mpya ya kusema kile ambacho ni cha muhimu zaidi—ujumbe kwamba Mungu anapenda utu wa waliopotea na amekuja kuwakomboa wanaume, wanawake, na watoto.

| Kiutamaduni | Ki lugha | |
|---|---|---|

### C. Vizuizi vya Kidini

Tunakutana na watu wanaotofautiana. wanaweza kuwa wakatoliki wa kimajina, Othodox, wasioamini kama kuna habari za Mungu au watu wa kidunia. Wanaweza kuwa wamejihusisha kwa namna moja na madhehebu yaliyojitenga au ya ibada tofauti. Wanaweza kuweka maana tofauti ya maneno yote na matendo tunayoyachukulia hivi hivi. Maneno kama “wokovu,” “imani,” na “kuamini” yanaweza kuhitaji maelezo ili kwamba watu waelewe maana yake. Inaweza kuwa faida kwetu kuwauliza hao tunaowasiliana nao kueleza wazi kuelewa kwao kwa maneno tunayotumia nao.

Matendo yetu, ishara, na hata mkao vinaweza kutisha wengine pia. Baadhi wanaona ugumu kuamini kwamba nyumba iliyoko mbele ya jengo la duka la zamani inaweza kutumika kwa kusudi la kumtumikia Mungu kwa kusanyiko dogo. Wanaweza wakatarajia jengo la ajabu lenye alama na maonyesho mengine ya kiufundi yanayoonyeha imani za dini. Wanaweza kusumbuliwa na ukawaida wa mtindo wa kuabudu na kumjua kwetu Mungu. Ni kazi yetu ya kuwapata wasiookoka. Ni lazima tutafute njia za kujenga daraja kutuunganisha nao.

| Kiutamaduni | Ki lugha | Kidini |
|---|---|---|

### D. Baadhi ya Vizuizi Vina Asili ya Kiroho

Vizuizi vya mwisho vinahusika na tofauti kutoka kwa zile zilizokwisha tajwa nyuma. Vizuizi hivi vya kikatili kwenye uinjilisti wa ufanisi ndivyo vinavyotenganisha walio hai kiroho kutoka kwa walio kufa kiroho. Isipokuwa tu Roho Mtakatifu anayeweza kutoa uhai kupitia injili tunayobeba. Peke yake anaweza kuhuisha na kukomboa waliopotea. Hatimaye, siraha ya maombi , neno la Mungu, na shuhuda zetu wenyewe ndivyo Mungu atakavyotumia kumshinda shetani na kuwaweka huru waliotekwa. Ni lazima tutambue upinzani tunaokutana nao hatimaye tunapotoka kwa shetani na kusimama dhidi yake kwa ajili ya Bwana.

| VIZUIZI VYA NJE | | | |
|---|---|---|---|
| Kiutamaduni | Ki lugha | Kidini | Kiroho |

## IV. VIZUIZI VYA NDANI KWENYE UINJILISTI WENYE UFANISI

### A. Vizuizi vya Mpokeo Yetu Wenyewe

“Haikuwahi kufanyika kwa njia hiyo kabla.” Pengine ni wakati wa kufanya mambo kwa njia mpya, siyo kwa sababu njia za zamani zina makosa, lakini kwa sababu zinaweza kuwa si za ufanisi tena. Mifumo ya zamani inawezekana isiweze tena kukamilisha kazi iliyokusudiwa. Tatizo la ngozi ya kuchujia bia, ya zamani na ya sasa, ni moja ambayo lazima izungumziwe. Hatutaweza kubadilisha injili yetu muhimu, lazima tusipatanishe uaminifu wetu, lakini tunaweza kubadili jinsi injili ilivyowekwa ili kuvuta nia nyingi na kupata wasikiaji.

| Mapokeo | |
|---|---|

### B. Vizuizi Vya Kuhukumu Kwetu

Kuna makundi ya watu katika kila mila walioachiliwa kama wasio wa maana au wasiofaa kufikiriwa. Wakristo, pia lazima washinde kuhukumu. Hukumu zetu zinaweza kuwa za kikabila kiasili (kumbuka mwanamke msamaria), au maadili, au uhalifu wa sheria (kumbuka Zakayo). Zinaweza zikawa maalumu tangu kuzaliwa au kutokana na ajali (kumbuka mtu aliyezaliwa kipofu). Tunaweza kutumia mda wetu na juhudi na watu wanaovutia na wenye mali na kuacha wahitaji ambao wangekuwa wepesi kukubali injili ya Kristo. Kumbuka makaripio ya Paulo kwa Wakorintho (1Kor1:18-31) na maneno makali ya Yakobo (Yak 2:1-13). Muulize Mungu asafishe moyo wako na kuufungua moyo wako na macho kwa wote wanaohitaji mwokozi.

| Mapokeo | Kuhukumu |
|---|---|

### C. Vizuizi Vya Hofu Zetu

Huduma ya uinjilisti ni huduma ya imani. Inahitaji moyo kujihatarisha wenyewe na sifa njema kwa ajili ya kuwatafuta hao ambao wanaweza wasiitikie kwenye injili yetu. Tunaweza kujisikia kutokutosha kwenye huduma, tukifikiri kuwa hatujui vya kutosha au hatuna ujuzi wa kutosha. Kusomea kunaweza kukasaidia, lakini hatimaye, ni lazima kila mmoja achague kumfata Bwana kwa imani na utii kukamilisha kazi aliyotupa. Ametupatia silaha ya Roho wake, maombi na maandiko. Zaidi ya hayo, Ameahidi uwepo wake pamoja nasi. Hata mtume Paulo, aliyeandika, “Ninayaweza mambo yote katika Kristo anitiaye nguvu,” (Flp 4:13) vilevile aliandika katika 2Korintho 4:7 kwamba ujumbe wetu wenye nguvu unakuja umefungwa kwenye “chupa ya mchanga.” Ni wazi kwamba nguvu haiko ndani yetu isipokuwa kutoka kwa Mungu. Uaminifu wetu mbele ya uso wa hofu unaleta utukufu kwa Mungu na watu katika ufalme wake.

| Mapokeo | Kuhukumu | Hofu |
|---|---|---|

### D. Vizuizi Vya Kupingana kwa Thamani Zetu Wenyewe

Wote tuna upungufu kwa maana ya rasilimali zetu—nguvu, mda, fedha, uwezo na vipawa. Ni lazima kila mmoja aonyeshe mbele za Mungu jinsi ya kuwekeza rasilimali hizi kama mtu binafsi na kusanyiko kukamilisha kila alichotuitia kufanya. Lakini lazima iendelee kuwa wazi kuwa kama watu wapya hawaji kwenye ushirika wetu kupitia njia ya kuwafikia kwa kukusudia, ukuaji wa kanisa haupo na hautatokea. Kila mmoja wetu lazima kwa maombi aonyeshe na kwa upatano mkamilifu na kuelewa kwetu kwa maandiko sehemu ya makusudio ya uinjilisti katika maisha yetu, ratiba na makadilio. Hakutakuwa kamwe na rasilimali za kutosha kukamilisha kila ambacho tungependa, kwa hiyo ni lazima tuchague kwa uthabiti kuwaleta waliopotea.

| VIZUIZI VYA NDANI | | | |
|---|---|---|---|
| **Mapokeo** | **Hukumu** | **Hofu** | **Thamani** |

## V. MKAKATI WA KUSHINDA VIZUIZI


Kushinda vizuizi hivi vya ndani na nje juhudi za kuazimia zitahitajika. Vizuizi vya nje vitahitaji kwa maana na ubunifu wa kushinda. Kwa kutazama vizuizi kijamii na kidini, tutahitaji kuweka mda katika kujifunza kutambua na kuelewa upana wa habari za nyuma za kusanyiko letu. Lazima tutumie ufahamu huu tunapokuwa tunajifunza kushinda vizuizi vya lugha ili kuweza kuwasiliana kwa ufanisi na wasioamini. Kwa kutazama vizuizi vya kiroho, lazima tukazanie kwenye maombi, tukimwuliza Roho wa Mungu Kufungua mioyo ya hao ambao tungewaleta kwa Kristo. Katika hali zingine tutajikuta wenyewe "tukiongelea kwenye desturi za madhehebu yetu wenyewe" kwa ajili ya injili. Maombi na kujiweka kwa ujasiri kunaweza kukahitajika kusahihisha vizuizi vya mda mrefu.

Vizuizi vya ndani pia lazima vikabiliwe. Katika Warumi 12:2, tunasoma kwamba tunatakiwa tusiifuatishe namna ya dunia hii lakini tugeuzwe na kufanywa upya katika nia zetu. Kama tunataka kuona ulimwengu wetu umebadilika, lazima tuone makanisa yetu yamebadilika. Kama tungeona makanisa yetu yamebadilika, lazima tuone mioyo yetu imebadilika. Kama tungeona mioyo yetu imebadilika, tunatakiwa kugeuza nia zetu kwa kujizamisha wenyewe kwenye usafishwaji kwa neno la Mungu.

Roho wa Mungu atatumia neno la Mungu kumulika akili zetu ili kwamba tuweze kuona vitu katika namna ya kimungu. Atakemea thamani na kuhukumu ambako hakumpendezi yeye. Atatupa ujasiri kufanya mabadiliko yanayotakiwa kukamilisha kusudi lake kuhusu uinjilisti. Atatupa imani ya kushinda hofu zetu tunapokazia kwenye utii wa neno lake lililoandikwa.

Katika Ziada 5A na 5B, Utakuta maandiko hasa yaliyochaguliwa kusaidia katika utaratibu huu wa kutayarisha mioyo yetu na akili zetu kuweza kwa ufanisi kuwafikia watu kwa injili ya Kristo.

**Kielelezo 5.1 Kushinda Vizuizi**



## MASWALI YA KUTAFAKARI, MARUDIO NA MATUMIZI

- Ni nini tunachoweza kufanya kupunguza ubatilisho na kuchanganyikiwa wanakojisikia wasioamini wanapotembelea ushirika wetu au majumbani kwetu?
- Ni aina gani ya vitu vinavyokufanya kutojisikia huru au wepesi katika hali isiyojulikana?
- Ni vizuizi gani mwenyewe umewahi kukutana navyo ulipofikiri kuwafikia watu kwa injili? Umevishinda? Kama ndiyo, Ni kwa njia gani umevishinda?
- Ni kundi gani kihistoria limeathirika kwa hukumu katika mila yako? Ni nini Bwana anachotaka ufanye kukabili hukumu hii?
- Ni mabadiliko gani unayoweza kufanya kivitendo katika wiki zijazo kushinda vizuizi na kuongeza uinjilisti wako wa kimataifa?

## UTEKELEZAJI WA AZIMIO

- Fanya mafunzo ya Biblia kwa kufata neno ya Yohana, sura ya 4. Tambua vizuizi ambavyo Yesu alishinda kujionyesha mwenyewe kwa mwanamke kisimani.
- Soma toleo katika Ziada 5A, “Kanisa kwa Watu Wote: Mazungumzo ya Moja kwa Moja Juu ya Somo Gumu,” Na Donald McGavran. Andika ukurasa mmoja wa mwitikio wa toleo hili. Unakubaliana/kutokubaliana na Donald McGavran? Ni jinsi gani toleo hili linagusa kufikiri kwako juu ya uinjilisti na mkakati wa upandaji kanisa? Jiandae kujadili mwitikio wako na mkufunzi au mshauri.

UINJILISTI
*ZIADA*
5A

# "Kanisa kwa Watu wote: Mazungumzo ya Moja Kwa Moja Juu ya Somo Gumu"

## NA DONALD A. MCGAVRAN

### UTANGULIZI NA RAPH D. WINTER

*Kwa njia nyingi hii ni "barua" isiyo ya kawaida zaidi iliyoandikwa na mwanamikakati ya kimishenari aliyejulikana zaidi katika karne ya ishirini. Hakuna uhakika sana kwamba mtu mwingine yeyote katika historia aliyetembelea sahemu nyingi zaidi kwa mguu, akitafuta habari kuhusu ukweli mgumu wa ukuaji halisi wa harakati za kikristo katika sehemu nyingi za mbali na kuzifikria kwa kina zaidi kuliko Donald A. McGavran. Mmishenari wa kizazi cha tatu India, huko ndiko alikoanzia tu, ingawa hata katika miaka yake ya tisini aligusa chimbuko tena katika bara hilo kubwa lililokuwa katika moyo wake.*

*Lakini huko ndiko alikofanya kazi yake kubwa. Kuwaka kwake, kuguswa kwake kwa upana kulimchukua kila mahali na pasipo huruma isiyoepukwa, ilimsukuma kufikiri juu ya ulimwengu unaotokeza. Hii Shahada fupi maalumu, ni kama barua ya tahadhari kwa vijana wanaokuja kumtafuta, ikiwaonya juu ya kurahisisha zaidi. Katika waraka huu mfupi, kisha, karibu na kutoa kofi, anatoa kanuni saba ambazo zinaunganisha kuelewa zaidi imara kwa vigezo muhimu katika misheni ya Ukristo kuliko ambavyo wamishenari wangekusanya katika maisha yao yote.*

**Barua ya Donald McGavran:**

Katika miaka kumi na minane ya karne ya ishirini, lengo la wamishenari wakristo ilitakiwa kuwa kuhubiri injili na, kwa neema ya Mungu, kupanda kanisa kila mkato wa kibinadamu pasipo kuwa na kanisa tunaoweza kuita-"kanisa" au "kishada cha kanisa linalokua"? Kwa hatua, kwa fungu hili dogo mkato wa ubinadamu" nina maana kuweka miji, maendeleo, madaraja, kabila, mabonde, tambalale, au watu wachache. Nitaelezea kwamba lengo linalolenga mbali lililoendelea kulitunzwa halitakiwi liwe la kwanza, lakini mara zote linatakiwa liwe la pili. Lengo siyo mkusanyiko wa waliojikusanya pamoja kwa kila watu. Badala yake, lengo linalolenga umbali (kuweza kufanyika kwa kuendelea kwa mtazamo wa miaka au karne nyingi lilipokuwa halikufikiwa) linatakiwa liwe kishada cha kusanyiko linalokua katika kila mkato.

### NJIA YA MMOJA -KWA MMOJA

Tunapofikiria sentensi hapo juu, tunatakiwa tukumbuke kwamba ni rahisi kawaida kuanzisha kusanyiko moja kwa kundi la watu wapya ambao hawajawekwa kanisani. Mmishenari anafika. Yeye na familia yake wanaabudu jumapili. Wanakuwa wajumbe wa kwanza wa kusanyiko, anajifunza lugha na kuhubiri injili. Anaishi kama mkristo. Anawambia watu juu ya Kristo na kuwasaidia katika matatizo yao. Anauza vijitabu au injili, au kuvitoa bure. Kwa miaka, wachache waliokata shauri wanapatikana kutokana na hilo. Wakati mwingine wanakuja kwa dhumuni wazi na la kiroho; wakati mwingine kwa madhumuni tofauti tofauti. Lakini hapa na pale mwanamke, mwanaume, mvulana, msichana anaamua kumfata Yesu. Walioajiliwa wachache na wamishenari wanakuwa wakristo. Hawa wanaweza kuwa mafundi washi waliojiliwa kusimamisha jengo, wasaidizi nyumbani, mtu aliyechukuliwa kutunzwa au yatima. Historia ya Umishenari Africa imejaa makanisa yaliyoanza kwa kununua watumwa, kuwatorosha na kuwaajili kana kwamba hawangerudi nyumbani kwao. Kuchagua huko kungewafanya kumkubali Bwana. Miaka mia na hamsini iliyopita hii ilikuwa njia ya kawaida ya kuanzisha kanisa. Kwa uharamiaji wa kiutumwa, hakika, ilisimamishwa kutumika.

Kusanyiko moja lililoelezewa linaloibuka kwa njia tu kama iliyoelezewa ni karibu mara nyingi kanisa lililojengwa kwa wajumbe waliokusanywa wa vipingili mbalimbali vya jamii. Wengine wachanga, wengine vijana, mayatima, mtu aliyeokotwa, wasaidizi (boyi) na wa kutafuta kwa nguvu. Watafutwaji wote wanachunguzwa kuona kama kweli wanakusudia kumpokea Kristo. Kwa mda uliopo jengo la kanisa linasimamishwa na, hu!, “kanisa linaanza kwa watu hao.”Ni kanisa lililokusanya. Limefungwa kwa makundi ya watu wa kila aina kutoka katika eneo. Hakuna kipingili cha watu kinachosema, “kundi hilo la waabudu ni sisi.” Karibu wako sawa. Sivyo. Hakika kikabila ni muungano wa jamii tofauti.

Njia hii ya kawaida kabisa ya kuanza utaratibu wa uinjilisti ni njia ya polepole ya kufuasa watu wa duniani-tambua katika wingi, “watu wa duniani.” Ngoja tuchunguze kwa karibu kinachotokea hasa kusanyiko hili linapokusanyika. Kila aliyekata shauri, anapokuwa mkristo, anaonekana kama ukoo unaotuacha “sisi” na kuungana “nao.” Anaacha “miungu yetu”na kuabudu “miungui yao.” Matokeo yake, jamaa yake wanamlazimisha kuondoka. Wakati mwingine anaondolewa kwa nguvu, kutupwa nje ya nyumba na mji wote; mke wake anatishiwa. Mamia ya waliokata shauri wamewekewa sumu au kuuawa. Wakati mwingine, kuondolewa kunakuwa kudogo na mara chache kunakuwepo na kutokukubalika kwa hali ya juu. Watu wake wanamuona kama msaliti. Kanisa linalotokana na utaratibu huu linaonwa na watu wa eneo kama kusanyiko la wasaliti. Ni mkusanyiko wa waliokusanywa. Linaundwa na watu pekee walio wa, mmoja kwa mwingine, wametokana na jami tofauti kadhaa, koo au kabila.

Na sasa kama mtu yeyote, kutaka kuwa mkristo, amelazimishwa, au anatoka katika jamii yenye muundo wa hali ya juu wa mgawanyiko, ukristo unasababisha kuleta mtu na kupoteza familia. Familia, watu wake, majirani zake wa kabila hilo wanakuwa na hasira kali juu yake. Wanakuwa wanawake na wanaume wale wale ambao hawezi kuongea nao. “Siyo wetu,” wanamwambia. “Umetuacha, unawapenda kuliko unavyotupenda. Na sasa unaabudu miungu yao na siyo miungu yetu.” Matokeo yake, kusanyiko la waliokusanywa, lililoundwa kwa waliokata shauri kwa mtindo huu, wanakua taratibu sana. Kwa kweli, mtu anaweza kuthibitisha kwamba, mahali ambapo kusanyiko linakua katika mtindo huu, kukata shauri kwa kikundi kimoja (kikundi cha watu) mahali wanakotoka wanafanywa kuwa wagumu mara dufu. “Wakristo wamepotosha mmoja wa watu wetu,” waliobaki ndivyo watakavyosema, “Tunakwenda kuhakikisha kwamba hawatapotosha mmoja wetu tena.”

Mmoja kwa mwingine, inakuwa rahisi kukamilisha. Pengine 90 kati 100 ya wamishenari wanaokusudia upandaji kanisa wanapata kusanyiko la watu wa kukusanya tu. Ninataka kusisitiza kwamba. Pengine 90 kati ya 100 ya wamishenari wanaokusudia upandaji kanisa wanapata kusanyiko la kukusanywa tu. Wamishenari kama hao wanahubiri injili, wanamsema Yesu, wanauza vijitabu vya injili na kufanya uinjilisti kwa njia nyingi nyingine. Wanawakaribisha wanaouliza, lakini ni nani wanayempata? Wanapata mwanaume hapa na mwanamke pale na mtoto wa kiume hapa na wa kike pale, ambao kwa sababu tofauti wako tayari kuwa wakristo na kwa uvumilivu kustahimili kutokubaliwa kwao na watu wao kidogo au zaidi.

Kama tunaelewa jinsi makanisa yanavyokua na kutokua juu ya ardhi mpya, kwa watu ambao hawajagushwa na ambao hawajafikiwa, ni lazima tutambue kuwa utaratibu niliomaliza kuelezea unaonekana kutokuwa halisi kwa wamishenari wengi. “Kile”, watakachodai, kinaweza kuwa njia nzuri ya kuingia kwa watu wote wa eneo hilo ambao hawajafikiwa kuliko kuwapata wachache kutoka miongoni mwao? Badala ya kutokea kwa kanisa lililofungwa unaelezea, utaratibu kwa hakika unatupa wazo kab la kuingia kwenye kila jamii ambayo aliyekata shauri ametoka. Na hii inaonekana kwetu kuwa hali halisi.”

Hao wanaotoa hoja kwa mtindo huu wamejua ukuaji wa kanisa katika ardhi ya wakristo wengi, ambako wanaume na wanawake wanaomfata Kristo siyo waliotolewa katika jamii, hawadhaniwi kama wasaliti, lakini badala yake kama hao waliofanya kitu cha maana. Kwenye jamii ya namna hiyo kila aliyekata shauri anaweza kuwa mapito ambayo imani ya wakristo inamiminika kwa jamaa zao na marafiki. Kwa kigezo hicho kunaweza kukawa hakuna malumbano. Ndicho kigezo nilichosisitiza nilipokiita kitabu changu, Madaraja ya Mungu.

Lakini katika jamii iliyo na mkazo kimuundo, ambapo ukiristo unaangaliwa kama dini inayovamia, na mtu pekee anatengwa kwa kosa zito, pale kupata watu kutoka katika vipingili kadhaa tofauti vya jamii, mbali na kujenga madaja ya kila moja ya haya, inasimamisha vizuizi vigumu kuvuka.

**NJIA—YA HARAKATI ZA WATU**

**Kanuni Saba**

Na sasa ngoja tutofautishe njia nyingine ambazo Mungu anafuasa watu wa sayari ya dunia. Hesabu yangu siyo maelezo lakini ni kunena kwa kiasi kwa ukweli unaoonekana kirahisi. Unapoangalia ulimwenguni unaona kwamba, wakati wamishenari wengi wanafanikiwa katika kupanda kusanyiko la watu wa kukusanya tu kwa njia ya " mmoja kwa mmoja kutoka kwenye kikundi cha jamii", kukuza makanisa ya vikundi vya hapa na pale kunatokea kwa njia ya harakati-za watu. Kunatokea kwa hekima ya-kabila, au harakati za hekima ya daraja la watu kwa ajili ya Kristo. Hii kwa namna nyingi ni njia bora. Ili kuweza kuitumia hii kwa ufanisi, Wamishenari wanatakiwa watumie kanuni saba.

**Kanuni ya Kwanza**

Kwanza, wanatakiwa wawe wazi juu ya lengo lao. Lengo siyo kanisa moja pekee la waliokusanywa kwenye mji au mkoa. Wanaweza kupata hilo tu, lakini kamwe hilo linatakiwa liwe ndiyo lengo lao. Hicho lazima kiwe kishada kinachokua, kusanyiko la wenyeji, kila mjumbe wao anabakia kuwa na mawasiliano ya karibu na ukoo wake. Kishada hiki kinakua vizuri zaidi kama kina watu wa aina moja, daraja, kabila moja, kipengele cha jamii moja. Kwa mfano, kama ulikuwa unamwinjilisha dereva wa teksi wa Taipei, kisha lengo lako halitakuwa tu kuwapata baadhi ya madereva wa teksi, walimu wa chuo kikuu, baadhi ya wakulima, na baadhi ya wavuvi, lakini kuanzisha makanisa yaliyo na namba kubwa ya madereva wa teksi, wake zao na watoto na mafundi wa magari. Unapowapata wakata shauri wa jamii ya namna hiyo, kusanyiko linakuwa la kawaida, lililojengwa –kwa mshikamano wa jamii. Kila mmoja anajisikia yuko nyumbani. Ndiyo, lengo lazima liwe wazi.

**Kanuni ya Pili**

Kanuni ya pili ni kwamba kiongozi wa taifa, au mmishenari na wasaidizi wake, lazima wakazanie watu wa aina moja. Kama unataka kuanzisha kishada cha kusanyiko linalokua mwa India, kisha uatahitaji kuweka wamishenari wako wengi na wasaidizi wao ili kwamba waweze kufanya kazi miongoni mwa Waneira. Wanatakiwa watangaze injili kwa Waneira na kusema wazi kwao, "tunatumaini kwamba katika watu wa aina, hivi karibuni kutakuwa na maelfu ya wafuasi wa Yesu Kristo, ambao watabakia imara kwa jumuia ya Waneira." Hivyo hawataabudu miungu yao ya zamani; lakini wengi wa Waneira-hawaabudu miungu yao ya zamani-Waneira wengi ni wajamaa, wanadhihaki miungu yao ya zamani.

Waneira ambao Mungu anawaita, waliochagua kuamini katika Kristo, watawapenda majirani zao zaidi kuliko walivyofanya zamani, na kutembea katika nuru. Wataokolewa na kuwa watu wazuri. Wataendelea kuwa Waneira, wakati huohuo wamekuwa wakristo. Kwa kurudia, kazania kundi moja la watu. Kama una wamishenari watatu, mmoja asiinjilishe kundi hili, na mwingine lile, na wa tatu kilometa 200 mbali kuinjilisha wengine bado. Hii ni njia ya uhakika ya kuhakikisha kwamba kila kanisa lililoanzishwa litakuwa dogo, lisilokua, kanisa la mmoja-kwa mmoja. Mapana ya jamii ya sehemu hizo yatafanya kazi kwa bidii dhidi ya mlipuko wa harakati za watu zinazokua kwa ajili ya Kristo.

**Kanuni ya Tatu**

Kanuni ya tatu ni kuwatia moyo waliokata shauri kubakia wakiwa wakweli kwa watu wao katika mambo mengi. Wanatakiwa kuendelea kula chakaula ambacho watu wao wanakula. Wanatakiwa wasiseme, "watu wangu ni wala chakula aina ya mazao, lakini nimekuwa mkristo,nitakuwa nakula nyama." Baada ya kuwa wamekuwa wakristo wanatakiwa wawe wala vyakula vya mazao zaidi kuliko walivyokuwa kabla. Katika hali ya uvaaji, wanatakiwa waendelee kuonekana sawaswa na jamaa. Katika swala la kuoana, watu wengi wanapenda kuoa watu wao , wanasisitiza kwamba "watu wetu wanaoe watu wetu tu." Wanaangalia kwa kutopenda kwa uoaji wao wa watu wengine. Na hata hivyo wakristo wanapokuja kwa mmoja kwa mwingine hawawezi kuoa watu wao wenyewe. Hakuna mmoja wao aliyekwisha kuwa mkristo. Wakati wachache waliojitoa kuwa wakristo, unapofika mda kwao au watoto wao kuoa, wanatakiwa wachukue waume au wake kutoka kwenye kundi lingine la watu. Kwa hiyo, jamaa yao inawaangalia na kusema, "ndiyo, geuka kuwa mkristo na kufanya watoto wako kuwa chotara. Umetuacha na umeungana nao.

Wakata shauri wote wanatakiwa kutiwa moyo kuchukulia kwa ukunjufu kutengwa, kukandamizwa, na kuteshwa ambako inaonekana watapata kutoka kwa watu wao. Wakati mtu yeyote anapokuwa mfuasi wa njia mpya ya maisha, anaelekea kukutana na kutopendwa kutoka kwa wapendwa wake. Inawezekana ni kwa kiasi kidogo; inawezekana ikawa kwa ukali sana. Anatakiwa achukulie kutopendwa huko kwa uvumilivu. Anatakiwa aseme katika kila tukio:

*"Ni kijana mzuri kuliko nilivyokuwa mwanzo; Ni baba mzuri kuliko nilivyokuwa kabla; Ni mme mzuri kuliko nilivyokuwa kabla; na ninakupenda zaidi kuliko nilivokuwa nikifanya kabla. Unaweza ukanichukia, lakini sitakuchukia. Unaweza ukanitenga lakini sitakutenga. Unaweza ukanifukuza nje ya nyumba ya mababu na mabibi; lakini nitaishi kwenye sebule yake. Au, nitapata nyumba mtaani. Bado ni mmoja wenu, ni mmoja wenu zaidi kuliko nilivyokuwa kabla."*

Watie moyo waliokata shauri kubakia wakamilifu kila mmoja kwa watu wake katika mambo mengi.Tafadhali tambua kwamba neno "zaidi." Hawawezi kubakia wamoja na watu wao katika kuabudu sanamu au ulevi au dhambi wazi. Kama wanatoka katika kundi la jamii inayopata kipato chake kwa kuiba, lazima "wasiibe tena." Lakini, katika mambo mengi (jinsi wanavyoongea, jinsi wanavyovaa, jinsi wanavyokula, mahali wanapokwenda, aina za nyumba wanazoishi), wanaweza kufanana na watu wao zaidi, na kutarajia kufanya juhudi kufanya hivyo.

**Kanunu ya Nne**

Kanuni ya nne ni kujaribu kuwafanya kikundi kuamua kumfata Kristo. Kama mtu mmoja tu anaamua kumfata Yesu, usimbatize mara moja. Mwambie, "wewe na mimi tutafanya kazi pamoja wengine watano au kumi au, Mungu akipenda watu hamsini kumkubari Yesu Kristo kama mwokozi wao ili kwamba unapokuwa umebatizwa , unabatizwa nao." Kutengwa kuna Mafanikio zaidi dhidi ya mtu mmoja. Lakini kutengwa ni dhaifu hasa kunapofanyika dhidi ya jozi ya kikundi cha watu. Na kunapofanyika kwa mamia ya watu kiutendaji hakuna msukumo kabisa.

**Kanuni ya Tano**

Kanuni ya tano ni hii: Dhumuni la hesabu ya vikundi vilivyopatikana vya watu kugeuka kuwa wakristo katika mtiririko-usiolingana kwa miaka. Moja ya kosa la kawaida lililofanywa na wamishenari, wa mashariki na hata wa magharibi, ulimwenguni kote ni kwamba wachache wanageuka kuwa wakristo pengine 100, 200 au hata 1,000-wamishenari wanatumia mda wao wote kuwafundisha wao. Wanataka kuwafanya wao kuwa wakristo wazuri, na wanajiambia "kama watu hawa wanakuwa wakristo wazuri kisha injili itaenea." Mpaka hapo miaka mingi wanayokazania kusanyiko la watu wachache. Kwa mda, miaka kumi au ishirini baadaye, ndipo wanaanza kuinjilisha nje ya kikundi, watu waliobaki hawataki tena kuwa wakristo. Hilo limetokea na kutokea tena. "Lakini," unasema, "hii si ndiyo njia hakika ya kuwapata wakristo masikini wasiojua juu ya Biblia? Kama tunafata kanuni hiyo mara tutaweza kuwa na wakristo 'wachanga'. Mara tutakuwa na jamuia pengine ya watu elfu tano ya wakristo wanaoelewa kidogo."

Ndiyo, hilo kwa hakika ni hatari. Katika hatua hii ni lazima tujifunze kwa uzito kutoka Agano Jipya, tukikumbuka maelekezo kwa ufupi ya wiki mbili au miezi aliyotoa Paulo kwenye makanisa yake mapya, lazima tumutumaini Roho Mtakatifu, na kuamini kwamba Mungu amewaita watu hao nje ya giza kwenda kwenye nuru yake ya ajabu. Kama ilivyo kati ya waovu wawili, kuwapatia mafundisho madogo sana ya kikristo na kuwafanya kuwa jumuia iliyofungiwa ambayo haiwezi kuwafikia watu wake, baadaye kutakuwa na hatari kubwa. Tunatakiwa sasa tuwaruhusu waliokata shauri wapya kuwa waliofunguliwa. Ni lazima tuendelee kuhakikisha kuwa mtiririko wa wastani wa waliokata shauri wapya wanatokea kwenye kundi la kusanyiko la aina moja linaloendelea kukua wakati wote.

**Kanuni ya Sita**

Sasa kanuni ya sita ni hii: Waliokata shauri, watano au elefu tano, wanapaswa au angalau kujisikia:
"Sisi wakristo tulioendelea ni walinzi wa watu wetu, wa kipande cha jamii yetu. Tunaionyeha jamaa yetu na majirani njia nzuri ya maisha. Njia tunayotangulia nayo ni nzuri kwetu tuliogeuka kuwa wakristo na itakuwa nzuri kwenu maelfu ambao hamjaamini bado. Tafadhali tuangalie siyo kama wasaliti kwa hali yoyote. Ni wana wazuri, makaka, na wake, watu bora wa kabila na daraja la watu wa aina moja, watu wazuri wa muungano wetu wa kazi kuliko tulivyowahi kuwa kabla. Tunaonyeha njia ambazo, wakati tukibakia kuwa wakamilifu katika vitengo vyetu vya jamii yetu, wote tunaweza kuwa na maisha mazuri. Tafadhali tuangalie kama waanzilishi wa watu wetu wa tunaoingia katika nchi ya ahadi."

**Kanuni ya saba**

Kanuni ya saba ninayokazia ni hii: Bila kukoma sisitiza juu ya undugu. Kwa wakristo hakuna Myahudi, hakuna Myunani, hakuna kifungo, hakuna uhuru, hakuna Mubarnaba, hakuna Musinthia. Wote ni kitu kimoja ndani ya Kristo Yesu, lakini, wakati huo huo, ngoja tukumbuke kwamba Paulo hakushambulia wizara zote ambazo hazikuwa kamili. Kwa mfano, hakufanya kuuondoa utumwa. Paulo alisema, "Uwe mtumwa mwema, "Aliwaambia wamiliki watumwa, uwe mtwala mzuri."

Paulo alisema pia katika fungu hilo linalojulikana kusisitiza umoja, “Hakuna mwanaume wala mwanamke.” Walakini wakristo katika shule zao za bodi na mahali wanapoishi yatima, wavulana na wasichana wanaendelea kulala katika vyumba tofauti!! Katika Kristo, hakuna tofauti ya jinsia. Wavulana na wasichana wanapendeza sawa mbele za Mungu. Wanaume kutoka kwenye kabila hili, na wanaume kutoka kabila lile ni wazuri sawa mbele za Mungu. Wote ni wenye dhambi sawa tuliookolewa kwa neema. Mambo haya ni kweli lakini, wakati huo huo, kuna mambo madogo madogo fulani ya kijamii ambayo wakristo wakati huu wanaweza kuchunguza.

Tunapoendelea kukazia undugu, Ngoja tuwe na uhakika kuwa njia ya mafanikio ya kupata undugu ni kuongeza idadi ya wanaume na wanawake inayokua wakati wote kutoka kila rangi, kila kabila, kila kundi la jamii kwenye uhusiano wa utii kwa Kristo. Tunapogawa wakristo katika kila kipande cha jamii, uwezekano wa undugu wa kweli, usawa, wema na haki utaongezeka isivyokawaida. Kwa hakika, njia nzuri ya kupata usawa, pengine njia pekee kupata haki, ni kuwa na idadi kubwa katika kila kipande cha jamii kujitoa kwa Kristo.

**SULUHU**

Tunapofanya kazi ya kuendeleza harakati za kikristo kwa watu wote, ngoja tusifanye makosa ya kuamini kwamba “mmoja kwa mmoja kutoka katika jamii kwenda kanisani” ni njia mbaya. Roho moja ya thamani iliyotayari kuvumilia kutengwa kwa hali ya juu ili kuwa mfuasi wa Yesu-ni roho moja yenye thamani inayojitoa pekee-ni njia ambayo Mungu amebariki na anabariki katika wokovu wa watu. Lakini ni njia ya polepole. Na ni njia ambayo mara kwa mara inayofungua watu wa aliyekata shauri kusikia zaidi injili.

Mara nyingine mmoja kwa mwingine ni njia pekee inayowezekana. Inapoweza, ngoja tumshukuru Mungu na kuishi na upungufu wake. Ngoja tuhoji wakristo wote hao wa ajabu wanaokuja kwa kubeba mateso na kukandamizwa, kuombea wapendwa wao na kufanya kazi bila kuacha ili kwamba watu wao wengi waamini na kuokoka.

Mmoja kwa mmoja ni njia Mungu anayoibariki kuongeza kanisa lake. Harakati za watu ni njia nyingine. Kuendelea kukua kwa kanisa kwa kiwango cha juu kwenye ardhi mpya isiyokuwa ya dini ya wakristo mara nyingi imetokana na harakati za watu, na kamwe siyo mmoja kwa mwingine. Karibu ni sawa kwamba mmoja kwa mwingine kwa watu ni njia ya kawaida ya kuanzia. Katika kitabu, Madaraja ya Mungu, amabacho Mungu alitumia kuvurumisha harakati za kukua kwa kanisa, nimetumia tabasamu, ninasema pale kwamba misheni inaanza kumtangaza Kristo kwenye jangwa-kama tambalale. Pale maisha ni magumu, idadi ya wakristo inaendelea kubakia ndogo. Kuwepo kwa wamishenari wengi kunahitajika. Lakini hapa na pale, wamishenari au waliokata shauri wanapata njia za kuvunja tambalale ngumu kama yabisi na kuendelea kwenye milima ya kijani kibichi. Huko idadi kubwa ya watu wanaishi, kule makanisa halisi yanaweza kupatikana; huko kanisa linakua kwa nguvu; hiyo ni ardhi ya harakati za watu.

Ninaamuru kutabasamu hiyo kwako. Ngoja tukubali Mungu anachotoa. Kama ni mmoja kwa mmoja, ngoja tukubali hicho na kuwaongoza hao wanaoamini katika Yesu kumtumaini kikamilifu. Lakini ngoja mara nyingi tuombe kwamba, baada ya mwanzo huo, tunaweza kuendelea kwenye ardhi ya juu, kwenye milima yenye malisho mabichi zaidi, kwenye ardhi yenye rutuba zaidi ambapo makundi makubwa ya wanaume na wanawake, wote wa jamii moja, wanageuka kuwa wakristo na hivyo kufungua mlango wa harakati za kuendelezwa ukristo kwa watu wote duniani. Lengo letu linatakiwa liwe harakati za kuendelezwa ukristo kwa kila kundi la jamii. Pale nguvu ya mshikamano wa jamii unasogeza mbele injili na kuongoza umati kutoka gizani kwenye maisha ya ajabu. Ngoja tuwe na uhakika kwamba tunafanya kwa kutumia njia yenye ufanisi zaidi.

UINJILISTI
*ZIADA*
5B

# Kujibu Vipingamizi Vya Kawaida

## TUMIA MAANDIKO KAMA MAMLAKA YAKO

Watu tunaokutana nao wanatoka katika maisha tofauti ya nyuma. Swali la unyoofu wanalouliza lina majibu. Unaweza kuwasaidia kugundua majibu kwenye maandiko kwa kukua wewe mwenyewe katika uzoefu wa kile Biblia inachosema kuhusu maswali haya yanayoulizwa- mara kwa mara.

**"Kama Mungu ana nguvu sana na mwenye upendo, kwa nini anaruhusu mabaya yote ulimwenguni? Kwa nini hayazuii?"**

Biblia inasema kwamba Mungu aliumba ulimwengu kamili, na mabaya ni matokeo ya kutotii kwa Shetani na mwanadamu na kumuasi yeye. Dhambi, siyo Mungu, inasababisha mabaya na mateso. Kwa hakika, Mungu amefanya kila kitu kushinda tatizo la mabaya kwa kumtoa Yesu Kristo kuteseka na kufa kwa ajili ya dhambi zetu. Lakini Mungu anaheshimu uhuru wa uchaguzi wetu. Tunaweza kuchagua kumpokea Kristo na maisha mapya anayotoa au kuendelea katika njia ya kutotii ambayo inazaa maovu.

***Kariri Warumi 1:28***

**"Siyo kiburi kwa wakristo kudai kuwa Yesu Kristo ni njia pekee ya kwenda mbinguni? Vipi juu ya wanaofata kwa unyoofu imani zingine?"**

Swala siyo unyoofu, isipokuwa ukweli. Mafundisho yanayopingana hayawezi yote yakawa sawa. Hakuna kiasi cha unyoofu kinachoweza kusababisha usio ukweli kuwa kweli. Mtu anaweza kuwa myoofu kwa uongo. Hata siyo mawazo ya wakristo yaliyo muhimu. Kilicho muhimu ni kile Yesu kristo alichodai.

***Kariri Yohana 14:6***

**"Vipi juu ya hao ambao hawakuwahi kusikia habari za Kristo? Wataadhibiwa jehanamu?"**

Yesu aliweka wazi kwamba hakuna hata mmoja atakayeingia mbinguni isipokuwa kwa kupitia yeye. Lakini Warumi 2:12-15 inasema kwamba hakuna mmoja atakayehukumiwa kwa kutokumfahamu yeye. Atahukumiwa kwa kile alichokijua na kufanya kulingana na kweli au makosa. Ukweli ni kwamba hakuna hata mmoja ulimwenguni ambaye ametunza kiwango cha maadili yake kikamilifu, kusema hakuna kiwango cha Mungu, ambacho hawezi au anaweza kuwa anafahamu.

***Kariri Warumi 1:19,20***

**"Biblia siyo tu mkusanyiko wa masimulizi ya uongo ya kidini yaliyoandikwa na mwanadamu? Si imejaa makosa?"**

Hao wanaojifunza Biblia wanajua mashitaka haya ni ya uongo na hafifu, yanayoonyesha kukosekana kwa uchunguzi binafsi wa maandiko. Waandishi wa Biblia wanadai ni uvuvio katika kupokea mafunuo kutoka kwa Mungu na kuongozwa na Roho Mtakatifu katika kuandika matukio yaliyokuwa na maana kwa ujumbe wa Mungu kwa watu. Jozi za utabiri zilizofanyika mamia ya miaka kabla, yametimizwa kwa undani wa dakika. Unabii mwingine unasubiri kutimizwa. Utabili kama huo unaweza ukatokana na Mungu tu.

***Kariri 2Petro 1:16***

**"Kama Yesu ni jibu kweli, kwa nini wakristo wengi ni wanafiki? Kwa nini hawafanyi wanachofundisha?"**

Siyo kila anayedai kuwa mkristo ndiye. Isipokuwa hao waliompokea Yesu Kristo kibinafsi kama Bwana na mwokozi wamezaliwa upya. Kila kikundi au shirika lina wajumbe wasio wanyoofu. Hatutupi chenji yote kutoka mifukoni mwetu kwa sababu tu senti moja inatokea kujigeuza. Hata

mkristo wa kweli hadai kuwa kamili. Anatambua hitaji lake la kusaidiwa kwa kila mara kutoka kwa Kristo. Kama mwenye mashaka anaangalia ukamilifu ataupata tu ndani ya Kristo. Kama anaangalia hali halisi ataipata kwa maelfu ya wakristo wanyoofu wanaotembea na Kristo.

***Kariri Warumi 14:12***

**"Kwa nini wasomi wengi wanakataa madai ya Kristo? Hii haihakikishi kwamba imani katika Kristo haipatani na mafunzo ya juu?"**

Imani ndani ya Yesu na elimu siyo havipata ni. Wengi wa wanasayansi wakuu, waliopita na waliopo, walikuwa bado ni waumini waaminifu katika Yesu Kristo. Swala Yesu analotoa ni la maadili, siyo la kisomi. Kwa hiyo, mtu aliyeelimika anakataa injili kwa sababu sawa na wanayotoa wasiosoma. Sababu ya wote ni kutokuwa radhi kujitoa kwenye mamlaka ya Kristo.

***Kariri 1Wakorintho 1:21***

## VYANZO

Navigators. *Personal Evangelism Scripture Memory Coursa*, Colorado Springs, CO: NavPress, n.d.

UINJILISTI

SOMO LA 6,7

# Utaratibu wa Kukata Shauri

## KUWASAIDIA WATU KUSOGEA KUELEKEA IMANI NDANI YA KRISTO

☞ **Kusudi la Somo**

Kusudi la somo hili ni ni kujadili utaratibu wa mabadiliko amabayo tunatakiwa tutarajie na tunayoshiriki.

☞ **Wazo Kuu**

- Ni lazima tuanze kushirikisha Kristo siyo tu mahali tunapojisikia huru, lakini watazamaji wetu walipo na uhuru.
- Kuna injili moja tu, lakini tunaweza kutumia njia nyingi kuishirikisha.

☞ **Matokeo Yanayotarajiwa**

Wakati yaliyomo katika somo hili yanapoeleweka, kila mshiriki anatakiwa:

- Kuwa mzoefu wa serikali ya mahitaji ya Maslow
- Kuwa mzoefu wa utaratibu wa harakati za mtu kuelekea imani ndani na kujitoa kwa Kristo.
- Geuka kuwa mzoefu wa ngazi nne za uinjilisti na anza kutambua watu tunaowahudumia katika ngazi hizi.
- Elewa kuwa ni lazima tuanze kushirikisha Kristo, siyo tu pale tunapojisikia uhuru, lakini watazamaji wetu walipo na uhuru, katika kuwasogeza watu kwenye imani.

☞ **Ziada**

6A Sura ya Mtu Unayetaka Kuinjilisha

6B Kanuni Tatu za Mkakati wa Uinjilisti

6C Kuchunguza Njia ya Yesu Kwa Binafsi

☞ **Matokeo Yanayotarajiwa**

Hili ni somo la masaa-mawili. Kabla hujaanza maelekezo yako, wafunzwa wafanye marudio ya baadhi ya masomo waliyojifunza katika mafunzo ya mifano ya udongo, Mathayo 13:3-9; 18-23.

Somo hili linahusu mawazo yaliyotolewa katika somo la vikundi kiini la 4, “Uinjilisti wa Kikundi Kiini.” Kama wafunzwa hawajalipitia somo hili, inashauriwa kwamba mkufunzi afanye marudio kwanza ya sehemu ya kwanza ya somo hili, “Aina mbili za Wasioamini”, kabla ya kulifundisha somo hili.

### UTANGULIZI


Katika mafunzo yetu ya mpanzi katika Mathayo 13, tumeona kwamba hali ya ardhi ambapo mbegu nzuri iliangukia ilionyesha matokeo ya mavuno. Mbegu iliyoleta mavuno mazuri ilikuwa imepandwa kwenye udongo mzuri. Yesu alisema hasa, “Yule aliyepokea mbegu iliyoangukia kwenye udongo mzuri ni mtu anayesikia neno na kulielewa” (V.23). Kabla ya kuanza uinjilisti wetu tunahitaji kuchunguza kwa uangalifu aina ya udongo ambapo mbegu itapandwa. Hii ni kwamba, tunahitaji kuangalia kwa uangalifu watu tunaotaka kuinjilisha kujaribu kuona ni nini tunachoweza kufanya kuwasaidia waelewe injili kwa uwazi. (Tambua katika mfano kwamba watu walikuwa na mioyo migumu kwa sababu hawakuelewa ujumbe.) Katika sehemu hii tunataka kuangalia katika baadhi ya

zana za kuchunguzia mahitaji ya watu na kutathimini hali zao kumwelekea Mungu kama hatua ya kwanza katika kuwasaidia kuelewa na kupokea habari njema.
Unaweza kuuliza, "kwa nini tunahitaji kujua mahitaji yote ya watu wakati tumeshajua *hitaji* lao kubwa ni kwa neema ya Mungu inayookoa?" Jibu ni rahisi. Inatusaidia "kuwakuta walipo." Tunapoelewa mahitaji ya msingi ya watu, tunweza kuonyesha upendo wa Mungu zaidi kwao kwa kuwasaidia kutimiza mahitaji hayo.

## I. KUCHUNGUZA MAHITAJI YA WATU


Abrahamu Maslow mtu achunguzaye mambo ya roho, akili na moyo wa binadamu alianzisha kimulimuli cha mahitaji ya kawaida ya mwanadamu. Mwisho aliofikia ilikuwa kwamba mtu hatatiwa changamoto kupata kiwango cha juu cha hitaji mpaka mahitaji ya chini yawe yametimizwa. Kwa mfano, kama mtu ana njaa, hitaji lake la msingi itakuwa kupata chakula, siyo kupata sifa, ambalo ni hitaji la juu. Kielelezo 6.1 ni ufupisho wa utawala wa mahitaji ya mwanadamu wa Maslow, ambao unaonyesha mahitaji mbalimbali pamoja na matatizo yanayotokana na kushindwa kutimiza mahitaji hayo.

**Kielelezo 6.1 Mahitaji ya Mwanadamu: Yaliyorithiwa Kutoka kwa Utawala wa Mahitaji ya Mwanadamu wa Maslow.**




Baada ya kufikiria kwa uangalifu mahitaji ya mwanadamu na matokeo ya kushindwa kutimiza mahitaji hayo (Kielelezo 6.1), angalia kielelezo 6.2 na angalia njia ambazo Mungu alizotoa kwa ajili ya mahitaji yote ya mwanadamu.

**Kilelezo 6.2 Matoleo ya Mungu Kwa Mahitaji ya Mwanadamu**




Yesu ni jibu kwa mahitaji ya kila mmoja. Lakini njia anazotolea mahitaji hayo kutimizwa ni kwa mwili wake, KANISA. Kama hatuelewi mahitaji ya mtu, hatutaweza kujua jinsi ya kusaidia kutimiza mahitaji hayo. Ni wapi katika jedwali hili utaweka watu unaowainjilisha?

## II. KUTATHIMINI WAPI WATU WALIPO KATIKA KUELEWA INJILI

Kuelewa mahitaji ya mtu ni hatua ya kwanza. Ili uinjilisti wetu kuwa wa mafanikio, ni lazima pia tujue wapi mtu alipo katika kumwelewa Mungu: ni mtu wa kidunia ambaye hata haamini kama kuna Mungu? Yuko anamtafuta Mungu? Amemkasirikia Mungu, n.k.?

Somo la 4 la Kikundi Kiini, "Uinjilisti wa Kikundi Kiini", linajadili makundi mawili ya wasioamini: "Aina ya A" na Aia ya B." Aina ya A ya wasioamini wanapenda kwa kiasi fulani habari za Mungu, Biblia, na wako wazi kwa maelekezo ya Mungu kwa ajili ya maisha yao. Aina B ya wasioamini ni hao wasio na haja na Biblia, ambao hawawezi kwenda kanisani, pengine hata hawaamini katika Mungu, na wanaweza wakawa wanapinga au hata kuwa adui wa ujumbe wa injili wazi wazi.

Kielelezo 6.3 kinaonyesha baadhi ya hatua mtu anazochukua kumwelekea Mungu. Soma kielelezo hiki kwa uangalifu. Baadhi ya aina B ya wasioamini wanaweza pengine wakawa hawako kwenye kielelezo hiki, wakati wengine wangekuwa katika moja ya ngazi ya hatua ya "Uvunaji" tu. Aina A ya wasioamini, kwa jinsi hiyo, wanaweza kuwa katika moja ya ngazi kwenye hatua za mwanzo wa "Uvunaji."

Jedwali hili linaweza kutumika kukusaidia kuona hali ya mtu ya kiroho, endapo ni Aina A au B ya wasioamini. Fikiria juu ya watu ambao unawaombea, kutumia mda pamoja nao, na kuwashuhudia. Unaweza kuwaweka wapi katika jedwali hili?

**Kielelezo 6.3 Hatua Kuelekea Kwenye Imani**

| | HATUA ZA KUITIKIA |
|---|---|
| MAANDALIZI | -12 KWENDA NJIA YAKE |
| | -11 UFAHAMU WA KUWEPO KWA MJUMBE |
| | -10 NIA YA MOYO MWEUPE KWA MJUMBE |
| | -9 UFAHAMU WA TOFAUTI KATIKA MAISHA YA MJUMBE |
| | -8 MWANZO WA KUFAHAMU KUHUSIANA KWA BIBLIA NA MAISHA |
| KUPANDA | -7 NIA YA MOYO MWEUPE KUHUSU BIBLIA |
| | -6 UFAHAMU WA MISINGI YA INJILI |
| | -5 KUELEWA MAANA YA INJILI NA MATOKE YAKE |
| | -4 NIA YA MOYO MWEUPE KWENYE INJILI |
| UVUNAJI | -3 UTAMBUZI WA HITAJI LA MTU |
| | -2 UAMZI WA KUTENDA |
| | -1 KUTUBU NA IMANI |
| | 0 KIUMBE KIPYA NDANI YA YESU! |
| UKUSANYIKAJI | +1 HAKIKISHO LA IMANI NA UIMARISHAJI |
| | +2 KUSHIRIKISHA KATIKA UANGALIZI WA JUMUIA YA WAKRISTO |
| | +3 UKUZAJI! UHAMASISHAJI KUKOMAA KATIKA KUFANANA NA YESU |
| | +4 KWENDA! UHAMASISHAJI "KUISHI KWA USHUHUDA" KWA WENGINE |

Unapokuwa mzoefu wa mchoro huu, jiulize mwenyewe maswali yafuatayo :

- Ni wapi watu ninaofanya nao kazi wanapofaa katika mchoro huu?
- Ni katika hatua gani vifaa na zana zilizopo kwa ajili ya uinjilisti zinapoweza kutumika zaidi?
- Ni katika hatua zipi kuna ukosefu wa hali ya juu wa vifaa vya kutumia kwa watu ninaofanya nao kazi?

## III. KUELEWA AWAMU NNE ZA SHUGHULI ZINAZOHUSIANA NA KUWALETA WATU KWA YESU

Tumeona katika mfano wa mpanzi katika Mathayo 13 kwamba Yesu alitumia kielelezo cha mpanzi kuelezea ukweli kuhusu mavuno, hasa juu ya hatua ya upandaji na uvunaji. Ingawa hapa Yesu hakugusia shughuli zingine maalumu zilizohusika katika utaratibu kwa ujumla, wazo la kulima liko kotekote kwenye maandiko (Mt 9:37; Lk 10:2; Yoh 4:35; 1Kor 3:5-0; Gal 6:9;). Tunapofikiria yote yanayohusika katika kuona mtu anakuja kwa Kristo, inaweza kusaidia kugawanya kazi ya uinjilisti katika awamu nne kama ilivyoonyeshwa katika kielelezo 6.4.

**Kielelezo 6.4 Awamu Nne za Shughuli Zinazohusiana na kuwaleta Watu Kwa Kristo**

| Shughuli | Uandaaji | Upandaji | Uvunaji | Ukusanyaji |
|---|---|---|---|---|
| **Maelezo** | Inazungumza kwenye moyo kupitia uhusiano wa kujaliana | Inazungumza kwenye akili kupitia maamzi na mawasiliano | Inazungumza kwenye utayari, ikihitaji majibu ya imani kwenye majadiliano | Inazungumza kwa mtu kamili kuhusu ukuaji binafsi ndani ya Kristo |
| **Msisitizo** | Kuwepo kwa Mjumbe | Kutangaza ukweli wa injili | Kushawishika kwenye uamzi | Kuhusika na kushiriki katika ushirika wa mtaa |
| **Mifano ya Kibiblia** | Yohana 3 & Yohana 4 | Yohana 4 na Matendo 8 | Yohana 4 na Matendo 16 | Matendo 2:40-47 na Matendo 8 |
| **Hatua Kuelekea Kwenye Imani** | -12 mpaka -8 | -7 mpaka -4 | -3 mpaka 0 | +1 mpaka +4 |

## IV. KUONYESHA MKAKATI WA UINJILISTI

Yafuatayo ni maelezo jinsi unavyoweza kuonyesha mkakati wako wa uinjilisti kutokana na habari ulizojifunza hapo juu. Karatasi ya mazoezi katika Ziada 6A ni maelekezo yanayosaidia ambayo unaweza kutumia kuanzisha sura za watu ambao unataka kuinjilisha.

### A. Mahitaji Msingi

Maria ni mwanamke kijana kutoka kwenye familia ambayo wazazi wameachana. Mtoto pekee, alikataliwa na baba yake. Mama yake alikuwa na kazi nyingi kuweza kutoshereza familia na kuwa na mda kidogo sana wa kukaa na binti yake. Yeye na mama yake waliishi kwenye mji mbali na familia yao pana. Sasa kama mtu mzima anajisikia kutopendwa. Unachunguza hitaji lake la kupendwa/upendo. (Tazama Utawala wa Maslow wa Mahitaji Kielelezo 6.1).

### B. Kupokelewa kwa Injili

Katika hatua zake kwenye imani (angalia Kielelezo 6.3), Maria yuko kwenye -12. Maria hakuwa na dini alipokuwa analelewa, hakuwa na mawasiliano na wakristo. Alikuwa na wazo lisilofahamika vizuri kwamba kanisa linadai kuwa sehemu inayomfaa, ingawa hajui chochote kuhusu madai ya Yesu Kristo.

### C. Tathimini ya Mkakati Wako wa Uinjilisti

Maria hayuko tayari katika kupanda mbegu. Kwako wewe kumpatia vijitabu vya injili au pengine Biblia isingefaa kuwa ya ufanisi. Anachohitaji ni kuonyeshwa upendo wa Kristo kwa uvugu vugu, kukubali anga, hatua ya maandalizi katika kielelezo 6.4. Unaamua kumualika kwenye kikundi kidogo ambapo kuna kujaliana kwa aina nyingi kwa mmoja kwa mwingine. Kisha unaweza kumhusisha katika mafunzo ya kiuinjilisti.

Unapouangalia mkakati wako wa kuwafikia watu hao ambao Mungu ameshaweka kwenye moyo wako, unaweza pia ukaanza kuomba kwa ajili ya kuwafikia watu ambao, kama wamefikiwa kwa injili, wanaweza kuwa mkakati katika kufikia eneo lako unalolenga kwa injili (tazama Ziada 6B).

## MASWALI YA KUTAFAKARI, MARUDIO NA MATUMIZI

Unajaribu kumkabili kila mtu kwa kutumia njia sawa ya uinjilisti au zana? Ni kwa jinsi gani unaweza kuongeza uwezo wako wa kufanya kazi?

## UTEKELEZAJI WA AZIMIO

- Fanyia kazi karatasi ya Kazoezi katika Ziada 6C kusaidia kuelewa kwako kutoka kwenye maandiko kwamba watu wanatofautiana mahitaji na lazima yakabiliwe kwa njia zinazotofautiana. Karatasi hii ya mazoezi inaangalia katika matukio tofauti kwenye Agano Jipya ambapo Yesu alikuwa anajidhihirisha mwenyewe kwa watu wa aina nyingi.
- Kwa kutumia karatasi ya mazoezi katika Ziada 6A kama kiongozi, fanya kazi na watu wengine wawili katika maombi yako ya utatu. Orodhesha majina ya watu wote mnaowaombea, chunguza ni wapi walipo kwenye mzani wa mahitaji, tathimini wapi walipo kwenye kuelekea kwa Kristo (Hatua Kuelekea Imani). Onyesha unachoweza kufanya kuwafikia kwa ufanisi kwa injili.
- Jifunze Ziada 6B, kanuni Tatu za Mkakati wa Uinjilisti. Ni akina nani walio mashuhuri “walinda mlango” katika eneo lako unalolenga? Ni nini unachoweza kufanya kuwafikia watu hawa kwa injili?

UINJILISTI
*ZIADA*

6A

# Sura ya Mtu Unayetaka Kuinjilisha

## KARATASI YA MAZOEZI

Habari muhimi tulizojifunza kwenye mfano wa kufanyia mafunzo kuhusu Mary zinaweza kufupishwa kwa msaada wa jedwali hapo chini. Angalia kwa karibu katika mfano huu, na kisha tumia mifano tupu kwenye ukurasa unaofata kuonyesha mahitaji na mwitikio wa hao unaoomba nao “Maombi ya Utatu” mnaoshirikiana.

| JINA | MAHITAJI YA MSINGI(ELEZA) (MCHORO 6.1) | MWITIKIO WA IMANI NDANI YA KRISTO (MCHORO 6. 4) |
|---|---|---|
| Mary | upendo/shauku<br>• mtoto pekee<br>• kutoka kwenye ndoa iliyovunjika<br>• kukataliwa na baba yake<br>• mama alikuwa ana kazi nyingi kuweza kuonyesha upendo | -12<br>Mary anakwenda njia yake mwenyewe.<br>Kuishi katika nchi ya Othodox, Anajua kwamba kanisa la mapokeo lipo lakini hajui kama lina cha kusema kwake. Hakuwahi kamwe binafsi kukutana na wakristo na hana habari juu ya madai ya Kristo. |

**TATHIMINI:** Katika hatua ya “maandalizi”. Inahitajika uhusiano wa kujali kabla ya kupanda kuweze kuwa kwa ufanisi.

**MFANO WA SURA YA KARATASI YA KUTUMIA KATIKA ZOEZI LA UTEKELEZAJI WA AZIMIO**

| JINA | MAHITAJI YA MSINGI (ELEZA) (MCHORO 6.1) | MWITIKIO WA IMANI NDANI YA KRISTO (MCHORO 6.4) |
|---|---|---|
| | | |

**TATHIMINI:** ____________________________________________

____________________________________________

____________________________________________

| JINA | MAHITAJI YA MSINGI (ELEZA) (MCHORO 6.1) | MWITIKIO WA IMANI NDANI YA KRISTO (MCHORO 6.4) |
|---|---|---|
| | | |

**TATHIMINI:** ____________________________________________

____________________________________________

____________________________________________

UINJILISTI
*ZIADA*

6B

# Kanuni Tatu za Uinjilisti Wa Kimkakati

Zifuatazo ni kanuni tatu za mikakati ambazo zitatusaidia katika kuwafikia hao wanaotofautiana katika upokeaji wa injili

## I. KUPANDA KIMKAKATI

Kila mpanda kanisa lazima ashughulike na swali la kipao mbele katika huduma. Miongoni mwa maswali haya ni swala la wapi pa kukazia juhudi zetu za kiuinjilisti. Tunakazania hao wanaoonekana kuwa wapokeaji, au hao wapinzani. Ingawa makundi haya yanaweza kuonekana yakiwa ya kipekee, mitume walionekana kujaribu kuweka uwiano wa usikivu kwa aina zote za watu.

### A. Hao Walio na Upeo Mkubwa wa Kuelewa Ukweli Wanaweza Kumsogelea Kristo Kwa Haraka

Unaposoma katika kitabu chote cha Matendo, jiulize mwenyewe swali kama: Wapi mtume Paulo alipokwenda alipoingia mjini? Ni nani wa kwanza aliyemkabili? Kwa nini alikwenda kwa watu hawa kwanza mpango wazi  wa Paulo ulikuwa kwenda kwa Wayahudi kwanza. Kwa nini Paulo mara nyingi zaidi alianza na Wayahudi?

Ninaamini kwamba Paulo alikuwa ameshawishika kwamba watu hawa wameshaandaliwa kupokea injili na wanaweza kuletwa kanisani na kuhamasishwa kwa ajili ya huduma wakati wa mwanzo iwezekanavyo. Wayahudi walikuwa tayari wanajua Agano la Kwanza, na kujua mambo mengi juu ya Mungu. Ni lazima tuelewe kwamba Paulo alitaka kuwafikia walio wengi kwa ujumbe wa injili mapema iwezekanavyo. Mtume alielewa baadhi ni wapokeaji kuliko wengine, wako tayari zaidi kusikia na kupokea ukweli wa kiroho. Ukweli kwamba hakuwa wakati wote akipokelewa kwa uvugu vugu na wao haina maana kwamba mkakati huu ulikuwa haufai. Kwa jinsi hiyo, Wakati Wayahudi katika mji maalumu waliikataa injili na mataifa wakadhihilisha kuwa wapokeaji zaidi, Paulo alikwenda kwa Mataifa. Tunaona namna hii ya Wayahudi-Mataifa ikiwa imerudiwa bila kukoma katika miji mingi aliyotembelea.

Ngoja tusisahau kwamba tunakusudia kueneza upandaji kanisa. Kadiri tutakavyohusisha watu wengi katika kazi hii, ndivyo inakuwa bora. Na mara watu wanapokuwa siyo shamba la mavuno, wanakuwa sehemu ya nguvu ya mavuno. Shirikisha habari njema kwa kila atakayesikia, lakini kusudia watu wanaoweza kwa haraka kuwa sehemu ya timu ya huduma ya Mungu.

### B. Hao walio na mguso mkubwa, walinzi-wa mlango", wanaweza kusogea polepole kwa Kristo, lakini mguso wao wa mda mrefu kwenye Injili unaweza kuwa mkubwa

Mfano mzuri ni Paulo mwenyewe. Alikuwa na sifa zote za kufanya makubwa kwa ajili ya Mungu. Alikuwa na jitihada zote. Lakini ilichukua mda kwake kutambua—hatimaye katika kukutana tu moja kwa moja na Kristo alieye hai—kwamba alihitaji kumugeukia Kristo. Paulo mwenyewe kisha alitamani kwenda Urumi na kushuhudia mbele ya kaisari—mtu mashuhuri ulimwenguni—hata kama ilimaanisha kwenda kama mfungwa kwenye minyororo (Matendo 25:11; 27:24). Kama Mungu amekupa moyo wa kufikia mtu mashuhuri katika jamii yako, vumilia katika uhusiano. "mwagilia maji" kikamifu. Una kitu ambacho mtu anakihitaji! Omba! Muombe Mungu kufungua milango na nafasi na kisha itumie. Kumbuka kwamba Sauli, mtesaji wa kanisa, aligeuka kuwa Paulo, mtume kwa mataifa.

## II. KUISHI KIMIKAKATI—WAKUTE WATU MAHALI WALIPO; SIYO TULIPO NA UHURU

### A. Kufikiriwa kwa Mtu Pekee Yohana 3, 4, 9

Bwana alipokuwa anaongea na watu pekee watatu maalumu katika sura hizi, tunakuta kwamba alimsaidia kila mmoja kugundua hitaji lake kwa njia tofauti. Na mfarisayo-aliyefundishwa vizuri, Yesu alimsaidia kuelewa kwamba hakuelewa ulimwengu wa kiroho kabisa. Na mwanamke msamaria kisimani, Yesu alimfanya kujisikia huru na kuamsha tena kiu yake ya kiroho kwa Mungu. Na mtu aliyezaliwa kipofu, Yesu alitimiza hitaji la kimwili, akiunda kiu ya uhusiano wa mtu binafsi. Kanuni moja tunayoweza kuiona wazi wazi katika mwingiliano huu ni kwamba Yesu hakuwatenda watu kwa "roho na masikio tu." Aliwaona watu kamili wenye mahitaji halisi na kutoa uhusiano halisi.

### B. Uinjilisti wa Kujilinganisha! Wakorintho 9:19-23

Mvuvi mwenye hekima anachunguza samaki anayetaka kumvua, kwa kujifunza aina ya chakula anachokula na mda anaokula, wapi na kwa kina gani anaogelea. Anachagua mtego au chambo ambacho kinakaribiana na tabia ya kawaida na kukitumia kumvutia samaki. Mvuvi mwenye busara haweki nyama yenye viungo vya muhungari kwenye ndoano kwa sababu tu anavipenda! Kama wainjilisti, ni lazima tuelewe njia ambazo wasioamini wanavyofikiri, kujifunza vitu wanavyovithamini, kujenga daraja kati ya mahitaji yake anapoyaelewa na mahitaji yake ya kiroho kadiri Roho na neno la Mungu linapoyadhihirisha.

## III. KUELEWA KIMIKAKATI—WATU WALIOTOSHEKA HAWATAFUTI MABADILIKO

### A. 1Wakorintho 1:18:31

Hao waliotosheka kwamba wameshajua majibu yote ni wagumu kuwaleta kwa Kristo. Kundi hili ni pamoja na wenye akili sana, matajiri, na hao wenye hali ya kidunia. Ni ukweli kwamba mara nyingi inamchukua mtu kupitia katika aina ya misuko suko binafsi kuweza kuwafanya kuweza kusikiliza ujumbe wa injili. Tunahitaji kuwa makini kwenye nafasi za uinjilisti ambazo zinaletwa na misukosuko kama hiyo. Tunahitaji pia kujenga maafikiano na watu hawa ili tujue wanapokuwa wanakutana na matatizo, ili kwamba tuweze kujibu kwa matumaini katika mda mwafaka.

### B. Mathayo 9:12

Mvuvi mwenye busara anakwenda kuvua samaki wanapokuwa na njaa, siyo mara tu wanapokuwa wamemaliza kula. Kama wainjilisti, kazi yetu ni kuwasaidia watu kugundua mahitaji yanayohitaji kutimizwa na kuanzisha haja ya njaa kwa Kristo. Ni lazima tutambue kuwa hao ambao wanaotambua mahitaji yao kwa haraka zaidi watakuwa tayari zaidi kufikiria suluhu la Kristo, kama kweli wanahitaji suluhu. Kama watu hawana njaa kwa ajili ya injili, muulize Roho wa Mungu kuanzisha njaa hiyo ndani yao.

## UFUPISHO

Kumbuka kwamba Uinjilisti wenye mafanikio unahusisha:

- Kuchukua hatua ya mwanzo, kwa nguvu na upendo wa Roho Mtakatifu, kumsaidia mtu kusogea hatua moja karibu katika utaratibu wa uamuzi kidogo wa-kumfata Kristo
- Kuwepo kutia moyo na kuwaongoza katika kujua jinsi ya kufanya uamzi huo
- Kuwaombea ili wafikie sehemu ya kutubu kikamilifu na kuamini ndani ya Kristo na kukutana na wokovu kwa imani peke yake, na
- kuwaleta wakamilifu kwenye ushirika na huduma ya kanisa la mtaa.

UINJILISTI
*ZIADA*
6C

# Kuchunguza Njia Aliyotumia Yesu Kwa Mtu Binafsi

## KARATASI YA KULINGANISHA MAZOEZI

Vitabu vya injili vimejaa mazungumzo ya kufurahisha kati ya Yesu na watu binafsi. Tunataka kuchunguza machache kati yake kuona baadhi ya tofauti na ulinganifu katika njia aliyotumia Yesu. Fanyia kazi kila fungu la andiko lililoorodheshwa kwenye jedwali na jibu maswali.

| Andiko: | Yohana 3: 1-21 | Yohana 4:5-26 | Yohana 9:5-7,35-39 | Marko 10:17-22 |
|---|---|---|---|---|
| **Yesu alikuwa akimwambia nani?** | | | | |
| **Nini tunachojua kwa mtu huyu kutoka kwenye fungu?** | | | | |
| **Ni namna gani mazungumzo yalianza?** | | | | |
| **Ni katika mstari gani mwelekeo wa mazungumzo unabadilika ?** | | | | |
| **Ni nini Yesu anachotaka?** | | | | |
| **Ni nini Yesu anachotoa?** | | | | |
| **Jinsi gani mtu pekee anaitikia?** | | | | |